Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 21 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne. S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**:-

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII**:-

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. NAOMI A. KIUHULA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo inaonekana mmeamka saa kumi maana inaonekana mpo kumi na tisa. Kwa hiyo, kazi iko kwa Mheshimiwa Spika, nitazingatia vyama, wale waliouliza karibuni na ambao hawatapata nafasi na hivyo ndivyo nitaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, huu ni utaratibu ambao upo na umeandikwa pia. Kwamba yanapokuja mazingira hayo basi utaratibu utakuwa hivyo. Tunaanza na Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeniyeye anaanza wakati wowote.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza. Swali langu kwa Waziri Mkuu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu imethibitika sasa kwamba Umeme ni tatizo sugu na kwa sababu kupitia Bunge lako Tukufu Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ilikataliwa, ni kielelezo tosha kwamba Wizara haijaweza kuwa na uwezo wa kuthibiti au kutatua tatizo la umeme. Sasa Swali.

**SPIKA:** Kwanza tunaomba tusahihishe kidogo, haikukataliwa, imeahirishwa. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wako lakini kwa sababu Bunge limeahirisha kupitisha Bajeti hiyo, ni kielelezo tosha cha udhaifu mkubwa wa maandalizi ya Bajeti hiyo.

Je, ili kuliepusha taifa na tatizo hili sugu na kwa sababu uchumi unaendelea kuathirika kwa kiasi kikubwa, Waziri Mkuu huoni sasa ni wakati muafaka kukubali ushauri wetu wa kuunda kikosi kazi cha taifa ambacho kitaishauri Serikali na kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba hata Bajeti yenu itakaporudi hapa Bungeni itakuwa ni Bajeti makini yenye kutatua tatizo hili ambalo linaliumiza taifa kwa kiwango kikubwa? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi namheshimu sana Mheshimiwa Mbowe na ushauri wake mara nyingi huwa sipendi kuupuza. Lakini kama nilivyosema mara ya mwisho suala la umeme tatizo lake linajulikana. Tumetoka wapi tuko wapi na tunatakiwa twende wapi. Mara ya mwisho nilieleza jitihada ambazo Serikali imeanza kuzifanya tangu mwaka 2008 na nikasema kwa namna tulivyojipanga ikifika tarehe 31 Agosti, 2011 tulitarajia tungekuwa tumefanya kazi nzuri tukabakiza *deficit* ya *Megawatt* 65.

Lakini nikasema Serikali imekwenda mbele zaidi kwamba hata kama tutafaulu kufikisha Watanzania katika hatua hiyo bado tunaona hatujajipa kwamba huo ndiyo uwe mfumo wa namna ya kuendesha. Kwa sababu likitokea jambo dogo tu tutapata tatizo. Kwa hiyo tukasema ule mtambo ambao Serikali imepanga kuununua wa *Megawatt* 100 utatumalizia hiyo *deficit* lakini bado kama Watanzania na hasa Serikali lazima tuwe na mpango ambao utatuwezesha kuwa na uhakika wa umeme. Ndiyo maana Bunge hili mlipokuwa mmetoa maoni yenu pamoja na ya Kambi ya Upinzani niliheshimu sana uamuzi wa kuomba tuahirishe jambo hili ili Serikali iweze kuja na Mpango wa namna ya kumaliza tatizo hili moja kwa moja, lakini ndani ya utaratibu wa kipindi hiki kifupi. (*Makofi*)

Sasa Serikali tumeanza kufanya hiyo kazi na matarajio yangu ni kwamba tutakapopewe nafasi ya kurudi tena mbele ya Bunge lako Tukufu tutakuja na huo Mpango wa kuhakikisha kwamba katika hatua hizi za muda mfupi lazima tuhakikishe tuna umeme wa kutosha, usiokuwa na mashaka na hili tunazungumza tunajaribu kutatua tatizo la muda mfupi. Sina tatizo na mpango wa muda wa kati na muda mrefu kwa sababu huko tumejipanga vizuri na ndiyo maana siku ile nilisema pengine katika hatua hii ya mwanzo si lazima tukafikiria sana jambo hilo kwa sababu Serikali nadhani tuna uwezo wa kulikabili na kulimaliza kwa ushirikiano na Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa majibu yake na ahadi aliyoitoa kwamba anapenda na hapuuzi ushauri wangu. Swali, pamoja na Waziri Mkuu kukiri kwamba wamejipanga tatizo ni giza na katika hili Serikali imezungumza ina mipango madhubuti na inalitambua tatizo la umeme tangu mwaka 2008, lakini leo tunapozungumza nusu ya nchi au robo tatu ya nchi iko giza usiku na mchana.

Ushauri wangu mwingine kwa mara nyingine kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa sababu nakutakia mema na naitakia nchi yangu mema, hatukwambii kwa sababu tuna nia mbaya, ushauri wangu, pamoja na kwamba mmeonyesha kwamba mmeshindwa kutatua tatizo la umeme kwa sababu nchi ina giza, narudia kauli yangu, kwanini unaona ni tatizo kubwa kupata ushauri kutoka kwa sekta mbalimbali katika taifa hili ili tutakapotatua tatizo la umeme tuwe tumelitatua moja kwa moja?

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Mbowe na mimi nasema hebu ipe Serikali hii nafasi kama ni kushikwa uongo tuje tushikwe uongo hapa. Hatujashindwa jambo hili hata kidogo. Mimi nashughulika na dharura lakini nimekwambia kwa maana ya Mpango wa muda mrefu mimi sioni kwamba tutashindwa. Kwa hiyo utaendelea kuniuliza jambo hili na mimi nitaendelea kulijibu hivi hivi. (*Makofi*)

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu zao la tumbaku mwaka huu limepata msukosuko mkubwa

sana, Makampuni yanayonunua tumbaku yanasema kwamba tumbaku ni nyingi sana duniani kwa hiyo hawawezi kununua tumbaku yote kwa wakulima mwaka huu.

Lakini katika hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu nimetambua juhudi zako binafsi za kuweza kutatua tatizo hilo na Serikali yako. Umepeleka watu Iran, China na kwingineko katika kuhakikisha kwamba tumbaku ya wakulima wetu ambao wamehamasika sana kuilima inanunuliwa. Nakuomba mambo mawili.

Kwanza naomba uwahakikishie wakulima wa tumbaku wa Chunya, Songea, Tabora na kote wanakolima tumbaku kwamba tumbaku yao yote mwaka huu itanunuliwa.

Pili, pamoja na huku kuringa kwa makampuni, wateuzi walioko kwenye masoko sasa hivi wanaringa kweli kweli wanafanya soko mara moja kwa mwezi au miezi miwili, wakati zamani au mwaka jana tulikuwa tunafanya soko mara mbili kwa mwezi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uhakikishe kwamba inawalazimisha hawa makampuni yanayonunua tumbaku wafanye masoko kama zamani ya kufanya masoko mara mbili kwa mwezi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Mwambalaswa ni kweli, bei ya tumbaku mwaka jana ilikuwa nzuri sana na imetoa msukumo mkubwa sana kwa wakulima wa zao la tumbaku kuongeza juhudi zaidi na ni kweli kwamba tumbaku safari hii ni nyingi zaidi kuliko mwaka jana.

Tatizo ninalolipata ni hili alilolisema kwamba udhibiti wa soko la dunia hauko ndani ya nchi yetu, Ni jambo ambalo linaamuliwa na soko lenyewe la tumbaku. Sasa taarifa anayoisema na sisi ndiyo taarifa tuliyonayo kwamba nchi zile ambazo mwaka jana hazikuweza kupata fursa ya kulima tumbaku zaidi safari hii wamelima zaidi na hawakupata mitikisiko wa tabia nchi na kwa hiyo tumbaku ni nyingi na hawawezi wanunuzi wale kununua tumbaku kwa kuwa na wao wanapima kitakachotokea kwenye soko la dunia. Changamoto ni yetu wote na ni ya Watanzania wote huo ndiyo ukweli na ndipo tulipofikishwa. Bei ya tumbaku mwaka huu sio kama ya mwaka jana, imeshuka kidogo kwa kuwa wanunuzi wanahofu kwamba wakinunua kwa bei ya mwaka jana watashindwa pengine kuuza tumbaku yote.

Kwa hiyo mimi nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba pengine tuendelee kuzungumza kuwasihi ikiwezekana tumbaku yote iweze kununuliwa kwa bei ambazo sasa hivi mmekubaliana na mimi nitajitahidi kusukuma jambo hilo kwa kadri itakavyowezekana. Ni kweli tumetuma watu Iran wakatuahidi kwamba kilo milioni tano kutoka Tanzania lakini bado hata kama wakinunua hizo kilo milioni tano bado tutakuwa na tumbaku nyingi sana imebaki.

Kwa hiyo tumaini langu ni kwamba maadamu bei hii sasa hivi inaonekana ndiyo bei inaweza kutusukuma tukazane yale aliyosema masoko mawili kila mwezi yaweze kutekelezwa ili tuone ni kiasi gani tumbaku inaweza ikanunuliwa. Kwa hiyo kama

Serikali tutajitahidi kuwabana wale wanunuzi ili wahakikishe kazi hiyo wanaitimiza inavyotakiwa.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH**: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Nchi hii inaongozwa kwa kufuata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. kwa mujibu wa kifungu.

**SPIKA:** Tuulize maswali kwa kifupi ili tupate watu wengi.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH**: Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaongozwa kwa kufuata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Ibara ya 47(1)(c), Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana mamlaka ya kufanya kazi zote za Rais kama hayupo au yuko nje ya nchi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 19/7/2011 katika Bunge hili ulitoa kauli ya kusema kwamba huna Mmalaka ya kumwondoa madarakani au ya kumwajibisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na kwa maani hiyo unamsubiri Mheshimiwa Rais kurudi safari. Swali je, huoni kwa kufanya hivyo umekwenda kinyume na taratibu za Katiba kwa sababu Mheshimiwa Makumu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwepo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah kanipa mtihani maana sikuwa nalitegemea hili. Lakini niseme tu kwamba ni kweli kwa Mujibu wa Katiba Rais anapokuwa hayupo ndani ya nchi ana acha Mamlaka ya kuisimamia nchi hii kwa ujumla kwa Makamu wa Rais na kama na yeye hayupo hata Waziri Mkuu wakati mwingine anaukwaa huo uzito.

Lakini kwa mujibu wa Katiba hiyo hiyo na kuisoma Katiba nyingine zote kwa ujumla si kila jambo ambalo Rais amepewa Mamlaka kulitekeleza sisi tunayopewa dhamana hiyo tutayafanya. (*Makofi*)

Siwezi mimi nikiachiwa au Makamu akiachiwa basi nikakaa pale nikaanza kutoa misamaha kwa wafungwa, nikaamua huyu sasa hapa, siwezi. Kwa sababu tunakikomo cha mamlaka yetu. Lengo la kipengele kile au Ibara hiyo nikuifanya nchi isionekane kwamba haina mtu wa kuuliza endapo kuna jambo linajitokeza.

Pili ni kuwezesha nchi vilevile kupitia Kiongozi huyo kuweza kuwasiliana na huyo mwenye mamlaka mapema iwezekanavyo kupata ushauri wake au maelekezo yake ili kutekeleza majukumu ya usimamizi wa nchi wakati yeye mwenyewe hayupo.

Kwa hiyo Makamu wa Rais asingeweza katika mazingira hayo akasema *"ohh basi nimeukata nakufukuza kazi!!!", Hapana*. Angeweza kufanya hivyo kama

amezungumza na Rais na Rais kasema basi fanya moja mbili tatu. Kwa kweli tusitafsiri kipengele kile kwamba, maana Rais akiondoka basi Mzee umepewa unga pale hapana. Ina *limitations* nyingi sana.

**SPIKA:** Unauliza kitu gani sasa? Haya uliza! Wapeni na wenzenu nafasi.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimefurahi kwa jibu lako lakini kwa muono wangu nasema kwamba Katibu Mkuu si suala zito la kutoweza kuamuliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna haja ya Katiba hii kuifanyia marekebisho. Unakubaliana na mimi suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Sasa mimi naheshimu sana maoni yako lakini mimi nadhani jibu langu acha libaki hivyo hivyo. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tarehe 20 mwezi wa sita mwaka huu ulizinduliwa msimu wa pamba kule Kasulu, na bei ya kuanzia *(floor price)* ilikuwa ni shilingi 1100/=. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi sasa uko mkanganyiko mkubwa kuhusu bei ya pamba. Bei ya pamba inasemakana imeshuka kutoka shilingi 1100/= mpaka shilingi 800/=, 900/= hata 700/=. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inatoa tamko gani? Kwa sababu hivi sasa mbali na kushusha, wakulima hawa wa zao la pamba wanakopa. Serikali inatoa tamko gani? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Ndassa kwamba hili ni eneo lingine tena ambalo limetupata safari hii kwenye zao la pamba, na mimi napenda niungane naye, lakini vile vile niungane na Watanzania wote wanaolima pamba kwamba tatizo hili ni kubwa sana kwa sababu limegusa wakulima wengi. Lakini, kilichotokea hasa ni nini; Bei ya dira katika zao la pamba safari hii ilipangwa na wadau wa zao la pamba. Walikutana Mwanza; wakulima, wanunuzi, Serikali kwa upande mwingine, wakalizungumza, wakaamua kwamba bei ya dira itakuwa shilingi 1100/=. Walikuwa wamejitumainisha sana.

Mheshimiwa Spika, katika siku chache tu hizi zilizopita, bei ya Dunia ya pamba tunaambiwa imeshuka ghafla kuliko ilivyotarajiwa. Na sasa kama anavyosema Mheshimiwa Ndassa, inawezekana bei sasa inayozungumzwa kwa ajili ya zao la pamba ni shilingi 800/= kwa kilo. Tofauti ni kubwa. Sasa Mheshimiwa Ndassa anasema Serikali mnasema nini? Mimi la kwanza ambalo nadhani ningeweza kusema, kwanza, ni vizuri jambo hili likaelezwa vizuri kwa Watanzania wanaolima pamba, wakaelimishwa vya kutosha, nini kimetokea katika mazingira haya ya soko la pamba Duniani. Kwanza, walielewe ili waweze kukubali ukweli unaotokana na hiyo hali ya soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili; ushauri wangu mimi kwa watu wa Mwanza, Shinyanga na maeneo mengine wanaolima pamba. Pengine katika mazingira kama haya, ni kutoa sasa uamuzi wa msingi wa kuruhusu ununuzi wa pamba kutoka kwa mtu yeyote ambaye anaona ana uwezo wa kununua pamba hiyo kwa bei ambayo anaona inafaa au

inaweza ikamtia nguvu mkulima. Kwa sababu hata walipoanza kuuza pamba kulikuwa na maneno mengi. Wanunuzi walikuwa wachache na ndiyo maana inaleta hisia kwamba inawezekana huu ni ujanja tu wa wanunuzi katika kujaribu kuteremsha bei. Ndiyo maana mimi nasema ushauri wangu ungekuwa, acheni wanunuzi wanunue pamba hiyo kwa bei wanayoona inafaa ili mradi isipungue kiasi kinachofikiriwa ni *fair* kwa ajili ya zao la pamba. Labda hiyo inaweza ikapandisha kidogo bei na pengine tukapata nafuu kidogo.

Lakini, nimeishaomba wenzangu suala hili vile vile tuli-*take up* tuone ni kweli soko limeshuka kiasi hicho, ni kweli kwamba bei sasa inaweza ikawa hiyo, ili tuweze kuwasaidia wakulima wa pamba kwa namna tutakavyoona inafaa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kumwuliza swali dogo tu. Endapo bei itashuka labda mpaka shilingi 800/=, na huyu mkulima wa zao la pamba alikuwa amezoea shilingi 1100/=; Serikali iko tayari kufidia shilingi 300/= au 400/= kama bei tapungua zaidi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, si rahisi kwa Serikali kuweza kutoa kauli nzito kama hiyo kabla hatujafanya tathmini ya kina kujua mzigo huo ni mkubwa kiasi gani na unafidia, unafidia namna gani. Lakini, ni rai nzuri, tunaweza tukaiangalia. Lakini, si vizuri nikasimama hapa nikasema hiyo tutafanya kwa urahisi. Hata kidogo! Kwa sababu tuna pamba, bado tuna tatizo la kahawa, bado tuna tatizo la mazao mengine vile vile. Kwa hiyo, ni vizuri tuktafakari kwa undani zaidi, ndiyo maana nimesema kwanza hatua ya kwanza ni elimu tu kwa Watanzania ili kwa pamoja tuweze ku-*appreciate* tatizo lilivyo kubwa.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niulize swali. Napenda kufahamu juu ya makampuni haya ambayo yamekuwa yanatapeli wananchi kama *DECI* na *Bayport* kwa sababu wananchi wamewekeza pesa nyingi huko na hawajui hatima yao mpaka sasa hivi. Sasa, ni kauli gani ya Serikali juu ya makampuni haya. Je, Serikali iko tayari kuyafunga na kuyazuia yasiendelee kuwalaghai wananchi maana wanapata shida na wanaendelea kuwa maskini? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yako baadhi ya makampuni ambayo yamejitokeza siku za nyuma na huenda yataendelea kujitokeza tu ambao wanakuja hapa kwa njia za ujanja wakitoa matumaini kwa baadhi ya Watanzania kwamba wanaweza wakatoa mikopo mizuri kwa Watanzania na hatimaye wanaingia katika matatizo makubwa. *Bayport* ni mojawapo ambayo nayo iliingia katika matatizo hayo, lakini *DECI* vile vile.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo hili tulishawahi kulisema siku za nyuma na nataka nirudie tena kuwaambia Watanzania, ni lazima tujihadhari sana na makampuni yoyote yale yanayojitokeza na kutoa matumaini ya kutoa mikopo nafuu bila kwanza kuchukua hatua za kujiridhisha na vyombo vinavyohusika. Na mara nyingi wanawalenga

watumishi na hasa walimu. Chonde chonde walimu msije mkawa chambo kwa mambo ambayo hayana utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya nini kwa wale ambao wanabainika kwamba wamefanya mambo hayo. Ni kama tulivyofanya kwa *DECI*. Bahati mbaya suala la *DECI* bado halijafikia mwisho, linaendelea Mahakamani. Lakini tutaendelea kushirikiana na Watanzania kuhakikisha vyombo vya namna hiyo kila vinapobainika, hatua za kisheria zichukuliwe. Lakini, kubwa ni rai kwa Watanzania wenzangu, tunakuwa wepesi mno tunapopewa matumaini ya faida za ajabu ajabu, tunaingia kule kichwa kichwa, halafu baada ya siku mbili tatu, unakuta hakuna faida unayoipata.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nina swali lingine la nyongeza. Kwa kuwa haya makampuni yalisajiliwa na Serikali. Sasa Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwarudishia wananchi pesa zao na kuzuia wafanyakazi ambao bado wanakatwa mishahara yao mpaka leo, kwa sababu ni hali ngumu na wengine wameshindwa kuendelea na maisha yao ya kila siku na wafanyakazi wameshindwa kufanya kazi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mkosamali, tatizo, unapokwenda kujiingiza kwenye jambo hili hukuiuliza Serikali yako ushauri wowote. Yanapoharibika mambo, unataka Serikali ibebe mzigo! Ndiyo maana nasema si sahihi hata kidogo. Rai yangu kwa Watanzania ni hiyo niliyoisema, kila mmoja asije akavutwa na kauli za vyombo hivyo. Kwa sababu vyombo vinakuja vinatumia kofia mbalimbali. Ni kweli vinajiandikisha chini Msajili wa Makampuni pale. Lakini, hiyo peke yake haitoshi. Mimi nakuja kukwambia ukinipa hivi, nitakupa, wewe fanya hivi. Kama *DECI* ilivyokuwa, sasa mtu kweli unaweza kuingia kwenye mtego wa *DECI* wa matumaini makubwa kiasi kile, faida mara tatu, nne, tano! Aha, wapi Bwana!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi alikuja katika Bunge hili akipongeza sana juhudi zilizofanywa na Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Rais Mstaafu pamoja na Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, Maalim Seif Shariff Hamad, ambaye sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais katika kufikia muafaka na hatimaye kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni zimejitokeza kauli za viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wakimkejeli Makamu wa Kwanza wa Rais na kuikejeli Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar ambayo imetokana na Kura za Maoni za Wazanzibari, Serikali inasema nini juu ya kauli hizi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid, ni rafiki yangu sana, tena mara nyingi sana tunakutana kutana, hili alikuwa hajaniambia hata siku moja. Lakini, nataka niseme kutoka moyoni kabisa kwamba kama ni kweli kuna baadhi ya Watanzania wanaweza kufikia hatua ya kukejeli hata hatua mliyofikia nzuri ya kujenga Umoja wa Kitaifa ndani ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi

nasema ni upungufu wa watu wenyewe hawa. Ehe, kwa sababu Mtanzania yeyote ambaye amekuwa akifuatilia hali ya kisiasa Zanzibar, hawezi kabisa akapuuza au kukejeli jambo jema lililotokea Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja kati ya hao ambao wanaoamini hatua ile ilikuwa ni hatua nzuri, hatua ya mfano, inatakiwa iigwe katika mazingira mengine yote. Kwa hawa *it's unfortunate* na hasa kama ni viongozi wa Serikali. Mimi nitawashangaa kweli. Sasa, kama unawajua rafiki yangu ninong'oneze tu, na sisi tutajaribu kuwaambia kwamba si vizuri mnavyofanya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kamnong'oneze, wapate *counselling*! Mheshimiwa Hamad, kwa kifupi sana!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni viongozi wa juu wa chama, mmoja ni Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Mchemba. Juzi karibuni katika magazeti walitoa hizo kauli za kumkejeli sana Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Shariff Hanad ambaye tunategemea 2015, *Inshallah* atagombea tena nafasi hiyo!

**WAZIRI MKUU:** Ahaa, kama yametoka kwenye magazeti, napata tatizo kidogo. Mimi huwa napenda sana yanayotoka kwenye Luninga kwa sababu pale namwona mtu mwenyewe anasema, namsikia. Haya magazeti inategemea gazeti lenyewe ni la nani na katika purukushani tulizonazo yuko na nani. Kwa hiyo, nitaheshimu sana ulilolisema, nitalifuatilia, lakini naogopa tu pengine chombo kilichoripoti inawezekana wakati mwingine kinaweza kikawa na upendeleo fulani fulani kutegemea tu kwamba anataka kusema nini. *(Makofi)*

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Kwa kuwa ajira Serikalini kwa watu wenye ulemavu ni tatizo kubwa. Je, Serikali inatuambia nini na ina mkakati gani kwa muda mrefu na muda mfupi katika ajira chache zinazojitokeza?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba walemavu wanatakiwa kwa kweli watazamwe kwa sura tofauti kidogo kwa sababu ya mazingira na maumbile yao. Wako ambao wanaweza kabisa kufanya kazi za aina fulani na wengine pengine si rahisi sana kufanya kazi katika mazingira fulani. Lakini, kwa mujibu wa sera ya walemavu na hata sheria ambayo tulikuja tukaipitisha hapa, Serikali tumeendelea na tutaendelea kuji-*commit* kwamba ni wajibu wa Serikali kwa walemavu wote ambao watakuwa na sifa za kuweza kufanya kazi ambazo tunaona wana uwezo nazo, tutaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, kama ni ajira Serikalini tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo moja ambalo nadhani ni muhimu zaidi ni hili eneo la kuwawezesha wao katika mazingira yao kuweza kumudu kazi ambazo zinaweza zikawapa kipato moja kwa moja kutokana na sehemu waliko. Sasa hili, halihitaji pengine mtazamo maalum namna ya kuwawezesha kuwapa mafunzo ili waweze kubuni miradi ambayo itawawezesha kuwasaidia moja kwa moja. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na jamii. Na mimi nataka niyashukuru sana madhehebu ya dini mbalimbali, *NGOs* ambazo

zimejikita sana kwenye eneo hili kwa ujumla wao, kwa kazi nzuri wanayojaribu kufanya kusaidia kundi hili katika maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Muda umepita. Tunakushukuru sana kwa namna ulivyojibu maswali, nawashukuru na Waheshimiwa Wabunge kwa namna mlivyouliza maswali na vile mlivyojitokeza kwa wingi. Kwa hiyo, mimi leo nilikuwa na neema kubwa sana. Wale ambao hawakupata nafasi, nategemea watapata nafasi siku nyingine. *(Makofi)*

## MASWALI YA KAWAIDA

### Huduma za Simu za Mkononi Tabora Kaskazini

Na. 278

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR** aliuliza:-

Simu za mkononi ni muhimu sana kwa maendeleo ya watu na uchumi kwa ujumla:-

Je, ni lini huduma hiyo itafikishwa katika Kata za Utuluma, Ndono, Usagali, Ibiri, Upuge, Magiri na Isikizya katika Jimbo la Tabora Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin A. Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa uhaba wa huduma muhimu ya mawasiliano ya simu ya mkononi katika maeneo mengi nchini yakiwemo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Kutokana na upungufu huo, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imeweka mkakati kuhakikisha kuwa maeneo yote yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara yanafikiwa na huduma hiyo ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu tayari umeainisha jumla ya Vijiji 21 vyenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 24,437 katika Mkoa wa Tabora ambavyo vitafikishiwa huduma ya mawasiliano katika kipindi cha miaka miwili ijayo ikiwemo maeneo ya Jimbo la Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, yanafanyiwa marudio ya utafiti yakinifu wa kimasoko na kampuni ya *Airtel* na inatarajiwa kuwa hadi itakapofika mwisho wa mwaka huu, tathmini itakuwa imekamilika. Vile vile kampuni ya *Vodacom* ina mikakati ya kuweka mitambo yake katika maeneo ya Uyowa, Bukumbi na Kashishi katika Jimbo la Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya simu ya *Zantel* kwa upande wake imeahidi kutanua mtandao wake kupitia miundombinu ya kampuni nyingine ili kuboresha huduma ya mawasiliano aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Aidha, kampuni ya simu Tanzania *(TTCL)* tayari imeahidi kuyaweka maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge katika mpango mkakati wa mwaka 2011/2013 wa kampuni hiyo. *(Makofi)*

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo madogo. Kwanza kabisa, naomba niseme kwamba Kijiji cha Uyowa na Kashishi, Vijiji hivi havimo katika Jimbo la Tabora Kaskazini.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba tu nimweleze kwamba utafiti huu unaonyesha utachukua muda mrefu na hali iliyopo kwa sasa ni mbaya sana. Wananchi pale wakiwa wanahitaji kupata mtandao inabidi wapande juu ya mti ili wapate mtandao.

Je, Waziri yuko tayari kwenda kujionea hali hiyo na atatusaidiaje ili mtandao huu tuweze kuupata haraka kwa sababu wananchi kwa kweli wanapata shida?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, maeneo niliyoyataja kweli hayako katika Jimbo la Tabora Kaskazini. Lakini, ninachozungumzia hapa, maeneo hayo yako karibu na kwa kuwa karibu kama nilivyosema, mtandao unapowekwa unakwenda zaidi ya kilomita 30. Kwa hiyo, kwa kuwa katika maeneo hayo mtandao utafika katika maeneo ya Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, vile vile ameniomba niende nikajionee. Niko tayari kufika kule kujionea katika kuhakikisha kwamba tunaweka huduma iliyo bora zaidi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na utafiti kuchelewa lakini ni muhimu tukajiridhisha kwamba pale ambapo mtandao utawekwa, wananchi watapata huduma iliyobora na inayokidhi mahitaji yao. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Hivi karibuni Serikali ilianzisha mfumo ama mtindo wa kusajili simu, madhumuni yakiwa ni kudhibiti matumizi mabovu ya simu. Sasa nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie, ni kwa kiasi gani hili zoezi limefanikiwa kwa sababu inavyoonekana bado kuna watu wanatumia simu vibaya lakini hakuna hatua zozote ambazo zinachukuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, japo swali ni jipya!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema swali hili ni jipya, lakini nimhakikishie tu kwamba usajili, makampuni ya simu yamefikia asilimia 90. Kutokana na ugumu wa kupata takwimu sahihi za wakazi mbalimbali makampuni yanaendelea kuwasajili wale waliobaki.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna mtu ambaye anahisi au kuna namba ambayo anaihisi kwamba inatumika vibaya, tuwasiliane ili atupatie taarifa kuna njia nyingine za kisayansi ambazo zitatusaidia kutatua tatizo hilo.

Na. 279

**Haki za Askari Waliofariki**

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. SAID MUSSA ZUBEIR)** aliuliza:-

(a) Je, ni askari wangapi ambao wamefariki wakiwa bado hawajastaafu kazi tangu mwaka 2008 hadi sasa?

(b) Je, ni wangapi kati yao waliofariki familia zao zimeshapata haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, swali lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya Askari 481 wamefariki kabla hawajastaafu kazi tangu terehe 1 Januari, 2008 mpaka 25 Mei, 2011.

(b)Mheshimiwa Spika, familia 97 zimekwishalipwa na waliobaki 384 bado hawajalipwa haki zao. Sababu kubwa zinazochelewesha malipo hayo ni kutokamilika kwa taratibu za mirathi mapema na kutowasilishwa kwa fomu za madai hayo kwa Jeshi la Polisi.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la Nyongeza.

Kwa kuwa, Kanda maalum ya Kipolisi Mkoani Dar es Salaam na Wilayani Tarime imeonesha mafanikio makubwa katika masuala yanayohusu Raia.

Je, Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuanzisha Kanda Maalum kwa upande wa Zanzibar ili kuwasaidia wanawake hawa ambao wanafiwa na waume zao na hawapati haki zao kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Spika, hizi Kanda maalum ndiyo maana naweka msisitizo katika neno Maalum, umaalum wake unatokana na hali halisi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, swali alilouliza Mheshimiwa Bura linahusu akina mama kule Zanzibar katika masuala ya mirathi, s idhani lakini tutatafakari kama suala kama hili linahitaji Kanda maalum. Kwanza inabidi kujua idadi wapo wanawake wangapi, lakini nafikiri linaweza likatizamwa katika mtizamo wa kuridhia zaidi kuliko suala la Kanda Maalum.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:**Mheshimiwa Spika nakushukuru sana. Naomba niulize swali dogo kwa Waziri.

Kwa sababu wafiwa wengi kati ya hao waliokufa kutoka kipindi hiki hawajalipwa mafao yao kutokana na matatizo ya nyaraka hazijatimia.

Je, hawa walikuwa ni askari walioajiriwa na kikosi hiki ambacho kilikuwa na kumbukumbu kamili za askari hawa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Spika, ingawaje swali lenyewe sikulipata, lakini tatizo ambalo tumekuwa nalo kwa suala la mirathi na ucheleweshaji huu, ni kwa sababu familia zenyewe kumekuwa na mgawanyiko sana kujua nani hasa wanaweza wakasimamia madai ya Marehemu katika upande wa Serikali. Pili kumekuwa na suala la nyaraka zinakuwa hazikukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya sasa hivi ambao ni utaratibu mpya, itakuwa sasa pale ambapo tunaona kwamba kunakuwa na ucheleweshaji katika madai sisi upande wa Polisi itabidi kuzifuatilia zile familia kwa kuwa tunazo rekodi zao na kujua kwamba ni kwanini imechukua muda na kitu gani kinaendelea kuhusu masuala ya mirathi yao.

Na. 280

**Sheria za Jeshi la Polisi**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Jeshi la Polisi limerithi sheria nyingi kutoka Jeshi kwa Jeshi la Kikoloni na sasa haziendani na wakati tulio nao.

(a) Je, ni Sheria ngapi zimefanyiwa marekebisho?

(b) Kama zipo. Je, ni zipi kwa majina?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Yahya kwa kuwa mdau mkubwa wa masuala ya Polisi na katika kuleta maswali ya Polisi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mbunge kwamba sheria nyingi za Jeshi la Polisi zimepitwa na wakati (*outdated*). Aidha, hakuna marekebisho ya msingi ambayo yamefanywa katika sheria hizo.

Mhehsimiwa Spika, kwa kulitambua hilo Jeshi la Polisi lilianzisha mpango wa maboresho yaani *Police Force Reform Programme*, ambao pamoja na mambo mengine utahusisha na kuzifanyia marekebisho sheria na kanuni zote zinazohusu utendaji wa Jeshi la Polisi. Tarehe 31Machi, 2011 Serikali iliridhia mpango huu wa maboresho na utekezaji wake unaanza rasmi katika mwaka huu wa fedha.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika nashukuru.

(a) Je, unaweza kuieleza ni sheria zipi mtazipa kipaumbele katika marekebisho hayo ambazo haziendani kabisa na wakati tulionao?

(b) Ni sababu zipi za msingi uliosababisha ucheleweshaji wa marekebisho ya masingi katika sheria hizi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, anauliza ni sheria zipi mimi namwambia kwamba tutazipitia sheria zote. Kwa hiyo, tutakuwa hatuchagui hii na kuacha hii. Tutazitazama sheria kwa ujumla wake na maboresho au mabadiliko yatatazamwa katika mtazamo huo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kishajibu swali lako la kwanza nitakuwa nimejibu swali la pili na kusema kwamba ucheleweshaji wa sheria hizi kama nilivyojibu katika swali la Msingi, haijawahi kufanyika marekebisho yeyote ya msingi katika sheria hizi, itakuwa ni mara ya kwanza na kwa maana hiyo tutazitazama zote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniona. Hivi karibuni taasisi ya haki za binadamu ya Jumuiya za Madola ilitoa ripoti ambayo inaonesha bayana kwamba sheria za Jeshi la Polisi Tanzania hazizingatii mikataba ya Kimataifa ya haki za binadamu na utawala bora. Kwa kuwa sasa Serikali imesema itafanya mapitio ya sheria, ripoti hiyo ilianisha mahsusi sheria ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2002 kwamba inamwelekeo wa ukandamizaji wa raia. Lakini vile vile ina mwingiliano wa wanasiasa kuingilia Jeshi la Polisi.

Je, kwenye marekebisho hayo ya kisheria yanayokusudiwa kufanyika, Serikali iko tayari kuzingatia mapendekezo ya ripoti hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Spika, taasisi aliyoisema zipo taasisi nyingi, na taasisi hizi zina malengo tofauti. Hii aliyoitoa ni *opinion* mojawapo katika *opinions* nyingi ambazo zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi, sheria zote zitatazamwa, na zitakapotazamwa zitaangaliwa kama sheria lakini pia zitazingatia maslahi ya Watanzania wote. Kitu ambacho siwezi nikakubali hapa katika Bunge ni pale wanaposema kwamba sheria mojawapo kama hii ya 2002 ni Sheria kandamizi na pale anapoendelea kusema kwamba wanasiasa wanaingilia vyombo vya Polisi. Mimi niseme tu kwamba haya ni

mawazo na mawazo yataendelea kuwepo. *Shades of opinions will always be there*, kwa sababu inategemeana na malengo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo nitamwambia Mheshimiwa Mnyika na ninataka nimpe *assurances* zetu ni kwamba sheria zote zitatazamwa na *interest* za Watanzania zitakuwa *taken fully into account*. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:**Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, sheria za Jeshi la Polisi ni za toka enzi za kikoloni na sheria nyingi za enzi za kikoloni katika taasisi nyingi zimerekebishwa hasa zilizokuwa haziendani na wakati.

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba wanawakandamiza Polisi hawa hasa kwa sheria ambazo haziendani an wakati dhidi ya Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sereweji tumekuwa tunazungumza mara kwa mara kuhusu sheria za Polsi. Kitu ambacho nitakuambia ni kama nilivyojibu katika majibu ya swali la msingi, kwamba hizi sheria hazijatazamwa kwa undani wake, na itakuwa ni mara ya kwanza wakati tutakapokuwa tunafanya hii *Policy Reform Programme* kwa sababu tutatazama sheria zote na zile ambazo Wabunge hapa ndani ya Bunge Tukufu wamekuwa wanasema kwamba ni sheria kandamizi ama ni sheria ambazo haziendani na utimizaji wa haki za Askari Polisi, zote zitatazamwa na kabla hata hazijapitishwa kama sheria zitatazamwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba hapatakuwa na wasiwasi kuhusu maslahi na haki za Askari kama raia wa nchi hii zitazingatiwa. *(Makofi)*

Na. 281

**Vigezo vya Kusajiliwa kwa Shule Binafsi**

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI** aliuliza:-

Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho namba 10 ya 1995 inatamka kwamba ili shule binafsi iweze kusajiliwa inatakiwa kukidhi vigezo vilivyowekwa kama vile majengo, uwepo wa stahili kwa ajili ya madarasa, maabara, maktaba na viwanja vya michezo.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa baadhi ya shule binafsi ambazo hazikidhi vigezo hivyo na kulazimisha wazazi kuchangia michango mbalimbali na kulipa ada kubwa?

(b) Je, kwa nini Serikali haijachukua hatua kudhibiti ada kubwa zinazotozwa na shule binafsi ambazo wazazi wengi hushindwa kuzimudu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chritina Lissu Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shule inaposajiliwa kuwa imekidhi vigezo vya kusajiliwa ikiwa ni pamoja na kuwa na miundombinu yote muhimu yakiwemo majengo, maktaba, madarasa na viwanja vya michezo, hivyo ni makosa kwa shule au chuo kusajiliwa bila kukidhi vigezo hivi. Aidha, ni kinyume na taratibu na miongozo ya Wizara kwa baadhi ya shule za binafsi kulazimisha wazazi kuchangia michango ya majengo na kutoza ada kubwa kuliko ilivyoelekezwa na Serikali. Waraka wa elimu Na.19 wa mwaka 2002 unawaelekeza wenye shule binafsi kutoza ada ya kiasi cha shilingi 380,000 kwa shule za bweni na shilingi 150,000 kwa shule za kutwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba shule za binafsi zimekuwa zikitoza ada kubwa pamoja na michango mbalimbali. Hali hii, pamoja na mambo mengine, imechangiwa na kupanda kwa gharama za uendeshaji pamoja na utashi wa baadhi ya wazazi kupenda kuwapeleka watoto wao kwenye shule ambazo zinatoza ada kubwa. Kwa kutambua jambo hilo, Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuangalia upya gharama za uendeshaji wa shule ili kupata gharama halisi ya kusomesha mwanafunzi mmoja kwa mwaka *(unit cost)* ili kuweza kutoa mwongozo kuhusu kiwango gani cha ada shule za Serikali na binafsi kinachoendana na gharama halisi za uendeshaji wa shule kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwaomba wadau wote wa elimu hasa wamiliki wa shule binafsi kuwa na moyo wa uzalendo, katika suala zima la utozaji wa ada na michango kwa kuzingatia hali halisi ya kipato cha Mtanzania wa kawaida.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa waraka huo wa elimu Namba 19 mwaka 2002 pamoja na miongozo iliyotolewa na Serikali inayokataza ada kubwa na michango ya majengo kwa shule za binafsi vimepuuzwa na shule hizi kwa kuwa zinaendelea kuchangisha michango na kutoza ada kubwa.

(a)Je, ni kwanini Serikali haijafuatilia utekelezaji wa waraka huo na miongozo hiyo ili kuzichukulia hatua shule ambazo zinakaidi?

(b)Baadhi ya shule za binafsi ambazo zimekuwa zikiendesha shughuli zake bila kusajiliwa jambo ambalo linawafanya watoto inapofikia wakati wa kufanya mitihani ya

kitaifa kushindwa kufanya mitihani kwa kuwa shule haijasajiliwa. Je, kwa nini Serikali haijafanya ukaguzi kuzibaini shule hizo ili kuepusha wazazi na wanafunzi kutokana na hasara wanayopata?

**NAIBU WAZIRI WA ELUMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba sasa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuweza kuona ni namna gani tuboreshe au tuweke *unit cost* kwa kuongeza ada kwa shule binafsi kwa sababu sasa ni miaka yapata tisa toka waraka wa mwaka 2002 ambao ulisema kwamba shule za binafsi kwa bweni ni shilingi 380,000 na kutwa ni shilingi 150,000, hali halisi ambayo kwa maisha ya sasa haiwezekani kabisa.

Kwa hiyo, miaka yote tisa wamiliki wa shule binafsi wamekuwa wakitoza ada holela na Serikali imeona kilio hicho ndiyo maana nimesema kwamba mwaka huu tunataka tuweke mfumo halisi ambao utawezesha kuona ni gharama gani shule hizi ziweze kutoza ada katika kiwango kinachotakiwa kutokana na maisha ya Mtanzania kwa leo. Kuhusu swali lingine ni kwamba zipo shule ambazo zinapewa vibali vya kuanza shule kibali cha kumtambua meneja, Mwenye shule na kuangalia vigezo vingine vyote vya usajili wa shule. Lakini kama wakaguzi wakifika kwenye shule wakiona bado shule haina sifa, walimu hakuna, vitabu, madawati na majengo ya utawala pamoja na mambo mengine, hutoa kibali tu kwa mwaka labda mmoja ili kwamba wale watoto waweze kufanya mitihani ya *form two* ya Kitaifa na baada ya mwaka mmoja wale watalaam wakirudi wakikuta tena bado shule haikidhi tena vigezo huwa zinafungiwa.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niwaambie wadau wengine wote wa shule za binafsi kwamba Serikali kupitia Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi huwa anatoa kibali kwamba anzisha shule na baada ya mwaka mmoja ukamilishe haya kadri ya taratibu na vigezo ili baadaye wapewe usajili kamili.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, zipo shule za binafsi za sekondari ambazo zimelengwa kwa ajili ya kuwapata wananchi wenye kipato cha chini, lakini shule hizi nyingi hazina walimu wa kutosha na zingine walimu waliopo hawana taaluma ya ualimu, matokeo yake wanafunzi wengi wanaosoma katika shule hizi hufanya vibaya katika mitihani ya kidato cha Nne.

Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kukabiliana na changamoto hii ili kunusuru Watanzania maskini wanaosoma katika shule hizo ili waweze kufanya vizuri kidato cha Nne?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtema naona Waziri hakulipata vema swali lako.

**MHE. REGIA E. MTEMA:**Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba zipo shule nyingi za binafsi za sekondari ambazo hazina walimu wa kutosha na walimu wengine waliopo hawana taaluma ya ualimu, hali hii inapelekea watoto maskini wanaosoma kwenye shule hizi wanashindwa kufanya vizuri kwenye mitihani ya Kidato cha Nne.

Je, Wizara imeandaa mkakati gani wa kukabiliana na changamoto hizi ili watoto wa Watanzania maskini wanaosoma kwenye shule hizi za jioni waweze kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya kidato cha Nne?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, mimi ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Regia Mtema kwamba, kama ana uhakika wa shule yoyote binafsi, ambayo anaona ina walimu ambao hawana vigezo, basi tuwasiliane tuweze kuitambua shule hiyo na ili tuweze kutuma Ukaguzi Maalum kwenye Kanda husika, kadiri utakavyokuwa ume-*mention* shule hiyo, waweze kuliangalia suala hilo ili tuweze kuwachukulia hatua stahiki zinazochukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Na. 282

**Usafiri Kwa Maafisa Utamaduni Wilaya**

**MHE. REBECCA M. MNGODO** aliuliza:-

Serikali kwa kutambua umuhimu wa Utamaduni wa Taifa imeweka Maafisa Utamaduni kwenye kila Halmashauri ya Wilaya lakini wanapata tatizo la usafiri katika kutekeleza wajibu wao:-

Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kuwapatia Maafisa hao usafiri angalau wa pikipiki na kuwatengea fedha ili waweze kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mngodo, kwa kuona moja ya matatizo yanayowakabili Maafisa Utamaduni, wanapotaka kutekeleza wajibu wao. Ninaungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba; ni vyema na muhimu kwa Maafisa Utamaduni hao kupatiwa usafiri, siyo tu wa pikipiki hata magari na kuwatengea fedha ili waweze kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi zaidi.

Hata hivyo, ninapenda kumjumlisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji, nchini ndizo zinazoajiri baadhi ya Maafisa wa Kada mbalimbali Serikalini, wakiwemo Maafisa Utamaduni. Hivyo basi, jukumu la kuwapatia usafiri Maafisa hao hata kama ni pikipiki kama alivyopendekeza ni la Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kutoa wito kwa Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji nchini, kuwapatia usafiri Maafisa Utamaduni na pia

kutekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kutenga fedha kwenye bajeti zao ili Maafisa hao waweze kutekeleza ipasavyo majukumu ya Kitaifa kama ilivyo kwa maafisa wa kada nyingine.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa wito kwa Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji nchini kutekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kutenga fedha kwenye Bajeti zao ili Maafisa wa Utamaduni waweze kupatiwa vyombo vya usafiri. Je, Serikali haina utaratibu wa kufanya ukaguzi katika Halmashauri zake wa utendaji kazi na hivyo ingekwisha kugundua mapema ya kwamba Maafisa Utamaduni hawana vitendea kazi na hasa katika Halmashauri ya Meru ambapo Afisa Utamaduni anakaa tu Ofisini bila kufanya kazi kwa ukosefu wa vitendea kazi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Serikali inatambua majukumu ya Maafisa Utamaduni na wamepangiwa mwongozo rasmi wa kuweza kufanya kazi zao thabiti kama walivyopangiwa kwa kufuata Sera yetu ya Utamaduni. Halmashauri inatambua kabisa kwamba, wana Maafisa wao na majukumu yapo yameainishwa vizuri. Kazi ya Halmashauri ni kuhakikisha kwamba, wanawasimamia Maafisa Utamaduni wao wafanye kazi zao kwa ufanisi.

Kwa upande wa Meru, sina uhakika hasa unazungumzia matatizo gani, kwa sababu kazi za Maafisa Utamaduni zinaeleweka wanatakiwa kuhakikisha wanasimamia masuala mbalimbali yanayoendana na shughuli za Utamaduni wa Taifa. Kwa mfano, kuhakikisha kwamba, majukumu mbalimbali yanayoendana na mila na desturi na lugha katika zile sehemu wanazosimamia zinasimamiwa vizuri. Sasa sijui huko upande wa Meru tatizo liko wapi, kama tatizo ni kuhusu mila na desturi hazijakaa vizuri na watu hawazifuatilii au vikundi vya sanaa vilivyoko hapa havisimamiwi vizuri, matatizo yao hayaeleweki, hilo siwezi kutambua lakini nitahakikisha kabisa tunawafuatilia Wakuu wa Halmashauri ya pale na kuhakikisha kwamba, Maofisa wao wa Utamaduni wanafuatilia hizo shughuli. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamekwisha.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kunakuwa na mwongozo mmoja kwa wakati mmoja.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7). Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa anajibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, kuhusu kushuka kwa bei ya pamba kutoka shilingi 1,100 kwenda shilingi 800, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kwamba; wao kama Serikali, wameshauri tu wawepo wafanyabiashara wengi wa kutosha, pengine ndiyo wanaweza wakanusuru wakulima. Ni ukweli usiofichika ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, mwongozo hutakiwi kuhutubia, wewe unataka kusemaje sasa?

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba mwongozo wako; kama Serikali ambayo ndiyo ilitangaza yenyewe bei ya pamba kule Kasulu tarehe 20 mwezi wa 6, lakini inakwepa kuwajibika kwenye matamshi yake kwa Wakulima wa Pamba. Ninaomba mwongozo wako, katika mazingira hayo mimi kama Mbunge ninaweza kufanya nini pale ambapo Serikali inakataa kuwajibika kwenye kauli yake?

**SPIKA:** Mimi ninadhani mwongozo wangu, ushauri wa Waziri Mkuu alioutoa mkaufuate.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi kitu ambacho ningekuomba, kuhusu utaratibu mzima wa kujiorodhesha kumWuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali ya kila Alhamisi. Utaratibu ambao tulianza nao, tulikuwa tunakuja saa 12.00 halafu watu wakaanza sasa kuja saa kumi na moja, saa kumi na nusu; utafika wakati watu watalala katika Ofisi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, huoni kwamba ni bora utafutwe utaratibu mwingine kwa sababu hata huu ambao upo watu huwa wanachakachukua kutokana na vyama vyao na uwezo wako uliokuwa nao? Hivi kwa nini tusijiorodheshe Jumatano halafu wewe ukafanya hiyo kazi na sisi tukakupa uhuru huo au ukapeleka kwenye Kanuni ya Bunge tukarahisisha hii ili tuondoe huu utaratibu wa kuja usiku sana, kwa usalama wa Wabunge wenyewe ambao hawapati nafasi akiwemo Mheshimiwa Mbunge jirani yangu ambaye leo alikuja saa kumi alfajiri? Ahsante sana.

**SPIKA:** Kwanza, uondoe maneno kuchakachua.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Ninaondoa, lakini imefahamika. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, anachokisema Mheshimiwa Sanya ni sahihi kwamba, bado kuna tatizo. Kama hivi leo, watu 19 wamewahi na wamefoleni pale; sasa unafanyaje? Wiki iliyopita bahati nzuri walikuwa wachache, wakawa sawa na idadi inayotakiwa, nikawa na bahati hiyo kwamba, ninaweza kuwataja wote. Kwa hiyo, bado kama anavyosema, kuna mengi ya kuyafanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Ukumbini; kwanza ninao wageni wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, ambaye ni Katibu Mkuu, Mheshimiwa Kijakazi Mtengwa. Tumefurahi sana na tunakupa hongera kwa uteuzi huo na ufanye kazi kwa kushirikiana na Waziri wako. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Mbunge wa siku nyingi katika Bunge hili, yeye alistaafu hasa hasa, maana wengine wakishindwa wanasema wamestaafu, kumbe walishindwa

wenyewe. Huyu amestaafu kabisa; ni Mheshimiwa Paulo Kimiti. Ameshashika nafasi ya Uwaziri kwa muda mrefu na kwa hawa mlioanzisha Chama cha *Population,* yeye ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wake, ambaye alikianzisha na akakikabidhi kama kilivyo. Kwa hiyo, ninadhani wanachama wale mtashirikiana naye kupata ujuzi wake kabla hajaendelea na safari yake. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hawa ni wawakilishi kutoka *Development Partners,* ambao wamefika kufuatilia Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wao nitawataja kwa majina; sijui wamekaa kwenye *Speaker's Galley?* Kuna Ndugu Victoria Mushi, anatoka SIDA Canada; yuko wapi? Mlipaswa kukaa pale.

Kuna Ndugu Margareth Lugambwa, naye SIDA Canada; kuna Ndugu Elasimina Masawe, anatoka *UN Women*; Ndugu Ludovick Tarimo anatoka USAID; Ndugu Lucy Malele kutoka Ubalozi wa Ireland; Ndugu Alisi Hamad kutoka *UN Women*; na Ndugu Margareth Chacha kutoka Benki ya Wanawake. Ninaomba wanaohusika muwahamishie kwenye *Speaker's Gallery* hawa wote. (*Makofi*)

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo: Wapo wanafunzi 50 na walimu kumi kutoka Shule ya Sekondari ya Makole Dodoma; walipo ninaomba wasimame. Ahsanteni, karibuni sana. Someni kwa bidii.

Tuna wanafunzi 50 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Bihawana Dodoma na wao wasimame walipo. Ninadhani watakuwa *bassement,* watapata nafasi mchana. Tuna wanafunzi 70 na walimu saba kutoka *Laskazone, English Medium Primary School Tanga*. Ahsante karibuni sana.

Tuna wanafunzi 12 wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, hii ni Kampasi ya Dar es Salaam na hawa wako wapi; wako kule. Ahsanteni sana. Tunaomba mkazane kusoma na kama nilivyosema jana, mkiwa na mambo makubwa mnazungumza, siyo vinginevyo. Kwa kufanya hivyo ndiyo tutafanya vizuri. Ahsanteni sana. Karibuni. (*Makofi*)

Nina matangazo ya kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na Kikao cha Kamati kuanzia saa saba, siyo saa tano katika Ukumbi Namba 227; mikutano yote inakuwa saa saba.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wa CCM, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya CCM, siyo ile ya kwangu, kutakuwa na Kikao leo tarehe 21 mwezi 7, saa saba mchana katika Ukumbi wa Spika, siyo wale wa kwangu wale ni wa CCM, kwa hiyo, msichanganye.

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mwenyekiti, sijui Mwenyekiti wa nini; yeye ameomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, leo kutakuwa na Kikao cha Pili cha Wabunge ambao Majimbo yao yanajishughulisha na uvuvi. Ajenda za kikao

zitatolewa hapo hapo kwenye kikao. Kikao kitafanyika Jengo la Utawala, Ghorofa ya Pili, Chumba Namba 219, saa saba mchana.

Ofisi yangu pia inawatangazieni Waheshimiwa Wabunge, ambao ni Wanachama wa *NSSF* kwamba, waende wakachukue kadi zao za uanachama kwenye *Desk* la *NSSF*, lililopo mapokezi, Jengo la Utawala. Kuna waliojiunga na *NSSF*, sasa kadi zao zimefika waende wakazifuatilie *reception* pale.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira); inanipa tatizo sielewi ni kitu gani! Anasema, kuna wageni wao wa *DUSE* wako hapa. Sasa kuna Wabunge, ninadhani walikuwa wanawasiliana na hawa ndugu wa *DUSE*, sasa mwakumbushwa kwamba, wako hapa na kwa hiyo, wakutane. Wanafuatilia sijui michango, ambayo walikubaliana nayo. Nimesema nina matatizo; ni kitu gani hasa!

Kwa hiyo, wanaohusika na *DUSE* hapa, Waziri anasema wapo wageni. Kwa hiyo, mtakutana nao; hakusema ni wapi, lakini wapo hapa hapa. Ninadhani vizuri ni kumfuata Mheshimiwa Waziri mwenyewe, atakuwa anaelewa wapi wanaweza kuonana.

Waheshimiwa Wabunge, jana tulitangaza tulikuwa na wageni wetu kutoka Bunge la Uganda, sasa inabidi nionane nao, kwa hiyo, nitamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabumba, aweze kuendelea na Kikao.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Massele Mabumba) Alikalia Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na utukufu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, nikiwa na afya njema na kusoma Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara yangu, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nitumie fursa hii, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya

Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita na kuweza kupata dhamana ya kuliongoza Taifa hili kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Nne. Aidha, ninapenda kumpongeza kwa kuiongoza nchi yetu vizuri katika miaka mitano ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne. Ninamtakia kila la kheri katika miaka mitano ijayo, aendeleze mafanikio hayo na kuongeza mengine ili maisha bora kwa kila Mtanzania yaendelee kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inaonesha ni jinsi gani Wananchi wanavyothamini mchango wake katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na hatimaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura nyingi, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na uhodari na uchapakazi wake ambao sisi sote tunaufahamu, ni wazi kwamba, Watanzania wote tunayo matumaini makubwa na uongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Anne Semamba Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa kushika nafasi hii yenye wajibu mkubwa wa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Hii ni nafasi inayohitaji hekima, umakini, busara na utulivu mkubwa. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika. Ni matumaini yangu kwamba, uzoefu wake wa muda mrefu, utalinufaisha Bunge hili na kwamba, atakuwa wa msaada mkubwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Vilevile ninawapongeza Waheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Sylivester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole, wewe mwenyewe, kwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchukua fursa hii, kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Makamu wake, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, kwa kuchaguliwa kwao kuiongoza Kamati hii na kwa kuichambua na kuijadili Bajeti ya Wizara yangu kwa kina. Maelekezo na ushauri uliotolewa na Kamati hiyo, umeweza kuboresha bajeti ninayoiwasilisha hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mara ya pili katika Awamu ya Nne. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, anijalie uwezo, ujasiri na afya njema ili niweze kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchukua fursa hii, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa Hotuba yake ya Bajeti ya

Mwaka 2011/2012, ambayo imeonesha mwelekeo na dira ya utekelezaji kwa shughuli za Serikali kwa kipindi husika. Ninampongeza pia Mheshimiwa Mustafa Haid Mkulo, Mbunge wa Kilosa na Waziri wa Fedha, kwa Hotuba yake ya Bajeti, ambayo imeainisha Misingi na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kupata ridhaa ya Wananchi ya kuingia humu Bungeni, lakini pongezi za pekee ni kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake na hasa Wanawake Vijana, ambao wanatoa michango mizuri, yenye uchunguzi ya *kidotcom*; hongereni sana. (*Makofi*)

Pia ninawapongeza sana Wabunge Wanawake wa Majimbo, kwa ushindi wao ambao umepelekea ujumbe kwamba, tunaweza na hatuogopi. Vilevile ninapenda niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge Wanawake, ambao Majimbo yao yalionesha imani kubwa kwao na walipita bila kupingwa; nao ni Mheshimiwa Makinda na Mheshimiwa Prof. Tibaijuka, ambao wamepita bila kupingwa katika Majimbo yao. Hiyo pia inaonesha kwamba, sasa jamii inawakubali wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika uchaguzi uliopita, tumeona mafanikio makubwa tulipoona kwamba, katika Jimbo moja la mwanamke nalo ni la Misenyi la Mheshimiwa Assumpter Mshama, alipata kura nyingi kuliko Majimbo mengine yote. Kwangu mimi ninaona fahari kusimama hapa na kuwapongeza na ninasema kweli mafanikio haya makubwa yameoneshwa kutokana na Sera nzuri ya Chama cha Mapinduzi ya kuleta usawa baina ya wanawake na wanaume na kuhakikisha tunakuwa na nafasi nyingi zaidi ndani ya Bunge na vyombo vingine vya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, ninaomba nichukue nafasi hii adhimu, kuishukuru familia yangu, akiwemo Alhaji Kitwana Kondo na watoto wangu Fred, Lawry, Liphod na Adnan; wao ni sehemu ya wanaonisaidia na kunitia nguvu katika kazi zangu za kila siku. Shukrani hizi ziende pia kwa ndugu na jamaa zangu, ambao siku zote wamekuwa karibu na mimi wakiwemo pia na wakwe zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kukushukuru wewe kwa jinsi ulivyokuwa ukiliendesha Bunge, tangu ulipopata nafasi hii, kwa jinsi ulivyokuwa makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu itazungumzia maeneo manne ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005; Hali halisi ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii na changamoto zilizopo; Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2010/2011 na Malengo ya Mwaka 2011/2012; na maombi ya fedha za utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha Januari 2006 hadi Desemba 2010, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, iliielekeza Sekta ya Maendeleo ya Jamii itekeleze maeneo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara yangu inaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF).* Kati ya mwaka 2006 hadi 2010, jumla ya Shilingi 1,048,000,000 zilikopeshwa kwa wanawake wajasiriamali katika Halmashauri 128 Tanzania Bara. Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii 265 kutoka ngazi za Kata, Halmashauri na Mkoa, walipatiwa mafunzo kuhusu kuhamasisha wanawake kujiunga na *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania *(TWB)*, ilianza kutoa huduma za kibenki tarehe 28 Julai, 2009, ikiwa na mtaji wa Shilingi bilioni 2.8. Hadi kufikia Desemba 2010, mtaji wa Benki hiyo ulikuwa shilingi bilioni 4.8. Benki hii imekuwa ikitoa mikopo kwa ajili ya mitaji ya kuendesha biashara pamoja na mahitaji binafsi kwa wateja wake. Hadi Desemba, 2010, Benki ilikuwa imetoa mikopo kwa wanawake na wanaume, yenye thamani ya shilingi bilioni 8.4, ambapo idadi ya wanawake ni 893, sawa na asilimia 70 na wanaume ni 383, sawa na asilimia 30. Tofauti na benki nyingine, benki hii hutoa mafunzo kwa wateja watarajiwa. Hadi Desemba, 2010 jumla ya wateja 5,246 wakiwemo wanawake 4,358 na wanaume 888 walipata mafunzo ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Serikali imechukua hatua za kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za Uongozi wa Kisiasa na Kiutendaji. Mheshimiwa Rais, amefanya uteuzi wa wanawake katika ngazi hizo. Kwa niaba ya Wizara yangu, ninapenda kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa jitihada za kuongeza wanawake katika ngazi za juu za uongozi. Hii inaonesha jinsi Mheshimiwa Rais, anavyojali na kuthamini michango ya wanawake katika maendeleo. Aidha, Wizara yangu imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kuiwezesha Tanzania Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika Nafasi za Uongozi wa Kisiasa na Kiutendaji. Rasimu hiyo ipo katika ngazi za juu za maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kuhusu mila zenye kuleta madhara: Wizara iliendelea kuratibu kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto, Vikongwe na Albino iliyozinduliwa mwaka 2008 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara iliratibu uundaji wa Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto, Vikongwe na Albino. Juhudi nyingine ni pamoja na Wizara kuandaa Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Familia, ambayo inatoa mwelekeo wa kukabiliana na mila zenye kuleta madhara katika jamii. Aidha, Wizara iliandaa mkutano wa Kamati ya Sekretarieti ya Kutokomeza Ukeketaji Tanzania na kutoa mafunzo ya kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake kwa wasimamizi wa sheria 316, wakiwemo Askari Polisi 110, Askari Magereza 110, Mahakimu wa Wilaya 60 na Kamati tatu za kuzuia Ukatili wa Kijinsia zenye jumla ya wajumbe 36. Wizara pia iliandaa sinema ijulikanayo kwa jina la "*Piga Vita Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto na Mauaji ya Albino,"* yenye maudhui ya kukabiliana na mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii. Sinema hii ilioneshwa kupitia Kituo cha Televisheni ya Taifa *(TBC)* na sehemu mbalimbali za Mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga kwa kutumia gari la sinema.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara yangu inaratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Haki na Ustawi wa Mtoto, ambayo nchi imeridhia. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kudurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 1996, ili kuelekeza namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika upatikanaji wa haki za watoto; kuandaa rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto wa Mwaka 2008; Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009, ili kuboresha upatikanaji wa haki za watoto na kuweka masharti maalum kwa ajili ya kuhifadhi na kulinda haki hizo. Aidha, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, liliimarishwa na mabaraza mengine yaliundwa katika ngazi ya mikoa 26 na wilaya 87. Vilevile taarifa za utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Haki na Ustawi wa Mtoto, ziliwasilishwa na kutetewa katika mikutano minne ya Umoja wa Mataifa iliyofanyika Accra (Ghana), Geneva (Uswisi), Addis Ababa (Ethiopia) na Dakar (Senegal).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau iliratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazolenga kupunguza vifo vya watoto wachanga. Baadhi ya mafanikio ni pamoja na kuandaa mkutano wa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika kuhusu Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, uliofanyika Arusha mwezi Februari, 2008. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, uliazimia kila nchi mwanachama iandae Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara iliratibu uandaaji wa sera hiyo ambayo kwa sasa imewasilishwa kwenye ngazi za juu za maamuzi ili ipitishwe kwa utekelezaji. Sera hiyo inasisitiza wazazi, walezi, jamii na wadau, kuwapatia watoto wadogo huduma muhimu kama vile lishe bora, chanjo na tiba ambazo pamoja na mambo mengine, zinasaidia kuzuia vifo vya watoto wachanga. Aidha, katika kufanikisha utekelezaji wa masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Wizara iliratibu uanzishwaji wa Kamati Elekezi na Kamati ya Utendaji, ambazo wajumbe wake wanatoka Wizara za Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni na Siku ya Familia Duniani tarehe 15 Mei. Vilevile Wizara ilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Ajira Mbaya kwa Watoto Duniani, tarehe 12, Juni. Katika maadhimisho ya siku hizo, Wizara ilielimisha na kuhamasisha jamii kuhusu wajibu na jukumu lake hususan kuzuia utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari zinazoathiri afya zao. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 36 na kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 120 katika mikoa 18 ya Tanzania Bara kuhusu haki za mtoto za kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushirikishwa na kutobaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara yangu inaratibu utoaji wa mafunzo ya ufundi na stadi za maisha katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu kupitia vyuo hivyo, imetoa mafunzo ya stadi na maarifa mbalimbali kwa Wananchi 151,428; kati yao wanawake ni 71,439 na wanaume ni 79,989. Mafunzo hayo yamewawezesha Wananchi kujiajiri na kuajiriwa, hivyo, kuchangia katika vita dhidi ya umaskini. Aidha, ukarabati na

ujenzi wa majengo na miundombinu uliendelea kufanyika katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 34. Ukarabati umeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, hivyo kuvutia Wananchi wengi kujiunga na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara iliratibu utoaji wa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada katika vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii. Katika kukidhi mahitaji ya Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ngazi za kata na kijiji, Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii viliendelea kutoa mafunzo ya ngazi ya astashahada na stashahada. Jumla ya wanafunzi 3,867, wakiwemo wanawake 2,794 na wanaume 1,073 walidahiliwa katika mafunzo ya Astashahada ya Maendeleo ya Jamii. Jumla ya wanafunzi 1,289 wakiwemo wanawake 905 na wanaume 384, walidahiliwa katika mafunzo ya Stashahada ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, jumla ya wahitimu katika vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii ni 1,968, wakiwemo wanawake 1,352 na wanaume 616. Wataalamu hawa huajiriwa katika ngazi za kata na kijiji hivyo wana umuhimu wa pekee katika kuleta chachu ya maendeleo katika ngazi hizo. Aidha, kazi ya kupitia upya mitaala ya ufundi kwa ngazi ya Stashahada na Cheti kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Ufundi vya Missungwi na Mabughai ilifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliratibu utoaji mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Stashahada ya juu na Shahada katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 973 wakiwemo wanawake 585 na wanaume 388 kwa mafunzo ya Stashahada ya Juu na Shahada ya Kwanza. Aidha, jumla ya wanachuo 728 wa Stashahada ya Juu walihitimu katika kipindi hicho, wakiwemo wanawake 406 na wanaume 322. Kuanzia mwaka 2009/2010, udahili wa stashahada ya juu ulisitishwa na badala yake ukaanzishwa udahili wa ngazi ya shahada. Wizara pia iliboresha mazingira ya kusomea na kujifunzia katika Chuo cha Tengeru, kwa kujenga majengo mawili ya mihadhara na kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Vyama Halali Visivyo vya Kiserikali: Katika kuyawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* kutambulika kisheria, Wizara yangu ilisajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 4,548 chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya Mwaka 2002. Kati ya hayo, mashirika 3,785 yamepatiwa Vyeti vya Usajili na mashirika 763 Vyeti vya Ukubalifu. Usajili wa Mashirika haya unayawezesha kuendesha shughuli zao kihalali katika ngazi zote kwa mgawanyo ufuatao: Wilaya (797), Mkoa (485), Taifa (3,090) na Kimataifa (176). Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la *NGOs,* iliratibu uandaaji wa Kanuni za Maadili ya *NGOs*, ambazo zilitafsiriwa katika Lugha ya Kiswahili na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua umuhimu wa uwazi, uwajibikaji na ubadilishanaji wa habari miongoni mwa wadau wa Sekta ya *NGOs*. Kwa kuzingatia hilo, Wizara ilianzisha Benki ya Takwimu na Taarifa za *NGOs* na Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*hppt://www.tnnc.go.tz*). Tovuti hiyo iliyozinduliwa rasmi mwezi Julai, 2009, imewezesha wadau 91 kutoa mrejesho kwa Wizara kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *NGOs.* Aidha, Wizara iliendelea kuingiza na kuhifadhi taarifa za *NGOs* kwenye Benki na Tovuti hiyo ili kurahisisha uratibu na

ufuatiliaji wa shughuli za *NGOs* nchini na kusogeza baadhi ya huduma za usajili na uratibu wa Mashirika haya karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeimarisha huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kwa kuajiri wataalam na kununua vitendea kazi. Vilevile, Wizara imekiimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma, kwa kukipatia vitendea kazi muhimu. Watumishi wawili wamepata mafunzo ya mawasiliano ya uandaaji wa vipindi vya redio na televisheni, ambayo yamewawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara yangu imewezesha watumishi kupata mafunzo mbalimbali ili kuwaongezea uelewa na kuwapa stadi na maarifa ya kutekeleza majukumu yao. Jumla ya watumishi 897 walipata mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kipindi cha 2005/2006 – 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa Wananchi kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, vyuo hivi vimepanda jumla ya miti 44,502 katika maeneo yanayovizunguka ili iwe mfano na hamasa kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa Wananchi wanaojiunga na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuongeza uelewa wao katika masuala ya UKIMWI. Jumla ya Wananchi 145,037 wakiwemo wanawake 67,667 na wanaume 77,370, wamepata mafunzo hayo. Aidha, elimu ya masuala ya UKIMWI mahali pa kazi imetolewa kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali ya sekta ya Maendeleo ya Jamii katika maeneo ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto, *NGOs,* ushiriki wa jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi imeendelea kuimarika. Kuimarika kwa hali hii, kumetokana na Sera nzuri za CCM katika kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi na jitihada za makusudi zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Taifa, Mkoa na Halmashauri ni ya kuridhisha. Hata hivyo, hali hairidhishi katika ngazi ya Kata na Kijiji, ambako wataalam hao wanahitajika zaidi kuwafikia Wananchi na kuwahamasisha ili kujiletea maendeleo yao.

Sera ya Maendeleo ya Jamii imeelekeza awepo angalau mtaalam mmoja wa Maendeleo ya Jamii kwenye kila Kata. Hivi sasa ni asilimia 56 tu ya Kata zote 2,637 zina Wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Hii ina maana kuna upungufu wa wataalam 1,213, sawa na asilimia 44 ya mahitaji. Changamoto inayokabili eneo hili ni kuwa na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa kutosha kujaza nafasi zilizo wazi katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usawa wa jinsia nchini imeendelea kuimarika. Hii ni kutokana na Wananchi wengi kuelimika na Serikali kuweka mkazo katika kuleta usawa wa jinsia, pamoja na kuzingatia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda inayohusu haki za wanawake na watoto ambayo nchi imeridhia. Kutokana na utekelezaji

wa Mikataba hiyo, hivi sasa uwiano wa wasichana na wavulana katika udahili kwenye Shule za Msingi na Sekondari umefikia asilimia hamsini kwa hamsini. Uwakilishi wa wanawake Bungeni umefikia asilimia 36. Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ameendelea kuwateua wanawake wengi kushika nyadhifa za uongozi katika ngazi za kisiasa na kiutendaji. Kwa niaba ya Wizara yangu, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuenzi usawa wa jinsia ambao ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, changamoto inayokabili eneo hili ni kuendelea kuwepo mila, desturi na imani potofu, zinazoathiri haki za wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hali ya watoto nchini inaendelea kuimarika. Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009, umewezesha upatikanaji wa haki za mtoto ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kushirikishwa, kulindwa na kutobaguliwa. Juhudi mbalimbali za Serikali na wadau katika maeneo ya elimu, afya, maji na kilimo, zimechangia kuboresha hali ya watoto nchini. Hata hivyo, changamoto bado ni kubwa. Baadhi ya watoto bado wanaishi katika mazingira hatarishi kama vile mitaani, katika ajira mbaya na kutumikishwa katika biashara haramu. Aidha, ukatili kwa watoto majumbani na shuleni bado unaendelea. Juhudi za makusudi, zinahitajika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu na jukumu la kutunza watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kuongezeka na kushiriki katika maendeleo ya jamii. Hii imetokana na nia ya dhati ya Serikali ya kuweka mazingira wezeshi kwa *NGOs* hapa nchini. Nia hiyo imedhihirishwa na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *NGOs* ya Mwaka 2001, Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya Mwaka 2002 na Kanuni za Maadili za *NGOs* za Mwaka 2008. Hata hivyo, Mashirika haya bado yanakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo na uendelevu wa huduma wanazozitoa kwa jamii na Taifa kutokana na utegemezi mkubwa kwa wafadhili wa nje na uwezo mdogo wa kushawishi na kupata rasilimali za ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Wananchi katika shughuli za maendeleo umeendelea kuimarika. Kumekuwa na ushiriki mkubwa wa Wananchi katika kubuni, kupanga na kutekeleza Miradi ya Maendeleo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* Programu ya Miradi ya Kilimo ngazi ya Wilaya *(DADPs),* Programu za Maji na Mazingira na Programu nyingine za Maendeleo kama vile ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, maabara na maktaba katika Sekondari za Kata. Ushiriki huu umetokana na matumizi ya mbinu shirikishi katika uandaaji na utekelezaji, ambazo zimewezeshwa na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata na Vijiji. Changamoto inayokabili eneo hili ni upungufu wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata na Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi imeendelea kuimarika kulingana na rasilimali zinazotolewa na Serikali. Katika kipindi cha miaka mitano, idadi ya Wananchi waliopata mafunzo katika vyuo hivi imeongezeka kutoka washiriki 25,486 mwaka 2005/2006 hadi 31,877 mwaka 2010/2011. Hata hivyo, hali ya majengo na miundombinu katika vyuo bado ni chakavu kutokana na ukosefu wa

matengenezo ya mara kwa mara. Changamoto nyingine ni uhaba wa vyombo vya usafiri, upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali, nyumba za watumishi, madarasa, karakana, mabweni, vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, ulifanyika kwa mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano mzuri tulioupata kutoka kwa wadau wetu. Aidha, katika mwaka 2011/2012, maeneo matano yafuatayo yamepewa kipaumbele:

(i) Kusimamia na kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na mafunzo ya maarifa, ujuzi na stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) Kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili washiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo hayo;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusu ustawi, haki na maendeleo ya wanawake, jinsia na watoto;

(iv) Kuimarisha usajili, uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi mbalimbali; na

(v) Kuwawezesha Wanawake kupata mafunzo kwa lengo la kujikwamua kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuunda vikundi vya Akiba na Mikopo sambamba na Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa ili waweze kukopeshwa kwa urahisi na Benki na Asasi nyingine za fedha.

Maeneo haya kwa pamoja yametengewa asilimia 78.3 ya Bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Jamii: Wizara yangu katika mwaka 2010/2011, iliwapatia Wananchi 31,877 mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali za maisha wakiwemo wanaume 16,468 na wanawake 15,409. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kudahili na kutoa mafunzo kwa Wananchi 34,750 ndani na nje ya vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu iliendelea na ukarabati katika vyuo tisa vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vitatu vya Maendeleo ya Jamii. Ukarabati huu ulianza mwaka 2008/2009, lakini haukukamilika kutokana na fedha zilizotengwa kwa kazi hii kutopatikana zote. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kufanya ukarabati na ununuzi wa samani katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Sofi – Ulanga Morogoro na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mabughai – Lushoto Tanga. Aidha, vyanzo vya maji vya Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mlale – Songea Vijijini Ruvuma vitajengewa uzio ili kuvihifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu ilidahili wanachuo 2,672, wakiwemo wanawake 1,864 na wanaume 808 katika vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii. Wanachuo waliodahiliwa katika ngazi ya Astashahada walikuwa 1,919, Stashahada 524 na Shahada 229. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu inatarajia kudahili wanachuo 2,700 katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliandaa programu ya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia sahihi kwa jamii kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Lengo ni kuwapunguzia mzigo wa kazi Wananchi hususan wanawake, kuongeza tija, ubora wa kazi na kuleta ufanisi na kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Programu hii kwa kuanzia ilivitumia vyuo vilivyopo katika mikoa sita inayozalisha chakula kwa wingi nchini, ambayo ni Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Morogoro na Kigoma ili kuleta msukumo katika utekelezaji wa agizo la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu hii, Wizara yangu ilinunua matrekta 18 ya kusukumwa kwa mkono (*Power Tillers*) na kuyasambaza katika vyuo vilivyopo katika mikoa hiyo. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu ilitoa mafunzo ya kufanya matengenezo madogo kwa matrekta hayo kwa wakufunzi 18 kutoka katika vyuo 14 vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vinne vya Maendeleo ya Jamii.

Mafunzo hayo yamewajengea uwezo wa kuyatumia kwa ufasaha na kupunguza uharibifu wa mara kwa mara. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia vyuo hivi, itaanza kutoa huduma na kuwajengea uwezo wa matengenezo madogo ya matrekta ya kusukumwa kwa mkono katika Halmashauri zenye matrekta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya teknolojia sahihi na kuzisambaza kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Jumla ya wakufunzi 236 wa vyuo 53 vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii, walipata mafunzo hayo. Sambamba na mafunzo hayo, aina saba za teknolojia sahihi zilinunuliwa na kusambazwa katika vyuo hivyo, ambazo ni wanyama kazi 28, majembe ya plau 14, mashine za kutengeneza matofali 19, mashine za kutotolea vifaranga 17, meko sanifu - 20, mashine za kuhifadhia mboga na matunda 20 na mikokoteni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tathmini iliyofanywa na Wizara yangu imeonesha kuwa, programu ya usambazaji wa teknolojia sahihi imeviwezesha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, kutumia teknolojia hizo kutolea mafunzo kwa Wananchi kwa urahisi zaidi na kwa vitendo. Aidha, kuwepo kwa teknolojia hizo vyuoni, kumewapa fursa Wananchi kuziona, kuzielewa matumizi yake na hivyo kuhamasika zaidi kuzinunua na kuzitumia, kuwapunguzia mzigo wa kazi na kuwaongezea tija. Kwa mfano, baadhi ya Wananchi wanaozunguka Vyuo vya Ifakara na Kihinga, wameomba uongozi wa vyuo hivyo, uwasaidie kupata matrekta ya kusukumwa kwa mkono. Vyuo hivi pia kwa kutumia teknolojia hizo, vimeongeza ufanisi katika suala la uzalishaji mali na kujiongezea kipato katika miradi ya kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia sahihi kwa Wananchi kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi. Teknolojia zitakazosambazwa ni pamoja na matrekta ya kusukumwa kwa mikono, mikokoteni, meko sanifu, mashine za kutotolea vifaranga, mashine za kufyatulia matofali, mashine za kuhifadhia mboga na matunda na wanyama kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mkutano huu uliwapa fursa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii na wadau wake, kutathmini mwenendo wake na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii nchini. Jumla ya washiriki 350 kutoka katika Halmashauri zote nchini, Sekretarieti za Mikoa, Sekta nyingine na Zanzibar walihudhuria. Katika mkutano huo, Wajumbe walikubaliana na kupitisha maazimio mbalimbali yaliyolenga kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao. Wizara yangu katika mwaka 2011/2012, itaandaa mkutano huu unaolenga kuimarisha sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Jinsia: Katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri, iliendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuwawezesha wanawake kiuchumi. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu kupitia Mfuko huo, ilitoa jumla ya Sh. 128,000,000 kwa Halmashauri 16 zilizokamilisha marejesho ya mikopo kwa ajili ya kuwakopesha wanawake wajasiriamali. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, imewezesha mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake 350. Baada ya mafunzo hayo, wanawake wajasiriamali walishiriki katika Maonesho ya 35 ya Biashara ya Kimataifa Jijini Dar es Salaam. Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuratibu na kusimamia ushiriki wa wanawake wajasiriamali katika Maonesho ya 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania, imeendelea kutoa huduma za kibenki kwa wateja wake hususan wanawake. Kwa mwaka 2010/2011, jumla ya Shilingi bilioni 9.7 zilikopeshwa kwa wateja mbalimbali ikiwa ni pamoja na vikundi vya wanawake wajasiriamali. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Benki ya Wanawake Tanzania itaendelea kuhamasisha Wananchi kufungua akaunti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2010/2011, iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda, inayohusu Maendeleo ya Wanawake na Jinsia. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara yangu iliratibu Mkutano wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, uliofanyika Arusha, tarehe 16 – 18 Machi, 2011. Mkutano huo ulipitisha nyaraka za uanzishwaji wa Kituo cha Kanda cha

Utafiti na Utunzaji Kumbukumbu za Wanawake, ambacho kimeanzishwa Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Aidha, kila nchi itaanzisha kituo chake ambapo kwa Tanzania kipo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ili kuendeleza haki na usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki katika Mikutano mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda, inayohusu Maendeleo ya Wanawake na Jinsia. Mikutano hiyo ilijadili na kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Maendeleo ya Wanawake na Jinsia katika nchi wanachama. Aidha, mikutano hiyo ilisisitiza umuhimu wa kila nchi mwanachama kuwezesha usawa wa jinsia. Hii ni pamoja na kudurusu Sera na Sheria zisizozingatia usawa wa kijinsia na kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi, kiutendaji, kisiasa na uwezeshaji wa wanawake na wanaume kiuchumi. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kushiriki na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ili kuendeleza haki na usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi na nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa. Maadhimisho haya hutoa fursa kwa wanawake, jamii na wadau mbalimbali, kutafakari mafanikio na changamoto zinazoikabili jamii hususan wanawake na kuzitafutia ufumbuzi. Maadhimisho ya mwaka 2011, yalifanyika katika ngazi ya mikoa na kaulimbiu ilikuwa; *Fursa sawa katika Elimu, Mafunzo, Sayansi na Teknolojia; Njia ya Ajira Bora kwa Wanawake.* Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika elimu ili kuhakikisha kuwa, wanawake pia wanapata ajira endelevu. Wizara yangu itaendelea kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha masuala ya Jinsia yanazingatiwa na kuingizwa katika mipango, programu na bajeti ya sekta mbalimbali, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2010/2011, iliandaa Kitini cha Wabunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali yanayozingatia masuala ya Usawa kijinsia. Aidha, Wizara ilitoa elimu ya jinsia kwa watumishi 42. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo hayo kwa Watendaji wa Dawati la Jinsia na Kamati za Kisekta za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliandaa mafunzo ya kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wasimamizi 80 wa sheria na Kamati za Kuzuia Ukatili wa Kijinsia katika Wilaya za Tarime, Rorya na Serengeti Mkoa wa Mara. Jumla ya washiriki 36 kutoka katika Wilaya hizo, walipata mafunzo hayo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo hayo kwa wasimamizi wa sheria na Kamati za Wilaya za Mikoa ya Shinyanga na Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/2011, Wizara yangu ilisambaza kwa Wananchi na Taasisi mbalimbali, Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 na kijarida cha Kiswahili chenye maelezo kuhusu Sheria hii. Wizara kwa kushirikiana na

wadau wa masuala ya mtoto, iliandaa rasimu ya tafsiri ya Sheria hiyo kwa Lugha ya Kiswahili na kuiwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuandaa mafunzo ya wakufunzi katika Kanda tano. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau, itachapisha Sheria ya Mtoto kwa Lugha ya Kiswahili na kuisambaza kwa jamii ili waielewe na kuizingatia katika utoaji wa haki za mtoto. Aidha, Wizara itaandaa kanuni za Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika mwaka 2010/2011, iliendelea kulitafutia ufumbuzi tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Katika kutekeleza azma hiyo, iliratibu mkutano wa wadau uliojadili namna ya kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi mitaani. Mkutano huo uliwahusisha Waheshimiwa Wabunge, Wastahiki Mameya wa Miji na Majiji ya Mwanza, Dodoma, Tanga na Dar es Salaam. Mkutano ulibuni mikakati ya kudhibiti tatizo na kuunda kikundi kazi kilichojumuisha taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuzihamasisha Halmashauri zitekeleze mipango ya kudhibiti watoto wanaoishi mitaani. Aidha, Wizara itakamilisha Mkakati wa Jamii wa Kudhibiti Tatizo la Watoto Wanaoishi Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ni muhimu kwa kuandaa Taifa madhubuti la kesho. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu iliandaa vikao vya maamuzi vya kamati elekezi na kamati tendaji ya masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Kamati zilipitia shughuli mbalimbali zilizoandaliwa ikiwemo miongozo ya utoaji wa huduma jumuishi na mpango maalum wa kuboresha maisha ya watoto wadogo. Katika kipindi cha 2011/2012, Wizara yangu itakamilisha na kusambaza Sera Jumui ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa jamii na kuandaa mpango wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba yote ya Haki na Ustawi wa Mtoto. Aidha, iliratibu uandaaji wa taarifa ya 3, 4 na 5 ya nchi ya utekelezaji na kuunda kikundi kazi kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara itawasilisha na kutetea taarifa hizo katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa, mwezi Januari, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, yaliyofanyika Kimkoa na Kiwilaya. Kaulimbiu yake ilikuwa ni "*Tuungane Pamoja Kuchukua Hatua za Haraka kushughulikia Tatizo la Watoto Wanaoishi Mitaani*." Vilevile, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani, yaliyofanyika Kimkoa na Kiwilaya. Kaulimbiu ilikuwa ni *"Kupambana na Umaskini katika Familia: Ni Jukumu la kila mmoja."* Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuratibu maadhimisho ya siku hizo ili kuhamasisha jamii kuhusu haki na ustawi wa mtoto na maendeleo ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 inatekelezwa kikamilifu, Wizara yangu katika kipindi cha 2010/2011, iliandaa rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wake. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itakamilisha mkakati huo na kuusambaza kwa wadau kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya usambazaji wa Kitini cha Jamii cha Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Mafunzo hayo yalilenga kutoa mwongozo wa jinsi ya kutumia kitini hicho. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kuongeza fursa ya ushiriki wa Wananchi katika maendeleo kwa kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 793. Kati ya hayo, 749 yalipatiwa Cheti cha Usajili na 44 yalipatiwa Cheti cha Ukubalifu. Mchanganuo wa idadi ya Mashirika haya katika ngazi mbalimbali ni kama ifuatavyo: Wilaya (88), Mkoa (48), Taifa (639) na Kimataifa (18). Ongezeko hili ni sawa na asilimia 17 ya Mashirika 4,548 yaliyosajiliwa chini ya Sheria ya *NGOs,* Na. 24 ya Mwaka 2002. Usajili huu umeyawezesha mashirika haya kuingia Mikataba mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao, kumiliki mali na kuaminika zaidi pale yanapotoa huduma kwa jamii; hivyo, kuyawezesha kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, Wizara yangu iliiwezesha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* kufanya vikao viwili katika Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro. Bodi hiyo pia ilikutana na wadau wa Sekta ya *NGOs* 286 katika mikoa hiyo, ambapo walibadilishana uzoefu wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *NGOs*. Utekelezaji wa maazimio na maamuzi yanayotokana na vikao na mikutano hiyo umeimarisha mahusiano miongoni mwa wadau wa sekta hii. Mfano, Halmashauri ya Mji wa Korogwe, imeanzisha ubia na *NGOs* katika kutekeleza shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchochea uwazi, uwajibikaji na ubadilishanaji wa taarifa na maendeleo ya *NGOs* nchini, jumla ya taarifa za *NGOs* 576 ziliingizwa kwenye Benki ya Taifa ya Takwimu katika mwaka 2010/2011. Taarifa hizi ziliingizwa pia kwenye Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Jumla ya wadau 4,286 kutoka Serikalini, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Fedha, Taasisi za Utafiti na Wananchi, walipatiwa taarifa mbalimbali kupitia Ofisi ya Msajili na Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs.* Aidha, jumla ya wadau 91 waliitumia tovuti hii kutoa mrejesho kwa Wizara kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kupanua wigo wa ushiriki wa Wananchi katika maendeleo kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuendelea kusajili Mashirika hayo. Aidha, Wizara itaendelea kuiwezesha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kutekeleza majukumu yake ya Uratibu ili kuimarisha uratibu na taswira ya Sekta ya *NGOs*. Vilevile, itaendelea kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa mbalimbali za Sekta ya *NGOs* kupitia Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs,* Ofisi ya Msajili, Mikutano na makongamano yanayoandaliwa na kushirikisha Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Mipango: Jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ni la kudumu. Lengo ni kuhakikisha yanakuwepo matumizi mazuri ya fedha na miradi husika kukamilika kwa ubora na katika muda uliopangwa. Katika mwaka 2010/2011, Wizara iliwezesha watumishi 22 wakiwemo Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Maafisa wa Bajeti kupata mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini za Sera. Aidha, Wizara ilifuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi yake ya Maendeleo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Tanga, Morogoro, Arusha na Ruvuma. Utekelezaji uliendelea taratibu kutokana na fedha kidogo zilizopatikana. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia, kufuatilia na kutathmini miradi itakayopatiwa fedha za maendeleo na kutekelezwa katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa awamu ya tatu ya Mradi wa Kituo cha Habari kwa Wanawake, ulikamilika mwezi Aprili, 2011 kwa kufungua na kuendesha vituo vidogo vinne. Vituo hivyo vipo katika Vyuo vya Rungemba (Iringa), Monduli (Arusha), Mamtukuna (Kilimanjaro) na Bigwa (Morogoro). Hivi sasa Mradi huo uliokuwa unapata msaada kutoka Serikali ya Italia, ufadhili wake umekwisha na Serikali itaendelea kuuendesha kupitia bajeti yake. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Kituo kitaendelea kukusanya na kueneza taarifa zinazohusu wanawake, watoto na jamii katika ngazi ya Taifa na Kimataifa. Aidha, Kituo kitaanzisha vituo vidogo vinne katika Vyuo vya Mwanva (Shinyanga), Singida (Singida), Mabughai (Tanga) na Uyole (Mbeya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuijengea uwezo Wizara kuhusu masuala ya Sera na Mipango kwa mwaka 2010/2011, jumla ya watumishi 39 wakiwemo Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Vyuo na Maafisa Bajeti, walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya uandaaji wa Mpango Mkakati. Mafunzo hayo yaliwawezesha kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano, kuanzia Julai, 2011 hadi Juni, 2016. Mipango yote ya Wizara ya kila mwaka itakuwa inaandaliwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati huo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliboresha tovuti na Benki ya Takwimu ya shughuli zote za Wizara kwa matumizi ya wadau wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii ili kupata taarifa mbalimbali za Sekta hiyo. Maboresho hayo yamewezesha upatikanaji wa taarifa za mafunzo na matokeo ya mitihani katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kupitia tovuti hii. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuimarisha miundombinu ya kutunza na kuhuisha taarifa mbalimbali za Wizara ili kuboresha Benki ya takwimu na mifumo ya taarifa ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuiwezesha Wizara kuwa na watumishi waadilifu na wenye ari, Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya haki na usawa. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ilitoa elimu kwa watumishi 120 kuhusu Sheria Na. 11 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2004. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia utendaji kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya watumishi 70 waliwezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi, kati na ya muda mrefu katika nyanja mbalimbali. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi wake kupata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwapatia motisha wafanyakazi, Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011, iliwapandisha vyeo watumishi 23, iliwathibitisha kazini watumishi 208 na kuwaingiza kwenye masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni watumishi 131. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wake kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Wizara yangu iliendelea na ukarabati wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara kwa kuweka transfoma, lifti, viyoyozi na mifumo ya mawasiliano. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea na ukarabati wa jengo hilo pamoja na kuweka mazingira mazuri ya ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa, utoaji huduma kwa Wananchi kwa kiwango cha juu na kwa wakati ni suala muhimu katika kufanikisha maendeleo ya Taifa. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imedurusu Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuondoa upungufu uliojitokeza. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara itachapisha na kusambaza Mkataba huo kwa wadau kwa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara iliendesha Kikao cha Baraza la Wafanyakazi mwezi Juni, 2011 kwa lengo la kuwashirikisha wafanyakazi katika masuala muhimu yanayowahusu. Wizara katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, itaendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi na kuratibu kikao cha ushirikiano na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kutoa elimu ya UKIMWI na kuhamasisha watumishi kuhusu umuhimu wa kupima afya zao. Aidha, Wizara iliwawezesha watumishi walioathirika na Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI, kwa kuwapatia viini lishe, madawa na chakula. Huduma hizi zimewawezesha watumishi hao kuboresha afya zao, kuishi kwa matumaini na kuongeza tija katika utendaji wao wa kazi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara itaendelea kutoa elimu na huduma hizo kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kwa Wizara yangu, ulifanyika kwa mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano tulioupata kutoka kwa wadau wetu. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau hao katika kutekeleza majukumu yake ya kuleta usawa wa jinsia, kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto, kuongeza ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo na

kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao binafsi na ya Taifa kwa ujumla. Kwa kufanya hivyo, Wizara yangu itachangia kupunguza umaskini na kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumalizia hotuba yangu, kwa kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Wizara, nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb.); Katibu Mkuu, Bibi Kijakazi Rajabu Mtengwa; Naibu Katibu Mkuu, Bibi Anna Tayari Maembe; Wakuu wa Idara; Wakuu wa Vitengo; Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, Bibi Margareth Chacha; Wakuu wa Vyuo pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Vyuo. Wote kwa pamoja, wamenipa ushirikiano ambao umenisaidia kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Michango yao ya mawazo na utendaji, imeniwezesha kufanya kazi yangu kwa urahisi na kwa mafanikio makubwa. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nitasahau kuwashukuru wadau wetu wa maendeleo. Peke yetu kama Wizara, tusingefikia mafanikio niliyoyataja. Kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Asasi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF),* Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP),* Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA),* Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania *(TAMWA),* Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania *(FAWETA),* Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania *(MEWATA),* Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake *(WLAC), REPOA,* Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii pia kuzishukuru kwa namna ya pekee, Serikali za Nchi Rafiki, kwa kuendelea kutusaidia kupitia Mashirika yao ya Maendeleo. Nchi hizo ni pamoja na Canada *(CIDA),* Ireland, Sweden (Sida), Denmark *(DANIDA),* Korea ya Kusini *(KOICA)* na Japan *(JICA)* na Marekani *(USAID).* Aidha, ninayashukuru Mashirika ya Kimataifa ambayo ni *UNICEF, UNDP, UNFPA, UNESCO, ILO* na *UN Women*. Vilevile, ninapenda kuwashukuru Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*, kwa kushirikiana nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2011/2012, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Shilingi 16,256,015,000; kati ya hizo, Shilingi 11,402,695,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 7,089,058,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 4,313,637,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges).* Aidha, Shilingi 4,853,320,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo Shilingi 3,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 1,853,320,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yako nzuri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa ninaomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Jenista Mhagama, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Kabla ya kuwasilisha, ninaomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu, kwa kunilinda, kwa kunitetea na kwa kuniwezesha kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ninapenda kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Nkenge, ambao walinipigia kura nyingi sana na hatimaye nikawa mshindi wa kwanza katika Bunge hili. Kwa kweli Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Pia ninapenda nimshukuru sana mume wangu mpenzi, Julius Mshama, kwa namna ya pekee kwa jinsi alivyoniwezesha na kwa anavyoendelea kunisaidia katika kazi hii niliyonayo pamoja na watoto wangu kwa maombi yao; ninaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, ninaomba nitumie fursa hii, kutoa Salamu za pole kwa Mheshimiwa Spika, kwa kufiwa na mama yake mzazi, mwanzoni mwa mwezi wa tano. Vilevile Kamati inatoa salamu za pole kwa Naibu Spika, kwa kufiwa na bibi yake mlezi, tarehe 18 Julai, 2011. Tunawapa pole na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu, awatie nguvu na ujasiri. Pia tunawapa pole Wabunge wengine na Watanzania wote, waliowapoteza ndugu zao, jamaa na marafiki katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ilifanya kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tarehe 31 Mei na tarehe 1 Juni, mwaka 2011 wakati wa Vikao vya Kamati Dar es salaam. Katika vikao hivyo, Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, alitoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 0/2011. Aidha,Kamati ilielezwa kwa kina kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2011/2012, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha, pamoja na kazi zilizopangwa kufanywa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

- Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilidahili na kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za maisha kwa Wananchi 31,877 wakiwemo wanaume 16,468 na wanawake 15,409. Aidha, Wizara ilidahili wanachuo 2,672 wakiwemo wanawake 1,864 na wanaume 808 katika vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii.

- Ukarabati wa majengo na miundombinu ya vyuo tisa vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vitatu vya Maendeleo ya Jamii, ambavyo ni Mabughai, Uyole, Mlale, Same, Nandembo, Kiwanda, Kilosa, Ifakara, Nzega, Bigwa, Gera na Malya.

- Katika kupunguza mzigo wa kazi hasa kwa wanawake na katika utekelezaji wa agizo la Kilimo Kwanza, Wizara iliandaa programu ya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia rahisi kupitia vyuo 18, ambapo vyuo 14 ni vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vinne ni vya Maendeleo ya Jamii, vilivyopo katika mikoa inayozalisha chakula kwa wingi, ambayo ni Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa na Kigoma. Teknolojia hizo ni pamoja na wanyama kazi, majembe ya kukokotwa na ng'ombe, mashine za kutengeneza matofali, mashine za kutotolea vifaranga, meko sanifu, mashine za kuhifadhia mboga na matunda na mikokoteni.

- Kufanikiwa kwa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mkutano huu uliwapa fursa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii na wadau wake, kutathmini na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo. Washiriki 350 kutoka Halmashauri zote nchini, Sekretarieti za Mikoa, Zanzibar na Sekta nyingine walihudhuria.

- Wizara imeendelea kutuma fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* kwenye Halmashauri mbalimbali. Mwaka 2010/2011, Halmashauri 16 zimepatiwa shilingi 128,000,000.00 hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2011.

- Benki ya Wanawake Tanzania, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2011 imetoa mikopo kwa wanawake na wanaume yenye thamani ya shilingi bilioni 8.4 ambapo wanawake ni 3,862 sawa na asilimia 81 na wanaume 855, sawa na asilimia 19. Vilevile benki imetoa mafunzo kwa wanawake wajasiriamali 5,668.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, imeomba shilingi bilioni 16.2, kiasi hiki ni pungufu ukilinganisha na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, ambayo ilikuwa shilingi bilioni 19.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huu kwa kiasi kikubwa utapunguza utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara ambavyo ni:-

- Kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili washiriki katika shughuli zote za utekelezaji wa Miradi na Mipango mbalimbali.

- Kusimamia na kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi.

- Kuimarisha usajili, uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali katika ngazi mbalimbali; na

- Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa inayohusu ustawi, haki na maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaunga mkono maombi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Hata hivyo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kupitia Hazina, kutoa fedha za Miradi katika muda mwafaka ili kurahisisha utekelezaji wa Miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inatamka umri wa kufunga ndoa kwa kijana wa kiume ni miaka 18 na kwa kijana wa kike ni miaka 15. Sheria hii inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, ambayo inamtaja mtoto kuwa ni yule aliye chini ya miaka 18; hivyo, kufanya Sheria ya Ndoa kuruhusu ndoa kwa watoto. Sheria hii imefanya kazi kwa muda wa miaka 40 na Kamati inaona kuwa, wakati mwafaka wa kuifanyia marekebisho ni sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya mila na mazingira ya kijamii ya Watanzania bado zina utamaduni wa kufungisha ndoa kwa watoto wenye umri wa miaka 18, Kamati inashauri Serikali kutenga fungu maalum kwa ajili ya kuielimisha jamii kuhusu athari za ndoa za utotoni kama sehemu ya mchakato wa marekebisho ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa, jamii ikielimishwa kuhusu athari hizo, kutakuwa na mwamko mkubwa wa kukataa ndoa hizi kuanzia ngazi ya jamii; hivyo, wasichana wengi hasa walio maeneo yenye mila hizo na vijijini, watapata fursa ya kupata elimu na mwisho wa siku Taifa litakuwa na jamii iliyoelimika, yenye nguvu kazi na isiyo na watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu. Tafiti zinaonesha asilimia 45 ya Watanzania ni watoto chini ya miaka 15; hivyo, nusu yao ni wasichana na kama wasichana hao wataolewa katika umri mdogo, hakuna shaka tatizo la vifo vya akina mama na watoto halitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya teknolojia na jinsia ni dhana mpya, lakini ya msingi kabisa kwa kuleta maendeleo, ingawa uhusiano na uwiano wa dhana hiyo unatakiwa kulinganishwa kwa wanaume na wanawake. Tumeshuhudia kwa kipindi kirefu sasa, watoto wa kike wamepoteza hamu ya masomo ya sayansi na kukosesha kundi la wanawake kupata upevu wa kuchangia maendeleo; mfano, mwaka 1994 *study* ya Bwana

Sakamoto, ilionesha watoto wa kike na wakiume, uwiano wao wakati wa matumizi ya kompyuta ni 1:4. Hii inaonesha matumizi ya teknolojia kwa wanawake na wanaume hayaridhishi na hivyo kuona umuhimu sasa wa kuviendeleza vyuo vyetu ili kuhakikisha vinatoa mafunzo kwa vijana wetu na hasa vijana wa kike, ukizingatia kuwa nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali, kwa kuzingatia umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ambapo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, vyuo saba vitafanyiwa upanuzi na ukarabati. Vyuo hivyo ni pamoja na Tengeru, Rungemba, Misungwi, Monduli, Buhare, Mabughai na Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilianza kutoa maarifa na stadi kwa Wananchi tangu vilipoanzishwa mwaka 1975. Wakati huo, vyuo vilipaswa kutoa maarifa na stadi kwa watu wazima waliohitimu katika hatua ya tatu na nne ya elimu ya watu wazima ili waweze kujiendeleza na kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi chote hiki, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, vinaendesha shughuli zake kwa kutumia rasilimali fedha kutoka Serikalini, Wafadhili mbalimbali kama vile Shirika la Maendeleo la Sweden *SIDA,* lililofadhili vyuo tangu 1975 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990. Hata hivyo, tangu ufadhili wa *SIDA* ulipositishwa, vyuo hivi vimekuwa vikipata fedha kidogo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake na kusababisha kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vyuo hivi vinatoa mafunzo ya elimu ya stadi za maisha, pamoja na mafunzo ya Elimu ya Ufundi Stadi kama yale yanayotolewa na *VETA*. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Mei, 2011, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilikuwa vimepata asilimia 48.7 ya fedha za matumizi ya kawaida na asilimia 13.6 ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa Elimu ya Ufundi kuwa ndiyo msaada mkubwa kwa vijana, hasa wimbi kubwa la wahitimu wa elimu ya sekondari; na kwa kuwa athari kubwa ya kupungua kwa bajeti ya Wizara hii ipo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; Kamati inashauri yafuatayo:-

- Kwa kuwa, Mfuko wa Elimu ya Juu umepata kodi ya kuimarisha utoaji wa stadi nchini *(Skills Development Levy)* ya asilimia nne; Kamati inashauri asilimia moja ya kodi ya kuimarisha utoaji wa stadi nchini *(Skills Development Levy),* itengwe kwa ajili ya kusaidia vyuo hivi.

- Serikali iongeze ruzuku inayopelekwa katika Vyuo hivi ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na iboreshe mazingira na miundombinu katika Vyuo vilivyopo pembezoni ili viweze kuwavutia walimu wanaopangwa kufundisha na hatimaye viweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuwajengea Wananchi uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Wizara ni kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Serikali *(NGOs)*na kuyawezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Katika

miaka ya sasa, michango ya asasi zisizo za Kiserikali imeonesha kukua na kuchangia maendeleo ya nchi yetu kupitia Sekta mbalimbali kama Afya, Elimu, Kilimo, Mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa bado hatujapata picha halisi ya namna gani na kwa kiasi gani mashirika haya yamesaidia hasa katika kupunguza umaskini wa watoto na wanawake. Hivyo, Kamati inashauri katika kila Sekta, Wizara itafute na kubainisha michango ya Sekta hizi ili kuondoa dhana ya kutoeleweka kwa mchango wa asasi zisizo za Serikali *(NGOs)*. Aidha, kwa kutambua michango ya taasisi hizi utasaidia kuelewa kazi za mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Halmashauri zihimizwe katika kuchangia asilimia kumi ya mapato yake kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kukwamua maisha ya wanawake hususan wanaoishi vijijini. Aidha, Halmashauri zizingatie kurudisha mikopo kwa muda mwafaka na pia vikundi vya wanawake vihamasishwe kurudisha mikopo mapema ili kuwezesha Halmashauri kuchukua mkopo tena Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Benki ya Wanawake Tanzania, kwa kuandaa rasimu ya mpango wa biashara kuanzia Mwaka 2010 hadi 2013, ambao unalenga kufungua matawi mengine mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kuwa, mambo mengi mazuri yapo mijini na inadhihirisha dhana ya kuwa mwenye nacho huongezewa. Zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanaishi vijijini na nusu yao ni wanawake; hivyo, kuna umuhimu wa Benki hii kusogeza huduma zake vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu benki hii sasa ijihusishe na *SACCOS* za wanawake pamoja na *Village Community Bank (VICOBA),* ili huduma ziwafikie wanawake vijijini na iangalie upya masharti ya dhamana, kwani bado dhamana za benki hii si za kufikika na wanawake walio wengi. Aidha, Viongozi mbalimbali, Wanawake kwa Wanaume, wakiwemo Wabunge, wahamasishwe kununua hisa pamoja na kufungua akaunti katika Benki hii, vilevile benki itoe elimu kwa wanawake wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha za ndani zilizotengwa katika Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2011/2012 ni shilingi bilioni tatu, ambapo kati ya hizo; shilingi bilioni mbili zinatakiwa kupewa Benki ya Wanawake na hivyo, Wizara kubaki na shilingi bilioni moja tu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kamati inashauri kuwa, Serikali kupitia Hazina, itoe moja kwa moja kiasi cha shilingi bilioni mbili kupeleka Benki ya Wanawake na kuiachia Wizara fedha zote za maendeleo (shilingi bilioni tatu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitafanya hivyo, kwa Mwaka huu wa Fedha, Miradi mingi ya Maendeleo ya Wizara haitotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), umetaja watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira

hatarishi *(Orphans and Vulnerable Children),* kuwa moja ya makundi yaliyo katika hali tete. Aidha, lengo kuu la Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) ni kuhakikisha kwamba, watoto wote wanastawi na kuwa na maisha bora kutokana na kupatikana kwa haki zao za msingi, ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kulindwa na kushiriki katika mambo yanayowahusu bila ubaguzi wa hali yoyote. Kwa kuzingatia haya, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Halmashauri zote zifuate na kuzingatia sheria ndogo zinazohusu watoto ili kuwapatia haki zao za msingi kama ilivotajwa hapo juu ili kupunguza wimbi kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;

- Serikali iweke utaratibu wa uimarishaji wa mifumo ya kijamii ya kutunza watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi; na

- Serikali kuyachukulia hatua za kisheria Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayojinufaisha kupitia migongo ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono na kuzidi kusisitiza kaulimbiu ya Siku ya Mtoto Duniani (15 Juni, 2011), ifanyiwe kazi. Kaulimbiu ya mwaka huu ni "Tuungane kwa Pamoja Kuchukua Hatua za Haraka Kushughulikia Tatizo la Watoto Wanaoishi Mitaani."

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ya Wizara, tunaomba Wizara kuhakikisha wanawake na watoto wanapata haya yafuatayo kwa kipindi tulichonacho sasa:-

(i) Kuendelea kusimamia utekelezaji bora wa Sera za Serikali zinazowezesha akina mama na watoto kuondokana na umaskini.

(ii) Kuendelea kuandaa mipango ya kuwawezesha wanawake kushiriki katika shughuli za ujasiriamali na kilimo cha kisasa ili kukabiliana na tatizo la ajira nchini.

(iii) Kuendelea kuwawezesha akina mama kufikia teknolojia mwafaka za kuwasaidia katika utendaji kazi zao za kila siku na afya zao.

(iv) Kuendelea kuwawezesha wanawake kupitia Sheria na Sera mbalimbali za umiliki ardhi.

(v) Kuendelea kuwahimiza wanawake kubadilishana uzoefu na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuongozi.

(vi) Kuwawezesha wanawake kuendelea kubadilishana uzoefu katika mambo ya maendeleo eneo kwa eneo.

(vii) Kuendelea na mkakati wa kuelimisha jamii kupinga vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maoni haya, ninaomba Bunge lako litambue kuwa, yapo masuala mengine ya kimtambuka na yanasimamiwa na Wizara tofauti, lakini kwa kuwa yanagusa masuala ya jinsia, tunaomba Serikali kupitia Wizara yetu ipokee na kushughulikia maoni haya ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, ninaomba kukushukuru wewe binafsi, kwa namna unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara na kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, ninampongeza Naibu Spika na Spika mwenyewe na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge, kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba, Mbunge, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mbunge; Katibu Mkuu, Ndugu Kijakazi Mtengwa; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Anna Maembe; na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kutekeleza kazi za Kamati. Kamati inawashukuru na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa kipekee, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu, kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza kazi za Kamati. Ninaomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge - Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Nkamia Suleiman, Mbunge - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Captain John Damian Komba, Mbunge, Mheshimiwa Dokta Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge, Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mbunge, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge, Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mbunge, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mbunge, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mbunge, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mbunge, Mheshimiwa Rebecca Michael Mgodo, Mbunge, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dokta Thomas Kashililah, akisaidiwa na Makatibu wa Kamati; Ndugu Hosiana John na Ndugu Grace Bidya, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Mshama kwa uwasilishaji wako mzuri. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kabla ya kuwakilisha hotuba kwamba kutokana na ufinyu wa muda, naomba kwamba *Hansard* irekodi hotuba yangu niliyowasilisha Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 99(7) Toleo la Mwaka 2007, nachukua fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema hata kuweza kusimama hapa kuwasilisha kero na matakwa ya watu wa Taifa hili. Nasema ahsante Mungu kwa mema yote unayotutendea mimi na Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wote wa Taifa hili, nakushukuru na kumpongeza sana Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuwa Spika mwanamke wa Bunge hili. Namshukuru kwa heshima kubwa aliyotuletea wanawake wote. Mungu azidi kumjalia, busara, umakini na uvumilivu mkubwa katika kuliongoza Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakishukuru Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kuniteua kuwa Mbunge katika nafasi maalum. Naahidi kufanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kutimiza majukumu niliyopewa na Chama pamoja na Watanzania wote kwa ujumla. Hakuna kulala mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa, namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi rasmi ya Upinzani na Mwenyekiti wa CHADEMA - Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Naibu Kiongozi – Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kuniamini na kuniteua kuiwakilisha Kambi katika Wizara hii nyeti, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za kipekee pia ziende kwa wanaharakati wote wa Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP),* Taasisi ya HakiElimu, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania *(TAMWA),* Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA),* Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC),* Chama cha Walimu Tanzania *(CWT),* Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania *(MEWATA),* Chama cha Wanawake katika Sheria Afrika *(WILDAF),*Chama cha Msaada wa Sheria kwa wanawake *(WILAC)* na Mtandao wa Jinsia na Ukombozi wa Mwanamke *(FEMACT).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, naishukuru familia yangu ya Mwakyoma na Kaihula kwa kuniunga mkono na kunivumilia wakati wote ninapokuwa kwenye hekaheka za kuwatumikia wananchi. Shukrani hizi pia ziende kwa wapiga kura wangu wa Ilala na Chuo cha Biashara *(CBE),* Mungu awabariki kwa kuniinua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 494 la Desemba 17, 2010, (*instrument*) moja ya majukumu makubwa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ni kushughulikia maendeleo ya jamii. Maendeleo ya jamii ni hatua zinazowawezesha watu kutambua uwezo walionao wa kubaini matatizo na uwezo wao wa kutumia raslimali zilizopo kujitatulia matatizo hayo, kujipatia na kujiongezea kipato na kujiletea maisha bora zaidi na hivyo kwa ujumla, kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maendeleo ya Jamii, Toleo la Juni, 1996, imeainisha viashiria vinavyotumika kuangalia kiwango cha maendeleo ya jamii, kama ifuatavyo:-

- Kuongezeka kwa kipato kinachowezesha kaya katika jamii kukidhi mahitaji yao na kujiwekea akiba;
- Kuongezeka kwa huduma za kijamii kama nyumba bora, afya, elimu, lishe, mazingira safi na maji safi na salama ya kutosha;
- Kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto wachanga;
- Kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya kisasa;
- Kuongezeka kwa matumizi endelevu ya mazingira; na
- Kutokomeza umaskini katika jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viashiria hivyo vya maendeleo ya jamii vinathibitisha mambo makuu mawili ambayo tunaitaka Serikali iyatilie maanani. Kwanza, viashiria hivi vinatoa ushahidi wa wazi kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kiasi kikubwa kabisa, ni Wizara isiyo na majukumu, kwani, majukumu ya kuhakikisha viashiria hivyo vinafikiwa, tayari ni majukumu yanayohusu Wizara na Idara zinazohusika na afya, kilimo, maji, nishati, mazingira, barabara na Wizara nyingine za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani hairidhishwi na muundo huu wa majukumu yanayojirudia katika Wizara zaidi ya moja. Hali hii inachochea urasimu usio na tija katika utendaji wa kiserikali na wakati mwingine inalazimisha fedha za umma

kutengwa zaidi katika kushughulikia suala moja, ambalo matokeo yake yanaweza kupatikana kupitia fedha zinazotengwa kwenye Wizara nyingine iwapo zitawajibika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa majukumu mengi yamekuwa yakitekelezwa zaidi na Wizara nyingine za kisekta kuliko hata Wizara yenyewe ya maendeleo ya jamii, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa Wizara hii ipewe jukumu la kusimamia maendeleo ya jamii, na sasa jukumu hilo liondolewe kwenye Wizara ya Afya na badala yake Wizara ya Afya ibakie na jukumu la kuzuia/kinga, utabibu na matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa Rais ndiye aliyepewa madaraka ya kikatiba kuunda Baraza la Mawaziri kwa kadri anavyoona yeye inafaa. Hata hivyo, kwa kuwa Bunge lina wajibu wa kushauri na kuisimamia Serikali, Kambi ya Upinzani inawataka Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Waziri Mkuu, wamshauri Mheshimiwa Rais kuondoa dosari hii ya kuwa na Baraza kubwa la Mawaziri, huku likiwa na majukumu yanayojirudia na kuingiliana kwa baadhi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, viashiria hivyo vya maendeleo ya jamii vinaonyesha kuwa, miaka 50 baada ya uhuru, licha ya raslimali na fursa nyingi za kimaendeleo tulizonazo, bado tuko nyuma sana katika maendeleo ya jamii. Kwa mfano, wakati moja ya viashiria hivyo ni ongezeko la kipato kinachowezesha kaya kukidhi mahitaji yake na kujiwekea akiba, Ripoti ya Utafiti wa Bajeti ya Kaya inaonyesha kuwa takribani asilimia 33.4 ya Watanzania bado wana umaskini wa mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kuwa kuna Watanzania zaidi ya million 12.3 wana umaskini wa mahitaji muhimu ikilinganishwa na Watanzania milioni 11.4 wa mwaka 2000/2001. Umaskini umebaki kuwa juu zaidi katika maeneo ya vijijini, ambako kuna asilimia 37.4 ya idadi ya watu wenye umaskini wa mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati moja ya viashiria vya maendeleo ya jamii ni kuongezeka kwa upatikanaji na ubora wa huduma za afya na kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto wachanga, Ripoti ya Umoja wa Mataifa ya Ufuatiliaji wa Malengo ya Milenia ya mwaka 2010, inaonyesha kuwa Tanzania ni moja ya nchi tatu zenye vifo vingi vya watoto wachanga katika nchi zote Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikizidi tu Nigeria na Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Congo *(DRC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya nusu ya vifo hivi vinachangiwa zaidi na utapiamlo unaoua theluthi nzima ya watoto hawa, ukifuatiwa na magonjwa ya malaria, kuharisha, na *neumonia*. Ripoti ya mwaka 2010 ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC),* imeeleza kuwa tatizo kubwa la upungufu wa zahanati, ambapo kwa wilaya ya Tunduru pekee, upungufu huo umefikia asilimia 57. Vifo hivyo vingeweza kukomeshwa kwa kusogeza zaidi Vituo vya Afya, vifaa na wataalam wa afya na kupunguza umbali mrefu wa kufikia tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akizungumza kwenye majumuisho ya mkutano wa mwisho wa Kamisheni ya Uwajibikaji wa Afya ya Mama na Mtoto ya Shirika la Afya

Duniani *(WHO),* Rais wa Jamhuri ya Muungno wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Kikwete alituambia kuwa vifo vya watoto Tanzania vimepungua kutoka vifo 162 mwaka 1982 hadi kufikia vifo 81 kwa kila watoto 1,000 mwaka 2010 na kwamba vifo vya wajawazito vimepungua kutoka vifo 578 mwaka 1982 na kufikia vifo 454 kwa kila wajawazito 100,000 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi haziridhishi hata kidogo kwa sababu kila siku wanafariki akina mama 24 kwa sababu ya matatizo yatokanayo na afya ya uzazi. Hii ni sawa na kusema kuwa kila saa moja tunampoteza mama mmoja kwa sababu za matatizo ya uzazi, yaani tangu Waheshimiwa Wabunge tuwe hapa, saa tatu asubuhi hadi muda huu wa saa sita mchana, tayari akina mama watatu wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, ilitarajia takwimu zenye kuonyesha mafanikio ya Wizara na Serikali ya tangu ilipoingia madarakani mwaka 2005 hadi sasa na siyo takwimu za kuanzia mwaka 1982 ambapo utawala, sera na mfumo mzima wa maisha pamoja na idadi ya watu vilikuwa ni tofauti kabisa na changamoto zilizopo mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati moja ya viashiria vya maendeleo ya jamii ni ongezeko la upatikanaji na ubora wa huduma za maji, Ripoti ya Bajeti ya Kaya imebainisha kuwa bado asilimia 48 ya kaya zote nchini na asilimia 60 ya watu wa maeneo ya vijijini wanategemea vyanzo vya maji ya kunywa ambavyo havijahifadhiwa. Pia ripoti hiyo imeeleza kuwa upatikanaji wa maji safi na salama umepungua kutoka asilimia 55.4 ya mwaka 2001 hadi asilimia 51.2 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mifano hiyo michache, ni dhahiri kuwa tuko nyuma sana katika suala zima la maendeleo ya jamii. Ili kuziwezesha familia nyingi kumudu gharama za msingi za kijamii, ikiwemo lishe, malazi, mavazi, afya na elimu, Kambi ya Upinzani inaendelea kuitaka Serikali ipandishe kima cha chini cha mishahara kutoka Sh. 135,000/= hadi kufikia Sh. 315,000/= na ipunguze kodi ya mshahara *(PAYE)* hadi kiwango cha asilimia tisa na kiwango cha juu mpaka asilimia 27. Tunaitaka Serikali ianze kutoa pensheni angalau ya Sh. 20,000/= kwa mwezi kwa kila mzee mwenye umri wa zaidi ya miaka 60. Hatua hii itasaidia kupunguza ukali wa maisha katika kaya nyingi za vijijini na angalau kuziwezesha kumudu baadhi ya huduma za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani pia inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za bajeti ya maendeleo vijijini zisizopungua shilingi bilioni 450 (ndani ya kipindi cha miaka mitano mfululizo kama bajeti mbadala ilivyoshauri) kwa ajili ya kusukuma zaidi sekta ya maji, nishati vijijini, barabara na kuhakikisha fedha zote zinazotengwa kwa bajeti ya afya hazipungui asilimia 15 ya bajeti yote, (kama tulivyoridhia katika tamko la Abuja).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba maendeleo ya jamii yatapatikana pindi Serikali itakapokubali kuweka kipaumbele cha kutosha katika sekta nyeti zinazogusa mahitaji ya watu wengi hususan wale wa vijijini na mfuko/akiba kwa maendeleo ya kijana mtoto wa Tanzania kuanzia umri 0 hadi miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na jamii inayowajibika, hatuwezi kujenga Taifa linalojitawala na kujitegemea. Miaka yote tutakuwa tegemezi kwa mambo mengi. Taifa halitaweza kufanya maamuzi yake kulingana na mazingira yake. Ni wakati muafaka wa kuacha kujitegemea katika makaratasi na kauli bali tutekeleze azma zetu kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa matatizo yote ya kiuchumi, rushwa, ujambazi, matumizi ya madawa ya kulevya na miji yetu kuwa katika hali mbaya ya uchafu chanzo chake ni jamii isiyowajibika. Ujenzi wa jamii inayowajibika ni jambo linalopaswa kuanzia katika malezi ya ngazi ya familia na kukuzwa na malezi ya shule, taasisi za dini, vyombo vya habari na hata sanaa na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujenga jamii mpya inayowajibika kwa manufaa ya leo na siku zote zijazo, Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali iandae mpango mahsusi na endelevu wa kupenyeza elimu ya maadili katika jamii yetu, ili angalau kama siyo kukinusuru kizazi cha sasa, basi tuweze kukinusuru kizazi kijacho dhidi ya mmomonyoko mkubwa wa maadili unaolitesa Taifa hivi sasa. Mpango huo uhakikishe maadili, uwajibikaji na uzalendo vinapenyezwa na kuhamasishwa kupitia mitaala ya shule, shughuli za Asasi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kidini, Vyombo vya Habari na shughuli za Wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine ambalo kwa sasa limesababisha jamii nyingi kukosa maadili na ni lile la wanawake kupigwa na waume zao na vile vile wanaume kupigwa na wake zao. Jambo hili limefanyiwa utafiti wa upande mmoja tu wa wanawake kupigwa, lakini ukweli ni kuwa hata wanaume wanapigwa na wake zao. Kambi ya Upinzani inaona kuwa jambo hili linazalisha jamii isiyowajibika kwani upendo na heshima katika familia unapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna tatizo ambalo limekuwa ni hatari na tishio kwa jamii ya vijana, nalo ni kuibuka kwa wanaume na wanawake wanaoshawishi wasichana na wavulana wadogo kushiriki nao tendo la ndoa (mafataki wa kiume na wale wa kike). Hii ni aibu kwa jamii na inasababisha kuwa na jamii isiyowajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuongelea masuala yanayohusu wanawake kwa undani, naomba niongelee hili linalohusu Benki ya Wanawake. Serikali kwa mwaka 2011/2012 kwa bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii imetenga jumla ya shilingi bilioni 4.8, lakini kati ya fedha hizo, shilingi bilioni mbili zinapelekwa kuimarisha huduma za Benki ya Wanawake.Kambi ya Upinzani inaona kuwa kutenga kiasi hicho cha fedha ambacho ni nusu ya fedha za maendeleo ya Wizara nzima kwenye Benki inayofanya kazi kibiashara na shughuli zake ziko Dar es Salaam peke yake, ni kutokuwatendea haki wanawake wengi wanaoishi nje ya Mkoa wa Dar es Salaam au waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tunaitaka Serikali kutoa majibu ya kina juu ya vigezo vilivyotumika katika kugawa fedha ile hali vyuo vilivyoko chini ya Wizara hii havina fedha na viko katika hali mbaya na hata fedha kwa ajili ya haki za watoto chini ya kasma 5415 kwenye kitabu cha maendeleo wametengewa Sh.7,400,000/= tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni muda umepita tangu wanawake waanze kudai kuwa na Baraza lao litakalowaunganisha wanawake wote wa Tanzania bila kujali itikadi zao za kisiasa. Hili lilianza kujitokeza baada ya kuingia kwa mfumo wa siasa za vyama vingi pale UWT ilipopoteza uhalali wa kuwa Umoja wa Wanawake wote wa Tanzania kwani ulikuwa ni tawi la CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inafarijika na kuupongeza kwa dhati mkakati ulioanzishwa na Umoja wa Jumuiya za Wanawake wa vyama vilivyo na wawakilishi Bungeni kuanzisha chombo kitakachowaunganisha wanawake wote bila kujali itikadi zao (ULINGO). Tunaamini huu ni mwanzo mzuri katika uundwaji wa Baraza la wanawake wa Tanzania. Kambi ya Upinzani inashauri Wizara husika zifanye kazi nao kwa ukaribu ili kuwanufaisha wanawake wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ndio wanaelewa matatizo yao, hivyo kungojea Serikali ifanye taratibu za kuanzisha Baraza ni kupoteza muda, kwani, watendaji tunaowategemea Serikalini hawaonekani kuchukua hatua. Napenda kumpa hongera sana Dr. Avemaria Semakafu kwa jitihada za kuhakikisha kuwa ULINGO unaundwa na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na asasi nyingi sana zinazotoa mikopo kwa akina mama kupitia Wizara hii, lakini hali halisi inaonyesha kuwa mikopo hiyo haiwafikii walengwa ambao ni akina mama waishio vijijini. Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna tatizo kubwa, inaweza kuwa ni dawati linaloshughulikia suala hilo halifanyi kazi zake kwa utaratibu unaotakiwa, au riba inayotozwa ni kubwa mno na pengine masharti yanayotolewa ni magumu kiasi kwamba walengwa wanashindwa kuyatimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za akina mama walionufaika ukiangalia karibu wote wanatoka maeneo ya mijini tabaka la juu, na hivyo takwimu hizo zinatolewa kijumla jumla tu. Kambi ya Upinzani inasema kuwa mtindo huu wa utolewaji takwimu za jumla unaifanya Serikali ishindwe kutatua tatizo la msingi la hali halisi ilivyo kwa akina mama waishio vijijini. Ili kutatua tatizo hilo, pangeonyeshwa takwimu kulingana na wanawake wangapi Wilaya, Kata, Kijiji fulani wamepata mikopo. Tunasema hivyo kwa kuwa idadi ya vijiji inajulikana kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine ambalo limeendelea kufanya wanawake waonekane kuwa wametengwa na Serikali yao, nalo ni suala zima la mirathi. Kwa sasa hakuna idara rasmi katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wajane wanaodhalilishwa kwenye kadhia nzima ya mirathi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliona hili, kwani ni kero kubwa. Serikali isiishie kusikiliza tu, bali Wizara zinazohusika kuchelewesha malipo ya mirathi ziwajibike kuongeza thamani ya fedha zilizocheleweshwa kwani zinapocheleweshwa zinapoteza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake tunaendelea kuihakikishia jamii kwamba tunaweza sana. Tuendelee kupewa nafasi ili tuzidi kustawisha jamii bora zaidi na yenye kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa hapa nchini ambalo linaongezeka kwa kasi kubwa sana la wanawake kubakwa. Ripoti ya hali ya haki za binadamu ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya mwaka 2010 inasema kuwa kati ya mwezi Machi na Juni, 2010 jijini Dar es Salaam pekee kesi za ubakaji 123 ziliripotiwa Polisi kwa kanda maalum ya Dar es Salaam pekee na ilikadiriwa kuwa kwa nchi nzima kesi 3,200 za ubakaji ziliripotiwa Polisi na uchunguzi ulikuwa unaendelea na kesi 169. Watuhumiwa walikuwa wametiwa hatiani kwa upande wa Zanzibar, wanawake 870 walikwenda kupata huduma za matibabu kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na madhara waliyopata baada ya kubakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa tatizo hili ni kubwa na hivyo ni budi sasa Wizara ikaja na mkakati mahususi wa kuweza kukabiliana na tatizo hili kwani tunaamini kuwa tatizo ni kubwa sana na ni kesi chache tu ndiyo zinaripotiwa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Tanzania kuridhia Azimio la Umoja wa Mataifa *(UN)* la kukomesha vitendo katili dhidi ya Mwanamke, Makubaliano ya Beijing ya mwaka 1995, na Azimio la mwaka 2003 kuhusu Haki za Wanawake katika Bara la Afrika, bado vitendo vya ukeketaji havijaisha nchini. Tanzania bado haijakidhi mkakati wa pamoja uliopitishwa mwaka 1997 na *WHO, UNICEF* na Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa wa idadi ya watu *(UNFPA)* uliokemea kwa nguvu zote ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukeketaji halikubaliki katika jamii ya watu wastaarabu duniani. Wanawake walio hatarini kukeketwa inabidi sasa walindwe. Kambi ya Upinzani inataka kuhakikisha suala hili linapewa umuhimu wa kipekee katika bajeti. Ukweli ni tumeshindwa kuwalinda wanawake hao hasa katika sehemu kubwa ya Mikoa ya Mara, Singida na Manyara ambapo ukeketaji hufikia hata 80% ya wanawake wote katika baadhi za Tarafa na Wilaya za Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo ni kuwa usiri mkubwa miongoni mwa jamii, wakiwemo waathirika hukwamisha vita dhidi ya ukeketeaji. Utafiti uliofanyika Wilayani Handeni mwaka 2009 watoto 47 walikeketwa Kata ya Misima ikifuatiwa na Kata za Kang'ata 42, Kivu 31, Sindeni 16, Kwasenga 11 na Kwamsisi 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya mwaka 2010 inasema kuwa Afisa wa Afya Wilaya ya Manyoni alisema kuwa mwaka 2009 wanawake 254 kati ya 1,046 waliojifungua kwenye hospitali hiyo walikuwa wamekeketwa. Nalo shirika lisilo la kiserikali la *AFNET* lilitoa ripoti yake ya mwaka 2009 iliyoonyesha kuwa watoto 47 kati ya 59 walio chini ya umri wa miaka mitano waliokwenda kwenye kliniki Singida walikuwa wamekeketwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto nyingine kubwa ni Wizara kushindwa kutumia fursa iliyopo katika Sheria zetu ikiwemo Sheria ya Kanuni ya Adhabu *(Penal Code)* ambapo kifungu cha 169 (a) kinaliweka kama kosa na kulipa adhabu tendo la kuhusika na ukeketaji kwa mtoto wa kike, ikiwalenga wazazi au Ngariba. Kambi ya Upinzani inasema, kwa kuwa tatizo la ukeketaji limekuwa na mwelekeo mpya kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na *AFNET*, hivyo basi, elimu ya kina ni muhimu sana kwa jamii ili mila na tamaduni za makabila husika ziweze kuachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunaitaka Serikali iwasilishe marekebisho ya sheria hii hapa Bungeni ili kosa hili lisiwe la kulipia faini kwa ngariba bali adhabu yake iweze kuwa kubwa kulingana na kosa na hii itasaidia katika kukomesha ukeketaji wa wanawake hapa nchini unaoendelea na kulitia aibu Taifa letu, kwani kosa hili mara nyingine husababisha vifo kwa waathirika. Pia marekebisho hayo ya sheria yawahusishe wazazi watakaohusika kuwapeleka watoto wao kukeketwa na wao wapate adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inauliza, kwa nini tunakuwa na Wizara zaidi ya moja katika kushughulikia suala moja? Hili linaitwa jambo mtambuka. Mathalani, suala la watoto, Idara zinazojikita katika kushughulikia masuala ya watoto, ziko katika Wizara tatu tofauti. Nazo ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya tatifi zilizofanywa mwaka juzi na baadhi ya Halmashauri nchini zinaonyesha kuwa jumla ya watoto 437,544 wapo katika mazingira hatarishi. Huu ni wakati wa jamiii kuangalia namna ya kuwaondoa watoto wa mitaani ili kuondokana na tatizo la kuzagaa kwa watoto hawa. Ni vizuri kukawa na mpango madhubuti wa kuwasaidia watoto waliopo mitaani na kuzuia wengine kutoingia katika hatari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto wa mitaani wanasababishwa na mambo mengi yanayozikabili familia. Yafuatayo ni baadhi ya mambo hayo:-

(a) Kutengana kwa wazazi (mifarakano katika ndoa) kumekuwa ni tatizo linalosababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Mara nyingi ndoa ikishavunjika watoto ndio wanaokuwa waathirika wakubwa wa mtafaruku huo;

(b) Mimba za utotoni ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na jinsi familia zinavyotoa malezi kwa watoto wao na hivyo kupelekea tabia binafsi ya mhusika;

(c) Watoto kuzaliwa nje ya ndoa ni tatizo lingine linalosababisha watoto wa mitaani kuongezeka;

(d) Vifo vya wazazi ni chanzo kingine cha kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Vifo hivi vinatokana na magonjwa na ajali mbalimbali vinavyozidi kushamiri katika nchi yetu;

(e) Ukatili, unyanyasaji na umasikini uliokithiri katika baadhi ya familia; na

(f) Jambo lingine ni familia kutowajibika kwa watoto wao na hivyo kupelekea watoto kutokuwa na msimamizi na mshauri kwenye ngazi hiyo muhimu katika makuzi ya vijana wetu.

Kutokana na sababu hizo, watoto hawa wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kutopata elimu, malazi, mavazi, matibabu, ulinzi na malezi bora. Matatizo haya kwa asilimia kubwa husababisha watoto hawa kukimbilia mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo hayo yote niliyoyaeleza hapo juu mengi hayaihusu Serikali, bali yanatuhusu sisi sote kama wazazi tuwajibike kwa familia zetu ili tujenge jamii ya vijana watakaokuwa wawajibikaji. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaishauri jamii ya Watanzania bila kujali itikadi za kisiasa, kidini na kimila kuwajibika kwa familia zao kwanza, na kuhakikisha tunawalea watoto wetu kwenye mila na tamaduni zetu. Kambi ya Upinzani inataka kujua Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa tatizo la watoto wa mitaani linamalizika na ni kiasi gani cha bajeti kimetengwa kwa ajili ya kulishughulikia tatizo hili? Kwani ni kubwa na linahitaji hatua za haraka kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari nyingine zinazotokana na kutokuwajibika kwa jamii ni kuzalisha watu wasio na maadili. Watu hawa wanapopewa dhamana ya kusimamia na kulinda raslimali za jamii, hawatimizi jukumu hili kwa uadilifu. Jambo hili linasababisha madhara ambayo tunayaona sasa ya wala rushwa, mafisadi papa na wale wote wanaotumia nafasi zao za kiutendaji kwa kujinufaisha binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya muundo wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwani shughuli husika kuwa katika Wizara hizi kuwa katika Wizara mbili tofauti ndivyo inavyokuwa vigumu kutoa huduma stahili kwa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa sheria mahususi ya mtoto imeishapitishwa lakini bado kanuni zake hazijapitishwa ili sheria hii ifanye kazi. Tunaitaka Serikali itaje ni lini kanuni hizi zitakuwa tayari ili tuweze kuepusha watoto wetu kuwa ombaomba mitaani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inajidhihirisha kutokana na ripoti ya utafiti iliyotolewa na Serikali ya hali ya Ukimwi na Malaria ya mwaka 2007-2008 *(National HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey of 2007-2008)* inaonyesha kuwa takribani asilimia 11 ya watoto wote Tanzania Bara wenye umri chini ya miaka 18 ni yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wengi hapa nchini wako kwenye kundi lililo hatarini kwani kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya mwaka 2010. Ripoti hii inasema kuwa katika Kata ya Buriaga Wilaya ya Tukuyu watoto sita waliuawa kutokana na imani za ushirikina, kuwa ukiua mtoto wa chini ya miaka mitano kwa kumbaka utapata utajiri. Hali hii imeenea sana maeneo mbalimbali nchini mwetu.

*(Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoomba ni kwamba kwa sababu ya muda, naomba hotuba yangu iandikwe yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto kuwa na vyeti vya kuzaliwa limekuwa kama ndoto, kwani kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya mwaka 2010 ni kuwa ni watoto asilimia 17 tu ya watoto wote ndio wana vyeti vya kuzaliwa hapa nchini. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kuwa Wizara na Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kuwa watoto hawa wanaweza kupata vyeti vya kuzaliwa hapa nchini. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu, kuna mikakati gani Wizara hii imeandaa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa watoto wanapata vyeti vya kuzaliwa? Ni muhimu pia Serikali ikamaliza kigugumizi cha kutoshughulikia Sheria ya Ndoa na Mirathi kwani ni sehemu ya utatuzi wa suala la ustawi wa mtoto na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo na ustawi wa jamii yoyote ile huanzia kwenye ushirikishwaji wa makundi yote muhimu ya watu kwenye vyombo vya maamuzi. Ili hilo liwezekane, mfumo wetu wa uchaguzi badala ya kuwa mfumo wa "mwenye nguvu mpishe", unapaswa kuwa ni mfumo unaotoa fursa ya makusudi kwa makundi yote muhimu katika jamii kuwa na uwakilishi mzuri kwenye vyombo vya maamuzi kama Bunge, Mabaraza ya Madiwani na Mabaraza ya Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikisema kuwa inafanya jitihada za kuhakikisha kunakuwa na uwakilishi sawa wa asilimia 50 kwa 50 ya wawakilishi wanawake na wanaume kwenye vyombo vya maamuzi ikiwemo Bungeni. Hata hivyo, katika kipindi kilichopita, Serikali ilishindwa kupata *formula* ya kuhakikisha kunakuwa na uwakilishi huo Bungeni, kinyume na ilivyokuwa imeahidiwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Matokeo yake Wabunge wote wanawake katika Bunge hili ni asilimia 36 tu ya Wabunge wote na siyo asilimia 50 kama ilivyokuwa imeahidiwa. Kwa mantiki hiyo, bado Serikali ina deni kwa wanawake, kwani kilichoahidiwa hakikutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kilicho muhimu zaidi ni kuongeza uwakilishi shirikishi wa makundi mengine muhimu ya watu kwenye vyombo vya maamuzi, ili kupanua demokrasia na kuhakikisha matakwa na maslahi ya jamii nzima yanawakilishwa kikamilifu kwenye vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa na ilivyo kwa wanawake ambao hatimaye wamepewa fursa ya makusudi ya uwakilishi kupitia viti maalum, yapo makundi mengine

ya watu katika jamii kama walemavu, ambao idadi yao ni kubwa sana (takribani milioni nne), lakini kwa sababu ya mifumo yetu ya kisiasa na kiuchaguzi na hali ya ulemavu wao imekuwa vigumu kwao kushindana na kupata uwakilishi mzuri kwenye vyombo vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo kundi kubwa la vijana ambalo ni kubwa sana lakini kwa sababu ya mifumo yetu ya kisiasa na kiuchaguzi na changamoto zinazowakabili kwa nafasi yao kama vijana, imekuwa vigumu kwa kundi hili kupata uwakilishi wa kuridhisha kwenye vyombo vya maamuzi. Lakini kwa sababu ya mifumo yetu ya kisiasa na kiuchaguzi ya mwenye nguvu mpishe au wengi wape, sehemu kubwa ya watu hawa muhimu imekuwa nje ya vyombo vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lengo la Kambi ya Upinzani kutaka kila Mtanzania awe Mbunge au Diwani, bali tunachopendekeza na kusisitiza ni kwamba, kuandaliwe mazingira ya makusudi ya kimfumo yatakayohakikisha kunakuwa na uwakilishi mpana na shirikishi zaidi wa jamii yetu katika vyombo vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo haki, kwa mfano kwa kundi kubwa la walemavu, lenye watu takribani milioni nne, karibu sawa na asilimia 10 ya watu wote, na lililo katika mazingira magumu kuwa na uwakilishi finyu Bungeni, tena unaopatikana katika mazingira yasiyo na uhakika ya ushindani wa kisiasa wa “mwenye nguvu mpishe”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kambi ya Upinzani, kwa nia njema kabisa na kwa manufaa ya Taifa hili, inaishauri Serikali na Bunge lako Tukufu kwamba siyo tu tuongeze uwakilishi wa wanawake Bungeni, bali pia tunapendekeza mfumo wetu wa uchaguzi na kisiasa ufanyiwe marekebisho makubwa, kwa kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2014 na 2015, tunakuwa na Mabaraza ya Halmashauri na Bunge la Jamhuri, lenye mchanganyiko mzuri wa uwakilishi kutoka watu wa kada na makundi mbalimbali, hususan walemavu na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, mfumo wote huu tunaopendekeza, unaitwa “*Mfumo Mchanganyiko wa Uchaguzi*,” yaani *Mixed Electoral System*, kwani utatoa Wabunge wa aina kuu mbili. Wabunge wa Majimbo na Wabunge watokanao na kura za uwiano, ambamo ndani yake tutakuwa na uhakika wa kuongeza Wabunge wanawake, walemavu, vijana na watu wengine watakaojitokeza, ambao vyama vyao vitaona ni muhimu waingie Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unaunga mkono hoja?

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana bado sijaunga kwa sababu kuna mambo ambayo yanapaswa kujibiwa na Mheshimiwa Waziri.  Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia, naomba tuwe *straight to points* kwa sababu tuko wengi na muda ni siku moja. Sasa namWita Mchungaji Dr. Rwakatare atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Faida Bakar na Mheshimiwa Devotha Likokola ajiandae.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Mimi pia ningependa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kuweza kuchangia katika Wizara hii. Vilevile ningependa nitoe pongezi kwa Wizara hasa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kutuletea hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka huu wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda nijikite moja kwa moja bila kupoteza muda kwenye ufinyu wa bajeti. Bajeti hii ni ndogo sana kulingana na majukumu ya Wizara hii mwaka hadi mwaka. Hapa Bungeni tumekuwa tukisema juu ya ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mwaka jana ilikuwa ni shilingi bilioni 19, mwaka huu wamepunguza imekuwa ni shilingi bilioni 16. Ni kama vile hawasikii kilio cha Wabunge tunapokaa na kusema kwamba waongeze bajeti hii. Shilingi bilioni 16 ni kama bajeti ya vitengo katika Wizara nyingine mbalimbali. Hii inaonyesha kwamba Wizara hii ni kama vile haitiliwi maanani, ni kama haina umuhimu na inawekwa pembeni, jambo ambalo linasikitisha. Jamani tunaposema jinsia, maana yake ni wanaume, wanawake na watoto. Wizara hii wanafanya kazi kubwa, ina mambo mengi, sasa unaposema kwamba bajeti ishuke tena kwa shilingi bilioni tatu nzima, yaani mpunguze, sasa tusemeje? Ni kwamba kazi zake zimepungua au vipi? Tunaomba, jamani msikilize vilio tunavyolia na maoni mbalimbali tunayotoa isionekane kama tunatwanga maji kwenye kinu. Hili jambo ni muhimu katika Kamati, tumekaa pia tumeona kwa kweli hili jambo ni muhimu watu hawa waongezewe bajeti. Hizi fedha, shilingi bilioni 16 ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba tuna vyuo takriban 55. Katika hivi vyuo 55 mmepanga bajeti ya shilingi milioni 300, hivi kweli kwa bajeti ya shilingi milioni 300 utafanyia nini? Hivi vyuo tumevitembelea, vingi tu wengine tumeona vilivyokuwa hoi bin taabani, yaani vinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Vingine havina Walimu, vingine vinahitaji vitendea kazi, sasa wanapopanga bajeti ya shilingi milioni 300, kweli tutaweza kufanyaje hiyo kazi? Watu hawa tutawalaumu bure, lakini kumbe ni ufinyu wa bajeti. Tuangalie jamani Wizara hii kwa jicho la huruma, waongezewe bajeti hizi hela, wanazopangiwa ni ndogo sana. Unajua tunalalamika kwamba vijana wetu hawana kazi, kumbe vyuo hivi vingeweza kusaidia sana, wale wanaomaliza Darasa la Saba wakajifunza ufundi stadi ili waweze kusaidia kabla ya *VETA* zinazotarajiwa kuletwa katika kila Wilaya hazijafanikiwa. Hivi vyuo vinafaa sana, vingeweza kutusaidia sana.

Kwa hiyo, naomba sana, jamani hivi vyuo tuviangalie kwa jicho la huruma na kuwapa bajeti inayostahili. Sasa wanaposema kwamba bajeti ya Wizara hii ni shilingi bilioni 16 maana yake nini? Halafu vyuo vyenyewe vimepewa shilingi milioni 300, yaani

wamebaki wamekwama na kwa maneno mengine kwa mfano ni kwamba shilingi bilioni moja sasa katika miaka hii 55 ndiyo vyuo hivi vyote vitakuwa vimekwishakarabatiwa kwa sababu ni lazima ukae miaka 50 kila mwaka hela ndogo, kila mwaka hela ndogo tutamaliza lini kuvikarabati? Tuangalie sana bajeti hii ni ya muhimu ichunguzwe na iweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kusema ni kuhusu watoto wa mitaani, watoto wanaoishi katika mazingira magumu, watoto yatima ambao labda kwa sababu moja ama nyingine wamejikuta wako mitaani.

Mimi naona kwamba suala hili linaachiwa tu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, lakini Wizara hii ni Wizara mtambuka. Watoto hawa ni wa Wizara nyingi. Naomba pia Wizara ya Sheria iweze na wao kuchukua mkondo kuweza kusaidia siyo kuwaachia tu Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa sababu hawa watoto ni watoto wa watu wote, kwa hiyo, tujaribu kwa hali zote kuangalia.

Kwa mfano, wanaposema mtoto eti anaolewa na miaka 14, anapoolewa na miaka 14 si ndiyo sababisho mojawapo la watoto kukimbilia mitaani? Maana mtoto anazaa mtoto, atawezaje kumlea huyu mtoto? Sababisho kubwa kabisa la watoto kukimbilia mitaani ni mahusiano mabovu ya wanandoa. Mahusiano mabovu ya wanandoa sasa hivi talaka zimeingia mpaka makanisani kwa sababu ya nini? Ni mahusiano yamemomonyoka. Kwa hiyo, tuangalie wanandoa tuwape semina mbalimbali katika Wilaya, Majimbo, Mikoa yetu na kadhalika ili ndoa ziimarike na sababu ni nyingi, ukiangalia ni kutekelezwa, baba amekimbia, labda pengine uchumi mbovu, ukiangalia nyumba ndogo na kadhalika. Yaani shughuli ni nyingi zinazosababisha watoto kwenda Mtaani. *(Makofi)*

Sasa kama kila mtu tu atakuwa na uwezo wa kuandika talaka kwamba wewe sio mke wangu, unatoka sokoni unakuta talaka inakungoja, jamani kweli tutakuwa na maisha ya namna gani? Tukemee talaka kama tunavyokemea UKIMWI maana talaka chimbuko lake ndiyo hilo watoto wa mitaani, UKIMWI, watoto kuzagaa kila mahali na kuhangaika. Hiyo yote ni kwa sababu ya talaka. Tujaribu kuangalia haya mambo ya kutengana, kutokujali watoto kwani mlipatana wenyewe, mkakubaliana wenyewe, mkazaa watoto, msiwaache kwenye mataa, watoto wapate matunzo yanayostahili ili na wao waweze kufurahia maisha ya utanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni lile la Benki ya akina mama. Kwa kweli tunaipongeza Wizara kwa juhudi na hata kwa ule Mfuko wa Maendeleo ya Akina Mama, ni mfuko mzuri. Lakini sasa nashauri kwamba ile Benki ingeshuka mpaka vijijini. Wanasema kwamba ni ngumu na kweli inaweza kuchukua muda mrefu, lakini pia tunaweza kushirikiana na *VICOBA*, siku hizi *VICOBA* viko kila kijiji. Tushirikiane pia na *SACCOS* za akina mama, tukishirikiana nao hakika kabisa tutapata ufumbuzi mzuri, kila mtu atafaidi na hiyo Benki ya Wanawake, isiwe tu inaitwa Benki ya Wanawake wakati wanawake wengi muhimu wa vijijini wameachwa pembeni na wao wafaidi na wasikie kwamba wanahusika na hiyo Benki.

Mambo mengi hakika kabisa ni mazuri yaliyosemwa na Kamati na yaliyosemwa hata na Waziri…

*(Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI :** Naomba uendelee, au umeshamaliza?

**MHE. DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tu niache ! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Basi nakushukuru sana Mheshimiwa Mchungaji. Sasa namwita Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia, nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Tanga kwa kuniwezesha kunipa nafasi ya kuweza kuingia katika Bunge hili Tukufu. Nawaahidi kwamba nitawawakilisha vizuri na ninamwomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na kuwapongeza Madiwani wa CCM Arusha pamoja na Madiwani wa CHADEMA kufikia muafaka wa kuhakikisha kwamba wanashirikiana ili kuhakikisha wanawaletea maendeleo wananchi wa Arusha kwa sababu wananchi wa Arusha waliwachagua kwa ajili ya kuwasimamia ili waweze kupata maendeleo. Hivyo, kitendo walichokifanya ni cha hekima na busara ili wananchi hawa waweze kupatiwa kile ambacho walikusudia pale walipokuwa wamewachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa niseme kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba nianze kwa kuelezea kusikitishwa na ufinyu wa bajeti. Bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, imepewa bajeti kidogo sana kama ambavyo mwenzangu amezungumza. Kwa mwaka uliopita tulipewa bajeti ya shilingi bilioni 19 na kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 16, tofauti ya shilingi bilioni tatu ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 18. Naomba tu niseme kwamba Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, sijui baadhi ya wenzetu wanavyoielewa. Wizara hii ya maendeleo ya jamii maana yake ni maendeleo ya wananchi wote, siyo maendeleo labda ya wanawake kama ambavyo wengine wanaweza wakawa wanaitafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi katika kuiangalia Wizara hii, ni vizuri tukawa tunaiangalia kwa angalau kuiongezea fedha ili iweze kujiendesha. Ni jambo la aibu tunapozungumzia masuala ya maendeleo halafu Wizara hii yenyewe tunaipatia fedha kidogo ambazo zinatakiwa kuwaletea maendeleo wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mazuri ya Wizara hii hayawezi kufikiwa kwa bajeti hii ambayo imetengwa. Kwanza kabisa tutashindwa kuchochea maendeleo ya wananchi wetu kwa sababu tunasema wananchi wapatiwe maendeleo, maendeleo yatachochewa na nini kama bajeti yenyewe hii ni finyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii kwa mfano shilingi bilioni 16 ni sawasawa na kitengo kimoja cha Wizara ya Nishati na Madini. Yaani hii shilingi bilioni 16 tuliyopewa ni sawasawa na kitengo kimoja cha Wizara ya Nishati na Madini. Hivi hii kweli ni haki? Naomba kila wanapokaa kupanga bajeti za Wizara hizi, basi Wizara hii iangaliwe kwa macho ya huruma kwa sababu ni Wizara ambayo inabeba maendeleo ya Jamii kwa maana ya wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ufinyu wa bajeti hii umeweza kusababisha Vyuo vya Maedeleo ya Jamii kwanza chakavu, havina vifaa vya kuandikia na vina wakufunzi wachache. Sasa bajeti yake ni kama ambavyo mmeiona kwamba, tumepewa shilingi milioni 300 katika vyuo 55. Hivi kweli kwa pesa hii vitawezeshwa kujiboresha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu ni chuo kimoja tu cha *SOFI* ambacho kitaboreshwa. Je, hivi vingine vitaweza kufikiwa kama tunapewa bajeti kidogo kwa kiasi hiki? Kwa bahati mbaya yawezekana kabisa fedha hizi wenzetu wa Wizara ya Fedha wasizitoe zote kutokana na utaratibu ambao nimeona katika Wizara nyingine. Nimeona kwenye utaratibu wa bajeti zilizopita kwamba fedha zilitengwa lakini hazikutolewa zote. Sasa kupitia Bunge lako Tukufu, tuiombe Wizara ya Fedha, kwa kuwa sisi Wizara hii tumetengewa fedha kidogo kwa mwaka huu, basi hizi fedha zitolewe zote angalau malengo yaliyokusudiwa yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala zima alilozungumza mwenzetu wa upinzani kwamba Wizara hii labda wanaomba ifutwe. Naona kwa kweli mwanamke mwenzangu aliyewasilisha hii taarifa hapa amejisahau kwamba Wizara hii ndiyo iliyotutetea sisi wanawake mpaka kuingia ndani ya Bunge hili. Sasa anapozungumzia kwamba labda Wizara hii ifutwe, simwelewi, maana yake yeye mwenyewe amefikishwa humu ndani na Wizara hii, kapitia viti maalum ambavyo wanawake waliweza kuitetea Wizara hii ili iweze kutetea wanawake.

**TAARIFA**

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha aliyetoa neno lisilo sahihi, Hakuna aliyewasilisha kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ifutwe. Mimi nimewambia kwamba itenganishwe na Ustawi wa Jamii na Mambo ya Afya, hakuna aliyesema ifutwe. naomba asahihishe usemi wake. *(Makofi)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikataa taarifa. Kutenganishwa huko ndiyo ambako sisi hatukubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mimi sijakuruhusu. Taarifa imetolewa, endelea.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikataa taarifa hiyo. Kwa hiyo, naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa niendelee kuchangia kuhusu suala zima la Sheria ya Ndoa. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inakinzana na Sheria ya Ndoa ya mwaka 2009. Mimi nilikuwa nafikiri iko haja sasa ya Serikali yetu kuhakikisha kwamba tunabadilisha Sheria hii ili tuweze kuwanusuru watoto wetu ambao wanalewa wakiwa na umri mdogo. Ukiangalia Sheria ya mwaka 1971 na 2009 inasema kwamba, "mtoto wa kiume ataruhusiwa kuoa akiwa na miaka 18, lakini mtoto wa kike ataruhusiwa kuolewa akiwa na miaka 15."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka hiyo 15 mtoto wa kike huyu bado anakuwa hata hana ule uwezo wa kufikiri, kuweza kuitunza na kuilea familia kwani anakuwa hajapevuka vizuri. Lakini wakati huo huo wakiishakuwa wamezaa watoto hawa ambao wana umri mdogo kwa kiasi hiki ndiyo wanashindwa kuwatunza na watoto hawa wanageuka wanakuwa wa mitaani. Nilikuwa naomba sana ikiwezekana sheria hii tuweze kuirekebisha ili ikiwezekana watoto wa kike waweze kuolewa angalau kama kweli tunahitaji wakiwa na miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nawaomba wazazi wenzangu, kwa sasa tunahitaji watoto wetu wa kike waweze kusoma. Pamoja na sheria hii ambayo tunasema ibadilishwe, tuombe watoto wa kike wasiolewe wakiwa na hiyo miaka 18, waendelee kupata elimu ili iweze kuwawezesha baadaye kupata maisha ambayo yatawawezesha kuishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la vitendo vya ukatili kwa wanawake. Wanawake wamekuwa wakipata vikwazo vingi vya kufanyiwa vitendo vya ukatili. Vyombo vyetu vya usalama kama vile Polisi na Mahakama, wanawake wengi wamekuwa wakishindwa kujieleza mbele ya umma.

Kwa mfano, kule Polisi unafika pale ambapo wanaandikishia sijui wanaitaje, '*reception'* unasimama na kuanza kueleza kwamba mimi nimefanyiwa hiki, nimefanyiwa hiki, siyo rahisi. Wanawake kwa jinsi tulivyoumbwa tuna uso wenye haya, hatuwezi tukaanza kujieleza maneno ambayo ni makubwa ambayo yametudhalilisha mbele ya watu walio wengi. Hivyo, ili wanawake wengi waweze kujitokeza, ni vizuri basi yakatengwa maeneo ambayo wanaweza wakakaa pembeni, wakajieleza ni namna gani wameweza kufanyiwa huo ukatili kwa sababu akiwa katika *chamber,* anaweza akasema vizuri kuliko akiwa kwenye umati wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Mahakama kwamba, kesi za aina hii zifanyike kwenye *chamber courts* ili angalau wanawake hawa waweze kuwa na nafasi ya kuweza kujieleza vizuri kuhusiana na jinsi ambavyo wamefanyiwa ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na wanaume hawa ambao wanawafanyia ukatili wanawake, iwepo sheria, ndugu zangu sasa ni wakati muafaka. Wanaume hawa wamekuwa wakitufanyia wanawake ukatili mkubwa, wanatufanya vibaya, sasa kutufanya vibaya huku ni vizuri ikawepo Sheria ili hawa watu hata kama hakuna ushahidi wafungwe, kwa sababu hawa watu tukiendelea kutafuta ushahidi na kitu kinaonekana kabisa, hivi ni kwanini tuendelee kusema kwamba mpaka upatikane ushahidi wa kutosha? Hawa wanaume wakikaa jela, wapumzike hata miaka miwili, basi inatosha watapata adabu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iangalie utaratibu wa namna ya kuwaadhibu hawa watu vikali ili kusudi iwe fundisho na wengine wasiendelee kuwatendea ukatili wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni tatizo la watoto wa mitaani. Tatizo kubwa la watoto wa mitaani linatokana na sisi wenyewe wazazi kwa sababu tumekubaliana, tumezaa watoto lakini tunafika mahali wanaume wanaamua kutelekeza wake zao. Naomba iwepo sheria ambayo itawabana hawa wanaume ambao wanaoa wanawake, wengine wanaamua tu kuzaa na wanawake halafu wanaacha kutunza watoto. Iwepo sheria ambayo itawabana wanaume hawa wasiweze kuwatekeleza wake zao, wasiweze kutekeleza watoto kwa sababu kuwatekeleza watoto hawa ndiyo kunakowapelekea kwenda mitaani. Maana yake, mama anaachiwa wale watoto peke yake, uwezo wa kuwatunza hana, siyo ajabu uchumi wake ni mdogo, hivyo afanyeje? Kadri anavyohangaika kusaidia watoto, wale watoto wanaamua kujitoa wenyewe na kujipeleka mitaani kwenda kutafuta chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba sheria ile ya kuwabana akina baba hawa ambao wanawatelekeza wake zao na watoto, basi iweze kutungwa na kuhakikisha kwamba wanabanwa ili waweze kutunza familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 (a) inasema bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mchangiaji, Mheshimiwa Mary Chatanda, anachangia ametoa taarifa ambazo siyo za ukweli baada ya kuanza kwa kusema kwamba, anawapongeza Madiwani wa Arusha wa Chama cha Mapinduzi na CHADEMA, kwa

kufikia muafaka. Juzi tulikuwa kwenye Kamati Kuu, Dar es Salaam na chama chetu hakijawahi kuujua huo muafaka. Lakini najua alijisikia raha kusema hivyo kwa sababu yeye ni chanzo cha mauaji ya Arusha Mjini, na hata leo wakati anatoa mchango wake pia alisema anawashukuru wanawake wa Tanga waliomchagua, lakini alikuja kufanya fujo kwenye Jimbo langu la Arusha Mjini. Mimi ni Mbunge na ni Diwani, Arusha Mjini hakuna muafaka, na kama unatafuta muafaka mama, endelea kuomba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulikuwa unatoa Taarifa au Mwongozo? Maana yake umeanza kumfahamisha mchangiaji kwamba Arusha hakuna Muafaka, hakuna nini, sasa ni kitu gani umeeleza hapa, Taarifa au Mwongozo?

**WABUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Ni Taarifa. Basi taarifa ameipokea.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hadi leo tukiwa tunavuta pumzi. Tunashukuru sana maana wengi wameshatangulia na tunawaombea mahufira. Kwanza naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza toka tuanze Bunge hili, napenda sana kukishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kulipitisha jina langu na wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, kunipitisha kuwa Mbunge wao. Nawaahidi kama kawaida yangu sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuipa hongera Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia kubwa sana. Tunawashukuru sana viongozi wetu kwa kufanya nao kazi pamoja na wakaweza kufikia hatua kubwa sana ya utekelezaji wa Ilani yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja katika nyanja tofauti, lakini nitaanzia na nyanja ya wanawake na amani. Wanawake tunatakiwa tuhimize amani katika nchi yetu ya Tanzania. Vilevile katika kuhimiza tuisimamie amani kwa sababu vita ni chungu sana, vita inashinda uchungu wa shubiri. Napenda kuwahamasisha wanawake wenzangu tuweze kuilinda amani yetu tuliyonayo kama wanawake kwa sababu vita ni vibaya sana. Tuangalie leo Somalia, vita vya Burundi, Libya, wanawake wengi wamepoteza maisha yao kwa sababu ya vurugu. Napenda kuwaambia wanawake wenzangu wa Tanzania tusipende kuwasikiliza watu ambao hawana msimamo mzuri, tukawa tunaendelea na kufanya maandamano ambayo siyo rasmi na kuweza kuvuruga amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaambia wanawake kwamba litakapotokea, wahenga walisema: "Vyako vyako, vyako na wenzio; vikikupata, vyako pekee." Mwanamke hana nguvu kumshinda mwanaume. Sisi wanawake tusibabaishwe na baadhi ya wanaume tukafanya maandamano katika nchi yetu na kuvuruga amani. Kikitokea wewe mwanamke na mtoto ambaye umembeba hapa, mmoja mgongoni, mmoja hapa, sijui mmoja hapa, utakwenda wapi? Na mwingine ana mimba juu! Kwa hiyo, naomba wanawake tudumishe amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchangia suala unyanyasaji wa wanawake, mfumo dume huu. Mfumo dume bado upo. Huu mfumo dume huu unajificha ficha, lakini sisi wanawake tumeugundua mfumo dume upo, mbali na kwamba Serikali yetu inafanya kila linalowezekana kutusaidia wanawake, maana wametuwekea *Fifty – Fifty* (50% - 50%) na inshallah Mwenyezi Mungu atujalie mwaka 2015 tutafikia hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu tulipokuwa tunaadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi, 2010, alisema, ninanukuu: "Tumeazimia kuongeza idadi ya Viti Maalum Bungeni kufikia asilimia 40 ya Wabunge wa kuchaguliwa, tunaamini kwamba asilimia 10 iliyosalia inaweza kupatikana kwa wanawake kugombea Viti vya Majimbo." Namaliza kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ina imani kubwa na sisi, na sisi wanawake wa Viti Maalum tuliomo humu Bungeni, tumekuja kwa mfumo uliokubalika. Nashangaa leo kuna wanaume hata humu Bungeni ambao ni Wabunge wenzetu wanatunyanyasa sisi wanawake wa Viti Maalum. Tunawaambia kwamba sisi tunaweza na namsema Mbunge mwenyewe maanake mimi simwogopi, huyu Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, wa Jimbo la Ziwani, Pemba *(CUF)* tunamwomba awe na nidhamu kama Wabunge wenzake wa *CUF* walivyo na nidhamu. Sisi Wabunge wa Viti Maalum wa vyama vyote, tunapinga kauli hiyo, tulimsikia na tulimwona kwenye Vyombo vya Habari anadhalilisha wanawake. Huu ni mfumo na tutakwenda nao na tutamalizana nao, itakayokataa ni Serikali siyo yeye. *(Makofi)*

Naomba kumwambia Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, kwamba mwaka 2015 Jimbo lile siyo la kwake, mwanamke wa Chama cha Mapinduzi ndiye ataenda pale na atachukua Jimbo. Kwa hiyo, tunamwomba, '*aste aste,* ujiti na macho, ncha ina hoho,' awe na nidhamu na sisi wanawake wa Viti Maalum, na viti hivi viongezwe kwa sababu huu ni mfumo tu. Namwambia kwamba mimi mwenyewe hapa niliyesimama ni Mbunge wa Viti Maalum, lakini nilikuwa Mbunge wa Jimbo la Wawi. Kwa hiyo, tunasema kwamba wanawake tusinyanyasike.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae kwanza.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba ninamheshimu sana Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 64

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 64 ngapi? Naomba uisome.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala na …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa SalIm samahani. Hoja iliyoko mbele yetu ni hoja inayozungumzia masuala ya Jinsia, Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa anayechangia, Mheshimiwa Faida Bakar amezungumzia masuala yote yanayohusu ustawi wa wanawake na kwa vile hajakwenda nje ya mjadala wetu, naomba aendelee.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunilinda na kumpasha yaliyo kweli Mheshimiwa Mbunge. Namheshimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa watoto yatima. Mtoto wa mwenzio ni wa kwako. Kuna wanawake wengine wanaoolewa na baba mwenye watoto waliofiwa na mama, wale yatima, akifika yule mama anajifanya kumpenda baba, lakini mtoto anamnyanyasa. Watoto yatima tunawaonea huruma, tuwapende kwa sababu ni watoto wetu. Ni kwa pande zote mbili wanawake na wanaume, nawaasa Watanzania wenzangu watoto yatima ni wa kwetu.

Tuchukueni mfano mkubwa wa Zanzibar, mtoto yeyote yatima wa Zanzibar analelewa na shangazi, dada na mama mdogo au mama mkubwa, iweje leo huku watoto wanazagaa mitaani? Iweje leo hawa watoto tunawachoma moto, tunawachoma kwa visu? Yaani ni mambo mengi wanayofanyiwa watoto yatima kwa sababu hao watoto yatima hawakupenda wazazi wao wafariki. Kwa hiyo, jamani kwa huruma kubwa, nawaomba wazazi wa nchi ya Tanzania yote muwe na imani kwa watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kwa kuwapatia mikopo wanawake mbalimbali hapa Tanzania kwenye *SACCOS*, *VICOBA* yaani vikundi mbalimbali vya ushirika, lakini mikopo haiwafikii walengwa. Mikopo mingi inakuja Dar es Salaam na sehemu za mijini, lakini huko ndani vijijini haiwafikii walengwa. Tunaomba sana mikopo, Mheshimiwa Waziri aende Tanzania nzima aone mambo yanavyokuwa huko Vijijini. Wengi hawapati mikopo na wana miradi mbalimbali, lakini hawana nyenzo, tunaomba iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia juu ya unyanyaswaji wa vikongwe. Wazee ni wetu tunaona hivi sasa mpaka kwenye TV kuna mzee mmoja mwanamke anaitwa mchawi, sijui ilikuwa Shinyanga siwezi kujua ni wapi pale, lakini nimeona mimi mwenyewe mzee anataka kufukiwa kwenye shimo akiwa hai. Jamani mzee wa mwenzio

ni wa kwako. Eti kwa sababu wazee wana macho mekundu; macho mekundu yanatokana na ule moshi wa kuni za kila siku toka mtu yuko kijana mpaka amekuwa mzee anapikia kuni. Kwa hiyo, macho mekundu yanakuwa kwa ajili ya hali hiyo. Lakini siyo kwa sababu wao ni wachawi, tuwaenzi wazee wetu jamani. Wananchi wa Tanzania tuwe na imani ya kuwaenzi wazee wetu, tusiwazike bado wapo hai. Nawaomba sana wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali yetu kutuanzishia Benki ya Wanawake Tanzania, lakini kinachoshangaza, Benki hii iko hapa Dar es Salaam tu na hivi sasa wanafungua Matawi tofauti pale Dar es Salaam. Ni kweli kwamba pesa inakuwa ni kidogo, lakini hiyo hiyo kidogo tugawane kidogo kidogo ivuke ije Zanzibar Benki ya Wanawake. Kila siku tunaahidiwa Benki ya Wanawake itakuja Zanzibar lakini hatuioni, lakini kwa sababu Serikali yetu ni sikivu, basi tunajua kwamba Benki hii ikishafanikiwa hapo Dar es Salaam itavuka kuja Zanzibar na masharti yake yapunguzwe. Naona kama masharti yake yako sawa sawa na Mabenki mengine. Mimi sioni tofauti sana, kwa hiyo, naiomba sana Serikali itusikie kilio chetu wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja moja, lakini msicheke ni kitu cha ukweli. Kuna tabia ya wanawake na wanaume kujifananisha tofauti. Tuna maadili gani hapa Tanzania na Serikali wala haileti sheria hapa Bungeni? Ilete sheria hapa Bungeni tuipitishe. Kuna wanawake wanajifananisha na wanaume na kuna wanaume wanajifananisha na wanawake, siyo tabia nzuri ya kimaadili ya Kitanzania. Ulivyoumbwa wewe na Mwenyezi Mungu ndiyo ulivyo, usimwone Mwenyezi Mungu hajakuumba vizuri, ni vibaya, hata kwenye dini zote ni vibaya. Kwenye dini yetu ya Kiislamu na dini nyingine, naamini ni vibaya. Nawaomba wanawake wenye tabia hii waiache kwa sababu wanatutia aibu sisi wanawake wenzao, na wanaume wenye tabia hiyo waache kwa sababu wanatia aibu wanaume wenzao na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**TAARIFA**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji aliyemaliza sasa hivi, taarifa aliyoitoa kwamba ana uwezo wa kulichukua Jimbo la Ziwani kwa tiketi ya CCM, nataka kutoa taarifa kwamba sio yeye wala chama chake ambacho kina uwezo wa kuchukua Jimbo lolote katika Kisiwa cha Pemba. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Taarifa imefika kwa mhusika. Naomba kumwita Mheshimiwa Devota Likokola na baadaye Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Taarifa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini. Mheshimiwa Likokola endelea.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pia naungana na Wabunge wenzangu kwanza kabisa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza maendeleo ya wanawake na jinsia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa mchango wangu katika mambo makubwa mawili tu. Kwanza nitatoa pongezi, lakini pili, nitatoa maoni. Nimesimama hapa kwanza kabisa kuwapongeza wale watu wote wanaothamini na kuheshimu kazi na uwezo wa wanawake katika dunia hii. Tuna tatizo kubwa sana, watu wengi hawathamini mchango na kazi za wanawake. Wanawake wengi wana uwezo na wanafanya kazi nzuri na kazi zao kwa kweli ukiziangalia na ukizilinganisha na za watu wengine utagundua rasmi kwamba kazi wanazopewa wanawake wanazifanya kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Umoja wa Mataifa tunaye Naibu Katibu Mkuu Mama Asha-Rose Migiro, wote tunaiona kazi yake ni nzuri na inaendelea vizuri. Sasa hivi Kiongozi Mkuu wa *IMF* ni mwanamke, kwa hiyo, kuna watu wametambua ule mchango wake na wameweza kumfikisha nafasi hiyo. Lakini vile vile tuna Marais, Rais wa Liberia, tunaye Spika wetu, Mama Anne Makinda, tuna Mawaziri hapa Mawaziri wanawake hapa. Jamani, tuseme ukweli kwamba kazi zao ni nzuri na zinafurahisha, zinatia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Wabunge wanawake, kazi zao hakuna ambaye atatia mashaka. Kazi zao ni za uhakika na zinakwenda kwa umakini mkubwa sana. Lakini vile vile tuna Majaji, Makatibu Wakuu na Madiwani wanawake. Kwa kweli nawapongeza sana Madiwani wanawake, wanafanya kazi nzuri, lakini vile vile tuna Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji wanawake hao, watu wote wanafanya kazi nzuri. Lakini niseme tu pia tuna wanawake katika jamii zetu kila familia, kuna wanawake, jaribu kulinganisha uwezo na kazi za wanawake waliopo katika familia na kazi kubwa wanazozifanya. Kwa hiyo, natoa wito kwa watu wote kuthamini na kuheshimu mchango mkubwa wa wanawake wa Taifa hili na wanawake duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachohitajika duniani hapa ni wanawake, wapewe nafasi, wanaweza kufanya vizuri. Nawashauri wanawake wenyewe ndugu zangu, tusingoje kupewa nafasi. Nafasi ni ya wote, kwa hiyo, tuchukue nafasi zetu tuweze kufanya kazi nzuri. Napenda sana kupongeza mchango ambao Mheshimiwa Rais anauonyesha. Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Jakaya Kikwete ametoa mfano mzuri sana, anawapa wanawake nafasi nyingi sana. Kwa hiyo, naomba Mawaziri wengine wafuate mfano huo, viongozi wengine Serikalini wafuate mfano wa Mheshimiwa Rais kwa kutoa nafasi kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ninatoa pongezi kwa wanawake wajasiriamali. Wanawake wajasiriamali wanafanya kazi nzuri sana na wote

sisi tumekuwa mashahidi. Tumekwenda kwenye maonyesho ya Saba Saba kuna wanawake wamefanya kazi nzuri sana, kwa hiyo, ninawatia moyo waendelee kufanya kazi zao vizuri. Lakini ninasema tunamshukuru sana Mama Esther Mkwizu - Kiongozi wa *Private Sector Foundation* kwa kazi nzuri anayoifanya kuhamasisha wanawake waunde Makampuni yao, wafanye shughuli zao na waweze kufaidi fursa ambazo nchi yetu inatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Getrude Rwakatare, Mbunge mwenzetu lakini amefanya kazi kubwa ya kuelimisha watoto wengi wa Taifa hili. Anafanya kazi nzuri sana, mashule yake watoto wengi wanasoma, ni lazima tuseme ukweli, mwanamke mwenzetu anafanya kazi nzuri na nampongeza sana kwa kazi hiyo anayoifanya. Pia ninaomba nipongeze Mashirika mbalimbali yanayofanya kazi ya kutoa elimu, kutoa mikopo, kutoa mafunzo kwa wanawake na kurahisisha maisha ya wanawake. Napenda kupongeza *TGNP* kwa kazi nzuri ya mafunzo, Shirika *Hans Foundation* kwa kutoa mafunzo kwa wanawake, lakini pia *SIDO* wanafanya kazi nzuri, *MEWATA* wamefanya kazi nzuri sana. Nampongeza sana Dada Serafina Mkuwa, dada yangu nakupongeza kazi nzuri ya *MEWATA* watu wote wameiona. Lakini vile vile napenda kupongeza *TATEDO,* wanatengeneza majiko sanifu kwa ajili ya wanawake kupikia. Nawapongeza *TDBP* na *CAMARTEC* kule Arusha kwa kutengeneza nyenzo nzuri ambazo wanawake wanazitumia. Lakini vile vile nawapongeza sana Taasisi nyingine ambazo zinatoa mikopo kwa wanawake kama vile kwanza kabisa Benki ya Wanawake. Tunakupongeza sana Mama Chacha kwa kazi nzuri unayoifanya. Lakini naipongeza Benki ya Twiga kwa kuweza kutoa mikopo mingi sana na kuwa Benki ya kwanza kuwadhamini Wana-*VICOBA* Tanzania.

Naipongeza Benki ya Twiga, mwendelee kutoa mikopo kwa Wana-*VICOBA* kwa sababu walikuwa wamekwama, hakuna taasisi iliyokuwa inawakopesha. Lakini sasa nafurahi kuwatangazia kwamba Wana-*VICOBA* wote msiwe na wasiwasi Benki ya Twiga ambayo ni Benki ya Serikali iko pamoja na nyinyi na inatoa mikopo. Kwa hiyo, muwahi kupeleka maombi yenu mpate mkopo mwendelee na ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko taasisi kama *FINCA* na *PRIDE* zote hizo zinafanya kazi nzuri. Naona kwamba katika pongezi zangu ninaishia na pongezi kwa wanawake wa Mkoa wa Ruvuma. Wanawake wa Mkoa Ruvuma jamani ni majasiri, ni hodari na ni wachapakazi. Nawapongeza sana na mwendo ni huo huo. Hakuna kulala tuendelee kuchapa kazi ili kuboresha maisha yetu. Maisha bora kwa kila Mtanzania yataletwa na kufanya kazi zetu za mikono na tutabarikiwa kwa kazi zetu na hatimaye maisha yetu yatakuwa mazuri sana. Nawaomba wale wanawake wote ambao bado wao hawajaamka na wakafanya kazi vizuri waje Ruvuma waone jinsi ambavyo wanawake wa Ruvuma wanafanya kazi vizuri wanazalisha chakula kwa wingi sana na mwaka huu tuna mahindi mengi sana ambayo wanawake wengi wamelima. Tuna kahawa ya kutosha, tuna korosho kule Tunduru, kwa hiyo nawapongeza sana wanawake wenzangu wa Ruvuma. Lakini vile vile wamebuni mitindo mbalimbali ya kujihusisha na ujasiriamali. Wana harambee zao wanaita majamanda. Wanawake wengi wamejenga nyumba nzuri, wamenunua magari, pikipiki pamoja na baiskeli. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niseme tu kwamba nina ushauri kwa Serikali yetu. Kwanza suala zima la uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi lipewe kipaumbele. Wanawake wakiwezeshwa kiuchumi hili Taifa litasonga mbele. Kwa hiyo, naomba mpango mzima wa kuwawezesha wanawake kiuchumi, uwekewe msisitizo na uwekewe bajeti ya kutosha. Bila bajeti ya kutosha, wanawake hawatawezeshwa. Wanawake wengi wanashindwa kwenda kujifungua hospitalini, hawana uwezo. Wanawake wengi wanashindwa kupata huduma nzuri, hawana uwezo, lakini ukimwezesha mwanamke kiuchumi umemaliza kazi. Kwa hiyo, nashauri Serikali ijitahidi katika mikakati ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Lakini ninashauri Serikali iangalie wazo la kuwa na Kamisheni ya Jinsia ili kuweza kuratibu shughuli zote za kijinsia zinazofanywa katika Wizara mbalimbali. Tuna *Desk Officer*s wa Kijinsia katika kila Wizara, lakini tukiwa na Kamisheni, Kamisheni ile itasaidia kuangalia madawati ya jinsia kila Halmashauri yanafanya kazi nzuri.

Ninashauri vile vile washirika wetu wa Kimataifa watusaidie sana hasa Mashirika ya Kimataifa. Nashukuru katika bajeti ya maendeleo safari hii angalau *UNDP* wameweza kutuchangia kama Sh. 800,000,000/= kwa ajili ya kufanya mambo mbalimbali ya *Planning*. Lakini vile vile *UNFPA* nao wamechangia Sh. 935,000,000/=, *UNICEF* wamechangia Sh. 116,000,000/=. Ninaomba wadau wengine wa Kimataifa wachangie kwanza tunaomba mtuchangie kwenye Benki yetu ya Wanawake. Ile Benki ipate pesa nyingi, iweze kuwawezesha wanawake kwa sababu tunashirikiana Kimataifa, basi msaidie kuchangia sasa. Tumeanzisha chombo kizuri naamini *World Bank* wanaamini katika masuala ya *finance,* basi wachangie ile Benki ya Wanawake ili iweze kukua sasa. Lakini vile vile naomba watupatie taarifa na *research* mbalimbali zinazofanywa juu ya masuala mazima ya wanawake na jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ujasiriamali na elimu ya fedha ni muhimu kwa wanawake, lakini vile vile masuala mazima ya ziara za mafunzo. Ninashauri ziara za mafunzo zifanyike, hapa Afrika tuna nchi ya Rwanda imefanya vizuri sana katika usawa wa kijinsia. Kwa hiyo, ni vizuri tukafanya ziara za mafunzo ili kuweza kujifunza zaidi, lakini vile vile nawakaribisha wananchi wote waweze kufika Mkoani Ruvuma kujifunza mambo mbalimbali ambayo tumeyafanya vizuri kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwapongeza watu wote na naunga mkono hoja. Ahsante kwa kuniruhusu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MARY P. CHATANDA:** Mwongozo Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia mwongozo wa kanuni ya 64(a na g) inayosema kama ifuatavyo: “Bila kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano

katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli", na ile ya (g) "Hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine".

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Mbunge Lema alipotoa taarifa hapa alisema kwamba chanzo cha mauaji kule Arusha ni Mheshimiwa Mary Chatanda. Mheshimiwa Mwenyekiti naomba mwongozo wako, kwani kitendo hicho ni cha kunidhalilisha na ni cha kuudhi na ni cha kunisingizia. Ningekuwa labda nimefanya hayo mauaji ningekuwa nimeshtakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae. Naomba nitolee mwongozo mwisho wa majadiliano ya mchana huu. Nitatoa mwelekeo. Naomba kumwita Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Amina Andrew ajiandae kama muda utaruhusu.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naimi nashukuru kawa kupata fursa hii niweze kutoa mchango wangu mdogo katika hoja hii muhimu sana ya maendeleo ya wanawake katika nchi yetu. Kwanza kabisa, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Sophia Simba, Naibu wake na Katibu Mkuu kwa uwasilisho mzuri wa hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango, naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni mdau mkubwa sana katika Wizara hii kwa sababu digrii yangu ya kwanza ni ya Maendeleo ya Jamii na Masuala ya Maendeleo ya Wanawake na kwa nafasi hii naomba pia nieleze kwamba Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani aliyesema katika ukurasa wa tatu, kwamba Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kiasi kikubwa ni Wizara isiyo na majukumu. Sasa na mimi kwa nafasi hii naikanusha kwa sababu digrii yangu yenyewe nimesomea nje na inahusu Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto na kwa hiyo ni suala linalotambulika Kimataifa. Ndugu zangu nadhani ni wakati muafaka wanawake dunia nzima tushikamane tuweze kuthamini mchango mkubwa ambao unatolewa na wanawake katika dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii, nitambue uwezo mkubwa wa wanawake wa Tanzania kwa kumpongeza Mheshimiwa Spika wetu, Mama Anne Makinda, kwa kutuweka katika ramani ya dunia kama Spika wa kwanza mwanamke katika nchi yetu. Tunamwombea maisha mema na Mungu amsaidie katika utendaji wa majukumu yake magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka, nichangie maeneo machache. Kwanza, nianze na maendeleo ya wanawake katika siasa. Nazungumza hili kwa sababu katika uongozi wetu wa kisiasa ambao tunaongozwa na Sheria na Kanuni mbalimbali na hasahasa niki-*refer* hapa Bungeni, tunaona bado tuna upungufu katika Kanuni na Sheria mbalimbali ambazo kwa nia njema tunaomba ziweze kurekebishwa ili utendaji wetu na ufanisi wa kazi zetu kama wanawake hapa Bungeni uweze kwenda vizuri. Naomba kutoa mfano kwamba sisi Wabunge wa Viti Maalum tupo Kisheria lakini kusema kweli Sheria na taratibu kidogo ziko *gender silent* ama hazijajionyesha vizuri ama zinatunyanyapaa kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mfano, Wabunge wa Viti Maalum walianza mwaka 2000 lakini kuna Sheria ambazo zinatunyanyapaa kwa sababu zilianza mwaka 1982. Naomba kutoa mfano wa barua hii, naomba nisome aya hii. Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI, inapenda kuwakumbusha Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwamba uundaji wa Kamati tajwa kwa maana kwenye Halmashauri zetu ambazo sisi ni watendaji ziko Kisheria. Wajumbe wa Kamati ya Fedha wametamkwa kwenye Sheria Namba 287 na 288 au Namba 7 na 8 ya mwaka 1992. Sasa kwa kipindi hicho hakukuwa na Wabunge wa Viti Maalum lakini bado Sheria inayotumika ni ile ya wakati huo. Tunaomba wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha atueleze ili sisi kama Wawakilishi wa wanawake katika Halmashauri na ukizingatia kule ndiyo haswa utendaji wetu unatakiwa kuonekana tuweze na sisi kushiriki ili tuweze kuwaendeleza wanawake hasa ngazi za Halmashauri zetu na Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye eneo la Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Tunashukuru na tunaona michango mikubwa sana ambayo inatekelezwa na mashirika ambayo yanalenga maendeleo ya wanawake kama *TGNP*, TAMWA kama ambavyo yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri ametusomea na sisi tunawapongeza. Kwa hivi karibuni mashirika haya mazuri ambayo mchango wao unakubalika kijamii kidogo yamejielekeza zaidi kwenye siasa na tunaona mashirika haya mengi yanashutumu Serikali na Chama Tawala, sisemi kwamba Serikali isikosolewe lakini tunajua mwelekeo wa mashirika haya, lengo la msingi ni kutetea masuala ya wanawake. Kwa hiyo, katika suala zima la ukosoaji labda kama wanawake katika Serikali inayokosolewa ndiyo wenye makosa lakini mimi nadhani ukosoaji huo ukumbuke zaidi kuwatetea wanawake. Nasema hivyo makusudi kwa sababu mwaka jana ulianzishwa Mfuko wa Jimbo na huo Mfuko wa Jimbo uliwalenga Wabunge wa Majimbo, lakini mimi nilidhani lengo kubwa la mashirika hayo pia kwa kipindi hicho ni kuhakikisha ni kwa nini Wabunge wa Viti Maalum kama Wanawake na wenyewe hawakuhusishwa na Mfuko huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake wenyewe walikuwa mstari wa mbele kabisa kuupiga vita na kuonyesha kwamba Mfuko huo haufai kabisa. Mimi nadhani suala la kwamba haufai au unafaa ni mtazamo wao lakini kama wanawake wenzetu kama lengo lao la msingi ni kutetea wanawake, wangeweza kuhoji ni kwa nini basi Wabunge wenzetu wanawake hawakuhusishwa na kama kuna sababu ingeweza kujulikana. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri ni vizuri pia na wewe ukatuwekea msimamo kwamba Mifuko hii jinsi ambavyo inawasaidia wananchi na sisi ni sehemu ya msaada huo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nichangie kidogo pia kwenye masuala ya Sera, Mikakati na Kanuni mbalimbali. Naomba kwa kuwa tunaelekea kwenye mchakato wa kuandaa Katiba ya Nchi yetu kwa nafasi hii na mashirika ya wenzetu niliyoyataja, nadhani ni wakati muafaka pia tuweze kuyaainisha, Katiba yetu iweze kuonyesha wazi kabisa kwamba *gender* ni *mainstreamed* katika Katiba ya nchi yetu. Ina upungufu mwingi sana na tumeona wenzetu nchi nyingine kama Rwanda wameweza kurekebisha Katiba yao na kwa hivyo imeweza kuweka ama kuingiza masuala ya jinsia na kuonekana vizuri kwa ufanisi mzuri wa shughuli za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nalotaka kuzungumzia, ni masuala ya Itifaki ama *Protocols* zinazoridhiwa katika nchi mbalimbali na ambazo zinaweza kuwanufaisha wanawake. Katika Hotuba ya Waziri nimeona ameweza kuzungumzia hizo lakini naomba Itifaki hizo na zenyewe kwa sababu ni kwa ajili ya manufaa ya wanawake wa Tanzania na wengineo ziweze kuletwa hapa Bungeni na sisi tuweze kujifunza kwa sababu mwisho wa siku watekelezaji wa Itifaki hizo ni sisi wanawake, ndio ambao tunaweza kuzisimamia na wengi wenzetu wanapata fursa mbalimbali, wanaenda kwenye makongamano mbalimbali huko nje wanajifunza. Nadhani iweze kutafutwa mikakati mizuri ili wanaporudi basi na sisi wanawake wenzao waweze kutuelimisha, tuweze kuzielewa kwa sababu nchi nyingine wanatumia hizo Itifaki hata kuwashtaki wale ambao wanaleta unyanyasaji dhidi ya wanawake na kwa hiyo kama hatutazielewa, ni wazi kwamba hatutaweza kuzifuatilia na watakaonufaika ni wale waliokwenda pengine na Spika ambaye atapata ripoti lakini sehemu kubwa ya wanawake hatutakuwa na taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu Benki ya Wanawake. Asilimia 74 ya wanawake wako vijijini lakini kusema kweli, pengine ni mapema sana kwa sababu imeanza sio zamani sana lakini ni ombi kabisa kwamba hii Benki ya Wanaweke iweze kufungua matawi haraka sana kule vijijini ambako kuna wanawake wengi kwa sababu Dar es Salaam na maeneo mengine wanawake wa kule wana-*accessibility* ya hata mabenki mengine na wana hata zile sifa za kupata mikopo lakini sio wanawake wa vijijini. Kwa hiyo, nadhani *primary objective* ama lengo la msingi, ni kwa ajili ya wanawake ambao hawana uwezo wa kupenyeza mikopo katika benki za kawaida na kwa hiyo tunaomba Wizara hii iweze kuangalia kwa umakini ili sehemu kubwa ya wanawake wa Tanzania na wenyewe wafaidi benki hii ambayo inabeba jina lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu mikopo ya wanawake. Nampongeza Mheshimiwa Devotha amezungumzia vizuri tu, najua kwamba mikopo hasa hii ambayo inapita kwenye Halmashauri, nimeshangazwa kidogo kuona kwamba fedha zinatengwa kila mwaka lakini kama ni mkopo ina maana inaurejeshaji. Takwimu tunazoona ndiyo maana nikasema mimi ni mdau na ninazo taarifa za miaka mingi ya nyuma. Nachoona ni takwimu za fedha zinazotolewa na Serikali kupelekwa kama mikopo lakini ufanisi wa mfuko wenyewe ungeweza kuonekana kwenye urejeshwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa**.**

**MWENYEKITI**: Naomba kwanza tuendelee. Namwita Mheshimiwa Amina Andrew.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia japo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa Bungeni kwa mara ya pili kuweza kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto. Shukrani zangu za mwanzo, namshukuru na nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na maneno yake mazuri yenye maana ya kututazama sisi wanawake na watoto na kutujali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba katika Wizara hii, kuna changamoto nyingi, changamoto zenyewe zikiwemo, ukatili wa kijinsia, vipigo vya akinamama kama sisi, unyanyasaji wa watoto, ukeketaji pamoja na uonevu wakati wa mirathi hasa kwa akinamama. Akinababa najua hawanyanyasiki wakati wa mirathi kwa sababu wao upande wao kila kitu kinakuwa chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujielekeza upande wa watoto wa mitaani. Watoto wetu wa mitaani katika nchi yetu imekuwa tatizo kubwa sana. Naiomba Wizara ishirikiane na Makamishna wa Ustawi wa Jamii kwa sababu wakubwa wanasema kidole kimoja hakivunji chawa, peke yao Wizara ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto hawawezi kulitatua suala hili. Kwa hiyo, nawaomba washirikiane na wadau mbalimbali ili kuliweka sawa jambo hili la watoto wetu wanaozurura hovyo mitaani. Hawa watoto tukiwachukua na kuwaweka pamoja, wakisoma, tukiwalea vizuri na wakiwa na maadili mema, watakuwa vizuri, watasoma, watapata elimu na baadaye hawa watakuwa viongozi, watatuongoza katika nchi yetu. Naiomba Wizara, kweli kuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 lakini Sheria hii naona imewekwa kama picha tu, haifanyi kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuiuliza Wizara, je, hizi Kanuni za Sheria hii ziko tayari na kama ziko tayari hapo tutakapokuja kuletewa hii Sheria na Kanuni pia zifuate, tuletewe pia na tuzione Kanuni zake. Pia napenda kuiomba tena Wizara na kuiuliza, je, pindi ikishafanya kazi hii Sheria mikakati gani itachukuliwa ili tatizo kama hili la watoto lisirudi tena, wakarudi na kuranda kwa kuomba barabarani na halafu watoto hao wakawa ndiyo majambazi wakubwa. Naomba Wizara itakapochukua Sheria hii na Mkakati wauweke ili watoto hawa wasirudi tena mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa sisi wanawake. Kuna jambo ambalo linapigiwa kelele kila siku lakini jambo hili naona halifanyiwi kazi ipasavyo na kama itachukuliwa Sheria na litafanyiwa kazi ipasavyo, linaweza likaondoka. Kwa sababu siku za nyuma kulikuwa kuna unyanyasaji, wanakatwa viungo walemavu wa ngozi, Serikali iliposimama imara ilipata asilimia kubwa kama asilimia themanini ya mambo haya ya unyanyasaji yakamalizika. Je, hili suala la ukeketaji jamani watoto wetu wanakeketwa, hawakeketwi kwa hiari zao. Wanachukuliwa watoto wadogo wanakeketwa, wanatiwa ulemavu wa makusudi. Jamani ulemavu akikupa Mungu unasikitisha, je, ukimchukua mtoto ukimpa ulemavu wa makusudi. Watoto hawa wakati wa uzazi wanapata taabu sana kwa sababu ya kukeketwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara yako Mheshimiwa Waziri, watume Maafisa wako kule katika Wilaya na Kata wafanye hizi kazi, muwasaidie, muwape vitendea kazi, mkiwapatia pikipiki watahangaika. Hawa wanaofanya ukeketaji si wanajulikana, watafutwe, waonywe na wapewe onyo kali kwa sababu Mwenyezi Mungu

alivyotuumba kaumba kila kiungo kina kazi yake, mtu unamtoa kiungo. Huu unywele mmoja ulioko katika ngozi una kazi, je, mtu unakuja kumtoa kiungo chake mtu huyu unamweka katika hali gani? Kwanza akiwa mtu mzima mtoto yule anaona aibu, hajisikii raha wakati wa kuzaa, akija wodini labda anataka kuzaa, ukimwambia mtoto anataka kutoka yeye anajifunika nguo, anaogopa. Jamani nawasihi sana wazee waliokuwa bado kwenye mila potofu, mila kandamizi za kumkandamiza mwanamke, kumnyima uhuru wake hapa duniani, kuishi kwa raha na amani, waache mara moja na Sheria kali zichukuliwe dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Serikali iweke mkakati wa nguvu wa kuwasihi watu hawa jamani wakaacha hizi mila potofu. Naiomba Serikali, chonde hizi mila potofu hazina maana yoyote, haisaidii chochote, hilo lengo lao walilokusudia kumfanya mwanamke ili asiwe na kitu fulani, ni uongo, wanajidanganya. Hebu naomba Wizara iwaelimishe hawa watu, watoto wananyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muda unanitosha, naomba nielekee upande wa Vyuo vyetu vya *FDC*. Hivi vyuo jamani vinafanya kazi lakini vimetupwa kidogo. Vyuo vimekaa kama magofu, vyuo havina Walimu, havina vitendea kazi, wala vifaa. Chuo maana yake kieleweke, kiwe na Walimu na kiwe na vitendea kazi. Chuo kikiwa jumba tu, gofu, hakifanyi kazi yoyote, ina maana hicho sio chuo. Naiomba Wizara na Serikali kwa pamoja vivitizame hivi vyuo ili vijana wetu wanapomaliza kusoma shule za msingi wakienda kwenye vyuo hivi wajifunze mengi mazuri waweze kujiajiri wenyewe. Vyuo hivi vitasaidia kundi la vijana kujiepusha na mambo mabaya kama madawa ya kulevya, ujambazi, watoto wa kike kutiwa mimba mapema kwa sababu watajiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sina muda mrefu, nashukuru, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

## T A A R I F A

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapa taarifa wale ambao hawakuisoma Hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani na kuitafsiri vinginevyo, Hotuba yetu, ukurasa wa tatu, juu kabisa, imesema kwamba, katika Hotuba hii hapa ambayo imesomwa ambayo si ya Kambi ya Upinzani, inasema kwamba kwenye ukurasa wa 14 na 15 kuna mambo ya mafunzo ya elimu, kuna mambo ya mawasiliano na kuna mambo ya UKIMWI. Masuala ya UKIMWI yana kitengo chake. Kwa hiyo, sisi katika kuelezea hapa tukasema kwamba suala la UKIMWI na masuala mengine kupewa Wizara hii inaonyesha kwamba naomba ninukuu:-

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kiasi kikubwa kabisa ni Wizara isiyo na majukumu kwani majukumu mengi yameongezwa na inashughulikia majukumu mengi kupelekea Bajeti inayopelekwa kwa ajili ya Mambo ya Jinsia, Watoto na Wanawake kwa ujumla inakwenda katika masuala ya mafunzo ya UKIMWI kama

tulivyoonyeshwa katika ukurasa wa 15. Kwa hiyo, pesa na Bajeti zinapungua kwa masuala ambayo sio kazi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa...

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Naomba kutoa taarifa kwamba si kwamba Wizara hii haitambuliki au haifai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa Kanuni, Spika au Wasaidizi wake wakisimama, wewe lazima uketi. Taarifa imepokelewa kwa wale uliokusudia waipate.

Naomba nitoe Mwongozo katika suala la Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Godbless Lema. Ni kweli kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a) na (g), haturuhusiwi kutoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli lakini pia haturuhusiwi kutumia lugha ya kuudhi. Mwongozo wangu ni kuwa suala hili liko Mahakamani kwa hiyo hatutakiwi kulizungumza hapa. Kama kuna mtu ametuhumiwa au amehusika, Mahakama itatupa matokeo yake. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

*(Saa. 6.58 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na hoja yetu. Naomba niwataje watakaochangia. Tutaanza na Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi wajiandae.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia machache katika hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa ili nami niweze kuchangia machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nianze kuongelea suala zima la watoto wa mitaani. Sipendi kuwaita watoto wa mitaani kwa sababu tunaamini watoto wote wana wazazi, wana baba, wana mama, kwa hiyo siyo watoto wa mitaani, ni watoto ambao wanaombaomba mitaani. Japokuwa kuna Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na Sheria ya Ndoa, lakini, bado tatizo hili la watoto wanaoombaomba mitaani linaongezeka. Natambua kuna changamoto nyingi ambazo zinasababisha watoto wengi waendelee kuingia mitaani kama ile ya umaskini wa kipato kwa wazazi, kwa familia zao, mimba za utotoni, tatizo la wazazi kutengana na hivyo watoto wengi wamekuwa hawapati zile huduma sahihi kutoka kwa wazazi wao kwa hiyo wanaamua kuingia mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumezuka tatizo lingine jipya ambapo kuna wazazi ambao wanawatumia kwa makusudi watoto kuomba mitaani, kuomba katika barabara zetu hasa katika Majiji kama Jiji la Dar es Salaam na Mwanza, wao wakiwa

wamekaa pembeni, watoto wanaomba barabarani. Sasa mimi najiuliza, je, hii Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inatekelezwa vipi? Kwa sababu tunaamini kwamba wazazi wote wanatakiwa watambue wajibu wao kwa kulea watoto wao, ni haki ya mtoto kupata elimu, ni haki ya mtoto kupata malezi bora kutoka kwa mzazi. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze, je, Wizara ina mkakati gani wa muda mfupi wa kuhakikisha kwamba wazazi hawa ambao kwa makusudi wanasababisha watoto wetu waendelee kuongezeka kwa wingi mitaani wakiwa wanaomba wakati wao ndio wanapaswa kutoa malezi yote kwa watoto hawa na watoto hawa wapate haki ya elimu na haki zote ambazo zinategemewa, lakini bado wanaendelea kuwatumia watoto hawa kama sehemu ya mtaji wa wao kupatia pesa? Je, Wizara ina mkakati gani wa muda mfupi hasa kwa wazazi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niongelee suala la Vyuo vya Maendeleo. Tunatambua kwamba vyuo hivi ni muhimu sana hasa katika maeneo ambayo yako Vijijini katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, kuna Chuo cha Maendeleo. Chuo hiki ni cha siku nyingi sana, zamani kilikuwa kinachukua wanafunzi vizuri, lakini kwa sasa hivi chuo hiki kinachukua wanafunzi 70 tu kutokana na ufinyu au uhaba wa majengo hasa katika mabweni na vitu vingine. Pia chuo hiki kinakumbwa na changamoto nyingi kama vile ya ukosefu wa Walimu, vitendea kazi, vifaa vya kufundishia na vifaa vinginevyo, sasa na bajeti kila siku inazidi kupungua, imetoka bilioni 19 na sasa iko bilioni 16. Je, kwa jinsi gani tunaweza kuboresha vyuo vyetu vya maendeleo? Kwa sababu ukiangalia kwa sasa hivi, kwa mfano katika Wilaya yangu ya Rufiji, zaidi ya watoto asilimia 60 waliomaliza Kidato cha Nne wameshindwa kufanya vizuri katika masomo yao lakini pia kuna watoto wa Darasa la Saba ambao nao pia wameshindwa kupata nafasi ya kujiunga katika elimu ya sekondari, je, watoto hawa tunawasaidiaje? Kama kungekuwa kuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, watoto hawa tungeweza kuwachukua hapo, wakapata ufundi ambao sasa ungewawezesha wao kujiajiri wenyewe na kuacha kuwa wavuta bangi mitaani, wanavuta unga na kuacha kuingia kwenye makundi ya vitendo vichafu. Naiomba Serikali iangalie sana bajeti ya Wizara hii kwa sababu tunasema hii ni Wizara mtambuka ambayo inachukua watu wengi zaidi na hasa ukizingatia hali ya sasa ya vijana wetu ili waweze kupata ufundi stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na waweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia mambo ya Mfuko wa Wanawake *(WDF)*. Mfuko wa *WDF*, tunatambua ni mfuko ambao upo katika Halmashauri zetu ambao upo kwa ajili ya kutoa mikopo yenye riba nafuu au tuseme isiyokuwa na riba kabisa kwa akina mama lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana ya Mfuko huu hasa katika kuwafikia walengwa kwa maana kwamba kiasi kinachotengwa kwenda kwenye mfuko huu katika Halmashauri zetu ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010, Serikali au Wizara ilifanikiwa kupeleka milioni 220 tu kwenye Halmashauri za Wilaya 30 ambazo zilifanikiwa kurejesha mikopo. Katika hotuba ya leo ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 26, tunaona kwamba mpaka ikifikia Aprili, 2011 jumla ya shilingi milioni 128 zimepelekwa katika Wilaya 16 ambazo zimefanikiwa kurudisha marejesho. Sasa tunavyosema kwamba tunataka kumkwamua mwanamke hasa yule aliye Kijijini, hapa mimi naona bado kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa sana kwa sababu tunajua kwamba wanawake wengi wa Vijijini ndiyo ambao hasa wanachukua majukumu makubwa katika kulea familia. Sisi sote tunaamini kwamba ukimwezesha mwanamke, basi ndiyo familia nzima umeikomboa, familia nzima umeiwezesha. Sasa, kwa pesa hii, ukigawanya, unaweza ukapata kama milioni nane kwa kila Halmashauri. Sasa milioni nane katika Halmashauri, ukiangalia kama Wilaya ya Rufiji jiografia ilivyo yake, ukianzia kule Utete, Mloka mpaka ufike huko *Delta*, milioni nane itagawanywa katika vikundi vingapi? Kwa hiyo, utakuta vikundi vingi vinakosa pesa, akina mama ambao ilitakiwa wapate pesa ambayo ina riba nafuu wanaikosa ambayo ingewawezesha akina mama hao kujikwamua kiuchumi na pia kukwamua familia zao kwa sababu mama ndiye nguzo ya familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai hapa, hasa kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenye jinsia ya (Me). Wanawake wa Tanzania sasa hivi wametambua kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa jinsia ya (Me) huwa wanawatumia wao wakati wa uchaguzi kama madaraja kupata uongozi baadaye huwabwaga kabisa. Wanawatumia kwa maneno mazuri sana kwamba nitawawesha, nitawaletea pesa na vitu vingi tu lakini baada ya hapo hawawatendei hicho ambacho wanasema, wamekuwa wanawarubuni lakini kama vile haitoshi wamekuwa wanawabeza na kuwaletea kejeli akina mama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanawake wa Tanzania wamenituma niwasemee kwamba wamewashtukia. Mwaka 2015 watapiga kura nyingi kwa wanawake wenzao wahakikishe kwamba wanaingia wengi kwenye Bunge hili ili waweze kuwatetea kama ambavyo wanaamini kwamba mwanamke ndiye mtetezi wa kwanza kabisa wa familia. Kwa hiyo, wamesema kwamba hawatapiga tena kura 2015 kuwapigia hao wanaume ambao wanawabeza kwa sababu wanaamini wanawake tunaweza. Kama mnavyoona tunaweza, tuna Spika mwanamke ambaye anamudu Kiti chake vizuri, hatetereki. Kwa hiyo, wanawake tunaweza, mwaka 2015 jiandaeni, tutakuwa wengi sana kwenye ukumbi huu kwa kupitia kwenye Majimbo na hivyo Viti Maalum ambavyo Mheshimiwa Rais anaviongeza kwa kasi. Kwa hiyo, nawapa rai wajue kwamba mwaka 2015 patachimbika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka niongelee kidogo suala la bajeti kuandaliwa kwa kuangalia jinsia. Natambua kwamba Wizara inafanya juhudi kubwa sana kuhakikisha kwamba bajeti zitaandaliwa kwa kuangalia jinsia zetu lakini bado kuna changamoto kubwa sana. Sera ya Wanawake ya mwaka 2000 inaonesha wazi kwamba asilimia 60 ya akina mama wa kule vijijini kwetu ni wazalishaji wakuu hasa katika chakula. Kwa hiyo, mimi naomba bajeti zote ziangalie vizuri sana akina mama kwa sababu akina mama ndiyo tegemeo la familia zetu, akina mama ndiyo ambao wanaweza kutunza vizuri familia zetu, naomba kabisa mgawanyo wa rasilimali wa nchi yetu uangalie sana jinsia kwa sababu jinsia ndiyo kitu muhimu hasa ukiangalia kwa akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hiyo *WDF*, napenda niongezee kitu kidogo hapa. Kumekuwa na malalamiko mengi sana katika huu Mfuko wa Maendeleo wa

Wanawake, akina mama wengi wanadai kwamba Mfuko huu unatoa mikopo yake kwa kuangalia itikadi za kisiasa. Mimi naomba Mheshimiwa Naibu Waziri au Mheshimiwa Waziri anapokuja kufanya majumuisho atueleze hapa kwa wazi kabisa kwamba, je, ni kweli mikopo katika Mfuko wa *WDF* inatolewa kwa kuangalia itikadi za kisiasa? Ndio maana inakwamishwa katika marejesho, marejesho yanakuwa machache kwa sababu wanaopewa mikopo wanashindwa kufuatiliwa kwa kuangalia itikadi zao za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanashindwa kufanya kazi vizuri, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii tunawabana katika kufuatilia marejesho ya mikopo yetu. Pia Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa wanakuwa na fedha chache sana za kuwawezesha kufuatilia marejesho hasa katika sehemu za mbali. Utakuta Wilaya iko mbali, kuna vijiji viko kilomita zaidi ya 160/170. Afisa Maendeleo ya Jamii hana pesa ya kutosha, fungu lake halitoshi, kwa hiyo anashindwa kufuatilia mikopo kwa ufasaha. Kwa hiyo, marejesho yanakwama, kwa hiyo akina mama wengi wanakosa mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru sana. Unaunga mkono hoja?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa hii nafasi na moja kwa moja napenda kuanza kuchangia kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Teresa wakati anapewa *Nobel Peace Prize* aliulizwa na Waandishi wa Habari kwamba tufanye kitu gani ili Dunia iweze kuwa mahali salama pa kuishi? Mama Teresa alijibu, akawaambia Waandishi wa Habari; *"go home and love your family"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza michango, ukazipitia hotuba zote pamoja na hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani na hotuba ya Serikali una-*realise* kwamba kimsingi kuna mambo mengi sana ya maana yanatakiwa yafanyike. Mimi mtazamo wangu kuhusu ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii, ni lazima kwanza kuwepo na mabadiliko ya fikra kutoka fikra hasi kwenda fikra chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mtazamo wa wananchi wengi wa Taifa letu, ukiangalia mtazamo wa viongozi wetu, ukiangalia maisha wanayoishi watu mitaani ambao ni wananchi wa Taifa hili, unaweza ukapata picha ya viongozi wanaoliongoza Taifa hili ni viongozi wa aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania wakati tunaanza kujitawala, mfumo wetu ulikuwa ni mfumo wa Ujamaa na Kujitegemea, wakati wenzetu Kenya mfumo wao ulikuwa ni mfumo wa Kibepari. Sasa, ukiangalia *attitude* ya mfumo wa Ujamaa na Kujitegemea ulikuwa ni mfumo ambao leo umejenga Taifa tulilonalo, Taifa lenye watu waoga, watu wasiotaka kujaribu na jamii ambayo haiko tayari ku-*dare* kwa mambo makubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia bajeti ya Wizara hii, ni *less than Tanzanian shilling five billion* (chini ya shilingi bilioni tano za Tanzania) lakini inaitwa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii. Unajiuliza kiwango kidogo cha pesa kama hiki kinastawisha jamii gani, zinaendeleza jamii gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Alhamis ya wiki iliyopita, kwenye Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu, nilimuuliza Waziri Mkuu swali kwamba ni kwa nini ajira ambazo Watanzania wangeweza kuzifanya, ajira hizo zinafanywa na watu mbalimbali kutoka Mataifa mengine wakati ajira hizo Watanzania wana *capacity* nazo. Waziri Mkuu alijibu vizuri, lakini baadaye akaongezea kwamba Watanzania pia ni wavivu na Watanzania wanapaswa kuwajibika lakini lazima kazi ya kiongozi ama kazi yetu sisi kama viongozi, wajibu wetu sasa ni kuangalia udhaifu huo na ku-*eliminate* sasa hizo *negative feeling* na *negative mentality* kwenda kwenye *positive mentality*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaingia kwenye ushindani wa soko la ajira wakati Afrika Mashariki tuko pamoja. Wakenya, Waganda, hawana uwezo mkubwa kwa sababu wana-*perform* vizuri *academically* ila wana uwezo mkubwa kwa sababu kuanzia mwanzo wakati wanajitawala wao *base* yao ilikuwa ni Ubepari na kwa hiyo walijifunza namna ya ku-*take risk*. Taifa letu haliwezi kubadilika kama viongozi hatutawajibika na viongozi tusipowajibika, maana yake wananchi hawawezi kuwajibika kwa sababu mtoto anajifunza kwa baba na siyo baba kwa mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajiuliza iko wapi *role of responsibility* ya viongozi wa nchi hii? Tunapigania maendeleo gani, tunapigania uwajibikaji gani kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu? Unaangalia *scandal* nyingi nyingi za rushwa kubwakubwa tena za hatari, lakini haoni watu wakiwa *responsible*. Kimsingi sisi tunasema wananchi hawawajibiki, lakini unajiuliza mbona sisi hatuwajibiki pale ambapo tulipaswa kuwajibika na tunasema wananchi hawawajibiki! Kuna haja ya kuanza sasa ku-*transform attitude* ya Watanzania. Nchi hii inaweza ikabaki ilivyo miaka 20 inayokuja kama fikra ya nchi yetu, watu wetu na viongozi sisi, tutaendelea kuwa kama tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakosa *solution* ya mambo mengi kwenye ustawi wa jamii yetu siyo kwa sababu hatuna pesa, siyo kwa sababu hatuna *resources*, ni kwa sababu hatujawa tayari kuwa *positive* kwenye mambo ya msingi na kuchukua *sacrifice* kwa ajili ya ukombozi wa nchi hii. Mimi ninaangalia, mfano pale Jimboni kwangu Arusha, unakwenda Hospitali ya Mount Meru, unakuta mwanamke mjamzito anajifungulia mtoto chini lakini kutoka Hospitali ya Mount Meru mpaka kufika ofisi ya Mbunge, ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ni chini ya mita 200, unakuta kuna viongozi ambao kama wangekuwa ni watu *sensitive*, ni watu *positive*, ni habari ya kuita wafanyabiashara usiku mmoja na kuchanga pesa za kununua vitanda na wale akina mama wakaanza kujifungulia watoto kwenye vitanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi sana hayatokei siyo kwa sababu nchi hii ni maskini. Nimeona wakati wa michango ya Mwenge kwa mfano, unaona *role* ya Mkuu wa Wilaya na watu wengine wanavyokuwa *serious* ku-*demand* mchango wa Mwenge, lakini inapofika kwenye masuala ya msingi, hauoni huo uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ambazo zimekuwa zikichangwa na wafanyabiashara mbalimbali kwa ajili ya kampeni za Wabunge mbalimbali tukiwemo sisi nchi hii, watu wakiingia kwenye mfumo huo huo wakaanza kuchangisha pesa kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii, tulikuwa hatuna sababu ya kumwacha Rais aende Marekani kuomba noti wakati tuna wafanyabiashara ambao wangeweza ku-*donate* chini ya shilingi elfu kumikumi tu na Taifa hili lingeweza kuondokana na mambo ya aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 – 2010, tulifanya utafiti na taasisi moja inaitwa *Positive Thinkers Network* na utafiti wetu ulibaini kwamba harusi, kipaimara na *sendoff* ambazo zinafanyika nchi hii kati ya miaka mitatu tu, vikao hivyohivyo na Kamati hizohizo zikakaa, zikaamua ku-*raise fund* kwa *style* hiyohiyo, pesa hizo zinaweza zikajenga Chuo kikubwa kuliko UDOM. Kwa hiyo, tatizo la ustawi wa jamii liko sana kwenye *attitude* kuliko ambavyo tunadhani. Leo hata ukiongeza fedha kwenye huu mfuko ukasema tunaipa hii Wizara shilingi bilioni 30, shilingi bilioni 50, bado unaweza ukashindwa ku-*achieve* kwa sababu wako watu wanapata pesa nchi hii, wako watu wanapata pesa nyingi kwenye madini, lakini siku ya mwisho wanakosea matumizi yao ya msingi kwa sababu hakujawepo na wajibu wa kutosha wa Serikali wa kuanza ku-*eliminate* watu *from negative mentality to positive mentality. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba huwezi kuibadilisha nchi bila kubadilisha mtazamo wa nchi. Leo mambo yote tunayoyapitia, ugumu wa maisha tunaoupitia ni kwa sababu ya *attitude* tulizonazo, *faculty* zote tunazoingia katika siasa ni kwa sababu ya *attitude*. Mimi nashauri, pamoja na mambo mengi ya msingi lakini sasa ni wajibu Wabunge tuanze kuwa kioo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kabla sijaja Bungeni niliambiwa Bunge la Bajeti huwa ni Bunge refu linakaa miezi mitatu, ni Bunge gumu sana, nikafikiri tukifika Bungeni tutakuwa *busy* kuanzia asubuhi mpaka jioni, lakini wafanyabiashara wa Dodoma wanakuambia kipindi ambacho wanapata wateja wengi wa pombe ni kipindi cha Bunge la Bajeti. Sasa unajiuliza hii *society* ambayo wao ni viongozi kama hawako *responsible*, kama sisi wenyewe tunatoka hapa saa saba, tunarudi hapa saa kumi na moja, tumepunguza hata muda wa kushika vifungu kutoka dakika tano kwenda dakika tatu, ili tuwahi kutoka Bungeni, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni maskini, muda mwingi unapaswa utumike katika kutumikia wananchi na ikiwezekana kubadilisha kabisa *mentality* za watu. Ili maendeleo ya Taifa hili na ustawi wa Taifa hili uweze kufanikiwa, kwanza kabisa ni lazima viongozi tuwe *responsible* kuanza kubadilisha mitazamo yetu ya jinsi tunavyoishi, ndipo tutakapowaambukiza wale tunaowaongoza, vinginevyo hatuwezi kuwa- *influence* watu wetu bidii, hatuwezi kuwa-*influence* watu wetu wawe na maendeleo wakati sisi wenyewe tupo *very irresponsible*. Kama hatutabadilisha mtazamo, pengine hata chama changu kikibahatisha kushika nchi na chama kingine pengine, lakini kwa mtazamo huu tulionao kama nchi, mtazamo ambao ni *negative perspective*, nchi hii inaweza ikachukua miaka mingi sana kubadilika. Naomba Wizara husika, pamoja na Serikali kwa ujumla, ione sasa umefika wakati wa kuanza ku-*address* mtazamo wa kifikra na kuanza

kuubadilisha, vinginevyo tukimaliza tatizo la umeme tutajikuta tuna tatizo la maji kwa sababu fikra ni zilezile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ustawi wa jamii ni pamoja na viongozi kuanza kuwajibika kwenye makosa kama ya rushwa na wizi. Humu ndani tuna watu wana kashfa za mabilioni ya pesa, tupo nao na bado tunaingia nao Bungeni, inaonekana ni kama kitu kidogo tu, sasa unamwambiaje mwananchi awe *responsible* wakati wewe kama kiongozi wa nchi, ama wewe kama Mbunge umeshindwa kumwajibisha mtu ambaye ana skendo ya wizi zaidi ya bilioni mia moja, bilioni mia mbili na amekuwa kama ngonjera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwataka wananchi wa nchi hii wawajibike, waache kuwa wavivu, waanze kufanya kazi, hiyo *influence* wataipata kutoka kwa viongozi na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina *comment*. *(Makofi)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama na kuweza kutoa mchango wangu jioni ya leo. Vilevile naomba nichukue nafasi hii kuwashukurru wananchi wa Tanzania na wanawake wa Tanzania kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ndani ya Bunge na nje ya Bunge, nawaambia wananchi na wanawake wa Tanzania kwamba sijawaangusha maana imani huzaa imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri Sophia Simba, Naibu Waziri, Ummy Mwalimu na Katibu Mkuu Mama Kijakazi na wote walioandaa bajeti hii muhimu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nawapongeza sana kwa sababu wameandaa vizuri sana randama ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kuchangia maeneo machache kama matano hivi ambayo nimeyachagua kuyatilia mkazo. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kueleza wasiwasi wangu kwamba bajeti hii ni ndogo sana na naomba niungane na Wabunge wenzangu waliotoa masikitiko yao kwamba bajeti hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara mtambuka, Wizara ambayo inasimamia shughuli zote za maendeleo na kuhamasisha maendeleo ya nchi hii, kwa kweli bajeti hii ni ndogo sana ukilinganisha na bajeti za Wizara nyingine. Kama ambavyo Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yetu, naiomba Serikali yetu Tukufu iangalie kwa macho ya huruma hasa ukizingatia kwamba jungu kuu halikosi ukoko, itazame namna ambavyo inaweza ikaisaidia Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake hasa katika lile Fungu la maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina Vyuo vya Wananchi zaidi ya 55, ina Vyuo vya Maendeleo ya Jamii tisa (9) na vyuo hivi mimi nimevitembelea, vina changamoto nyingi sana. Vyuo hivi ndivyo vinayotusaidia hata kuwaandaa vijana wetu wanaoshindwa kuendelea na masomo, ndiyo vyuo pekee vinavyowapokea vijana wa darasa la saba, vinawaandaa ili wakitoka hapa waende kujitegemea. Vyuo hivi tisa (9) ndivyo vinavyotoa wataalamu wetu, unapozungumzia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, kuna baadhi ya watu wanabeza na mimi nimekuwa nikisikitika sana, jinsi unavyoona bajeti hapa ilivyo finyu hata kule kwenye Halmashauri zetu siku zote Wizara ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikiwekwa nyuma lakini huwezi ukasema Kilimo Kwanza, huwezi ukasema kuhamasisha suala la chanjo za watoto, huwezi kuzungumza suala la kupunguza vifo vya wananwake na watoto kama hujagusa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani Serikali yetu ni sikivu, Serikali inatambua umuhimu wa Wizara hii, kwa sababu nakumbuka hata historia ya kuanzisha Wizara hii, akina Bibi Titi Mohamed wakishirikiana na Mheshimiwa Mama Sophia Kawawa na Waasisi wengine walikaa kabisa kwenye vikao vya Kikatiba vya Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) waliidai Wizara hii kwa nguvu, waliuza mali zao, walitembea kwa miguu, walijenga hoja kwa Serikali yetu Tukufu ikakubali kutupatia Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yetu. Kwa hiyo, naomba sana kama ambavyo Serikali ilidhamiria kuunda Wizara hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na wanawake, naomba tena katika mwaka wa fedha unaokuja tuangalie Wizara hii kwa macho ya huruma sana, kwa sababu Wizara hii ni Wizara mtambuka. Naomba nipingane na wale wote wanaofikiria kwamba Wizara hii ni ya wanawake peke yao na nawaomba sana akina baba, vijana na wananchi wote wajue kwamba Wizara hii ni yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee kuhusu Benki ya Wanawake, naomba pia nirudi kwenye historia kuwashukuru sana viongozi wa nchi hii ambao walifanya kazi kubwa sana tangu enzi za Mama Sophia Kawawa na baadaye akina Mama Anna Abdallah na mimi nikiwa Mjumbe, tulikaa na kudhamiria tukachangishana fedha, mimi nakumbuka kwa mara ya kwanza nilichangia shilingi mia moja na kikao kilichofuata nilichangia shilingi elfu moja tukiwa tunadai kupata Benki yetu ya Wanawake. Serikali yetu sikivu ikatusikia, mwaka 2009 Julai Benki yetu ikaanza rasmi. Serikali yetu Tukufu ikatuanzishia na mtaji wa shilingi bilioni mbili. Naipongeza sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akaonesha dhamira na kuahidi kwamba kila mwaka wa fedha Serikali itatenga shilingi bilioni mbili kila mwaka, kipindi cha miaka mitano (5) kwa ajili ya kuisaidia benki hii mtaji ili iweze kukua na iweze kutoa huduma mpaka vijijini kama ambavyo misingi yake ilivyo. Naomba nipongeze sana kuona katika bajeti ya mwaka huu pia wameendeleea kutenga shilingi bilioni mbili, nauunga mkono kabisa uamuzi huo mzuri sana kwa maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa isichanganye fedha za Benki ya Wanawake na Fungu la Mfuko wa Maendeleo ya Wizara hii. Kwa sababu ukiangalia pamoja na dhamira hii nzuri lakini fedha zote zimekwenda kwenye Benki ya Wanawake, fedha za maendeleo ukitazama kwenye vitabu vya maendeleo hapa ni kidogo sana

ukilinganisha na changamoto zilizopo kwenye Wizara. Naiomba Serikali yetu Tukufu iwe inatenga fedha hizi moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina badala ya kuwa inapitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto, kwa sababu Wizara hii haihudumii wanawake peke yao, hii ni benki ya Wizara zote na watu wote, tena siyo wanawake peke yao ni Benki pia ya wanaume na hata ukiangalia benki wakati inaanza ilikuwa na wateja wachache sana, sasa hivi wateja wa benki ile wameshafikia karibu elfu kumi na sita, katika wanachama wale wanaume wapo elfu tatu na wanawake zaidi ya elfu kumi na mbili. Naomba niombe Serikali yetu iendelee kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuiwezesha benki hii, badala ya bilioni mbili kila mwaka iongeze zaidi pesa ili Benki yetu iweze kutoa huduma zaidi na ikiwezekana kila Wilaya tuwe na tawi na kusaidia Benki kumudu shughuli zake za uedeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la pili, naomba kutoa wito kwa wafanyabiashara na wakulima na wafanyakazi wa nchi hii, twende tukafungue akaunti katika Benki yetu ya Wanawake. Ni benki inayojali wateja, ni benki iliyo tayari, ni benki ambayo imeonesha mwanga, naomba sana Wabunge twende tuoneshe mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye suala la mimba za utotoni. Nimekuwa nikisikiliza mijadala mbalimbali ya Wabunge na baadhi ya wadau wakizungumza kwamba mimba za utotoni zimekuwa zikisababishwa eti na shule zetu tulizojenga kila Kata kwa vile hazina mabweni. Mimi nataka kusema kwamba sababu hiyo siyo ya kweli, kwa sababu wakati akina Mama Anne Makinda, akina Anne Abdallah na hata mimi mwenyewe tulikuwa tunatembea kilomita nyingi na huko njiani walikuwepo mafataki tulikuwa tunakutana nao barabarani lakini kwa sababu Wazazi walikuwa na utaratibu wa kusema na watoto wao hasa watoto wa kike hapakuwa na mimba kwa wakati ule. Leo tunasingizia shule za Kata ndiyo zinasababisha mimba kwa sababu hakuna hostel, hii siyo kweli kwa sababu shule hizi zimesaidia sana kupunguza mimba na ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeona nizungumze kabisa kwa uchungu na hapa nitoe rai kwa jamii nzima ya Watanzania na hasa sisi akina mama kurejesha maadili kwa watoto wetu, tuzungumze na watoto wetu, tuseme nao na kuwataka kusubiri. Kuna makabila ya nchi hii yana maadili mema ya kulea familia. Mimi nakumbuka wakati nakua mzazi wangu alikuwa anasema soma mpaka ufike Chuo Kikuu na ukimaliza Chuo Kikuu utamchagua mume unayemtaka na utakuwa na maisha mema, hayo maadili yamekwenda wapi? Mimba za utotoni tusiiachie Serikali yetu peke yake, tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha tunarejesha maadili kwa familia yetu, tunazungumza nao, tofauti na sasa ambapo tumeacha watoto wakitoka shule wanaingia kwenye televisheni, anacheza *game*, anachoangalia huko hujui, mwisho unabaki kuilaumu Serikali kwa ujenzi wa Shule za Kata, naomba hapa tujitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa kuhusu sheria zinazokandamiza na kuwanyanyasa wanawake na watoto, Sheria ya mwaka 1971. Sheria hii si Sheria nzuri, imetoa mwanya kuruhusu watoto wetu wa kike wadogo chini ya umri wa miaka kumi na nane kuolewa. Hii ni hatari sana hata kwa usalama wao. Miongoni mwa sababu zinazosababisha wanawake kufa wakati wa kujifungua ni pamoja na sababu

hii ya watoto kuolewa wakiwa bado wadogo, kwa sababu unakuta mtoto anakuwa hana uwezo wa kuhimili vishindo vya ndoa, hana uwezo wa kuhimili kubeba mimba matokeo yake wamekuwa wakifariki. Naomba utaratibu wa kurekebisha Sheria hii uharakishwe ili Sheria mpya nzuri itengenezwe na Sheria hii ya kusema watoto wanaolewa kabla ya umri iweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mirathi pia itazamwe upya, akina mama wajane, watoto yatima wanadhulumiwa sana na watu wasiokuwa na maadili. Kuna baadhi ya makabila inapoteka msiba kwao ni faraja, akina mama walioachwa na waume zao wanateseka na watoto wao. Tuiangalie Sheria hii na hasa zile Sheria za Kimila, kuna baadhi ya makabila yanawakandamiza akina mama wajane na watoto wanaofiwa na waume zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii angalau nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafuatilia kwa karibu sana kuanzia hotuba ya Waziri baadaye taarifa ya Kamati ya Wizara husika, pamoja na michango inayoendelea ya Waheshimiwa Wabunge. Ni ukweli usiopingika tukianza na Kamati wanasema kwamba pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wizara hii hazitoshi kabisa, lakini cha kushangaza Kamati inaunga mkono hoja, sasa nashindwa kuelewa kama uungaji mkono wa hoja ni *fashion* au tunatakiwa kuunga mkono hoja kwa sababu ya uhalisia wa masuala yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeweza kuongea, matatizo ya Wizara hii ni makubwa na kwa sababu matatizo ya Wizara hii ni makubwa, ni kweli tunatakiwa sisi kama Wabunge tuweze kuyabeba kwa ujumla wake kwa ajili ya kuweza kuisaidia Wizara hii pamoja na walengwa katika Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikifuatilia kwa mfano katika hotuba ya Waziri, page ya 53, ambayo ilikuwa inajaribu kuainisha asilimia ya wanawake ambao wanashika nyadhifa mbalimbali katika Idara za Serikali, Bunge na sehemu nyingine muhimu. Hii inaonesha kwamba wanawake bado wako nyuma katika nafasi muhimu za kuongoza nchi hii ukilinganisha na nafasi za wanaume. Naamini kwamba wanawake wanaweza lakini labda wakiondoa ile kauli ya kwamba wanaweza wakiwezeshwa. Kama wanawake wanaweza wao wenyewe, mimi naamini kwamba kuna haja kubwa kabisa ya kuweza kuwafanya akina mama zetu, Wabunge wetu wanawake pamoja na jamii nzima, waweze kujikwamua na waweze kuonekana kwamba kweli wana uwezo mkubwa katika Taifa hili. Ukiangalia pia mchango wa wanawake hata ukiangalia taarifa mbalimbali za kiuchumi, wanawake wanachangia kwa kiasi kikubwa sana katika pato la Taifa ukilinganisha na wanaume wanavyochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ambazo Wizara inaziandaa kwa ajili ya kwenda kwenye Benki ya Wanawake, sina matatizo na kiwango ambacho Wizara ina-*propose*, lakini pia kama Wizara itaamua kuweka nguvu zaidi katika Benki ya Wanawake peke yake, tukaacha taasisi zingine ambazo zinatoa mikopo vijijini na misaada mingi sana kwa wanawake, Wizara hii itakuwa inakosea. Taasisi kama *FINCA, PRIDE AFRICA, BRAC,* hizi ni taasisi ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa sana katika mikopo kwa ajili ya wanawake ambao wanataka kuendeleza biashara zao ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kuona kwamba kuna umuhimu sasa wa kuziangalia Taasisi hizi kwa sababu hata riba inayotolewa na hizi Taasisi ni kubwa sana. Kama mama anakwenda kukopa mkopo ambayo riba yake ni asilimi 24, sidhani kama kweli tunawasaidia hawa akina mama au tunawaangamiza. Naiomba Wizara iweze kuliona suala hilo, ione kwamba ni suala ambalo ni muhimu sana ili basi tuzisaidie hizi Taasisi na kama kuna uwezekano riba ziweze kushuka, ziwe za chini ili katika marejesho ambayo akina mama wanafanya yasiwe ni kero bali yawe na tija ili waweze kujisaidia katika kujipatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kipengele kingine cha ubaguzi katika utoaji wa uraia kwa wanandoa. Hili limekuwa tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Inatokea kwamba mwanaume anapoamua kuoa mtu ambaye siyo Mtanzania na yule mwanaume akaja na yule mama hapa Tanzania, Wizara pamoja na Taasisi zote zinazohusika hazioni kuwa na tatizo la kutoa vibali vya kufanya kazi na uraia kwa huyu mama ambaye ameolewa Tanzania lakini inapokuja kinyume chake, inatokea mwanamke sasa ameamua kuolewa na mwanaume ambaye siyo Mtanzania, tatizo ndio hapo sasa linapoanzia. Ili tu kupata *passport* lazima kwanza awe ameshakaa si chini ya miaka mitano ndani ya Tanzania ili waweze kuishi hapa na kufanya kazi kwa amani lakini pia lazima awe ameshakaa siyo chini ya miezi 12 kabla ya kuomba *passport* yenyewe ili aweze kukaa hapa na kuendelea na shughuli zake. Mimi naiomba Wizara hii husika ikishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria waweze kuifanyia marekebisho sheria hii mapema ili basi nao akina mama waweze kujiona ni nafasi ya jamii ndani ya Tanzania kwa Utanzania wao walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kuongelea *NGO's*. Katika *NGO's* hizi, napenda kuiongelea *NGO* ya (*THT)-Tanzania House of Talents.* Wizara hii ndio Wizara yenye dhamana ya kusajili *NGOs* zote ndani ya nchi ya Tanzania lakini kwa bahati mbaya sana, *Tanzania House of Talents* wakati inaanzishwa ilikuwa na malengo ya kusaidia watoto yatima ili kuweza kujiendeleza katika fani ya muziki na usanii ndani ya nchi ya Tanzania. Kwa bahati mbaya sana, napenda pia labda kama Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana husika ataliambia Bunge lako Tukufu, pamoja na Watanzania kwa ujumla kama Taasisi hii ya *THT* ilishabadilika na kuwa kampuni. Kwa sababu kazi ambazo ilikuwa izifanye wakati *THT* inaanza na malengo ambayo sasa hivi *THT* inafanya, yamekuwa ni tofauti kabisa. Sasa hivi imekuwa inafanya kazi kibiashara, inatumia wasanii wetu ambao ni vijana, ambao bado wana nguvu, ambao wanakubalika katika jamii hii, wanawafanyisha kazi kwa ujira mdogo tofauti na mapato ambayo *THT* inapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wetu hawa wanapokwenda *Tanzania House of Talents,* lengo lao ni kwenda kutimiza ndoto yao kwamba siku moja nao waweze kuwa ni wasanii wakubwa ndani ya Tanzania, waweze kusifika mpaka nje ya Tanzania lakini matokeo yake na kwa ushahidi uliopo, wasanii wetu hawa ambao wengi wao ni akina dada wanaishia kupata mimba na kupangishiwa katika nyumba za uswahili ambalo siyo lengo lao na makusudio yao kufika katika Taasisi hii. Naomba Wizara inayohusika basi iweze kuliambia Bunge lako Tukufu kama ambavyo nimesema hapo awali iweze kutueleza kama *THT* ni kampuni na kama siyo kampuni basi iweze kurudi kwenye malengo ya awali ambayo ndio iliyosababisha usajili wake, vinginevyo tunapoteza fedha nyingi sana ambazo hazilipwi *TRA*, hazilipwi katika maeneo ambayo ni ya msingi ambayo yangeweza kusaidia katika matatizo haya tuliyonayo kwa sababu malengo yake yamebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo na kwa vile mimi huwa si mrudiaji kwa yale ambayo yameshasemwa, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika kuwaletea Watanzania maendeleo wakiwemo wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, niende kwenye suala la Benki ya Wanawake, wenzangu wote wamechangia kuhusiana na fedha kidogo ambazo zinatengwa lakini napongeza Serikali kwa kuwa na utaratibu wa kuongezea mtaji. Napenda huu mtaji uongezwe na pia wanawake wapewe huko vijijini mikopo hii kupitia kwenye *SACCOS* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuona wanawake wa Mkoa wa Iringa, ambao ndio Mkoa mmojawapo wa wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula, wapate mikopo hii kupitia kwenye *SACCOS* zao kwa fedha hizi zilizotolewa msimu huu. Nina uhakika Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ni mpenda maendeleo ya wanawake na wananchi kwa ujumla, atalitilia umuhimu na kulipa uzito unaostahili kwamba Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ambako ndiko tunakotegemea kilimo kikubwa cha mazao ya chakula, wapewe mikopo ili waweze kuzalisha chakula cha kutosha ambapo wanaweza kulisha Mikoa ya Dar es Salaam ambap hao ndio wanaopata mikopo hii kwa wingi. Tuigawe kwa usawa ili wale tulioko vijijini pia tuone umuhimu wa benki hii kwamba imeanzishwa kuwakomboa wanawake na Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa suala la ukatili au unyanyasaji wa kijinsia. Wenzangu wamelizungumzia, kila mwaka, kila siku kuna matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake au kwa watoto. Uliwekwa utaratibu kwamba kama ni watoto wananyanyaswa zipigwe simu ili watoto waweze kusaidiwa. Sasa sielewi ni watoto wangapi wameshasaidiwa katika mpango huu ambao

umeelekezwa kwamba wawe wanapiga simu? Watoto wananyanyasika, wanawake wananyanyasika, naiomba Wizara kwa kupitia ile *program* ambayo imezinduliwa mwaka huu na Waziri Mkuu akiwepo Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, uweze kutekelezwa kwenda huko ngazi za chini ili kupunguza unyanyasaji wa kijinsia ambao umepelekea wanawake wengi pia na watoto kuambukizwa virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasikiliza mazungumzo yaliyoendelea humu, nilisikia kulikuwa kunatolewa taarifa humu na ikaelezwa kwamba Wizara hii imeelekezwa pia kufanya masuala ya UKIMWI ambayo siyo ya kwao. Nimesononeka na hilo, mimi nilifikiri kwamba Wabunge wote tunaelewa kwamba mzigo mkubwa wa tatizo la UKIMWI umemuelemea mwanamke. Nilikuwa nategemea kwamba wanawake wanaochangia, baadhi yao walisema hii Wizara imepewa kipengele hicho siyo mahali pake, wangesisitiza kwamba Wizara hii iongezewe fedha ili wanawake waweze kufikiwa, watoto wa kike wapewe elimu, hivi ni watoto wangapi wa kike ambao wanaumia kila siku na tatizo hili? Labda aliyekuwa anaeleza suala hili alipitiwa tu akasahau, napenda kusema kwamba umuhimu wa kwanza Wizara hii ilitakiwa iongezewa fedha ili iweze kutos elimu kwa kila mtu kwa sababu hii Wizara ndio Wizara ambayo imepewa kazi ya uratibu wa masuala ya UKIMWI kwenye Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, inatakiwa hii Wizara iwe na wataalam wa kutosha ili elimu iweze kumfikia kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Tumeelezwa kwamba ni asilimia 56 tu ya Kata zote hapa nchini ambazo zina wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Kuna upungufu wa wataalam 1213 sawa na asilimia 44 ya Kata zote hapa nchini hazina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kwa maana hiyo, Kata hizo pia maendeleo yao yako chini kwa sababu anayetegemewa kuhamasisha, anayetegemewa kutoa elimu mbalimbali ni Afisa Maendeleo ya Jamii akisaidiana na wataalam wenzake wa Ugani kwenye Kata zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kama Vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii vimefundisha Maafisa Maendeleo ya Jamii, waliomaliza cheti wengine wanasoma katika Chuo cha Ruaha pale Iringa, naelewa kwamba wapo pia waliomaliza Diploma lakini hawana ajira, kwa nini hatujaajiri kuziba huu upungufu mkubwa ili tuhakikishe kwamba maendeleo yanafika kwa wananchi? Kwa hiyo, nashauri Serikali iwaajiri Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wale ambao wamemaliza vyuo na hawana ajira wakati kuna upungufu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la miradi ya wanawake. Mkoa wa Iringa ni moja ya Mikoa ambayo tunatengeneza vikapu vya asili, tunatengeneza vyungu ambavyo havipatikani kokote, kwa mfano, pale Lungemba wanawake wengi ndio wanaofanya miradi hii pale barabarani, wanafanyia shughuli zao juani. Mheshimiwa Waziri naomba wajengewe jengo/soko pale barabarani ili wasinyeshewe mvua, ili wasikae juani na waweze kupata soko la uhakika, pale ni barabarani. Naomba tushirikiane na Taasisi nyingine ili kuwajengea soko hawa akina mama. Mheshimiwa Waziri, pale barabarani tunapita na tunawaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi za Mkoa wa Iringa akina mama wanatengeneza vikapu lakini vikapu hivi vinanunuliwa na wafanyabiashara wanakwenda kuviongezea thamani, wanauza kwa bei kubwa, akina mama wao wanaambulia kupata fedha kidogo. Tunaomba wapewe utaalam waweze kujiunga kwenye vikundi na wako kwenye vikundi vyao na Wizara iwatafutie masoko ili wao pia wafaidike na kazi ambayo wanaifanya, kazi ya mikono ambayo ni kazi ya asili na ni kazi muhimu sana. Ukienda kila sehemu mpaka nje ya nchi unaona watu wana vikapu vya Iringa, haviko sehemu nyingine lakini hawa akina mama hawajafaidika na kazi ya mikono yao, tunataka wafaidike na kazi ya mikono yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Naomba kuchukua nafasi hii kupongeza kazi nzuri na kubwa inayofanywa na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Naishukuru Serikali kwa kuwa na uamuzi wa kuwa na vyuo hivi. Vyuo hivi kama wenzangu walivyosema vinafanya kazi kubwa sana. Napenda nichukue nafasi hii kupongeza Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Njombe. Chuo hiki kimefanya kazi kubwa sana. Nampongeza Mkuu wa Chuo hiki amefanya kazi kubwa sana kushirikiana na Taasisi ya Uchumi wa Nyumbani *(Tanzania Home Economic Association)* kufundisha masomo ya ufundi watoto yatima wa Wilaya ya Makete, Wilaya ya Mufindi, Wilaya ya Iringa Vijijini, sasa wanaweza kujitegemea. Chuo hiki kiendelezwe na kipewe mtaji, majengo mengine yamechakaa, pia kiweze kupata usafiri wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanafunzi wakishamaliza mafunzo yao basi wasaidiwe kupata mitaji ili waweze kujitegemea. Watoto wengi ni yatima na watoto hawa pia wanatoka katika mazingira magumu, mafunzo wanayoyapata basi waweze kupata mitaji. Pia tenda zinazotolewa vijijini kwa mfano za ujenzi wa shule na vitu vingine na wenyewe wafikiriwe ili waweze kujitegemea na kulisha familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba. Niliwahi kuomba hapa Bungeni, nikiomba Wizara ya Nishati na Madini, wawasaidie umeme kile Chuo ni Chuo cha Historia, kiliachwa wakati ule wa enzi wa ukoloni, kilikabidhiwa ili kiweze kutoa mafunzo kwa wanawake na sasa hivi tunashukuru kwamba Serikali imekiendeleza kinatoa Diploma, tunaomba umeme wa uhakika kwenye chuo kile. Chuo kile kipate umeme wa *grid* ya taifa ili kiweze kusaidia kijiji kizima na wale wote akina mama wanaotengeneza vyungu watakuwa wamefaidika kupata umeme kutoka pale. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, tafadhali uende ukakione kile chuo na kipewe umeme wa uhakika badala ya kutegemea umeme wa jenereta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wizara kwa kuweza kuweka Dirisha la Habari kwenye vituo mbalimbali kikiwemo Chuo cha Lungemba, mimi napongeza hilo lakini nashauri hivi vituo vya habari viwekwe kwenye Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Mkoa ili wananchi wengi wakiwemo wanawake waweze kufaidika. Kwa mfano, kama ukiweka kwenye chuo peke yake ni wale wanaotembelea pale chuoni ndio wanaweza kupata hizo habari lakini kama kingewekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya au kwenye Makao Makuu ya Mkoa ina maana kwamba wananchi wengi wangeweza kupata habari kupitia vituo hivi. Hii ni hatua ya kwanza lakini naomba

Wilaya zote za Mkoa wa Iringa ikiwemo Makao Makuu Mafinga, pale wapate, Wilaya ya Kilolo wapate, Wilaya ya Iringa Vijijini pia wapate hata Njombe ili kuweze kuwa ni mahali ambako ni kitovu cha habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi na teknolojia. Naomba utumike utaratibu wa simu, sasa hivi wananchi wengi wana simu wakiwepo wanawake vijijini. Tunaomba Wizara ishirikiane na Makampuni ya Simu kuweza kutuma ujumbe wa elimu kupitia njia za simu kwa sababu simu zimesajiliwa kila mtu anajulikana namba yake ni ipi ili taarifa hii iweze kufika mpaka vijijini, ni njia mojawapo tu kwa sababu simu zinafika mpaka vijijini. Napongeza kabisa Serikali kwa kuwa na mitandao ya simu na wanawake pia wengi wana simu hata ambao hawana simu wanaweza kupata ujumbe kupitia kwa akina mama wenzao. Njia hii inaweza kutumika kutoa elimu ya afya, lishe, uzazi salama na mazingira. Hebu tubuni njia nyingine kwa kutumia sayansi na teknolojia kwa sababu Siku ya Wanawake Duniani ilikuwa na ujumbe huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Siku ya Wanawake Duniani, tunatimiza miaka 50 ya Uhuru na humu ndani Wabunge walikuwa wanaelezea jinsi ambavyo wanawake wameshiriki katika harakati za uhuru na maendeleo kwa ujumla. Tunaomba siku hii iwe ni siku ya mapumziko ili iwawezeshe wanawake kushiriki kikamilifu, hii inafanyika hata nchi ya Uganda. Siku ya Wanawake Duniani wanapumzika maana siyo kupumzika maana yake ni kwamba kujadili, kutafakari pia kushirika katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano, ikitokea ni siku ya kazi wale wanawake ambao wako kazini hawawezi kushiriki kikamilifu, wanakwenda muda mfupi tu wanarudi kazini. Tunaomba mwaka huu miaka 50 ya Uhuru siku hii itangazwe ni siku ya mapumziko wanawake waweze kutafakari maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HAMAD ALI HAMAD**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara muhimu sana ndani ya Tanzania yetu na kwa umuhimu wake, ndio maana imekuwa na wajibu na majukumu ya kuelimisha na kulea jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii katika hotuba ya Waziri, kuna mifuko mbalimbali ambayo husaidia maendeleo ya wanawake wa Tanzania na tukiitaja Tanzania basi ieleweke kwamba ni pamoja na Zanzibar. Mifuko ya mikopo ya wanawake kuanzia 2006 - 2010 imetoa mikopo katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara ikiwemo Halmashauri nyingi ndani ya Wilaya za Bara pekee, yanayoshangaza ni kwamba Zanzibar hakuna hata Halmashauri moja iliyofaidika na mifuko hiyo ya wanawake. Mwaka 2010 shilingi 1,048,000,000 zilikopeshwa kwa wanawake wajasiriamali kwa upande wa Bara pekee. Hivi Zanzibar hakuna wanawake wanaofaa kufaidika na mifuko hii? Mbona mikopo yote inaelekezwa Bara pekee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009 – 2010, Wizara ilipewa shilingi bilioni 19.9 na iliweza kufanya baadhi na mengine hayakuwezekana kutokana na

tatizo la fedha na kwamba kwa bajeti hii Wizara imetenga shilingi bilioni 16,256,015,000 hizi ni fedha ndogo ukilinganisha na malengo ya Wizara. Hivyo basi, naiomba Serikali iongeze fedha kwa Wizara hii ili shughuli zilizopangwa na Wizara zisikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Kitabu cha IV (Nne) kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Wizara imetengewa kiasi cha Tshs.bilioni 4.8 tu, kwa maoni yangu hiki ni kiasi kidogo sana cha fedha kwa shughuli za maendeleo. Aidha, kati ya fedha hizo kiasi cha Tshs.bilioni 2.0 kimetengwa kwa ajili uwezeshaji wanawake; (Vote 53, Sub.vote 3001, item 4943) bila shaka ni kwa ajili ya Benki ya Wanawake. Ukiondoa kiasi hicho, kiasi kinachobaki ni Tshs. bilioni 2.8 tu kwa ajili ya shughuli zote za m maendeleo. Najua Wizara hii ina kazi nyingi sana ikiwa ni pamoja na ukarabati wa Vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi. Najua Vyuo hivyo zaidi ya 50 vipo katika hali mbaya sana. Kiasi cha Tshs.393,167,000/= kilichotengwa kwa kazi hiyo ni kidogo sana ukizingatia uchakavu wa majengo pamoja na samani zilizopo katika Vyuo hivyo. Nataka kujua Wizara itatumia miujiza gani katika ujenzi, ukarabati na ununuzi wa samani katika Vyuo hivyo? Nashauri kiasi kidogo hicho kinachotengwa kisimamiwe vizuri. Nashauri pia Wizara ijenge hoja madhubuti ili bajeti ya Wizara iongezwe katika bajeti zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya kutoa mikopo kwa wanawake ili kuwaendeleza kiuchumi, lakini yapo malalamiko kwamba mikopo hiyo huwanufaisha zaidi wanawake watumishi. Inawezekana malalamiko hayo yana ukweli. Ombi langu, Wizara ifuatilie kwa ukaribu zaidi kwenye Halmashauri za Wilaya ili kuhakikisha kwamba pesa hizo zinaenda kwa walengwa. Nashauri pia kuwe na usimamizi mzuri ili kuhakikisha kwamba mikopo hiyo inarejeshwa ili wengine wakopeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana maendeleo ya Benki ya Wanawake kwa kuanza kazi vizuri. Naomba jitihada zaidi ziongezwe ili wanawake na wanaume wengi zaidi waweze kufaidika na mikopo kutoka benki hiyo. Hata hivyo, sina hakika ni kwa kiasi gani wanawake na wanaume nje ya Dar es Salaam wanafaidika na mikopo kutoka Benki hiyo ukizingatia umbali. Nashauri huduma za Benki hiyo zisogezwe kwa wanawake wa Mikoani ili nao wafaidike na mikopo. Nasema hivyo kwa sababu kwenye hotuba ya Waziri hajaeleza lolote kuhusu usogezaji wa huduma za Benki hiyo Mikoani. Nataka pia kujua ni wanawake wangapi kutoka Mikoani wamepata mikopo kati ya 893.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 50 ya Uhuru bado wapo Watanzania wanaoendeleza mila potofu zinazosababisha mauaji kwa Watanzania wenzao. Kwa mfano, ukeketaji wanawake, mauaji ya walemavu wa ngozi (Albino), mauaji ya vikongwe kwa kuwasingizia uchawi. Hali hii haiwezi kuachwa iendelee, lazima Serikali ikabiliane na vitendo hivyo kwa nguvu zote. Napongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa hatua mbalimbali ambazo zimeendelea kuchukuliwa dhidi ya vitendo hivyo viovu. Pamoja na hayo, nashauri elimu zaidi itolewe kwa makundi yote hasa katika maeneo

ambayo vitendo hivyo hujitokeza mara kwa mara. Pili, Sheria kali zichukuliwe kwa wale wote watakaobainika kufanya vitendo hivyo viovu ambavyo haviwezi kuachwa kuendelea wakati tunatimiza miaka 50 ya Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sheria hiyo kimsingi imechoka, imepitwa na wakati, miaka 40 tangu itungwe ni dhahiri imechakaa! Sheria hii pamoja na mambo mengine mabaya inaruhusu watoto wadogo (wasichana) miaka 14 kuolewa! Hali Sheria Kuu, Katiba ya nchi, inamtambua mtu mzima kuwa ni yule aliyetimiza miaka 18. Sheria ya Ndoa kwa maana hiyo ni batili kwa kuwa inakinzana na Sheria Kuu ya nchi. Naomba Waziri alieleze Bunge hili ni lini Sheria hiyo italetwa hapa Bungeni ili iandikwe/itungwe upya? Nashauri iwe mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawasilisha.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa jinsi wanavyowajibika kusimamia kazi za Wizara hiyo. Aidha, nawapongeza kwa jinsi walivyoandaa bajeti yao ambayo imeonyesha jinsi wanawake watakavyofaidika na mipango ya kupunguza umaskini. Baada ya maelezo hayo, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake, naipongeza Wizara kwa jinsi wanavyosimamia na kuwezesha Benki hii na vilevile kwa muda mfupi kufikia shilingi bilioni 4.8 kutoka shilingi bilioni 2.8 vilevile kwa jinsi inavyotoa elimu kwa watendaji. Naishauri Serikali iendelee kuitangaza Benki hii na baadaye waanze kufungua matawi katika Mikoa. Napenda kujua mpango wa Wizara wa kuhakikisha Benki inaongeza mtaji na lini Benki hii itaanza kufungua matawi Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hawa ambao wako chini ya Halmashauri wanashindwa kuwajibika na matokeo yake wanafanya kazi ambazo sio zao na kupoteza maana ya Idara au Wizara hii ya kuelimisha wananchi. Tunaomba Wizara iangalie utaratibu ambao utawawezesha kufanya kazi kwa kuwatengea fedha za kutosha na kuzipeleka katika Halmashauri. Hata hivyo upandaji wa madaraja unachelewa sana na kubadilisha mishahara yao. Tunaomba Serikali ilione hili na kulishughulikia mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Serikali imeandikisha/kusajili *NGOs* nyingi za kuisaidia Serikali kuharakisha maendeleo ya wananchi. Hata hivyo tungeomba Serikali izifanyie utafiti kama zinatimiza wajibu wao kama zilivyoomba. Kwa kuwa *NGOs* hizi ziko kila Mkoa na nchi nzima na nyingi zimejuhusisha kutoa elimu kwa wanawake, waathirika wa Ukimwi na kadhalika kuwepo na utaratibu wa kutoa taarifa kwenye vikao vya Kamati za Halmashauri ili kuona misaada wanayopata na jinsi inavyotumika kama inawasaidia walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza vyuo hivyo. Naishauri Serikali

iwashirikishe wananchi katika maeneo yaliyo na Vyuo ili kuviwezesha Vyuo kutumika ipasavyo ili wananchi wafaidike na Vyuo hivyo. Hata hivyo, Serikali Kuu itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuendesha Vyuo hivi. Vilevile tunaomba Serikali itoe maelekezo kwa Halmashauri ili itenge fedha kwa ajili ya vyuo hivi vilivyopo katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina mzigo mkubwa sana lakini imepewa fungu dogo sana, naomba Serikali iongezee fungu Wizara hii kwa sababu ina mzigo mkubwa sana. Vyuo vingi vya Ustawi wa Jamii ni magofu matupu wakati tunategemea tupate wataalamu wa kusaidia jamii yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda leo hii Waziri atakapokuwa anajibu hoja zetu anipatie jibu kuhusu Agizo la mwaka 1995 la Waziri Mkuu aliyekuwa madarakani wakati huo kuwa kila Halmashauri itenge 10% ya mapato yake kwa ajili ya kusaidia wanawake na watoto. Je, Halmashauri hapa nchini zinatekeleza Agizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa Serikali kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Wanawake wa Tanzania lakini nathubutu kusema Benki hiyo imekuwa ni Benki ya Wanawake wa Dar es Salaam, sababu bado ina mpango wa kuendelea kufungua matawi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ni lini wanawake waliopo Mikoani hasa wa Mkoa wa Iringa watafaidi benki yao? Nashauri kuwa Benki hii ianze sasa kufungua matawi Kikanda ili wanawake wote wapate haki sawa ya kutumia Benki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Benki hii imekuwa na masharti magumu sana ya mikopo tofauti na tulivyotegemea. Wanawake wengi wamekuwa wakinyanyasika na baadhi ya Taasisi za Fedha kunyang'anya vifaa vya ndani mpaka kufikia ndoa kuvunjika. Naomba sana leo hii tupatiwe majibu ya Benki hii kufikishwa Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu sheria. Sheria nyingi za ndoa na haki ya mtoto zimepitwa na wakati mpaka kusababisha ongezeko kubwa sana la watoto wa mtaani, wanawake sana hapa nchini wananyanyasika. Ukienda huko vijijini bado wanawake hawajui haki zao za msingi, bado sheria za mirathi hazitekelezwi na wanawake hawana msaada wowote. *NGO* nyingi zimefunguliwa mijini hakuna chombo chochote kinamsaidia mwanamke kujua sheria na haki yake ya msingi kwa kuwa katika Kitabu cha Hotuba kimeainisha kuwa jukumu mojawapo la Wizara ni kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuyawezesha kufanya kazi kwa uwazi na ufanisi zaidi. Naomba atakapokuwa anajibu aliweke wazi ili wanawake wote mpaka vijijini watendewe haki sawa na mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Kitabu cha Hotuba, ukurasa wa 17, Kifungu Na.31, utaona jinsi watoto wasivyotendewa haki na Sheria ya mwaka 2009 kumwezesha mtoto kuishi, kuendelezwa, kushirikishwa, kulindwa na kutobaguliwa. Watoto wetu wananyanyasika sana, kuna baadhi ya wazazi na walezi wanawatumia watoto wetu mpaka kuwatumia kuombaomba barabarani, Serikali ipo wapi? Sheria inasema nini? Mbona hakuna hatua yoyote inayochukuliwa dhidi yao? Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kutumia watoto kuomba barabarani. Je, Serikali inatuambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo udhalilishaji mkubwa sana unafanyika kwa watoto wanaofanya kazi za ndani, waajiri kuwabaka na kuwapatia magonjwa na mimba na kuwafukuza. Je, nani atawasaidia hawa watoto, wengine wanaachishwa shule, mbaya zaidi hata kima cha mshahara hakieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweke Maaskari waliopitia Ustawi wa Jamii kwenye Vituo vya Polisi ili waweze kusikiliza matatizo yanayoripotiwa na kuweza kuyashughulikia inavyotakiwa. Kwa kuwa kesi nyingi sana za unyanyasaji wanawake wanashindwa kwenda kuripoti katika vituo vyetu kwa kuona aibu kuipeleka kwa Askari ambaye ni mwanaume. Naomba hili nalo nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nitoe masikitiko kwa baadhi ya Wabunge wanaume kuwadharau Wabunge wa Viti Maalum kwa kuwa sisi pia jamii imetuchagua kuwawakilisha. Naomba Wizara itoe tamko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa nafasi mbalimbali za wanawake hapa nchini. Niwapongeze wanawake wote walioteuliwa na Rais kwa kutotuangusha. Naomba wanawake wote tupendane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia M. Simba (Mb).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya fedha zilizotengwa kwa Halmashauri zetu kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mwaka 2010/2011, ni jumla ya Shs.bilioni 1,048,000,000/= Napenda kujua ni kwa nini Halmashauri ya Meru kwa miaka minne mfululizo haijatengewa Fungu lolote? Kiasi cha Milioni 8,000,000/= mwaka 2006/2007 kilitengwa na hivyo maendeleo ya wanawake hayaendelei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha jamii inasimamiwa ipasavyo katika kupata na kulinda haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara kusimamia hadi kufunguliwa kwa Benki ya Wanawake, lakini hatujawatendea haki wanawake wengine kwa vile Benki hiyo ipo Dar es Salaam tu. Naiomba Serikali ijikite katika kuhakikisha Benki hiyo inafunguliwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, lakini pia upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano (Zanzibar kwa maana Unguja na Pemba).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya linaathiri sana jamii ya Watanzania na hasa watoto wetu na hili Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hakuligusia hata kidogo. Je, Serikali kupitia Wizara hii inasemaje kuhusiana na ongezeko la watoto wetu wanaoathiriwa na madawa ya kulevya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukeketaji bado ni tatizo sugu kwani kuna usiri mkubwa baina ya huyu anayefanyiwa tendo la ukeketaji lakini baya zaidi ni kwamba jamii zenye mila hizo haziwezi kuacha jambo hilo kwani wenyewe wana-*appreciate* kwa imani kwamba bila kukeketwa hawezi kuolewa. Kwa msingi huo basi wanaume wana mchango mkubwa katika jambo hili kwani wanalazimisha kuoa mwanamke aliyekeketwa. Hivyo, naiomba Serikali itoe elimu zaidi kwa wanaume katika jamii zinazoendelea na mila hii potofu. Ni lazima Serikali itafute mbinu mbadala katika kupambana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto wa mitaani linatia aibu kwa Taifa letu la Tanzania. Kadri siku zinavyokwenda ndivyo tatizo linavyozidi, je, Serikali inasemaje? Inawezekana hili linachangiwa na mimba za utotoni. Wakati mwingine watoto ambao wanashindwa kuendelea na masomo yao kutokana na umaskini wa wazazi wao lakini pia akina mama wengine huwatuma watoto wao makusudi kwenda barabarani ili kuomba kwa ajili ya kupata mahitaji. Naiomba Serikali kuandaa mkakati madhubuti ili kumaliza tatizo hili, kwani wazazi wengine wanajiweza kabisa na wana nguvu za kufanya kazi bali hawataki kujituma tu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28/7/2009, Benki ya Wanawake Tanzania ilianza kutoa huduma. Kuna malalamiko makubwa ya wananchi kuwa Benki zimeweka riba kubwa kwenye mikopo inayoitoa matokeo yake mikopo hiyo badala ya kuwasaidia wakopaji huwa inawadidimiza. Je, hii Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) imeweka riba ya asilimia ngapi inapotoa mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu uundaji wa Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto, Vikongwe na Albino katika suala zima la kupambana na ukatili wa jamii husika. Nionavyo mimi uwepo wa Kamati ya Kitaifa peke yake ya kupambana na ukatili hatuwezi kupata mafanikio yanayoridhisha. Je, hali ikoje kwenye maeneo ambayo wanaishi wananchi, kuna vyombo gani vinavyosimamia kuondoa ukatili huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mtoto, Na.21 ya mwaka 2009, msimamizi mkuu wa Sheria hiyo ni Wizara hii. Kutunga Sheria peke yake hakuwezi kuleta mabadiliko ya jamii mpaka pale Sheria hiyo itapotekelezwa. Haiwezekani Sheria ya Mtoto, Na.21 ya mwaka 2009 kuleta mabadiliko kwa kutegemea Polisi peke yake, ni

lazima Wizara iwe mstari wa mbele katika kuona Sheria hiyo inatekelezwa. Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kuwa Sheria hiyo inatekelezwa. Je, Wizara imetenga fedha kwa utekelezaji wa Sheria hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 18, ukurasa wa 10 wa Hotuba ya Waziri imeeleza juhudi za Wizara katika kukabiliana na utumikishwaji wa watoto. Katika aya hiyo haionekani hatua hata moja iliyochukuliwa kwa wale wanaowatuma watoto. Ajira kwa watoto hazitaondoka kwa maadhimisho na kutoa elimu peke yake bali kwa kuchukua hatua za kuwashtaki wale wanaowatumia watoto kinyume na sheria. Wizara imejipanga vipi katika hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs),* ni wadau wakubwa wa huduma na huleta maendeleo hapa nchini lakini pia yapo mashirika mengine utendaji wao hauridhishi badala ya kuleta manufaa kwa wananchi wanajiletea manufaa wenyewe. Wizara hii inasajili mashirika haya na ni mengi, je, Wizara imejiundia utaratibu gani wa kuhakikisha utekelezaji wa mashirika unafanywa kwa mujibu wa kanuni walizojiwekea? Kwa sababu mashirika haya yanatumia fedha kutokana na michango ya wahisani mbalimbali, je, Wizara ina wataalamu wa mahesabu ili kukidhi haja ya ukaguzi huo wa mahesabu? Ahsante.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie bajeti ya Wizara yetu mlezi kwa njia ya maandishi. Eneo la kwanza ambalo napenda kuchangia ni misukosuko ya kijamii na haja ya kuwa na mshikamano wa kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekerwa na tatizo la watoto yatima katika jamii ambao wanaongezeka kwa kasi. Pamoja na ongezeko hili, bado kuna haja ya kuelimisha jamii kutumia utamaduni wetu wa kale ambapo yatima alikuwa analelewa na jamii nzima. Kabla ya mwaka 1980, sehemu kubwa ya Taifa mtoto aliyepoteza wazazi wote aliweza kulelewa na asijue kuwa hana wazazi wa kibaiolojia. Tuainishe wadau wanaoweza kuhamasisha jambo hili dhidi ya utaratibu wa kuwaweka watoto kwenye makambi au kuwaita watoto majina yanayowaathiri kibailojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Muleba Kaskazini neno “Maisha hatarishi, yatima” na “maisha magumu” nahamasisha yasitumike kumuelezea mtoto mwenye matatizo ya aina hiyo, natumia neno “wahitaji” (*the needy).* Kwa kuondoa madhara ya neno hilo naeleza kuwa binadamu wote ni wahitaji ndiyo maana tunaomba kwa Mwenyezi Mungu. Ila nabainisha kuwa uhitaji hutofautiana ndiyo maana tunalazimika kusaidiana. Maneno makali yanayomkumbusha mlengwa machungu yaepukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuwepo kwa *NGO* za kieneo, *Community Based Organization*. Ni ushauri wangu kuwa pale ambapo Tarafa inacho chombo cha aina hii, Idara inayohusiana na Wizara hii na masuala yake iwekwe. Aidha, Tarafa zote zingeshawishiwa kuanzisha *CBO* na kupitia chombo hiki tuongeze kasi ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linalohitaji ushauri na marekebisho ni Watendaji wa sekta hii ambao wanapaswa kuwepo kuanzi ngazi ya Kata. Napendekeza Wizara hii itumike kama mfano, Kata zote zipatiwe Watendaji hawa. Zaidi ya kupanga wataalamu inabidi wapewe majukumu na malengo kwa vipindi, mwezi, miezi mitatu, nusu mwaka na mwaka. Tuna tatizo kama Serikali kwa kutokuwa na *Performance Management Programmes,* kimsingi tulio wengi hatujui tufanye nini na wale wanaojua wanatenda bila malengo au utamaduni wa kutathmini malengo. Nimeichagua Wizara hii kutokana na umuhimu wake kwa jamii ili tuitumie kuendeleza jamii yetu ili tulete mshikamano wa kijamii. Kwa maeneo hayo matatu niliyoainisha yakioanishwa na walengwa wakatengewa mikopo ya Shs.200 bilioni kwa mwaka ili ziwekezwe kwenye fursa zenye faida, jamii yetu itaendelea kwa kasi kubwa.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia suala zima la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Watoto hawa wanaoishi katika mazingira magumu ni janga la Taifa zima. Watoto hawa wanatokea katika Mikoa mbalimbali na wanakimbilia katika Miji mikubwa mfano Dar es Salaam inaonesha ni jinsi gani Serikali yetu imeshindwa kudhibiti hali hii. Wageni mbalimbali wanapokuja kutembelea Tanzania wanakutana na hii hali ya hawa watoto wanaoombaomba, hii ni aibu kwa Taifa. Hawa watoto wanakimbilia wageni hawa na kwenda kuwaomba hivyo wanawapa usumbufu wageni. Watoto hawa wanaoishi katika mazingira magumu wanakutana na matatizo mengi mfano kwa watoto wa kike kama kubakwa, kujiingiza katika biashara za ngono katika umri mdogo na hatimaye kwa watoto hawahawa wa kike kubeba mimba za utotoni na hatimaye kuwatupa watoto wanapojifungua na hili linakuwa ni tatizo kwa Taifa. Kwa upande wa watoto wa kiume nao wanapata matatizo kama kulawitiwa na kuwa mashoga. Naishauri Serikali iangalie Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, itenge Fungu la kutosha, watoe semina endelevu kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Serikali ihakiki ile Mikoa yote ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuhakikisha Fungu hilo lililotengwa linawafikia watoto hawa na Serikali kuwadhibiti watoto hawa waweze kubaki katika Mikoa yao wasiende katika Miji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kumekuwa na watu wanaoanzisha vituo hivi kwa maslahi yao binafsi na sio kwa malengo husika. Wanawatumia watoto hawa kama kwenda kuwaombea misaada katika mashirika mbalimbali ya nje na misaada hii haiwafikii walengwa na kujinufaisha wenyewe. Watoto hawa wamekuwa wakitoka katika vituo hivyo vilivyoanzishwa na kuweza kuzagaa mitaani na kuombaomba. Kwa hiyo, naishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ikishirikiana na Ustawi wa Jamii kuhakiki hivi vituo vinavyolelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu kama vipo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la akinamama wenye umri mkubwa kuwachukua watoto wenye umri mdogo na kuwalaghai kwa pesa zao na kuwapotezea

watoto hawa masomo na watoto hawa wanaathirika kisaikolojia na jingine baya hawa wanawake wengi wanakuwa ni waathirika wa gonjwa hili la UKIMWI. Naomba Waziri akija kutoa majumuisho aniambie Sheria ya Mtoto inasemaje kuhusu hawa akinamama wanaowarubuni watoto wadogo na kuwaingiza katika masuala ya mapenzi na wengi wao ni waathirika wa Ukimwi na itachukuliwa hatua gani endapo akinamama wenye tabia hiyo watagundulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Wafungwa magerezani, Wafungwa hawa watendewe haki kama suala la ndoa mfano mwanandoa mwanaume na mwanandoa mwanamke ambao wanafungwa kifungo cha muda mrefu, nashauri Serikali na Wizara kama Sheria hii haipo basi ipitishwe Sheria ya Wanandoa hawa wafungwa wa muda mrefu kukutana Magerezani ili kuepusha wanaume kuingiliana kinyume na maumbile na kuepusha wanawake hawa kujamiiana wenyewe kwa wenyewe. Wafungwa hawa pia wana haki kama binadamu wengine kufanya tendo la ndoa na kuepusha maambukizi ya VVU. Serikali iwaangalie wanawake hawa wafungwa wanateseka sana Magerezani. Hawapati mahitaji yao muhimu kama nguo zao hazikidhi mahitaji yao, wakiwa kwenye siku zao za hedhi hawawapi pedi, sabuni na kadhalika kwa hiyo, Wizara na Serikali iangalie kwa makini suala hili ili nao waweze kupata haki zao kama binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushirikina limekithiri na kuchangia kuzorotesha maendeleo ya jamii yetu kwa mfano, ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi wanavyochukuliwa na kufanywa chanzo cha utajiri. Kwa hiyo, Serikali iangalie suala hili kwa makini. Tatizo hili halipo kwa walemavu wa ngozi peke yao hata baadhi ya akinamama wanachukuliwa baadhi ya viungo vyao vya mwili na watoto nao wamekuwa wakipotea katika mazingira ya kutatanisha. Hivyo basi naishauri Serikali watakaokamatwa na wenye kushiriki vitendo kama hivyo wapewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Benki ya Wanawake, kama kweli Mheshimiwa Rais aliona umuhimu wa wanawake na akaweza kuanzisha Benki ya Wanawake Tanzania, Benki hii inufaishe wanawake wote wa Tanzania Bara na Visiwani na walio pembezoni na isinufaishe wanawake wachache. Suala la masharti pia liangaliwe kwa makini yasiwe ni masharti ya kumkandamiza mwanakmke wa kijijini aliyekuwa na elimu ndogo. Benki hii isifananishwe na benki nyingine iwe ni benki kweli ya kuweza kumkomboa mwanamke. Benki hii masharti yake yasifanane na masharti ya Benki nyingine. Wanawake wengi wamekuwa wakidhalilika na mikopo wanayochukua yenye riba kubwa na hatimaye kushindwa kurejesha. Kama kweli benki hii imekusudiwa kumsaidia mwanamke asidhalilike kwenye mikopo yenye riba kubwa basi ihakikishe inakuwa na matawi mengi hadi Vijijini. Aidha, Benki itoe semina endelevu kwa wajasiriamali wa Vijijini kwa sababu wengi wao hawajui umuhimu wa Benki. Endapo watapata semina hii hawataweka fedha zao ndani kwa sababu wajasiriamali wengi wa Vijijini hawajui maana ya Benki. Hivyo basi semina hii itamsaidia mjasiriamali huyu wa Kijijini naye anaweza kujua umuhimu wa Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja endapo niliyoyaandika humu nitapatiwa majibu.

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Sophia M. Simba (MB), Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu (MB), Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya kutekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake bado wananyanyasika sana katika mambo kadha wa kadha katika jamii. Wanawake ambao hawakubahatika/hawajabahatika kufanya kazi au biashara bado hawajui haki zao katika masuala yahusuyo mirathi, malezi ya watoto pale mke na mume wanapotengana, Sheria ya Ardhi na kadhalika. Nashauri kuwepo kwa Dawati la Ushauri kwa wanawake katika Halmashauri zetu ili kutoa ushauri kwa wanawake wanaodhulumiwa mali zao waume zao wanapofariki dunia, kuwashauri wanawake kuhusu umiliki wa ardhi, malezi ya watoto wanandoa wanapotengana. Malalamiko yapo mengi sana katika jamii katika masuala niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Sheria iwabane wazazi wanaowaacha watoto wakirandaranda mitaani na kukosa elimu na huduma muhimu kwa watoto. Wengi wa watoto walioko mitaani wakiombaomba wana wazazi japo mzazi mmoja. Kwa kuwa Serikali haijaamua kuchukua hatua kwa wazazi husika hali hiyo imeendelea katika miji yetu, mwisho wa siku tutakuwa na Taifa ambalo wananchi wake hawapendi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali iliridhia kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake Tanzania. Nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Wanawake kwa kazi kubwa ya kuendeleza Benki ya Wanawake kwa kipindi kifupi sana. Nashauri Benki hii kufungua matawi katika Mikoa mingine ili wanawake wasiendelee kunyonywa na Taasisi za Kifedha kama *Pride, Finca, Seda* na kadhalika. Benki hii pia inaweza kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanawake kwa kushirikiana na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi bado hawajanufaika na shughuli zinazofanywa na Asasi zisizo za Kiserikali zinazotumia migongo ya waathirika wa Ukimwi na watoto wa mitaani/wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa kujinufaisha binafsi. Wengi wao wanaitisha semina za Soda moja kwa wahusika na kuandika taarifa isiyo na ukweli kwa Serikali na kwa wahisani. Naishauri Serikali kufuatilia kwa karibu shughuli zinazofanywa na Taasisi hizo badala ya kusubiri taarifa mezani. *NGOs* zisaidie kupunguza umasikini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kutumia baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii au Vyuo vya Wananchi vitumike kama Vyuo vya *VETA*. Kwa sasa kuna upungufu wa Vyuo vya Ufundi *VETA* katika maeneo yetu, wakati kuna Vyuo hivyo vinavyoweza kutumika kutoa elimu ya ufundi kwa vijana wetu. Kwa kuwa bajeti ya Wizara hii ni ndogo, fedha zinazotengwa kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na zile za *VETA* zikiunganishwa pamoja katika Vyuo hivi tutafaidika kwa vijana wengi kupata nafasi ya elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana katika suala zima la kutoa elimu na huduma mbalimbali kwa wanawake na watoto ili kutekeleza azma ya haki ya kimsingi ya kila binadamu kupata haki yake kama vile elimu, afya na huduma nyingine za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wimbi kubwa la watoto wanaozagaa ovyoovyo mitaani na kuwa ombaomba na hatima yake wanakosa kupata elimu, afya na malazi na hatimaye kukumbwa na maradhi mbalimbali na mwisho wake ni kifo. Hivyo, Serikali ikishajenga mabweni na shule italazimika kukusanya watoto wote kwa pamoja ili kuwapa huduma muhimu kama elimu, chakula, matibabu na malazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imetengewa fedha kidogo mno, bila kutambua Wizara hii inayo majukumu makubwa sana ambayo mtandao wake unatakiwa utawanyike hadi Vijijini kuliko na uduni mkubwa na wimbi la umasikini linalotokana na kukosa uelewa na mwamko wa kimaendeleo. Hivyo waajiriwe Mabwana Maendeleo waende huko kutoa elimu ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inalo jukumu kubwa la kuwafikia akina mama wa Vijijini ili waweze kutambua haki yao ya msingi ikiwa ni pamoja na kutambua kuwa wana haki sawa na wanaume na wanao uwezo wa kushiriki katika shughuli zote za kimaendeleo, kiutawala, kwani wanawake wanaweza. Mama akielewa maana yake familia imeelewa, akinamama wanaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata wasaa huu ili niweze kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kuhusu Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kutumia Mifuko ya Wanawake ya Maendeleo *(WDF), SACCOS* na Benki ya Wanawake kumekuwepo na upungufu mkubwa sana pamoja na juhudi za Serikali kutaka kuwainua wanawake, nikianzia na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* wanawake wengi wamekuwa hawafaidiki sana na Mfuko huu na hasa kwa kuwa wengi wao hawana ufahamu wa mfuko huu. Maafisa Maendeleo Jamii wamekuwa hawawafikii walengwa wa mfuko huu hususani Vijijini. Nashauri Serikali kuhakikisha kila Kata inakuwa na Afisa Maendeleo wa Jamii ili kuweza kufikisha mafunzo na ujumbe kwa walengwa. Naamini mwanamke akifikiwa na hata vijana watajijenga kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake bado haijajitanua vya kutosha, iko Dar es Salaam tu. Wanawake walio wengi waishio Vijijini hawaijui na hata kuisikia. Aidha, mikopo katika Mabenki au SACCOS, kunahitajika uwepo wa dhamana ndipo mtu akopesheke, sasa je, hawa wanawake ama vijana maskini wasio na mitaji watafaidika vipi na Mabenki haya? Tunaomba maelezo katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kumekuwepo na ongezeko la watoto wa mitaani. Sheria ilitungwa mwaka 2009 ya kuwabana wanaosababisha hali hii. Binafsi sijaona kama Sheria hii inafanya kazi kwa kuwa hawa watoto wana wazazi wao, ni kwa nini wazazi hawa wasiowajibika kwa familia zao hawachukuliwi hatua madhubuti? Nini kikwazo? Tena watajwe hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la wazee ambalo limesahaulika kabisa kwa sababu lengo la Wizara hii ni kushughulikia maendeleo ya jamii wakiwemo wazee. Hakuna mpango wowote wa kuonyesha kuwajali wazee hawa, pengine unafuu kidogo ni kwa wale ambao walibahatika kuajiriwa hivyo tunaitaka hii Mifuko ya Hifadhi za Jamii mfano *NSSF* kuhakikisha yanatoa ile michango kwa wakati ili kukabiliana na makali ya maisha. Vilevile kwa wale ambao hawanufaiki na mifuko hii basi Serikali iandae mpango wa kuwatambua kwa kuwapatia fedha kidogo kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ubakaji na ulawiti kwa watoto wa kike na wa kiume limekuwa ni tatizo kubwa sana kuliko ambavyo jamii ya Kitanzania inaliona. Tatizo hili linatokana na ukosefu wa maadili miongoni mwa jamii nzima ya Tanzania kwa sababu, hata watu wazima au wazee wamekuwa wakiripotiwa kuwabaka na kuwalawiti watoto wadogo wa kike na wa kiume. Kwa kuwa suala hili mara nyingi limekuwa haliripotiwi kwenye vyombo husika kwa hofu wanayopewa watoto kwamba wakisema watauawa, imekuwa si rahisi kupata idadi kamili ya watoto waliofanyiwa kitendo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza tatizo hili, naishauri Serikali kutoa elimu kwa nguvu zote kwa kila rika kuanzia wazazi mpaka watoto juu ya tabia hii mbaya. Mtoto akifundishwa vizuri na ikithibitishwa kwamba kwa bahati mbaya kabakwa asisite kuwaeleza wazazi wake na kwamba hatapata tatizo kwa mbakaji, mtoto huyo atakuwa na ujasiri wa kueleza uovu huo bila hofu na hii itasaidia kuwaogopesha wahalifu hao na kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo hivi vichafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manyanyaso kwa wanawake ni suala ambalo linaeleweka katika jamii nzima ya kiafrika, Tanzania ikiwepo. Wanawake wamekuwa wakionekana kama ni jinsia ambayo ni ya chini isiyoweza kujitegemea na hivyo kuwa chini ya wanaume. Manyanyaso haya yanaambatana na vipigo na hata vifo kwa wanawake wengi kama tunavyoshuhudia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mila potofu ndizo zinazopelekea wanawake kupigwa wakati mwingine bila kupewa hata nafasi ya kujitetea. Makabila mengine mfano Wambulu, Wanyaturu, Wakurya na Wagogo hayampi nafasi mwanamke kusema popote pale au kwa mtu yeyote pindi anapopigwa, kitendo cha mwanamke huyo kuelezea kipigo nje ya familia yake kitamfanya apigwe tena na kuumizwa kwa mara ya pili. Serikali

inatakiwa kupitia Asasi za Kiraia na Zisizo za Kiraia kutoa msisitizo wa haki za binadamu ili kuwaepushia wanawake na adha hii ya vipigo vya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ubaguzi mkubwa katika kutoa haki kati ya mke aliyeolewa na kwa mume. Haki hizi ni kama zifuatazo:- Inapotokea mume ameoa mwanamke wa Taifa lingine, hasa anapokuwa nje ya nchi, anaporudi nchini, *automatically* mke wake anakuwa raia au anapewa uraia wa Tanzania lakini pindi mwanamke anapoolewa na raia wa nje anaporudi nyumbani mume wake anatakiwa aishi kwa Visa na hapati uraia *automatically* kama inavyokuwa kwa mwanaume. Kwa nini suala hilo linafanywa hivi? Serikali haioni huu ni ubaguzi wa kijinsia kati ya mume na mke? Naitaka Serikali itoe tamko kuhusu ubaguzi huu ili wanawake wajue kwamba wao hawana haki ya kuchagua wenza wao hususani wakiwa ni wa nje ya Tanzania na kwamba ili waishi kwa amani ni lazima waolewe na Watanzania wenzao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa nchi yetu imekuwa ikiadhimisha Sikukuu ya Mtoto kufuatia kumbukumbu ya watoto waliouawa kinyama South Africa. Suala hili ni zuri kwani linaonesha jinsi tunavyotambua umuhimu wa watoto wetu. Tatizo linalojitokeza ni kwamba Serikali haijatilia mkazo kabisa katika kumjali mtoto wa Kitanzania na hii inajionesha kupitia wimbi kubwa la watoto wa mitaani ambao si kwamba hawana wazazi bali wengine wamekimbia majumbani kutokana na manyanyaso wanayoyapata nyumbani. Serikali ina mkakati gani wa kuliondoa tatizo hili la watoto wa mitaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno jinsia pia limekuwa likitumika vibaya kwa kumaanisha jinsia ya kike tu na si kwa pamoja na wanaume. Inapotamkwa jinsia hasa kwa watoto, isiangaliwe jinsia ya mtoto wa kike tu, bali na mtoto wa kiume pia apewe umuhimu wake. Hivyo natoa rai tafsiri ya neno hilo ipewe uzito wake ili liweze kutoa haki sawa kwa watu wote (Mwanamke na Mwanaume).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine ni kwamba ili kuweka uwiano ulio sawa katika jinsia zote, ni vema Wizara hii ikaongozwa na Mawaziri wa jinsia zote mbili, Waziri akiwa Mwanamke basi Naibu awe Mwanaume na *vice versa* ili kila jinsia inayozungumziwa kwenye Wizara ipate haki sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukeketaji japo limepungua kwa kiasi kikubwa lakini tatizo hili bado lipo katika Mikoa ya Mara, Singida, Dodoma na Manyara. Ukeketaji kwa watoto wa kike unahusishwa zaidi na mila potofu kwamba mtoto asipokeketwa basi ataanza ngono mapema na hataweza kujizuia pindi anapowaka tamaa. Historia ya ukeketaji kwa jamii zenye mila hiyo inaonesha kwamba wanawake walikuwa wanakeketwa ili kuzuia tamaa ya kutoka nje ya ndoa pindi waume zao wanapokuwa vitani na hivyo kuwafanya watulie kwenye ndoa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na matatizo ya uzazi yanayowapata wanawake waliokeketwa kwa kutokwa na damu nyingi kunakosababishwa na kuchanika kwa kovu lililosababishwa na ukeketaji, wanawake hawa wamekuwa wakikandwa na maji ya moto yaliyochemka kupita kiwango ili waweze kurudi katika hali ya kawaida baada ya

kuchanika wakati wa kujifungua. Maji haya ya moto yanaweza kuua *cells* ambazo ni *sensitive* katika masuala ya kujamiiana na hivyo kumnyima mwanamke furaha ya tendo la ndoa katika maisha yake yote. Hii ni pamoja na tendo zima la ukeketaji kwani linamnyima mwanamke furaha ya tendo la ndoa na badala ya kutulia kama ilivyokuwa imekusudiwa matokeo yake anakuwa hatosheki na hivyo kuanza kutangatanga nje ya ndoa akidhani pengine mumewe hawezi kumridhisha na kumbe ni kukosa kiungo muhimu *(clitoris)* katika suala zima la tendo la ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kutoa elimu katika ngazi ya Kaya, Vijiji ili kuwaelimisha wanajamii ubaya wa mila hii, maana kwa sasa umezuka mtindo wa kuwakeketa watoto wakiwa bado wana umri wa wiki mbili tu ili kukimbia mkono wa sheria na hivyo kuwa vigumu kuwabaini wahalifu hawa. Elimu itolewe ili wazazi wote (mume na mke) waone umuhimu wa kuacha kuwakatili watoto wao wa kike ili waweze kufurahia maisha yao ya ndoa hapo wanapokuwa watu wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nyingi za Wilaya hazijaweka msukumo katika kuwasaidia wanawake hasa kwa kupitia vikundi vyao vya kujiletea maendeleo na hivyo zimeshindwa kutilia maanani kuvitengea vikundi hivyo fedha kwa ajili ya maendeleo, kama sheria ya nchi inavyozitaka kutenga asilimia 15% ya mapato yao ya ndani na hivyo kushindwa kuwasaidia wanawake hasa wale wa Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza zifanyike tathmini kujua hadi sasa kila Halmashauri inadaiwa shilingi ngapi na kila Halmashauri iagizwe kuzitoa upya kwa Wilaya za Mkoa wa Rukwa, Nkasi, Sumbawanga Vijijini, Sumbawanga Manispaa na Wilaya mpya ya Kalambo ambayo nayo tunahimiza Serikali iiwekee miundombinu *(Infrustructure and other facilities)* ili ianze kazi na wananchi wa Kalambo wanufaike na maendeleo yatakayoletwa na Wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba ya 15% inayotozwa mikopo hiyo ni mikubwa, napendekeza ipunguzwe hadi 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai yangu kuwa Benki ya Maendeleo ya Wanawake ianzishe Tawi lake Rukwa, kwani Mkoa huo kuwa pembezoni sana umesahaulika mno na hivyo kuwafanya wanawake wa Rukwa kuwa nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu pia kuwa kwa makusudi kabisa mwanamke wa Tanzania na Rukwa wapewe/ waelimishwe sana kuhusu Sheria kama vile Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijijini, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi, Sheria ya Unyanyasaji wa Kijinsia *(SOSPA)* ili kumkomboa mwanamke kutokana na unyanyasaji na kukandamizwa na mila na desturi zilizopitwa na wakati ikiwa ni pamoja na ukandamizaji wa mfumo dume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya nayo itilie maanani upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika ngazi zote za Vituo vya Tiba *(health facilities)* ili kupunguza/kumaliza vifo vya wanawake na watoto vinavyotokana na huduma duni. Naomba bajeti hii iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. OMARY A. BADWEL**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nyingi za Wilaya hazitengi fedha za kuwakopesha wanawake kama Sheria ya nchi inavyozitaka kutenga 15% ya mapato yao ya ndani na hivyo kushindwa kuwasaidia wanawake katika shughuli zao mbalimbali za kuzalisha mali ili kuongeza uwezo wao wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani umefika wakati Serikali kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa Watendaji hao wa Halmashauri kwa kushindwa kutimiza wajibu wao na kwa kutokujali juhudi za wanawake kujikwamua kiuchumi. Napendekeza zifanyike tathmini kujua hadi sasa Halmashauri kila moja inadaiwa shilingi ngapi na kila Halmashauri iagizwe kuzitoa upya kwa wanawake wa Wilaya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya ya Bahi ni Wilaya mpya na imeanzishwa miaka saba iliyopita, lakini hadi sasa haijawahi kupata fedha za kukopesha vijana toka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Sasa nataka kujua sababu za Wilaya hiyo kutopata fedha hizo na lini basi Wilaya hii ya Bahi itapata fedha hizo. Pili, riba 15% inayotozwa mkopo huo ni kubwa ukilinganisha na aina za kazi wanazofanya vijana hususani maeneo ya vijijini, nashauri ipunguzwe na kubaki 10%.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara ambayo ina haki na wajibu wa kuangalia hali halisi ya maendeleo yalivyoboreshwa au yalivyodumazwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kimaendeleo bado Tanzania tuko nyuma ingawaje dhamira ya Wizara hii ni kuwaletea maendeleo ya kweli Watanzania licha ya kubakia kama jamii ya watu ambao tuko kwenye ndoto. Hatuwezi kujigamba kwamba Watanzania tuna maendeleo wakati Watanzania walio wengi wanaishi kwa kutopata afya nzuri, kutokana na kukosa matibabu bora, elimu duni kutokana na kukosekana kwa Walimu mashuleni, ukosefu wa chakula na lishe kwa Watanzania kiasi cha kuwafanya Watanzania 68 kila watu mia kuishi kwa kula chakula mara moja tena duni badala ya mara tatu. Katika hali hiyo vipi tunaweza kusema kwamba kuna maendeleo ambayo yamepatikana. Wizara ina wajibu wa kupitia na kuratibu kwenye mashirika mbalimbali kwa kuandikiana mikataba ambayo itatekelezwa na sio kutelekezwa kwa Wizara kutokana na mikataba hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia masuala ya jinsia, napenda kusema kwamba mpaka leo kwa upande wa Tanzania Bara kuna maeneo ambayo baadhi ya makabila kama mwanamke hajapigwa haoni kwamba eti anapendwa na mume wake jambo ambalo halikubaliani na haki za binadamu ulimwenguni kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wale wote ambao wanawataka watoto wa kike wasiozeshwe waume wakiwa chini ya umri wa miaka 18 yaani kumi na tano (15) hii inatokana na wazee ambao wameweka maslahi yao mbele badala ya kuangalia hatma ya mtoto wa kike baadaye. Mtoto wa kike kwa baadhi ya makabila wanatumiwa kama mitaji wa wazee kujipatia utajiri na kuwakosesha watoto hao elimu na pia kuwadumaza juu ya hatma yao ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina wajibu wa makusudi wa kuishauri Serikali juu ya kudhibiti suala la watoto wa mitaani kwa kuwajengea na kuwatengea maeneo maalum ili waweze kulelewa na pia kuwapatia elimu, ambapo hatimaye Taifa litaweza kujipatia wasomi wenye vipawa mbalimbali kutoka katika kundi la watoto na vijana hao wa mitaani na pia Taifa litapunguza wimbi la ombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwekeza katika Taifa lolote ni miongoni mwa masuala muhimu sana hivyo basi tuna wajibu wa kujikita kuwekeza katika mashule, afya, elimu, vikundi vya ushirika wa kilimo cha mbogamboga, matunda, mifugo ya kuku, ng'ombe wa maziwa, mbuzi wa maziwa na hata biashara nyinginezo halali zitakazokubaliwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya wanawake yatapatikana kwa Wizara kuwapigania na kuwatetea wanawake kuhakikisha kwamba wanapatiwa fedha za kuwaendesha na kuwaendeleza katika miradi mbalimbali ya maendeleo yatakayokuza vipato vyao, jambo ambalo litawaondoshea ukali wa maisha na pia kuweza kuhudumia familia zao kielimu, kiafya na pia kuwalinda katika kushawishika kuingizwa katika biashara za kulevya, umalaya jambo ambalo litawajengea heshima na mustakabali wa maisha yao ya baadaye, ambapo tutajenga Taifa adilifu, sikivu na endelevu.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa kujikita kwenye baadhi ya matatizo ya kimaendeleo yanayolikabili Jimbo la Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bukombe ni miongoni mwa Wilaya ambazo bado ziko nyuma sana kimaendeleo, katika nyanja karibu zote elimu, afya na kadhalika. Watu wengi wanakabiliwa na tatizo la kipato kwa kuwa kipato cha wengi hutegemea uuzaji wa mavuno wanayoyapata mara moja kwa mwaka, wengine ni wafugaji ambao wana ahueni kidogo kwa kuwa wanaweza kupata kipato kwa kuuza mifugo yao wakati wowote. Wapo pia watu wenye ufukara wa mahitaji muhimu. Hata kwenye ngazi ya kaya ufukara wa mahitaji muhimu na /au wa kipato unajidhihirisha katika makazi duni waliyo nayo na hali duni za maisha yao ya kila siku. Katika hali hii, wananchi wa Bukombe wanahitaji msaada wa Serikali kutokana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nafasi ya mwanamke imebanwa na mfumo dume tulionao ambao bado umezongwa na mila mbalimbali zenye madhara kwa haki za wanawake. Changamoto ambazo wanawake wa Bukombe wanazikabili ni pamoja na kujikwamua kutokana na ufukara, kupambana na unyanyasaji wa kijinsia na kuboresha maisha yao kielimu, kisiasa na kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Serikali katika kuwasaidia wanawake wa Bukombe kujikwamua na ufukara bado ni mdogo sana. Kwa mfano fedha kwa ajili ya mikopo inayotengwa kwa ajili ya wanawake ni kidogo sana, ni vikundi vichache tu vya akina mama ambavyo hupata mikopo hiyo. Mikopo yenyewe ni Shs.500,000/= kwa kila kikundi cha watu watano, yaani Shs.100,000/= kwa kila mwanamke. Kiwango hiki ni kidogo sana na hutolewa kwa wanawake wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi Bukombe bado wananyanyaswa kijinsia na mara nyingi hupigwa na wanaume kwa uonevu. Hali hii itapungua pindi tu elimu ya msingi na sekondari itakapoimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya watoto yanakabiliwa na changamoto za uyatima (kutokana na wazazi kufa kwa Ukimwi, n.k), vifo vya watoto chini ya miaka mitano (5), tatizo la watoto wa mitaani na mimba za utotoni. Haya yote bado ni matatizo Bukombe na Tanzania kwa ujumla. Inasikitisha kuwa Serikali imetenga kiasi kidogo sana (katika bajeti 2011/2012) kushughulikia matatizo haya. (Tazama Kitabu cha Bajeti, Juzuu la IV, Ukurasa wa 104, kifungu cha 3002, kiasi cha Shs.116,941,500/=). Napendekeza Serikali ianze kufikiria namna bora ya kushughulikia changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii. Hakuna tija ya maana inayopatikana kwa kutenga bajeti finyu kwa Wizara yenye majukumu mazito kama hii.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuteuliwa kuwa Waziri na pia kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri sana.

Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri anayoifanya hapa Bungeni na katika Taifa kwa ujumla. Umahiri wake wa kujibu maswali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, inaonyesha ni jinsi gani ana uelewa wa mambo ya sekta hii. Nichukue fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu na watendaji wote wakuu pamoja na wanawake wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kuwa mimi ni Afisa Maendeleo ya Jamii *proper,* niliyebobea kwenye fani na niko *committed* sana katika sekta hii kwani ndiyo pekee yenye taaluma ya kuhamasisha, kushawishi na kuimarisha masuala mbalimabli ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utagundua kwamba Idara za Maendeleo Jamii kwenye Halmashauri hazijawezeshwa na kama zipo zipo tu. Idara hii imebakia kudandia masuala kama UKIMWI na kadhalika. Nashauri Idara hizi ziwezeshwe kwani kwa tunaofahamu sekta hii ni muhimu sana, laiti zingetumika ipasavyo mambo mengine ya uwezeshwaji wa wananchi na ushirikishwaji yangekwenda kwa kazi na kuleta ufanisi mkubwa. Idara hii haina hata usafiri. Gari la *TASAF* siyo la Idara. Hivyo uangaliwe uwezekano wa kupatiwa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwezeshaji wa wanawake kushika nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia chini kabisa. Nipongeze jitihada za Mheshimiwa Waziri za kuhamasisha wanawake na kutusaidia kwa hali na mali kupata nafasi hizo, kwa upande wa Mawaziri na Naibu Mawaziri ikiwezekana Rais akumbushwe ahadi zake. Hadi sasa ni *only 19%* ilhali nchi zingine zina asilimia kubwa zaidi, angeongeza tungefarijika. Hata hivyo tunamshukuru sana kwa kutujali kwenye maeneo mengine mengi hili nadhani alipitiwa. Tumkumbushe kwa upendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ni ndogo sana. Hii imekuwa ikijirudia mwaka hadi mwaka, tunaomba mwakani wanapoanza kuweka vipaumbele katika Bajeti yetu basi na sisi Wabunge tuhusishwe ili tuweze kuweka shinikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba pamoja ni pembezoni sana niwaombe Waziri na Naibu wake kutembelea Kilindi ili kuwatia moyo Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hii itanipa nguvu, mwanamke pekee Mbunge wa Jimbo katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja nina tatizo moja ambalo ninaomba Wizara inipe maelezo juu ya mustakabli wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanva kilichopo nje kidogo ya Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo hiki ni cha siku nyingi, majengo yake yamechakaa lakini hawana vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vifaa vya kufundishia. Tangu mwaka 2008, kila mwaka wakati wa Bajeti huwa napewa ahadi tutakarabati majengo, walimu watapewa fursa ya kujiendeleza, chuo kitapatiwe usafiri lakini hadi leo hakuna lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Waziri anipe ufafanuzi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuweza kuchangia mchango katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wizara ya hii Bajeti yake ni finyu sana kwani haitoshelezei kabisa kulingana na changamoto kubwa inayoikabili Wizara hii, naiomba Serikali iongeze Bajeti yake mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake walio wengi katika nchi hii ndio wanaoshughulika zaidi na uchumi wa nchi hii, vijijini wazalishaji wakubwa kwenye shughuli za kilimo ni akinamama. Kwani akinamama wengi ndiyo wasimamizi wakubwa sana katika shughuli za ujasiriamali na kuhakikisha watoto wanakua katika malezi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linalowakabili wanawake walio wengi ni ukosefu wa mitaji ya kuendesha shughuli za ujasiriamali. Naishauri Serikali iongeze mitaji hasa kwa wanawake wa vijijini kwani mikopo mingi inaelekezwa sana maeneo ya

mijini tu. Ni wakati sasa Serikali ipeleke mikopo hiyo maeneo ya vijijini na hasa Jimbo la Mpanda Vijijini ambako bado sana wanawake hawajawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la benki niombe Serikali ielekeze benki maeneo ya Wilaya ambako ndiko kuna walengwa kwani Benki ya Wanawake imekuwa ikiwanufaisha wanawake wa mkoa wa Dar es Salaam tu. Hivyo ni vizuri Benki hii ikatoa huduma katika nchi nzima ili iwanufaishe wanawake walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusU *NGO's* zinazoshughulikia watoto yatima naomba sana Serikali izingatie kwa makini sana kwani kuna watu wengi wamekua wakitengeneza *NGO* za kiutapeli kwa ajili ya kupata misaada ambayo haiendi kwa walengwa na kuwafanya watoto yatima kutumiwa kama kitega uchumi cha wale waliounda *NGO* hizo. Niombe Serikali ichunguze sana *NGO* hizo ambazo zinaletwa kwa madhumuni tofauti kwa kile kilicho kusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe akinamama wakatili waache tabia mbaya ya kutupa watoto kwenye majalala na wafuaatiliwe wanapobainika wachukuliwe hatua kali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana awe anatembelea katika maeneo ya nchi hii ili aone mazingira ya watoto yatima wanavyoishi na akinamama hasa wa vijijini awaone pengine anaweza kuwaonea huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ya mwaka 2011/2012. Aidha, nachumua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa Bajeti hii kwa umakini mkubwa na ameainisha mipango mizuri ya kuendeleza kuwakomboa Watanzania kiuchumi na kijamii. Bajeti hii inazingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyodhamiria kuimarisha taasisi ambazo ni majumba ya maendeleo, vyuo vya maendeleo ya wananchi vya kuwapatia wananchi maarifa na stadi ili kuwajengea uwezo, kuandaa na kusimamia rasimu za sera za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, watoto na *albino* na pia kutokomeza mila na desturi potofu katika jamii ambazo zinawaathiri kuchangia katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara hii kuwa na majukumu yake mazito yanayoigusa jamii moja kwa moja, kwa maana ya kusimamia maendeleo, heshima, utu na usawa katika haki ya kuishi. Bado kuna changamoto nyingi ambazo kwa sasa hivi inawapa shida sana wananchi na hasa wale wengi walioko vijijini kutambua na kuelewa majukumu ya Wizara hii na hasa Idara ya Maendeleo ya Jamii, yanavyowanufaisha. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa uwajibikaji wa maofisa wake walioko katika ngazi mbalimbali kuanzia mikoani, wilayani na Halmashauri ambao wanatakiwa kushuka kwa wananchi kutoa huduma na kuhamasisha jamii kujiletea maendeleo yake yenyewe.

Huduma za wataalamu hawa zinahitajika sana hasa katika ngazi ya kati hadi kaya kwani kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha pamoja na maendeleo katika nyanja nyingi kwa mfano maendeleo ya mtandao wa mawasiliano, umaskini katika jamii, tamaa ya utajiri wa haraka, ulevi wa pombe na dawa za kulevya pamoja na milipuko ya magonjwa ya mara kwa mara yote haya ymesababisha maadili yaporomoke sana na kusababisha kuwepo na watoto wengi wanaoishi katika mazingira hatarishi ambao wengi wao wako mitaani na hasa mijini badala ya kuwa shuleni au majumbani katika familia zao. Mauaji ya *albino* ni matukio ya kustua yaliyoibuka siku za karibuni. Mauaji haya yamesababishwa na imani potofu za kishirikina pamoja na tamaa ya kupata utajiri wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo wa mmomonyoko wa maadili katika jamii unatokana na umaskini uliokithiri katika jamii. Hali mbaya ya uchumi katika ngazi ya familia (umaskini), ukosefu wa ajira na kukata tamaa ya kuondokana na hali duni ya maisha, ukame katika maeneo mengi, ukosefu wa maeneo yaliyotengwa rasmi kwa shughuli za ufugaji na ukulima ambapo kumekuwa na migogoro ya kugombea ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Kushuka kwa kiwango au ubora wa elimu ambapo wanafunzi wengi wanaomaliza darasa la saba, kidato cha nne na cha sita na wahitimu katika vyuo mbalimbali hapa nchini kushindwa kupata ajira inayoweza kuwapatia kipato endelevu. Mambo yote haya yamechangia sana kuathiri uchumi na kuongeza umaskini katika jamii. Wahitimu hawa wangeweza kusaidiwa na Wizara hii kwa kuwapa mafunzo ya maarifa na stadi za kuwawezesha kuwa katika ushindani wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi, maarifa na stadi vilivyo nchini havijatosheleza kutoa mafunzo kwa wananchi walio wengi kupata kiwango cha stadi za kuwawezesha kujiajiri wenyewe hasa katika ngazi za kata. Hata maofisa waliohitimu katika vyuo hivi ni wachache mno na pia hawajaandaliwa mazingira ya kufanya kazi vijijini. Watumishi wengi wanaopelekwa kufanya kazi katika maeneo mbalimbali vijijini baada ya muda mfupi hukimbia kwa kuwa hawapo tayari kukabili hali ngumu ya maisha au umbali wa huduma za msingi, hali hii inaongeza tatizo la upungufu wa wataalamu wa fani hii vijijini. Kwa kuwa fani hii ni muhimu katika kunyanyua maendeleo ya jamii hapa nchini, ningeshauri Halmashauri zihusishwe katika kuangalia kwamba wanaokwenda katika vyuo hivi wanaajirwa katika maeneo yao. Hapa namaanisha kwamba wanaokwenda katika vyuo hivi, wachaguliwe kutoka katika kata na baada ya mafunzo warudi kutumikia katika kata zao kwani wataalamu hawa watakuwa na ufahamu mzuri wa matatizo ya kata zao kijamii, mila, imani, umaskini na hata rasilimali zilizopo ambazo zinaweza kutumika vizuri kuendeleza maendeleo katika kata husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuona matatizo ya wananchi wengi ambao hawana uwezo wala nyenzo za kukopesheka na hivyo kuhimiza na kuanzisha mfuko wa uwekezaji ambao ni maarufu kwa jina la mabilioni ya JK ambao umewezesha wananchi kiuchumi na kuongeza wajasiriamali. Mifuko hii imesaidia sana kuwezesha wanawake wengi kutumia fani, vipaji na stadi mbalimbali na wengi wao kuwa wajasiriamali maarufu. Juhudi hizi za Mheshimiwa Rais ni za kupongeza na kuunga mkono, hata hivyo pamoja na malengo mazuri ya mifuko hii, bado wananchi wengi wanaoishi vijijini hawajahamasishwa vya

kutosha kuelewa fursa zinazotolewa na mifuko hii. Ni wakati muafaka kwa Wizara hii kuhakikisha kwamba maofisa husika wanatoka maofisini na kwenda katika kila Mikoa, Wilaya, Jimbo na kushuka chini katika kata kuhakikisha wanachi wote wanashikana mikono kwa kupata fursa sawa kwa wote kunufaika na mifuko hii katika kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo, sina budi kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwa kutambua uwezo wa wanawake na juhudi zao katika kuchangia maendeleo ya Taifa hili na kuongeza ushiriki wao kwa kuwateua kuongoza katika ngazi mbalimbali za kisiasa na kiutendaji. Hili ni jambo la kuungwa mkono na wakuu wa mashirika, taasisi na vitengo mbalimbali kwa kufuata nyayo za Mheshimiwa Rais kwani naamini wapo wanawake wengi wenye elimu nzuri, uwezo, uaminifu, uadilifu na ari ya kulitumikia Taifa hili lakini kutokana na historia ya mfumo dume wanawake hawa hawapewi fursa sawa na wanaume au wanajengewa mazingira yanyowazuia kusonga mbele na kupata vyeo wanavyostahili. Hii ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia na mambo mengi wanayofanyiwa wanawake ambayo yanawatia woga na hofu ya kuyaweka wazi ili kupata haki zao. Ni wazi kwamba pamoja na kuwepo sheria za kuwalinda wanawake na makundi mengine kama *albino* na watoto, Wizara hii inatakiwa kufanya tafiti mara kwa mara za kugundua mbinu mbalimbali na aina ya manyanyaso wanayopata makundi haya na matokeo ya tafiti hizo yawekwe bayana kwa jamii na pia kuwezesha kukazia sheria ambazo zinawalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atalikumbuka Jimbo la Kibaha Vijijini kwani uchumi wa wananchi wa Jimbo hili wanategemea ufugaji na ukulima na kipato chao ni kidogo sana. Naomba kwa kuwa Jimbo hili ni changa kwa maana limegawanyika toka Jimbo la Kibaha Mjini. Katika Bajeti hii, kijengwe chuo cha kutoa maarifa na stadi mbalimbali zitakazowajengea vijana wa Jimbo la Kibaha Vijijini uwezo wa kuajiriwa na kujiajiri ili waondokane na umaskini. Ingekuwa vizuri kama chuo hiki kingejengwa katika Kata ya Mgindu ili kuwaelemisha jamii ya wafugaji kuondokana na baadhi ya mila potofu kama za kukeketa wanawake, kuoza mabinti wakiwa katika umri mdogo na kutumikisha watoto kwa kazi za kuchunga mifugo badala ya kuwapeleka shule. Chuo hiki kingesaidia sana wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini kuwajengea stadi mbadala badala ya kutegemea pato litokanalo na ufugaji au kilimo ambapo wakati wa ukame mifugo inakufa kwa wingi na pia mazao yananyauka hivyo kuwaongezea hali ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo hiki pia kitasaidia kutoa mafunzo yatakayoelimisha makundi mbalimbali, wanawake, vijana na walemavu jinsi ya kujiunga pamoja katika ushirika na kutumia rasilimali ziliko kuweza kukopesheka. Maofisa Maendeleo watakaohitimu katika chuo hicho watalenga kutoa mafunzo kwa jamii nzima ya Jimbo ili wananchi waweze kuondokana na mila, imani na maadili potofu yanayosababisha mauaji ya walemavu wa ngozi *(albino),* watoto kuishi katika mazingira magumu, ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Pia wataweza kufundisha mambo muhimu ya afya, ujasiriamali na ushirika. Kwa kuwa chuo hiki kitawakusanya wananfunzi kutoa sehemu mbalimbali itasaidia kuongeza mzunguko wa watu wenye

uzoefu, maarifa na mawazo mbalimbali vyote hivi vitachangia kuwezesha kuharakisha maendeleo si katika Jimbo la Kibaha vijijini tu bali kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawapongeza kwa kazi nzuri ambayo ni ngumu.

Kuhusu Mashirika yasiyo ya Serikali, imeripotiwa tuna mashirika 793 yaliyosajiliwa. Je, hayo Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanafanya nini. Kama tukiweka vigezo kumi au *area* kumi kubwa ambazo mengi yanachughulikia ni yapi? Ni mangapi yanashughulikia masuala ya vijana. Makampuni chini ya *BRELA* yanautaratibu au kawaida ya kujaza fomu kila mwaka kuelezea kazi zao *for record keeping*.

Je, mkakati upi upo wa kupata urejesho wa utendaji kazi wa hayo Mashirika kwa maana ya kutekeleza dira na malengo waliyoyaainisha wakati wa kujisajili. Mafunzo ya ujasiriamali 5,698 yaliyotolewa kwa wanawake ni ya muda gani *(two weeks, one week or one month) or less than a week?* Je, wangapi kati yao ni vijana wasichana umri katika ya *15 to 35 years?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba nzuri. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iweze kuijali Wizara hii kwa kuipa *budget* inayotosha kwani vyuo na Idara za Serikali wametelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vipewe walimu wa kutosha na pia idara zimekosa wafanyakazi wa kutosha. Tunaomba sheria izingatiwe ya kulinda haki za watoto na Wizara isimamie kwa ukali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Bibi Kijakazi Mtengwa, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Sera na mipango mikakati ya Wizara na taasisi hizo. Nimefurahishwa sana na juhudi wanazofanya kuzua unyanyasaji kwa wanawake na watoto. Natumaini kuwa mipango ya baadaye italenga kuzuia unyanyasaji kwa wanaume kwani yamekuwa yakitolewa bila kutangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nilifuatilia kwa muda mrefu shughuli za maendeleo ya jamii nchini. Nikilinganisha utendaji wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kuanzia miaka ya 1960 hadi miaka ya 1990 na hali ilivyo sasa utaona kuwa huko nyuma idara hii ilichangia sana maendeleo ya jamii. Ilihamasisha wananchi kuanzisha na kutekeleza miradi mbalimbali na maafisa wake walikuwa wakitembelea wananchi na kuwafundisha kwa vitendo stadi zenye kuwanufaisha kiuchumi. Naomba idara ijitathmini na kujipanga vyema na kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika jedwali namba moja takwimu za Halmashauri zilizokopeshwa kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Sijaridhika kabisa na kiasi cha fedha zinazotolewa kwa mwaka kwani ni kidogo sana. Ni vizuri Serikali iongeze fedha kwenye mfuko huo ili wanawake wengi zaidi waweze kukopa. Kwa vile mfuko huu ulianzishwa kwa sababu ya kutambua wanawake wengi hawafiki viwango/vigezo vilivyowekwa na taasisi za fedha hizi sasa haki inazidi kubadilika. Wanaume wengi hawamiliki ardhi wala mali isiyohamishika. Ni vizuri madhumuni ya kuwepo mfuko huu yarekebishwe ili ujumuishe jinsia zote badala ya kulenga wanawake pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza na kusoma hotuba ya Waziri. Kwa sehemu kubwa dhana ya jinsia haina maana kwani kwa sehemu kubwa Wizara imetoa hudumu kwa wanawake tu. Hakuna sehemu ya hotuba inayoonesha kuwa kuna mpango mahsusi kwa ajili ya wanaume. Nashauri kuwa mapungufu haya yasahihishwe ili kukuza usawa wa kijinsia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malezi kwa watoto, watoto waishio kwenye mazingira hatarishi nimeona na nashukuru kwa mikakati inayoandaliwa na Wizara ili kutatua kero ya watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi. Hata hivyo naomba kujua mpango wa muda mfupi na wa kati wa kusaidia watoto hao kujiendeleza kielimu na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Wizara inaendelea kupanga mikakati ya kuendeleza malezi ya watoto, ni vizuri kueleza mafanikio yaliyopatikana hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya maendeleo ya jamii/wananchi kwa mwaka jana nilitembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli na kukuta hali isiyoridhisha. Hakuna maji na huduma nyinignezo. Nashauri kuwa hali hiyo irekebishwe.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hotuba nzuri aliyoitoa, pia kwa kazi nzuri anayoifanya yeye pamoja na Naibu Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na wataalamu wote walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa ambayo wanawake wake ni wachapa kazi na ambao ni wazalishaji wa mazao ya chakula. Pia

watengenezaji wa kazi za mikono ikiwemo usukaji wa vikapu na ufinyanzi na kilimo cha mboga mboga.

Ushauri, naomba wanawake hawa wapewe mikopo ya kuendesha biashara zao. Shughuli za usukaji vikapu, vikundi vya wanawake wa Mufindi na Nyololo wapewe mikopo na mafunzo ya uendeshaji wa miradi yao na kuboresha ubora wa bidhaa hizo na kupata masoko. Wanawake wa kijiji cha Rungemba wanaofinyanga vyungu, wajengewe jengo la soko ili kuweza kuuza bidhaa zao. Pia kuwasaidia kujikinga na mvua, jua na hata ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake napongeza benki hii kwa kazi nzuri waliyofanya katika kipindi kifupi imeweza kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na kutoa mikopo. Naomba mikopo hii iwafikie wanawake vijijini kupitia *SACCOS* zao kwa mfano *Wanawake Iringa SACCOS* naomba Mkurugenzi wa Benki atembelee *SACCOS* hii Mkoani Iringa ili kuweza kuwapa mafunzo na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Rungemba kipate umeme wa uhakika kupitia *TANESCO.* Pia dirisha la habari (kituo cha habari) cha Rungemba kipanulie ili kuwepo na kituo kama hiki Wilaya ya Mufindi na pia vituo mikoani ili wanawake wengi waweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru, wanawake wametoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Tanzania ni moja ya nchi ya kwanza Afrika kutoa wanawake kwenye nafasi za juu duniani, ikiwa ni pamoja na Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa. Hivyo Siku ya Wanawake Duniani iwe ni siku ya mapumziko ili kuwapa fursa wanawake wote kutafakari na kushiriki kikamilifu katika maadhimisho haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi napongeza kazi nzuri inayofanywa na vyuo hivi. Nampongeza Mkuu wa Chuo na Walimu wote wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Njombe kwa kazi nzuri wanayoifanya, pia kwa ubunifu wao. Kwa kushirikiana na Taasisi ya *Tanzania Home Economics Association (TAHEA)* wameweza kutoa mafunzo kwa watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi. Chuo hiki kiongezewe rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ituambie pia mchango wa *NGO's* zinazofanya kazi katika jamii hasa katika masuala ya jinsia na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu wake Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa juhudi kubwa wanayoifanya katika kuwaendeleza wanawake pamoja na kuwajengea uwezo hasa katika ngazi ya juu *(Macro Level).* Pia nitoe pongezi kwa ujumla timu yote ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napedna kuongelea juu ya Mifuko ya Jamii yaani *NSSF, PSPF* na kadhalika kuwa mifuko hii imelenga hasa katika kuwawezesha wafanyakazi walioajiriwa. Matokeo yake wale akinamama wakulima na wafanyabiashara ndogo ndogo inakuwa ni ngumu kwao kufaidi mfuko huu, kwani kima kilichopangwa cha shilingi 16,000/= kwa mwezi *(minimum)* ni kubwa kwa mtu maskini hasa kule vijijini. Ni vyema mifuko hii iangaliwe upya kutengeneza *product* ambayo itaweza kuwachukua watu wa kipato cha chini hata kama watachangia shilingi 5,000/= kwa mwezi. Hata hivyo nawapongeza sana *NSSF* kwa kupata ushindi wa jumla wa kwanza katika Maonesho ya Sabasaba kwa kuhudumia vyema jamii yetu. Maafisa Maendeleo Vijijini/Kata wawepo na wanaume wengi walioajiriwa wapo katika maeneo mengine kama waratibu elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Jimbo Wabunge wa Viti Maalum hawana uwezo na mfuko huu lakini pia umeweza kuwa chanzo cha kuwafanya Wabunge wanawake au wagombea wanawake washindwe kupata majimbo huko mbele. Mfumo wa Viti Maalum uangaliwe upya kwani Wabunge wa Majimbo wasipofanya vizuri husababisha vyama kuadhibiwa kwa kupunguza idadi ya viti vyake maalum kwa kutumia *ratio* ya kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamlaani mwanamke mwenzetu aliyeandika habari mbaya katika gazeti la Mwananchi kwa kubeza juhudi za Serikali za kutenga Viti Maalum na kuwachukulia Wabunge wa Viti Maalum kuwa hawana tija. Ili kuharakisha uwiano wa wanawake/wanaume katika ajira/maamuzi ni vema kuwe na *time frame* ya kufikia malengo hayo 50/50 ama sivyo watu huwachukua wanawake hasa wanapoenda kwenye mikutano ili kuwaridhisha watu kuwa wanajali jinsia lakini kumbe nafasi zao ni za chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajane wanapata shida katika kudai mafao yao kutokana na utunzaji mbaya wa mafaili ya wafanyakazi. Kila Wilaya iwe na mafaili yaliyohifadhiwa vizuri na uhakiki wa taarifa za wafanyakazi ufanyike ili kuondoa usumbufu.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwa Bajeti ya Wizara, ni finyu haikidhi haja, inakatisha tamaa. Bajeti ya mwaka 2010/2011 ilikuwa shilingi bilioni 19.8 na Bajeti ya mwaka 2011/2912 ni shilingi bilioni 16.2 tu tofauti ni shilingi bilioni tatu takribani 18% kwa ufinyu huu wa Bajeti. Wizara hii itawezaji kusimamia majukumu yake? Majukumu ya Wizara kama yalivyo katika ukurasa wa vii ni mazuri na endapo yakitekelezwa jamii yetu ya Kitanzania itapata maendeleo ya kutosha, nashauri Serikali iangalie namna ya kuongeza Bajeti hii na kuongeza mwaka hadi mwaka badala ya kupunguza kila mwaka tena punguzo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni *cross cutting* na katika Halmashauri zetu za wilaya mipango mbalimbali ya miradi, Maafisa Maendeleo ya Jamii wanaachwa pembeni, ni vema hawa wangehusishwa moja kwa moja kwa kuwa ndiyo wapo karibu na wananchi wao, wanawake kwa wanaume, amani Maafisa Manedeleo ya Jamii nafasi zao zilikuwa zinatambuliwa sana katika jamii kutokana umuhimu wake. Nashauri, Wizara

iwawezeshe watumishi/Maafisa Maendeleo ya Jamii, iwajengee uwezo ili katika kazi zao za kila siku katika Halmashauri za wilaya wawe chachu na kichocheo cha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Bajeti ya Wizara ya shilingi milioni 300/= inawezaje kuvikwamua na kuviwezesha kufanya kazi zake vema? Vyuo vimechakaa, majengo mabovu, havina wakufunzi wa kutosha, havina vifaa vya kufundishia kama karakana. Kwa Bajeti ya mwaka huu Wizara imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Sofi – Ulanga, Serikali haioni kwa utaratibu huu wa chuo kimoja kwa mwaka mmoja itatuchukua miaka mingi kukamilisha ukarabati wa vyuo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vimeongezeka sana, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na *National Multi Sector Task Force* 28% ya wasichana na 13% wavulana chini ya umri wa miaka 18 wanabakwa na kulawitiwa na 72% ya wasichana wanapigwa mangumi, makofi na mateke na wavulana saba kati ya kumi wanafanyiwa vitendo vya ukatili huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili huo unafanywa na ndugu wa karibu na mara nyingine hairipotiwi, ni vema Serikali ikaingilia kati suala hili kwa nguvu sana ili kupunguza idadi ya watoto wa mitaani, ukatili dhidi ya watoto unasababisha kwa kiasi kikubwa kuwa na watoto wa mitaani na kukosekana kwa upendo katika jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majukumu yake ya kiidara ni kuwawezesha wanawake kisheria kufuatilia urekebishaji wa sheria zinazowakandamiza wanawake na kutunga sheria zitakazohakikisha wanawake wanapatiwa haki zao za msingi. Kwa kipindi kirefu inaonekana hakuna marekebisho ya sheria yaliyofanyika kwa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mirathi ya Kiserikali, hizi mbili zinakinzana na Katiba ya nchi na Mikataba ya kimataifa. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inawataka watoto wa kike waolewe kwa umri wa mwaka 16 au 14/15 kwa ridhaa ya Mahakama. Athari zake ni nyingi sana, kisaikolojia, kifamilia, kijamii na kiuchumi. Mara nyingi Wabunge wanauliza maswali hapa Bungeni kuhusu sheria kandamizi. Ni wakati muafaka sasa Wizara iharakishe mchakato wa kuendesha mjadala wa Kitaifa *(white paper)* ili sheria hizo zirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 Tume ya Kurekebisha Sheria ilitoa taarifa kwa Waziri wa Katiba na Sheria na kupendekeza umri wa kuoa uwe miaka 21 kwa mwanaume na miaka 18 kwa mwanamke, mpaka sasa ni miaka 17. Wizara inawaambia nini wanawake wanaowaongoza kupitia Wizara hii? Tukumbuke kuwa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 haikugusa umri wa mtoto wa kuolewa au kuoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nawasilisha.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwanza napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Naibu wake mahiri kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha kuwa wanawake wanasonga mbele na katu hawatarudi nyuma na napenda kuchangia machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la Bajeti kuandaliwa kwa kuangalia jinsia. Natambua juhudi zinazofanywa na Wizara kuhakikisha kuwa Bajeti zetu zinazingatia masuala ya jinsia katika ugawaji wa rasilimali za nchi yetu lakini changamoto bado ni kubwa na mimi naendelea kuishauri Serikali iliangalie suala hili kwa makini kwa sababu ili mipango mingi itekelezeke ni lazima wanawake washiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Wanawake ya mwaka 2000 inatueleza kuwa asilimia 60 ya chakula kinachozalishwa vijiji wazalishaji ni wanawake. Sasa je, tunaweza kutekeleza Kilimo Kwanza kama tutamuweka mwanamke pembeni kwenye fursa ya kukopeshwa zana za kilimo na pembejeo. Hii haiwezekani ni lazima Wizara isimame imara kuhakikisha kuwa dawati la jinsia linafanya kazi katika kila Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kuendelea kushuka kwa Bajeti ya Wizara kila mwaka. Mwaka 2010/2011 ilikuwa shilingi bilioni 19 na mwaka huu wa 2011/2012 ni shilingi bilioni 16. Je, Bajeti hii itawezaje kumkwamua mwanamke aliye kijijini? Mwaka 2009/2012 tulikuwa na kauli mbiu inayosema miaka 15 baada ya Beijing wanawake wanaweza wapewe nafasi. Ni kweli wanawake tunaweza basi Bajeti ya Wizara hii ambayo ni mtambuka ipate pesa ya kutosha ili wanawake wapate mitaji ya kutosha na waoneshe uwezo wao wa kujikwamua kiuchumi. Ahsante.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inakinzana na sheria ya mwaka 2009 juu ya umri wa kufunga ndoa. Sheria hii ipo haja ya kufanyiwa marekebisho ili kuwaokoa watoto wa kike waweze kupata muda wa kupata elimu, kupevuka kwa akili itakayomwezesha mtoto huyu wa kike kuweza kuhimili mambo yanayoikabili familia ndani ya ndoa, ikiwemo kuzaa na kumlea mtoto/watoto akiwa na akili iliyopevuka. Hivyo naishauri Serikali kubadili sheria hii kwa mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 18. Kwani kuzaa akiwa na umri mdogo kuna hatarisha maisha yake. Hivyo elimu iendelee kutolewa kwa wazazi ili kuepukana na kumruhusu mtoto kuolewa chini ya umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendo vya ukatili, lipo tatizo upande wa vyombo vya sheria vikiwemo polisi na mahakama kutokuwa na maeneo maalum *(chamber)* yatakayowawezesha wanawake kujieleza kwa uhuru zaidi juu ya matukio yanayowakuta watoto/wanawake kubakwa kikatili, kushindwa kutamka lugha au matamashi mabaya mbele ya hadhara ya watu wengi. Hivyo nashauri Serikali, vituo vya polisi na mahakama kuwepo maeneo ya faragha ambayo wanawake/watoto wa kike wanaweza kujieleza bila woga hii itasaidia kupatikana ushahidi mzuri utakaowezesha kuwatia hatiani wale wote wanaohusika kufanya udhalilishaji huo wa kikatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto wa mitaani, tatizo hili linakuwa kwa kazi katika nchi yetu hasa kutokana na wazazi hususani wanaume kutelekeza familia zao na wanawake wengi bado hawana uwezo wa kuzilea familia hizo na ndipo inapelekea watoto wengi kuanza kujitafutia riziki kwa kuzurura mitaani, kuacha shule na kadhalika.

Aidha, ndoa za utotoni nazo zinachangia kwa asilimia kubwa kwani uwezo wa kuwatunza watoto wanaozaliwa unakuwa mdogo kutokana na kutokuwa na uchumi na kumwezesha kumlea mtoto wake. Napenda kuishauri Serikali ili mtoto apate haki zake, kila mzazi/wazazi awajibike kulea watoto wao kwani kila mtoto anayo haki ya kuishi, kupata elimu na kusikilizwa. Hivyo Wizara ya Afya iimarishe Kitengo cha Kamishna wa Ustawi wa Jamii ngazi ya Mkoa/Wilaya na Kata ili waweze kujua watoto ambao hawapati haki ili waweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayowakabili wanawake napenda kuishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wanawake ili wajue haki zao. Kuwasaidia wanawake mikopo ili waweze kujiendesha kiuchumi na waweze kupata kipato cha kuendesha maisha na familia zao.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia kuwa hali ya uzima na kuweza kunifikisha katika Bunge lako Tukufu, nikiwa na hali ya uzima. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba yake nzuri iliyojaa hekima na matumaini kwa Watanzania ambao wanahamu ya maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba hii kwa kujikita upande wa watoto wa mitaani (ombaomba). Watoto hawa imekuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu, imepelekea kuwa hata nchi yenyewe kuwa na mtazamo mwingine juu ya watoto hawa lakini ukiangalia kwa dhati hakuna mtoto asiye na mzazi au asiye na kwao. Kwa maana hiyo watoto wote wana wazazi wao na familia zao. Siku hizi ombaomba imekuwa ndio mchezo katika baadhi ya miji nchini na wazazi wa watoto hao wamegundua ni kazi kama kazi nyingine ambayo inamuingizia kipato. Nashauri tutengeneze sera maalum juu ya watoto hao ili kuweza kuiondoa hali mbaya ya watoto hao, kwani nao ni miongoni mwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nichangie kwenye upande wa unyanyasaji wa jinsia. Unyanyasaji unazidi katika jamii zetu, watu wamekuwa wanayafumbia macho kana kwamba hawaoni athari yake kwa jamii. Jamii imekuwa ikiendelea na ukeketaji wa wanawake, upigaji wa wanawake, hata kuwanyima mirathi na kuwaweka katika maisha duni. Naishauri Wizara ijikite katika kutoa elimu kwa jamii na elimu hiyo zaidi ijikite vijijini ndio sehemu ambayo inaongoza kwa unyanyasaji, bila ya kuelimishwa watu hawa huwezi kuwatungia sheria na ikaweza kufanya kazi. Kwani ni bora kuwaelimisha ili kuweza kujua madhara yake, hapo ndipo tunaweza kutunga sheria kali dhidi ya ukatili wa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara hii haiwezi kuiwezesha kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika sera ya jamii toleo la Juni 1996 yaani kuongezeka kwa kipato kinachowezesha kaya katika jamii kukidhi mahitaji yao, kuongezeka kwa huduma za jamii kama nyumba bora, afya, elimu, lishe na kadhalika, Wizara hii ndiyo inapaswa kupima hatua za mendeleo ya watu, kukusanya takwimu za walemavu, wajane, wazee, yatima, watoto wa mitaani Ili ishauri sera za kuweka ulinganifu wa mahusiano. Kazi hii inahitaji Bajeti inayotosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi wamekuwa na mwamko wa kujiendeleza katika nyanja ya kilimo na biashara. Walio wengi hupata mitaji kupitia mikopo na hasa kupitia mashirika binafsi kama *PRIDE* na *FINCA.* Wanawake wanakopa katika mashirika haya kwa sababu hawawezi kutimiza masharti ya mabenki. Mashirika haya yapo kibiashara na yanatoza riba kubwa. Hayana mahusiano na wateja kufuatilia na mwenendo wa biashara kwa wateja wao na hasa pale wanapokwama marejesho mkopo. Wanawake hudhalilishwa kwa kunyang'anywa mali zao hasa vifaa vya ndani. Napenda kujua udhibiti wa Serikali juu ya mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya sheria ya uraia mwanamke ambaye siyo Mtanzania anaweza kupata kibali cha kuishi nchini kwa sababu ya kuwa ameolewa na mwanaume Mtanzania. Mtanzania aliyeolewa na mwanaume ambaye si Mtanzania, mwanaume huyo hawezi kupata kibali cha kuishi nchini Tanzania na anapaswa afuate utaratibu uliowekwa kisheria ambao ni pamoja na kuwa amekaa nchini kwa kipindi kisichopungua miaka mitano, pale muda wa kuishi nchini utakapokuwa unajumlishwa na awe katika kila kipindi alichoomba uraia amekaa nchini kwa miezi 12. Sheria hii ni mfano wa sheria za kibaguzi kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee malalamiko ya wafanyakazi wa Wizara hii. Wanalalamikia Bajeti ya Wizara hii ambayo husababisha watendaji hawa kukosa nyenzo za kufanyia kazi. Pia wanalalamika kukosa uwezo wa kuendesha vyuo vilivyopo mkoa wa Kagera Chuo cha Gera Wilaya ya Missenyi, Rubondo Biharamulo na Ilemera Ngara. Pia kuna Chuo cha Migara Bukoba Vijijini, chuo cha walemavu. Vyuo hivi vilikuwa vinatoa mchango mkubwa kwa kuelimisha Wanakagera wa umri mbalimbali ngazi ya chini kabisa walikuwa wanapata stadi na manufaa katika kilimo, ufundi, usanifu na hata usanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri anieleze hatima ya vyuo hivyo nilivyovitaja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo wanajituma katika kuleta harakati za kimaendeleo na kuhakikisha wanawake wa Kitanzania wanachangia katika kuleta mapinduzi ya kimaendeleo nchini. Kuanzishwa kwa Benki ya Akinamama ni moja ya viashiria ambavyo vinaleta chachu kumkomboa mwanamke wa Kitanzania kutoka katika mfumo dume ambao uliwagubika kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kila sababu kwa wanawake wa Tanzania kusherehekea miaka 50 ya Uhuru wetu wakiwa na matumaini makubwa ya kusonga mbele. Mbali ya uchumi wetu kutetereka kutokana na mambo mbalimbali na matukio kadhaa kuikumba dunia ikiwemo na mabadiliko ya tabia nchi lakini wameweza kuzalisha wajasiriamali wengi kwa kupitia *SACCOS* na *VICOBA*. Nampongeza Rais Jakaya Kikwete kwa kuona umuhimu wa wanawake katika nchi hii na kuwapanga katika nyadhifa mbalimbali Serikalini na kuwaongezea mtaji Benki ya Akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni msemo mzuri wa Kiswahili unenao; "abebwaye hujikaza." Ni wakati wenu umefika na ninyi kuonyesha uwezo wenu katika kusaidia, kuongeza na kunyanyua Pato la Taifa ili isijekuonekana ya kwamba mwanamke wa Kitanzani ni mzigo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri bado haijaonyesha ni kiasi gani wanawake wanaweza kuchangia katika Pato la Taifa. Wakati wa kukaa na kulalamika umekwisha ni wajibu wenu sasa kusimama kidete na kutetea maslahi yenu hasa katika suala zima la kufaulisha wanafunzi. Umangimeza/unyanyaswaji, rushwa ya ngono katika maeneo ya ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wa mitaani, ni kweli mtaa hauzai mtoto lakini ngono zembe, ukali wa maisha, ukosefu wa huduma muhimu, mgawanyo mbaya wa rasilimali za Taifa na umaskini huzaa watoto wa mitaani. Watoto wa mitaani hukumbwa na matatizo makubwa na kuvunjiwa haki zao za msingi na kufanyiwa vitendo viovu vya kulawitiwa. Kesi nyingi zimeweza kuripotiwa katika vyombo vya sheria lakini inaonekana bado Wizara haijalishughulikia suala hili na kesi nyingi bado zipo mahakamani huku watuhumiwa wakiendeleza vitendo viovu vya ubakaji na kuwalawiti watoto hao kwa kuwashawishi kwa vitu vidogo vidogo. Wimbi hili la kulawitiwa watoto sasa hivi limekuwa kubwa na linaashiria hali ya hatari kwa nchi yetu kwani litazalisha walawitiwa wengi ambao baadae wanaweza kulitia doa na msukosuko Taifa letu. Mfano, ni jamii ya jinsia moja kuitaka Serikali kutambua na kuhalalisha ndoa zao kitu ambacho kinakwenda kinyume na maadili na mila zetu za Kitanzania na zinakinzana na sheria za dini zetu. Wakati umefika kwa Wizara hii pamoja na Serikali kwa ujumla kutoa/kutangaza kaulimbiu ya kupiga vita ulawiti na usagaji hususan kwa watoto wetu, pia naiomba Wizara kuitisha mjadala wa Kitaifa utakaojadili suala zima la unyanyasaji huu wa watoto kwa njia ya kulawitiwa au kusagana, ili kujenga Taifa lililo imara baadaye.

Pia Serikali kupitia Wizara hii kuziangalia upya sheria zote zinazohusiana na unyanyasaji huo ili ziwe na nguvu zaidi. Pia Wizara itafute wanasheria watakaosaidia kutoa msaada wa kisheria kwa wale wote wanaothirika na matatizo niliyotaja pamoja na ubakaji. Ikiwezekana Wizara kuwa na mahakama yake itakayoweza kutoa haki kwa madai hayo. Wizara iombe kufuta Sheria ya *PF 3* ambayo hutolewa na polisi kwa muathirika kabla ya kuchunguzwa au kupatiwa matibabu na ni vyema muathirika atibiwe/kuangaliwa kwanza na baadaye ndio apatiwe *PF 3* kwa ajili ya kufungua mashtaka.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumuuliza Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuwa

katika Fungu la 53 inaeleza kukusanya shilingi 1,000 tu katika mwaka 2010/2011 kwa kuuza vifaa chakavu (ukurasa wa 2) lakini ndani ya Bajeti ya mwaka 2010/2011 uliomba zaidi ya shilingi milioni 85.4 kununua samani na kompyuta mpya. Je, hivyo vilivyochakaa viliuzwa kwa shilingi 1,000 tu? Kama vimeenda wapi? Havijatolewa maelezo.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa shukrani zangu za dhati kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kushiriki kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika kuchangia hotuba hii, kwanza ningependa kujua wao wanawake je, wanajua umuhimu na ukubwa wa nafasi waliyonayo? Mwanamke ni chombo muhimu sana katika jamii popote duniani. Mwenyezi Mungu amemtukuza na kumpa heshima kubwa. Heshima ya kwanza kama hayupo mwanamke basi dunia ingekuwa duni sana kwa sababu watu wasingeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke yeye mwenyewe kwanza anatakiwa ajenge heshima yake mwenyewe, mwanamke ajiheshimu kwa tabia nzuri katika shughuli mbalimbali, ikiwemo malezi bora na uzazi bora ambao ni msingi wa kuindeleza dunia bora. Jambo baya sana ambalo ni dhambi kwa wanawake ni kuchukua mimba kwa hiyari kisha wanapojifungua wanawatupa watoto au wanazika na roho. Hili ni jambo baya sana na ambalo haliwezi kuvumilika.

Mimi naomba Serikali ipange mipango maalum kwa akinamama wenye tabia hii mbaya Serikali iweke ofisi maalum ambayo ipokee watoto wachanga wasiotakiwa na wazazi wao. Serikali iandae malezi mazuri kwa watoto kama hawa. Baada ya kuandaa malezi mazuri mwana mama yoyote atakayemtupa mtoto lazima apewe adhabu kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumza kuhusu maambukizo ya UKIMWI kwa akinamama. Serikali inafanya juhudi kubwa kudhibiti gonjwa hili hatari la UKIMWI. Pamoja na kwamba UKIMWI unaambukizwa kwa njia tofauti lakini njia kubwa ni kujamiiana. Mimi nasema bado Serikali imekosa udhibiti wa vyanzo vya maambukizi ya UKIMWI. Umbile la mwanamke yeyote pamoja na uhuru alionao lakini inapasa avae nguo ambayo itamuhifadhi vizuri ili kuondoa vishawishi kwa wanaume wenye roho nyepesi. Kinyume na hilo akinamama wanavaa nguo ambazo hazisitiri maumbile yao, hivyo wanawashawishi wanaume. Kwa hiyo, utakuta UKIMWI haumaliziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri Serikali pamoja na uhuru wao lakini Serikali iwaongoze vizuri katika kuvaa nguo ambazo nzuri na zenye kusitiri. Hakuna uhuru usio na mipaka na uhuru wenye madhara si uhuru mzuri. Mimi naomba tuchunge UKIMWI ni hatari kwa Taifa. Ahsante.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepewa dhamana ya kushughulikia masuala ya watoto ikiwemo matatizo yanayowakabili watoto yatima, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kufuatilia mikataba na sheria mbalimbali zinazohusu kusimamia haki za watoto. Kwa mujibu wa majukumu ya Wizara utaona Bajeti iliyopitishwa kwa mwaka 2011/2012 haitoshelezi kabisa Wizara kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wamekuwa wakikandamizwa na sheria mbalimbali za kimila na mfumo dume, kwa sasa wanawake wamepIa hatua kubwa katika kujikomboa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Wanawake pamoja na majukumu ya kifamilia wameweza kujishughulisha na ujasiriamali na shughuli zingine za kuongeza kipato cha familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo yenye dhamana ya kusimamia shughuli za wanawake na kuhakikisha wanapata mafunzo ya kuwajengea uwezo. Naiomba Serikali katika Bjeti ijayo naomba iongeze Bajeti ya Wizara hii ili iweze kuwafikia wanawake wengi na kuratibu shughuli mbalimbali za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote natanguliza shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hoja hii katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nitoe shukrani zangu kwa Waziri anayehusika na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuwasilisha hotuba hii iliyojaa vipaumbele na mikakati inayoelekeza matumaini kwa wananchi wa Taifa letu. Wasiwasi wangu ni kutokuwa na fungu dogo lililotengwa kwa Bajeti ya Wizara hii nyeti, ambayo ndiyo inayohitajika kutoa heshima ya mwanzo katika suala zima la malezi na maadili ya watoto na wanawake ambao ndio wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahitaji kupanga mikakati rasmi na ya uhakika kuhusu maadili. Maadili ya watoto wetu yameshuka kwa asilimia 50 na hii inasababishwa na Serikali yenyewe. Hii inatokana na kuacha mila na utamaduni wetu ulio bora na kutoa visingizio vya haki za binadamu na haki za mtoto japokuwa ulezi kufuatana na mila zetu, malezi mengine yamepitwa na wakati lakini zipo taratibu nyingine zinafaa na zimeachiliwa mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la UKIMWI limesababishwa na mambo tofauti mfano, ulevi, uzinifu na kadalika. Suala la maambuzi ya UKIMWI, Serikali inachangia kwa kiasi fulani si kosa kuruhusu starehe, lakini kutokana na leseni na vilabu vya pombe kuruhusiwa kupita kiasi, ulezi na uzinifu umezidi kupita kiasi, kwa sehemu kubwa unapotokea unyanyasaji sababu zake nyingi hutokana na watu wanaotumia ulevi kupita kiasi. Ahsante.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nachukua fursa hii

kuipongeza Wizara na watumishi wote pamoja na Serikali kwa jitihada wanayofanya katika kuleta na kuhamasisha maendeleo katika jamii, watoto na masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali iangalie namna ya kuwapatia Maafisa Maendeleo ya Jamii usafiri na nyenzo za kufanya kazi hasa katika maeneo ya vijijini. Pia Serikali kupitia TAMISEMI ingetoa maelekezo katika Halmashauri zetu nchini Idara hii nyeti na muhimu ipewe pia fursa, umuhimu na Bajeti kutokana na fedha za ndani. Mara nyingi Maafisa Maendeleo wa Jamii wanashindwa kutimiza wajibu wao kwa kukosa fedha, usafiri na Bajeti finyu inayotokana na fedha ya maendeleo kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu zaidi ingetolewa katika vijiji, shule zetu za sekondari na vyuo mbalimbali ili sheria zote zifahamike na pia maoni mbalimbali kutoka katika jamii yachukuliwe ili baadhi ya sheria zirekebishwe. Pia naishauri Serikali kuchunguza baadhi ya *NGO's* na watu binafsi ambao wamegeuza watu wenye hali duni ya maisha na watoto yatima na watoto wa mitaani kuwa mitaji katika maisha yao. Wasamaria wengi wenye nia ya kuchangia wamekata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Jimbo langu la Babati Vijijini hakuna chuo cha aina yoyote na pia vikundi mbalimbali ya akinamama vijana na wenye matatizo mbalimbali kuhusu msaada wa mtaji, mikopo na fursa ya kupata huduma za kisheria. Naishauri Benki ya Akinamama ya mkoani Manyara kufungua tawi ili akiwamama wa Manyara wapate mikopo. Pia hatua kali zichukuliwe na vyombo vya dola na Serikali dhidi ya wanaotumikisha watoto katika ajira. Pia kuchukua hatua za kisheria dhidi ya ndugu, wazazi, walezi wa watoto wanaonyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri vyuo vianzishwe mahali ambapo hakuna mfano Jimbo la Babati vijijini, kuna Chuo Mbulu ambacho kinahitaji msaada mkubwa na pia kituo cha elimu ya watoto wenye ulemavu wa kusikia na kuongea Dongobesh inayomilikiwa na Kanisa pia kinahitaji msaada mkubwa. Kwa sehemu kubwa mjini ndipo huduma na sheria ndiyo inapewa msukumo. Vijijini bado maisha ni duni kwa vikundi vya akinamama, vijana na walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isaidie Kituo cha Muleya wasiokuwa na uwezo magugu (Ustawi wa Jamii) hali ya majengo, vifaa mbalimbali vya muhimu hakuna na viliopo vina hali mbaya sana. Maji ni ya shida kabisa. Nawashauri wenye mifuko mbalimbali pia watoe huduma yao vijijini na wasiishie mjini au maeneo jirani na mjini tu. Wengi wenye kukopeshwa huwa ni wajanja wa mjini au ambao wanajua na viongozi mbalimbali wilayani na wenye mfuko, lakini wale wa vijijini huwa hawapati kabisa. Mfano mwingine ni ule mfuko wa Mheshimiwa Rais wa mabilioni ya JK. Mkoa wa Manyara hasa Jimbo la Babati Vijijini haukupata hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ingekuwa mstari wa mbele ya kufungua njia na kuwaonesha jamii ya vijijini mahali pa kupata mikopo, misaada na huduma ya kisheria ili wanyonge wasinyanyasike. Pia sheria ya ndoa na ya watoto ungerekebishwa mapema

ili akinamama wapate haki, watoto yatima wapate haki na pia watoto wa mitaani wapate haki, wengine wanazo familia na huwatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri Serikali ingekuwa inatoa fedha nyingi katika Wizara hii na vifaa mbalimbali ya usafiri ili wataalamu wetu wafanye kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante na nashukuru.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Pamoja na kazi nzuri ya Wizara naomba nichangie haya machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania inafanya kazi nzuri lakini bado haijaweze kuwasaidia akinamama wengi ambao wanaishi vijijini na pia masharti ya mkopo haipishani sana na mabenki ya kawaida ya biashara. Nashauri huduma hii nyeti ya Benki iweze kufikishwa ngazi ya Mkoa na Wilaya ni wanawake walio wengi waweze kunufaika na kazi nzuri ya Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iangalie namna ya kuzuia ukeketaji, hakika mila potofu isipewe nafasi na wasichana wapewe ulinzi wa kisheria katika karne hii ya 21. Ni jambo la kushangaza Serikali ambayo inaongelea masuala ya teknolojia inashidwa kuzuia ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara hii ni makubwa mno, huduma hii bado haijaweza kunufaisha akinamama na watoto wengi waishio vijijini, wanawake wengi wa vijijini wananyanyaswa sana na waume zao, pia wanaume wengi wa vijijini wanadhani kwamba kumzalisha mwanamke watoto wengi ni ishara ya kuwa mwanaume wa kweli, hawafahamu kwamba kuzalisha mwanamke mmoja watoto wengi ni kumdhoofisha kiafya, elimu kama hiyo haijawafikia wengi vijijini. Lakini pia kuna wanaume wengi vijijini ambao wanaoa wake wengi ili tu kuongeze nguvukazi katika mashamba yao ambapo baada ya mavuno na mauzo baba anatumia kiasi kikubwa cha fedha ya mauzo yao ya mwaka mzima katika mpango usio sahihi au kutumia fedha hizo kwa kuoa mke wa ziada. Elimu itolewe ili akinamama waweze kuhusika kupanga Bajeti za familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna haja ya kulinda haki za watoto wetu, sidhani kama kuna mkoa wowote Tanzania ambao hauna watoto wa mitaani, ni jambo ambalo kwa sasa linachangia sana kusababisha watoto wa kike kuingia katika biashara ya ukahaba ambayo inaendeleza kueneza magonjwa ya zinaa pia kuongeza idadi ya watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Bajeti kwenye ukurasa wa 51 Wilaya ya Uyui na Mkoa wa Tabora, wilaya ambayo ina Majimbo mawili ya uchaguzi, Wizara hii ndani ya miaka mitano iliyopita imeweza kutoa mkopo kwa akinamama jumla ya kiasi cha shilingi milioni nane tu. Wizara iangalie upya namna ya kusaidia wanawake waishio vijijini.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake wengi wameanzisha Vikundi vya *SACCAS* na *SACCOS,* wameitikia vizuri wito huu, lakini bahati mbaya hawajaweza kupata elimu ya ujasiriamali; hivyo kutokana na ukosefu wa elimu hiyo, wameshindwa kukopa kwenye mabenki. Nilikuwa ninaomba Serikali itenge pesa kwa ajili ya kwenda kutoa elimu ya ujasiriamali maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu inayofundishwa ni ya kuweka na kukopa, lakini elimu hasa ya ujasiriamali haiwezi kuwafikia Wananchi. Ninaomba Serikali itenge fedha ili kupeleka elimu ya ujasiriamali kwa Wananchi ili Wanawake wengi waweze kuamka kwa kupatiwa elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZAYNABU M. VULU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote, kwa juhudi zake kwa Watanzania na kusimamia harakati za Ukombozi wa Watoto, Wanawake na Wanaume. Pia ninakuchukua nafasi hii, kuiuliza Serikali ni lini Wizara hii nyeti kwa jamii itapata fungu angalau la kuweza kuwawezesha kufanya kazi zao kwa umakini na kuwafikia walengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wimbi kubwa la unyanyasaji wa Watoto wa Mitaani na ongezeko la Watoto hao wanaotokana ama kwa kufiwa au kutokuwa na walezi kwenye familia au migogoro ya wazazi. Je; ni mkakati gani mahususi ambao Serikali imepanga ili kupunguza tatizo hilo au kulitokomeza kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiulizia na kufuatilia suala la Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ambayo kuna baadhi ya mambo yamepitwa na wakati. Je, Wizara katika hili imejipangaje na tuitarajie lini kuletwa hapa Bungeni ikiwa pamoja na Sheria ya Mirathi? Marekebisho ya Sheria hizi yatasaidia sana kupunguza matatizo mengi ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kupunguza Watoto wanaoishi katika mazingira magumu (Watoto wa Mitaani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali inieleze toka Sheria ya Kujamiiana ianze kutumika nchini; je, imepunguza matatizo ya udhalilishaji na ubakaji kwa kiasi gani? Kama tatizo linazidi kuongezeka; je, kuna upungufu wowote uliojitokeza? Je, kuna mkakati gani wa kuboresha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninarudia kusema kwamba, Serikali iiangalie kwa umakini Wizara hii kwa kuwaongezea fedha za bajeti yake. Baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake tangu ianzishwe inahudumia Wanawake wa Dar es Salaam tu; ni lini itawafikia Wanawake vijijini hadi Mvomero?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGOs* zinahangaika kulea Watoto wa Mitaani na waishio katika mazingira magumu, lakini Serikali haichangii kwa kiasi kikubwa kumudu gharama za kuendeshea vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inatengewa fedha chache wakati ni Wizara mtambuka. Ninaishauri Serikali iitengee fedha za kutosha Wizara hii.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la unyanyasaji na ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na *Albino* bado lipo na linatakiwa kuendelea kupigwa vita. Je, Serikali haioni kuwa bado elimu inatakiwa itolewe kwa njia ya kuonesha filamu Wananchi wengi watahamasika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watoto wa Mitaani, limekuwa ni tatizo la muda mrefu sasa; je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na wimbi hili?

**MHE. WARIDE BAKARI JABU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuchangia kwenye Benki ya Wanawake. Kuna taarifa zisizo rasmi kuwa, kuna ubadhirifu mkubwa na hii italeta tatizo la Benki hiyo na huenda ikafilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kujua utendaji wa Benki ya Wanawake kwa mwaka 2009/2010 na 2010/2011 ilipata faida au hasara ya kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii, lakini kuna tatizo la *under utilization,* matumizi ya vyuo hivi kulingana na majengo yake yalivyo mazuri na elimu inayotolewa ni ndogo; kwa mfano, upishi au ushoni kwa *intake* ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iangalie kozi zitakazoendeleza Wanawake katika kuongeza kipato au kuweza kupata cheti kitakachomfanya apate ajira na kadhalika. Hivyo, jitihada ziwekwe kwa kuimarisha Elimu ya Amali (Mitaala).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kufanya jitihada za kumkomboa Mwanamke katika nyanja mbalimbali, lakini bado tunaona Watanzania hasa Wanawake, wapo nyuma kipato. Wanawake wengi ndiyo wanaohudumia jamii (Watoto, Wazee, Wagonjwa na kadhalika), lakini hawapati fursa za kuongeza kipato. Hii utaiona unapotembea barabarani, Wafanyabiashara wengi wa kipato kidogo ni Wanawake wanauza kwa ajili ya kupata chakula tu cha leo au siku na hawawezi kuongeza mtaji ili biashara zao ziweze kupata faida. Hivyo, tunaomba Wanawake wawezeshwe kwa mitaji na ujasiriamali. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwawezesha Wanawake hasa wa vijijini kuongeza kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuwadhibiti Wanaume wanaowatelekeza Watoto na Wake zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuwadhibiti Wanawake wanaotembea na Watoto wao barabarani au sehemu mbalimbali wakiwaongoza kuombaomba na Wanawake hawa ni wazima na wanakuwa na afya za kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukombozi wa vijana wa jinsia zote ni kupatiwa elimu bora kwa kujikomboa katika maisha yao. Kwa Jimbo langu la Kisarawe, ninaomba Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kiwezeshwe vya kutosha ili vijana waweze kupata elimu bora ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwezeshaji kwa akina mama ni muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu. Ninaiomba Serikali itumie Mifuko ya Jamii iliyopo nchini mwetu kuiwezesha Benki ya Wanawake ili kuwapatia mikopo Wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu, wanafanya kazi kwa kiwango cha chini sana. Idara zimesheheni Wataalam wengi wenye sifa, lakini ubunifu wa Miradi umekuwa ni wa kiwango cha chini sana. Ninaiomba Wizara iangalie kwa kina Idara za Maendeleo ya Jamii, kwa kuwaweka Wakuu wa Idara ambao wataleta mabadiliko ya kweli katika Halmashauri zetu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Taifa letu. Nami niungane naye kusema kuwa, Wizara hii ni muhimu sana kwa Ustawi wa Jamii yetu. Hata hivyo, ninasikitika kuwa Wizara hii hutengewa fungu dogo ukilinganisha na wajibu ilionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo inayoshughulika na maisha ya kila siku ya Wananchi wetu, lakini ndiyo yenye bajeti ndogo kabisa katika Serikali Kuu na hata kwenye Halmashauri za Wilaya. Uendeshaji wa shughuli zake unategemea sana ufadhili wa nje kiasi kwamba, inaifanya Wizara iwe tegemezi. Tufahamu kwamba, mara

nyingi fedha ya nje huwa ina masharti yake kiasi kwamba, mipango au vipaumbele vyetu vinaweza visizingatiwe na wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja kubwa kwa Watumishi wa Idara walioko Wilayani na Vijijini/Katani kwanza ni wachache mno ukilinganisha na mahitaji, lakini pia hawana vitendea kazi hususan vyombo vya usafiri. Kazi za hawa watu siyo za maofisini zaidi, sasa kama hawana usafiri wanafanyaje kazi? Ninaiomba Serikali kama ilivyofanya kwa Walimu, izalishe pia wafanyakazi wengi wa Maendeleo ya Jamii ili kukidhi mahitaji, ikiwezekana walau kila Kata iwe na Afisa Maendeleo. Pia Serikali iweke utaratibu wa kuwakopesha vyombo vya usafiri ili iwawezeshe kufanya kazi kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja muhimu, Watendaji hawa wangesaidia kuimairsha na kuanzisha vikundi vya kiuchumi vya akina mama, kuwasaidia kuelewa ujasiriamali ili waweze kujikomboa kiuchumi. Watendaji hawa wawe wanapewa malengo yanayopimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani. Pamoja na mambo mengine, hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na umaskini wa familia. Hapa ndipo inapojengwa ulazima wa Wizara hii kujielekeza katika uchumi wa ngazi ya familia. Ongezeko hili la Watoto wa Mtaani ni bomu linalosubiri wakati; ni hatari kubwa. Bahati mbaya sana, Serikali imelitekeleza jambo hili kwa Taasisi zisizo za Kiserikali na ambazo zina uwezo wa kuhudumia watoto wachache tu. Hivi Serikali haioni wajibu huu au inasubiri makundi makubwa ya vijana watakapoanza kuhamasishwa na Vyama vya Upinzani kufanya maandamano yakishinikiza kuangushwa Serikali kama ilivyotokea Misri, Tunisia na Yemen? Kundi hili lisipoongozwa sasa ndilo litakalosababisha machafuko katika nchi, kwani wao wapo tayari kuandamana kwa ahadi au kwa ujira mdogo sana kama ambavyo dalili tumeanza kuziona nchini. Lazima Serikali ianze kuchukua hatua madhubuti sasa. Hiyo ni rasilimali kubwa inabidi iongozwe vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa watoto wa kike bado inasuasua, licha ya juhudi ya Serikali. Hili ni tatizo hasa kwenye jamii za wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iendelee kusimamia sheria zake kuhakikisha Watoto wote wa Kike wanapata fursa sawa za kujiendeleza kielimu. Mazingira ya Watoto wa Kike kama vile mabweni ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Watoto wengi wa Tanzania wanaishi katika mazingira magumu kimaisha na jamii inaelekea kuwachoka. Tanzania ina Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, takwimu zilizochukuliwa katika Halmashauri 91 kati ya 133 zilizopo nchini, zimeonesha kwamba, kuna watoto 813,372 wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini na athari za UKIMWI vimechangia kuwaweka baadhi ya Watoto nchini katika mazingira hatarishi kutokana na kukosa malezi, matunzo na ulinzi katika familia na jamii inayowazunguka. Ukubwa wa tatizo hili umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kadiri ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia yanayojitokeza. Kama Wizara; mnalishughulikia vipi jambo hili? Ninamwomba Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho alieleze Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa, Watoto wengi hawasomi licha ya kuwa wanayo haki ya kusoma na kupatiwa elimu katika nchi yao; na hata wale wanaosoma hawapati mahitaji muhimu yatakayowasadia kusoma, kufaulu na kuelewa kile wanachofundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtoto ana kila sababu ya kudai haki yake na ni jukumu la Serikali na jamii kwa ujumla, kuhakikisha Mtoto anapatiwa kila anachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtoto wa Tanzania anaishi katika changamoto nyingi ambazo zinamkabili. Mazingira wanayoishi Watoto wengi hapa kwetu ni magumu, ya hatari na yenye mashaka makubwa. Wengi wao wanaishi katika mateso makubwa na hawapati hata zile haki zao za msingi zikiwemo elimu, chakula na malazi. Kikubwa zaidi, wanashindwa kupata haki yao ya kielimu, kusikilizwa, kupendwa na matibabu. Watoto wengi wanajitegemea, ukipita katika maeneo mengi hasa maeneo makubwa au miji mikubwa, utashuhudia Watoto wengi wakijiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wao ndiyo wanauza pipi, maji, mayai na wengine wanaosha vioo vya magari barabarani, kana kwamba ni watu wazima wanaotegemewa na familia zao. Wapo wengine ambao wametumbukia katika maovu kama ya umalaya, kuuza na kusambaza dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya Wanawake ni waathirika wakuu wa mambo mbalimbali, yakiwemo maradhi, uchumi na wao ndiyo waangalizi wakuu wa familia zao, lakini ni watu wenye shida mno katika jamii. Tabia za kimila zinawasumbua sana Wanawake; ukeketaji bado ni balaa kwa Wanawake, elimu itolewe kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazazi wanaotelekeza Watoto; sheria zifanye kazi kwa ukamilifu na isiwaonee haya watu. Serikali iwasaidie Wanawake kiuchumi ili kuweza kusaidia familia zao. Wizara itoe elimu ya kutosha kwa Wanawake ili waweze kujua haki zao na sheria zinazowahusu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ina wajibu wa kuongoza harakati za kuwakomboa Watoto wa Kitanzania, ambao wanateseka kwa kiasi kikubwa na ambao wamefungwa katika minyororo ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitisha sheria kadhaa zinazotambua Mtoto ni nani, sheria hizo zitakuwa hazina maana kama haziwasaidii Watoto kuondokana

na matatizo mengi wanayokabiliana nayo, ambayo yanaathiri ukuaji wao. Wizara izisimamie sheria hizi na kuwasaidia Watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge lilipitisha sheria ikimlenga zaidi Mtoto wa Tanzania, lakini inamsaidia vipi huyu Mtoto kutimiza nia na makusudio yake? Hapa ninashauri kuwa, Siku ya Maadhimisho ya Watoto Duniani itakuwa na maana kama itatumiwa kuangalia ni wapi kama jamii tumefika katika kumkomboa na kumsaidia Mtoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watoto wanayo nguvu na ushawishi wa hali ya juu, endapo wataamua kudai haki zao; lakini ni vyema kwa jamii nzima ya leo kuhakikisha inatoa haki kwa Watoto, kuepusha matumizi ya nguvu zao endapo wataamua kuitumia kudai kile wanachopaswa kukipata lakini kwa makusudi wananyimwa. Wizara ni vyema ikatoa elimu kwa kutumia njia mbalimbali mfano, redio, TV, mikutano ya hadhara na maigizo kwa kuanzia Taifa hadi Vijijini angalau wimbi hili likapunguzwa.

**MHE. AMINA N. MAKILLAGI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, niweze kutoa mchango wangu juu ya hoja hii muhimu ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki kuandaa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi, ninaomba nijielekeze katika kuchangia maeneo machache ya Bajeti hii, ambayo nimeyachagua kutilia mkazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga Sh. 16,256,015.00 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, ninaomba niseme wazi kuwa:-

Fedha zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni kidogo, ukilinganisha na majukumu makubwa iliyonayo Wizara hii Mtambuka kwa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Taifa letu. Kwani ni ukweli usiopingika, Maendeleo ya Taifa letu hayawezi kupatikana kama Wizara hii ambayo ni mtambuka haitatekeleza wajibu wake kikamilifu, kuhamasisha Wananchi wapende kufanya kazi kwa hali na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali itazame uwezekano wa kuiongezea fedha Wizara hii ili itekeleze wajibu wake kikamilifu, kwa kutoa maofisa na kwenda vijijini kuhamasisha ujenzi wa shule, zahanati, vituo vya afya, kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Serikali ijipange kuongeza fedha katika bajeti hii ya Maendeleo hasa katika fungu la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Serikali ya kuhakikisha Wanawake wanapata fursa iliyo sawa, bado zipo sheria mbalimbali ambazo zinamkandamiza Mwanamke; mfano, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ambayo imetoa mwanya kwa Mtoto chini ya miaka 18 kuolewa. Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ardhi na Sheria za Kimila. Ninaomba kuishauri Serikali iharakishe utaratibu wa kurekebisha sheria zote zinazomkandamiza Mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009, Bunge lilipitisha Sheria ya Haki za Mtoto. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, jukumu la kuleta mtoto limebaki kwa mzazi yeye mwenyewe na Uongozi wa ngazi za Vijiji, Mtaa na Halmashauri za Wilaya. Pamoja na kuwepo Sheria hiyo, bado haijasimamiwa vizuri kwa sababu Sheria hiyo haijafahamika vizuri kwa Viongozi wa Vijiji na Mitaa. Matokeo yake bado kumeendelea kuwepo na wimbi la Watoto wanaokimbilia mitaani kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itoe elimu juu ya utekelezaji wa Sheria hii kwa Viongozi wa Vijiji, Mitaa, Kata na Wadi ili kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi inayofanywa na Serikali, Wadau na Wazazi hasa Wanawake katika kulea familia katika maadili yaliyo mema, bado lipo tatizo kubwa la mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu; kitu kinachosababisha vijana wetu wa kike wapate mimba za utotoni. Ninaiomba Serikali ijitahidi kufanya kila linalowezekana, kuhamasisha jamii ili irejee katika misingi yetu ya kulea familia, tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kujenga shule nyingi za sekondari kila Kata, ambazo zimesaidia sana kupunguza ndoa za utotoni na mimba za utotoni kwa kiasi kikubwa, tofauti na miaka ya nyuma, Mtoto alikuwa akimaliza darasa la saba anaolewa katika umri mdogo na wengine kujiingiza katika magenge yasiyofaa na anashindwa kuhimili ndoa na wengine wanafariki dunia wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafaniko yaliyopatikana ya kupunguza mimba za utotoni, bado lipo tatizo kubwa la ndoa za utotoni na mimba za utotoni zinazosababishwa na sababu ya kuporomoka kwa maadili kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii, kuwaomba Wazazi tutekeleze wajibu wetu wa kuhakikisha tunawalea Watoto wetu katika malezi yaliyo bora. Wazazi tuwe na utaratibu wa kukaa na Watoto wetu na kusema nao, kuwataka wasubiri na kuwapa elimu ya madhara yatakayowapata baada ya kukatisha masomo kwa kupata mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze Serikali kwa kupokea ombi la Wanawake la muda mrefu kuitaka ianzishe na ifungue Benki ya Wanawake, ambayo ni Ukombozi kwa Wanawake. Serikali imechukua hatua ya kufanya maamuzi ya kutenga shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa miaka mitano ili ziweze kuongezea mtaji wa kuanzisha Benki hiyo. Ikiwa ni pamoja na kutenga kila mwaka shilingi bilioni mbili kwa

miaka mitano, kwa ajili ya kuiongezea mtaji benki ili iweze kutoa huduma kwa wanawake na Wananchi.

Pongezi kwa Waziri na Timu yake kwa kuhakikisha Benki hii ya Wanawake inaimarika siku hadi siku. Benki ilianza na mtaji wa shilingi bilioni mbili, sasa ina thamani ya shilingi bilioni nane, imeshafikisha wateja 12,647 Wanawake na Wanaume 3,168. Vikundi vya *SACCOS* na *VICOBA* ni 445. Imeshakusanya amana shilingi bilioni kumi na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iendelee kutenga kiasi kikubwa zaidi cha fedha kila mwaka kwa ajili ya kuiwezesha Benki kupata fedha za uendeshaji na mtaji wa kutosha na kuiwezesha kufungua Matawi katika Wilaya na kutoa huduma ya mikopo kwa Wananchi hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dhamira ya kutenga kila mwaka shilingi bilioni mbili ni dhamira na ahadi ya Rais, ninaomba Serikali ifikishe fedha hizo kwa Benki ya Wanawake kupitia Hazina, badala ya kupitia Wizara ya Maendeleo Jamii ili kutotoa mwanya Wizara kukosa fedha za Miradi ya Maendeleo; mfano, katika Bajeti ya Mwaka 2011, Wizara imetengewa shilingi bilioni moja tu kwa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa akina mama hasa Wabunge kuwa, cherekochereko na mwenye mwana; kama ambavyo tulitumia akili, juhudi na maarifa ya kuiomba Serikali ianzishe Benki hii na Serikali ikakubali ombi letu, ninawaomba akina mama wenzangu mkiwemo Wabunge, kwenda kufungua akaunti katika Benki yetu ya Wanawake. Niwaombe pia akina baba, ambao siku zote mmekuwa mstari wa mbele kushirikiana na akina mama katika masuala yote ya kumkomboa Mwanamke kisiasa, kijamii na kiuchumi, mkafungue akaunti katika Benki ya Wanawake *(TWB)*. Benki ambayo inatoa huduma bila ubaguzi.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii haisaidii Wanawake na Watoto, kwa sababu pengine kiasi cha fedha wanayopewa ni kidogo. Ninashauri Serikali iongeze fedha ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi kwa Watoto na Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya *FDC* vilivyoko katika Halmashauri za Wilaya viko *under utilized*. Vinaweza kutumika mbadala wa Vyuo vya *VETA* ili visaidie vijana wanaomaliza Kidato cha Nne, ambao hawatafaulu kujiunga na Kidato cha Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wao Wizara ya Wanawake wanaweza kurekebisha *curriculum* zao wakaanzisha *certificate courses* za elimu ya jamii ili wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne wasome kwa mwaka mmoja au miwili baadaye waweze kujiunga na kozi za diploma na hatimaye *degree*. Kwa mtindo huu, Maafisa Ustawi wa Jamii/Maendeleo ya Jamii katika Kata ni rahisi kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Maendeleo ya Jamii walioko katika Kata wawafundishe Wanawake malezi bora ya Watoto wa Kike, watoe elimu kuhusu Janga la UKIMWI na madawa ya kulevya na matumizi ya chakula bora; mfano, mafuta ya kupikia yanayofaa, aina ya chumvi ya kutumia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii itembelee mikoa ili ifahamu kero za Wanawake na Watoto. Itembelee Vituo vya Watoto Yatima na Walemavu ili kuona namna gani Serikali itaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itueleze kuhusu Benki ya Wanawake. Kuna fununu kuwa Benki haifanyi vizuri, haifuati Kanuni na Sheria za Benki Kuu na hivyo inaweza isiwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wanawake waelewe mafanikio/changamoto ya Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Sophia Simba (Mb), nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa si muda mrefu tangu Benki ya Wanawake inzishwe, ni bora pia benki hiyo ikaongeza kasi ya kufungua Matawi katika Mikoa yetu. Inaweza ikaanza ngazi za Kanda na hatimaye Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia elimu itolewe zaidi kwa Wananchi ili kuondoa dhana kuwa Benki hii ni ya Wanawake pekee. Ndiyo maana hata idadi ya Wanaume waliopata mikopo ni ndogo; Wanaume ni 383 ilihali Wanawake ni 893.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri elimu zaidi ikatolewa ili ukeketaji wa wanawake uzidi kupungua. Pia ni ukweli kuwa bado kuna jamii ambazo zinaendelea kuamini kuwa, wanawake wenye heshima katika ndoa zao ni wale ambao wamekeketwa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu bado linaendelea na aibu ya Watoto wa Mitaani. Sasa ni muda mwafaka kwa Wizara kuwa na mpango madhubuti ili kuondoa Watoto hao wa Mitaani ambao wanaleta fedheha kubwa sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kuwa si Watoto wote wa Mitaani hawana Wazazi/Walezi ila pia baadhi ya Wazazi/Walezi hao huwatuma Watoto hao waende mitaani kwa nia ya kuombaomba; ni wakati sasa vitendo hivyo vikomeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondoe dhana kuwa Wizara hii ni ya Wanawake na Watoto pekee. Kuna muda fulani Wizara hii ilikuwa wazi kwa Wanawake na ndiyo maana katika kupanua majukumu yake, likawekwa neno Jinsia likimaanisha makundi yote mawili ya Wanawake na Wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake ameonekana akielezea zaidi habari za Wanawake kuliko Wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawasilisha.

**MHE. ISMAIL A. RAGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Halmashauri zilizokopeshwa fedha kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake; nina masikitiko makubwa sana kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba, mara ya mwisho fedha zilitolewa katika Jimbo langu mwaka 2006/2007 na fedha iliyotolewa ni Sh. 8,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuelewa kwa nini Jimbo la Tabora Mjini halijatengewa fedha tangu mwaka 2008, 2009, 2010 na 2011/2012?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora ni Mkoa ambao hauna hata kiwanda kimoja, unategemea sana kilimo na kilimo hicho wanaohangaika siku zote ni akina nmama. Ninaiomba Serikali, Jimbo la Tabora lifikiriwe hata ikibidi yafanyike marekebisho katika bajeti ilimradi Wananchi wa Tabora waendelee kuwa na imani na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani ya kuwa, suala hili utalipa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watoto wa Mitaani katika Mji wa Tabora wameongezeka kwa haraka sana na si kwamba Watoto hawa hawana Wazazi wao ila ni kutokana na umaskini uliokidhiri ndiyo maana Watoto wa Mitaani wamekuwa wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake uongezewe uwezo ili kusaidia kutatua tatizo kubwa la Watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kiundwe Kitengo cha kusaidia kupunguza dhuluma kubwa inayofanywa na ndugu wakati Mke anapofiwa na Mume wake. Mke anadhalilishwa sana hata wakati mwingine kufukuzwa ndani ya nyumba, jambo hili ni baya sana. Wizara isitegemee Mashirika Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika wa kuzifuta mila potofu zinazowadhalilisha Wanawake ili kulinda heshima ya Mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, hakuna kama mama.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia hoja ya Wizara hii kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yaliyopangwa, ninaiunga mkono hoja na ninampongeza sana Waziri na Naibu Waziri wake, kwa Hotuba nzuri, yenye mpangilio mzuri sana. Nina maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ikiangalie Chuo cha Maendeleo ya Wananchi – Ulembwe kwa jicho la huruma sana. Kwanza, majengo yake yamechakaa sana na hayafanani na hali ya sasa. Ninaomba Chuo hiki kiongezewe bajeti ili kiweze kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali ili kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Halmashauri ya Njombe kwa mwaka 2010/11 ilipata Sh. 8m/= . Fedha hizi ni kidogo sana na Wanawake wengi sana hawakuweza kuzipata. Kwa kuwa fedha hizi ni za mkopo, ninashauri fungu hili liongezwe ili kuinua hali ya akina mama ambao ni wachapakazi sana na wanaopenda kujiendeleza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vimekuwa vikitoa mchango mkubwa sana katika kutoa ajira kwa vijana, kwa kuwapa ujuzi mbalimbali wa kuweza kujiajiri wenyewe. Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nchini vipo 57, lakini sasa vimechakaa na vingine kugeuka magofu na kushindwa kuendelea kutoa mafunzo kama vilivyokuwa vikifanya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo hivi ni muhimu sana kwa vijana ambao wengi wao wanakosa nafasi za kundelea na masomo ya sekondari au elimu ya juu; hivyo, badala yake kupata nafasi ya kujiunga na Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa kuna Vyuo vya *VETA* kila Kanda, lakini kutokana wingi wa vijana wanaomaliza Darasa la Saba na Kidato cha Nne ni wazi kwamba, Vyuo vya Ufundi *VETA* vimeelemewa, mbali ya kwamba, Serikali ina mkakati wa kujenga Chuo cha *VETA* kila Wilaya ili vijana wengi wapate ujuzi na kujiajiri wenyewe; ni wazi kwamba, mkakati huo ni wa muda mrefu na hauwezi ukamaliza ukubwa wa tatizo. Je, Serikali kupitia Wizara husika katika bajeti ya mwaka huu imetenga shilingi ngapi kwa ajili ya kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mbali na ukarabati kutokana na changamoto ya ajira na wingi wa vijana wanaomaliza Darasa la Saba na Kidato cha Nne; Wizara imejipanga vipi kwa kipindi kijacho kutenga bajeti angalau ya kuongeza Vyuo vingine vya Maendeleo ya Jamii kwa kila Mkoa wa Tanzania Bara na Visiwani?

**MHE. BENEDIC NGALAMA OLE NANGORO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara, kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake itengewe uwezo na kuelekezwa kufika kwa Wanawake waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iandae Elimu na Programu Maalum ya kuuelimisha umma juu ya kupiga vita mila potofu na kutokomeza *stereotypes* zinazodhalilisha Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, waongezwe kwenye ngazi ya Halmashauri, Tarafa na Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitini viandaliwe na kuuelimisha umma juu ya Haki za Mtoto na kudhibiti ajira ya Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ihimize Elimu ya Watu Wazima kwa Wanawake wasiojua kusoma wala kuandika ili waweze kujiendeleza kielimu na kutumia uwezo huo kusimamia biashara zao ndogo ndogo na kuondoa umaskini.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa Hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ningependa kuzungumzia mikopo ya Wanawake Wajasiliamali hasa katika Wilaya yetu ya Mufindi. Nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo kuhusu vigezo vinavyotumika kupeleka mikopo katika Halmashauri kutoka katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, kwani Wilaya ya Mufindi toka uzinduliwe huu Mfuko mwaka 2006/2007, tumepelekewa pesa hizo mara moja mwaka 2008/2009; ninaomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kuishauri Serikali kuwa, umefika wakati mwafaka kukibadili Chuo cha Maendeleo Rungemba kutoka kwenye utoaji Stashada hadi kwende Shahada na kuwa Chuo Kikuu cha Kwanza cha Maendeleo na Wanawake hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii ya kipekee kuipongeza Serikali, kwa mkakati wake mkubwa wa kuanzisha Benki ya Wanawake; ni ukweli usiopingika, Wanawake wakiwezeshwa, tutakuwa tumewasaidia Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii, Benki hii isionekane ya biashara zaidi, ifanye kazi iliyokusudia ya kumsaidia Mwanamke. Usifanyike upendeleo katika kufungua Matawi ya Benki hii na yaende kwenye maeneo yote tuweze kuwakomboa Wanawake hasa wasiokuwa na uwezo, akina mama wa vijiji ambao wana matatizo makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii, kuishauri Serikali kuhusu Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Serikali ianzishe vituo rasmi viambatane na shule, pamoja na Vyuo vya Ufundi kuwasaidia na kuwaweka Watoto hawa ambao hawana matunzo ya kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja. “Nani kama mama?” Hakuna.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri Sophia Simba na Naibu wake, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa kuwatetea Wanawake na Watoto. Hadhi ya Mwanamke imepanda na karibuni hivi pengo kati ya Wanaume na Wanawake litazibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Wanawake wasibweteke katika nafasi za upendeleo, wala wasipende Wanaume wawawezeshe. Wafurukute wenyewe na wanaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa juu ya Mtoto wa Kike irekebishwe. Miaka kumi na tano kuolewa ni sawa na kumbaka Mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ya ukeketaji lilaaniwe kwa nguvu zote na litungiwe sheria kali. Kukeketa kunaharibu uhai, haiba na mateso makubwa kwa Mtoto wa Kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Watoto wa Kike waliozaa kurudishwa shuleni kusoma pamoja na wasichana wengine halifai. Ninashauri watafutiwe shule au vyuo maalum vyao peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi vipewe kipaumbele ili kuharakisha maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwasilisha kwako, mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri. Ninampongeza kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, ninampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji. Siachi kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kwa uwezo mkubwa aliouonesha kwa kipindi kifupi tu ambacho ameingia katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo moja tu ambalo ningependa Wizara hii ilichukulie kwa uzito mkubwa sana; tatizo la Watoto wa Mitaani. Kadiri siku zinavyokwenda, wanazidi kuongezeka na kama tutaendelea kuwaacha ni hatari sana kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pamoja na jitihada zenu za kutatua tatizo hili, ipo haja mshirikiane na Jeshi la Kujenga Taifa ili ikiwezekana katika Kambi zao waangalie uwezekano wa kuwaweka pale kama kijiji ili wapate kutunzwa na kupata haki nyinginezo za msingi ikiwepo elimu, ungalizi wa afya na hata ajira katika maeneo husika katika Jeshi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaunga mkono hoja.

**MHE. OMAR R. NUNDU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kutokana na magonjwa yanayokatisha uhai wa wazazi wote wawili kama vile UKIMWI, Watoto wengi wamejikuta wakiwa katika mazingira magumu ya kimaisha. Baadhi yao wangeepukana na adha hiyo kama haki za Wazazi wao zingelipwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo Wizara inayoshughulikia mirathi, nasaha yangu ni kuiomba Wizara hii ilivalie njuga suala la mirathi ya marehemu wanaowaacha Watoto wadogo ili malipo yao yaharakishwe kutoka Ofisi za Serikali husika. Nina mifano kadha wa kadha, Jimboni Tanga pekee ambapo malipo haya hayajafanywa kwa muda mrefu. Mfano mmoja ni Mwalimu Stambuli Omari Stambuli, aliyekuwa akifundisha katika Chuo cha Ufundi Arusha, ambaye tangu alipofariki Januari, 2003 na kuwaacha watoto wadogo wanne hadi leo hawajalipwa mafao ya baba yao pamoja na msimamizi wa mirathi hiyo kufuata maelekezo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya Wilaya hususan Tanga, Pangani na Mkinga, Mkoani Tanga, akina mama wengi wanajishughulisha kwenye shughuli za biashara mbalimbali za kujikimu kimaisha. Wengi wa Wananchi hawa bado hawapati mafunzo ya msingi ya kufanya shughuli hizo. Ombi langu ni kuwa mafunzo mliyopanga kutoa mwaka huu, toeni kipaumbele kwa akina mama wa Wilaya hizi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo Mifuko ya kuwakopesha Wajasiriamali Wanawake, bado katika baadhi ya Wilaya hususan Tanga, wajasiriamali hao hasa wale wadogowadogo, bado hawajafaidika kwa Mifuko hiyo ipasavyo. Ombi langu ni kuwa, Wizara iandae mikakati ya kuwajuza na kuwarahisishia taratibu za Wanawake hao kuweza kupata mikopo hiyo na urejeshwaji mwepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iweke nguvu za ziada katika kushughulikia Watoto wa Mitaani, kwa kufahamu kuwa, kuna wale ambao ni lazima wasaidiwe kwa vile hawana wa kuwalea na wale ambao wanaonewa kwa kukatishwa kwenye ombaomba na Wazazi au Walezi walewale wanaotakiwa wawatunze. Suala la Watoto kutumwa na Wazazi/Walezi wao kuwa ombaomba, litungiwe sheria ya kulikomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wangu wa Wilaya ya Siha, ninaomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina, ambayo ameitoa asubuhi hii. Ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba nichukue fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kushirikiana na Mheshimiwa Waziri, kuhakikisha kwamba, Wizara inafanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Wizara iweke mkazo na msisitizo mkubwa katika kuviimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyomo nchini. Vyuo hivi vikisimamiwa vizuri, vitasaidia sana katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninazishukuru Serikali za Awamu zote Nne, zimejali Jinsia ya Kike wakiamini kuwa Wanawake ni wengi kuliko Wanaume. Wanawake wengi ndiyo wakulima (Sensa ya 1988). Wanawake ndiyo wanaobeba matukio ya kila siku na mapambano ya kila siku ya kuhakikisha kuwa, familia inakula chakula na ipo salama. Kumbagua Mwanamke katika mipango ni kuendeleza umaskini. Kwa hiyo, tunataka Wanawake wawezeshwe na washirikishwe katika mipango mbalimbali ya maendeleo kisiasa, kielimu, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumtenga mwanamke katika mipango ya maendeleo ni kuendeleza mnyororo wa umaskini. Tunaiomba Serikali izidi kuwaendeleza Wanawake, wala msichoke kwa mambo haya, kuangalia sheria zilizopitwa na wakati zinazomhusu mwanamke; Sheria za Mirathi, Sheria za Ndoa na kadhalika zirekebishwe. Vyombo vya mikopo visitozwe riba kuwa na wanawake pia wapewe mikopo. Mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke zipigwe marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki za Wanawake ziende vijijini pia. Watoto wa Kike wasitumikishwe sana kiasi kwamba washindwe kusoma. Sheria ya Elimu ya 1978 inamtaka kila Mtoto asome shule. Mimba mashuleni zipigwe marufuku. Mabweni ya shule yajengwe ili Watoto wa Kike walale ili wasipate mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Kisiasa visiingilie Ukombozi wa Mwanamke. Kila chama kiweke mazingira ya kumwendeleza Mwanamke kwani Wanawake wote bila kujadili itikadi, wote wana matatizo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati mwafaka wa kutathmini ajenda kuu zinazomhusu Mwanamke; tumefika wapi, tumefaidi nini, tuna matatizo gani tena. Tunataka tuambiwe Wanawake wote wamefaidi vipi; walioolewa na wawasioolewa; Wanawake wa Vijijini; wa mijini; Wakulima; Wafanyakazi; Wanawake Vijana; Wanawake Wazee; Wajane na Mtoto wa Kike. Makundi yote haya yafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajenda ya 1979 ya Kimataifa ya Kuridhia Mkataba wa Kufuta Unyanyasaji wa Kijinsia; Ajenda ya Beijing; Ajenda ya Abuja na Ajenda ya CRC ya Haki za Mtoto wa Kike; Ajenda za Maputo; zote zinamsaidia Mwanamke kujikomboa kutokana na ubaguzi, unyanyasaji, ukandamizwaji na mfumo dume. Tunaomba zote ziangaliwe tujue matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanaume ambao wanafikiria kuwa Mwanamke ni mtu tu wa kupendeza kama maua, anayeendeleza kizazi na kurithisha mila kizazi kwa kizazi; waache. Wote washirikishwe katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie *NGOs.* Sheria Na. 24 inasema kuwa, NGOs ni budi kusaidia Serikali pale inapobidi, lakini utakuta zingine ndiyo kwanza zinakuwa wa kwanza kuandamana kupinga maamuzi ya Serikali; waache tabia hiyo. Serikali ihakikishe vilevile *NGOs* zinakuwepo mpaka vijijini. Ninaishukuru *NGOs* za Mama Mwinyi, Mama Mkapa na Mama Kikwete, kwa kusaidia jamii kwa namna moja au nyingine; ninasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mabughai Lushoto kiimarishwe, kuna tatizo la majengo na eneo kuwekewa uzio kutokana na hofu ya kuvamiwa na Wananchi kwa kutoelewa mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha kwa Watumishi wa Idara itolewe. Wafanyakazi wengi wamekata tamaa; kupandishwa vyeo na kuendelezwa kielimu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake ifungue Matawi. Ahsante.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, imejitosheleza katika maelezo yake. Mimi binafsi, ninaunga mkono hoja ingawa kuna changamoto nyingi ambao zinaikabili hii Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya mama na mtoto katika Nchi yetu ya Tanzania bado haijatiliwa umakini wake hasa vijijini. Katika Jimbo la Mufindi Kusini, bado Wananchi wangu hawajafikiwa kikamilifu na elimu ya haki ya Mama na Mtoto. Nitafurahi sana kama Wizara inaweza kufanya kazi katika Jimbo langu. Hii inasababisha maambukizi makubwa ya Ugonjwa wa UKIMWI katika Wilaya ya Mufindi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mufindi Kusini, kuna Wanawake wengi sana ambao wameunda vikundi vya ujasiriamali, lakini tatizo kubwa hawajawahi hata siku moja kusaidiwa kupata fedha ya MKUKUTA. Tunasikia tu kuwa kuna fedha ya kusaidia Wanawake waliojiunga katika vikundi vya ujasiriamali wanaweza kusaidiwa fedha ili waweze kuinua mitaji yao. Ninaomba Wizara iwafikie Wanawake hawa wanyonge ili wapatiwe msaada wanaouhitaji. Pia itakuwa jambo zuri sana, Mheshimiwa Waziri alitembelee Jimbo langu la Mufindi Kusini ili asalimiane na Wanawake wa Jimbo hilo. Ninadhani Wanawake hawa watafurahi sana kukuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake inavuma sana kuwa ipo Dar es Salaam, Wanawake wanaomba Benki hii iende hadi Jimbo la Mufindi Kusini. Jimbo langu lina Wanawake ambao wanajishughulisha katika biashara ndogo ndogo kama vile migahawa, kilimo cha alizeti, biashara ya mbao, chai, uuzaji mbogamboga, viazi, maharage na biashara ya nyanya. Nitafurahi sana Waziri akitamka leo katika Bunge hili kuwa, yupo tayari kufika Jimbo la Mufindi Kusini ili aweze kubadilishana mawazo na Wanawake wa Jimbo la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watoto wetu wanamaliza Shule ya Sekondari wakiwa bado wadogo, pia hawapati bahati ya kuendelea na masomo ya *'A' Level*, hujikuta wanaanza kufanya kazi katika viwanda vya upasuaji mbao, ambavyo vipo katika Wilaya ya Mufindi. Sasa je, Wizara imejipanga vipi ili kuwasaidia Watoto hawa ambao bado wana umri mdogo kati ya miaka 14 – 17; kwa kuwa unasema jukumu mojawapo la Wizara ni kuwapatia Watoto haki ya kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kutobaguliwa na kushiriki katika Maendeleo ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara itengeneze *Pilot Project* kwenye Halmashauri moja kama vile Morogoro au Tanga, Halmashauri hiyo ifundishwe na ihamasishwe namna ya kulea na kukuza Watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi. Baada ya hapo, *Project* hii ikifanikiwa, basi Halmashauri zingine nchini ziige hapo na iwe ni wajibu wa kila Halmashauri kulea na kuwakuza Watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake Wajasiriamali: Mbeya ni Mkoa tofauti na mingine katika hili. Kwenye masoko yote, asilimia zaidi ya 80 ya wajasiriamali sokoni ni Wanawake! Ninaiomba Wizara iwahamasishe hawa; na kuwahamasisha waanzishe *SACCOS* ambayo inatawasaidia kuinua mitaji yao na pia kuwaongezea ujuzi na maarifa ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara ianze sasa kuitawanya Benki ya Wanawake kwenye Mikoa yote nchini ili kuwasaidia Wanawake wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto ya 2008, imeelekeza Watoto wawe wanalelewa na familia zao na wale ambao wanazagaa mitaani, wachukuliwe na kurejeshwa kwa Wazazi wao. Sera hii bado haijafanya kazi kama Serikali ilivyoahidi, kwani kuna wimbi kubwa la Watoto wanaopita mitaani wakiomba, wanafanya kazi za hatari kama kuchimba mchanga, kubeba zege na kazi nyingine nzito na ukitazama wengi wao ni wadogo sana, wenye umri usiozidi miaka 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote haya yanasababishwa na Wazazi na Sheria haichukui mkondo wake. Sheria hii ni ya Mwaka 2009, yenye lengo la kulinda Haki za Mtoto na Serikali za Vijiji zimetakiwa kuwachukukulia hatua Wazazi wote ambao wanawatelekeza Watoto wao. Ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii sasa iwe na meno juu ya haki hii, kwani ukipita kwenye Miji Mikubwa sasa hivi kama ni Mzazi au Mlezi mwenye huruma, unaweza kulia jinsi Watoto walivyojaa katika barabara na jinsi wanavyotumikishwa. Ikiwa Serikali za Mitaa waliopewa jukumu la kuwachukuliwa hatua Wazazi kama sheria inavyosema wameshindwa, ninaomba jukumu hili lipelekwe sehemu nyingine. Pia ninaiomba hii Sheria iseme pia wale watu ambao wanatumikisha hao Watoto wapewe adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi vipaumbele vya Taifa ni Kilimo Kwanza, kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa Wanawake ili waweze kukabiliana na umaskini wa kipato. Kuhusu hili, Serikali kupitia Wizara hii, inafanya ubaguzi mkubwa katika pande mbili za Muungano, kwa sababu imeshindwa kufungua angalau Benki mbili Unguja na mbili Pemba, kwa lengo la kuwasaidia Wanawake; jambo hili halileti sura ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari wanapodai mambo kama haya, kuna kauli kuwa hawataki Muungano; kwa hiyo, tunaiomba Wizara iwatupie macho Wanawake wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyakazi wa Majumbani; wengi ni wadogo mno. Wafanyakazi wa majumbani huwa wanateswa sana na kupewa kazi nyingi; akiamka asubuhi huwa hapumziki mpaka saa nne za usiku; na mazingira ya ndani ya nyumba mfanyakazi huwa hawekwi kama *part of family*. Sehemu ambayo anatakiwa kulala siyo nzuri, nguo anazopewa kuvaa huwa haziridhishi na sehemu ambayo anatakiwa akale chakula siyo nzuri. Sina haja ya kueleza yote kwa Wizara kwani mnayajua na pia mishahara yao ni midogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara iunde Chombo Maalum cha kufuatilia mambo yote ya Wafanyakazi za Majumbani.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara mtambuka inayoangalia masuala ya Maendeleo ya Jamii. Jambo la kusikitisha kila mwaka Wizara hii imekuwa ikipewa fedha kidogo na hivyo kuonekana haina umuhimu wa kuwepo na hivyo iwe idara tu. Hoja hii inapata mashiko zaidi kwa kuwa masuala ya ustawi wa jamii yameondolewa huku na kupelekwa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii pamoja na bajeti ndogo sana imetumia takriban asilimia hamsini ya fedha yote ya miradi ya maendeleo kupeleka kwenye Benki ya Wanawake. Hii inaonesha wazi miradi mingine imetengewa fedha ndogo sana hasa ikizingatiwa Vyuo vya Maendeleo havijatengewa fedha kwa ajili ya ukarabati. Ni utaratibu gani uliopo wa kutoa mikopo kwa wananchi, maana kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu utoaji wa upendeleo kwa waombaji na wengi wakisema ni benki ya wake wa viongozi na viongozi tu kama vile Wabunge!! Tuelezwe ni akina nani wanaofaidika

na benki hii, kama benki hii ni ya biashara ni kwa nini Serikali inaendelea kuwapatia fedha zikiwemo bilioni mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa nini wakati Katiba iko wazi na inaeleza aina za Wabunge lakini wananchi wengi hususan wanaume wamekuwa wakitoa kauli za kudhalilisha kuhusu uwepo wa Wabunge wa Viti Maalum wanatumia bure fedha za walipa kodi. Nataka ufafanuzi kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi na watoto wa kike wamedhalilishwa sana na mila potovu za ukeketwaji. Madhara ya ukeketwaji yanajulikana lakini Wizara haijafanya *Educational Sensitization* ya kutosha kuhusu madhara na kuchukua hatua kali kwa wahusika wote wa matendo hayo wakiwemo mangariba na wazazi. Siku hizi wazazi wamekuwa wakijihusisha kwa kutoa watoto wachanga kwa kuogopa wakikua watapata uelewa na hivyo kukataa kukeketwa. Dhana kuwa bila ukeketwaji wanawake hawataolewa ni potofu. Wanaume waelimishwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa mitaa haizai watoto lakini dhana hii ni sahihi kwani watoto wamekuwa wakiishi mitaani. Ni wazi watoto hawa wanaongezeka kutokana na maisha magumu, ndoa kuvunjika lakini kubwa ni kutowajibika kwa wazazi. Kinachoshangaza sasa hivi tuna *DNA machines* ambazo zinatambua baba mzazi wa mtoto. Pamoja na gharama kubwa sana 500,000/=. Basi ni ushauri wangu kuwa Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla ipunguze gharama hii kwa wanawake wanaotaka kujua baba watoto wao wapunguziwe gharama na akinababa hao walipie gharama. Hii itapunguza sana tabia mbaya ya wanaume wetu wanaojamiiana bila kujua wajibu wao baadaye.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Folk Development Colleges (FDC)* zimekuwa zikisaidia sana vijana wetu hasa katika kupata elimu hata na stadi za ufundi. Hivi sasa inaonekana vyuo hivi havijapatiwa kipaumbele na moja ya sababu yake inawezekana ni udhaifu wa Wizara hii katika kujenga hoja ya kupata fedha za kutosha. Imekuwa ni kawaida kila mwaka Wizara hii kupatiwa fedha ndogo sana. Eneo hili ni changamoto, watendaji na wataalam wabuni mikakati ya kuondoka kwenye *trap* hii ya kutotengewa fedha nyingi, labda ni tatizo la mtazamo wa majukumu muhimu sana yanayotekelezwa na Wizara hii, Maendeleo ya Jamii ni broad na ipo haja ya Wizara kui-*portray* hivyo ili ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri inayoeleweka ila nina shaka na utekelezaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti (fedha) zilizokadiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ina majukumu ya kuratibu, kuandaa miongozo, kutunga sera zinazohusu watoto, wanawake, jinsia na maendeleo ya nchi wakati sasa umefika kwa Serikali kutenga rasilimali fedha na watu ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wizara imeeleza kuwa kwa mwaka 2011/2012, itawawezesha wanawake kupata mafunzo ya kujikwamua kiuchumi nasisitiza uwezesho huu ujikite vijijini zaidi kuliko mijini kwa sababu wanawake wa vijijini ndio walio wengi hawana stadi za kitaalam za kiuchumi hivyo kutumia uzoefu wa bibi na mababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Wanawake unaotoa fedha katika Halmashauri zetu kwa muda mrefu sasa wanawake wenye ulemavu katika Halmashauri nyingi hawafaidiki na Mfuko huo ingawa malengo yake ni kuwainua wanawake hao kiuchumi. Hivyo, nashauri Wizara itoe mwongozo kwa Maafisa Maendeleo katika Halmashauri na Kata kuwahusisha wanawake wenye ulemavu katika shughuli za uwezeshaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba Wizara imeeleza kuwa ilitafsiri Sheria ya Mtoto kwa Kiswahili jambo ambalo nalipongeza sana kwa sababu itasaidia walengwa wengi kuelewa yaliyomo. Hata hivyo, nashauri hata hizo kanuni za sheria hiyo nazo zitafsiriwe kwa Kiswahili kwa lengo lile lile la kuwezesha wanajamii kuelewa na hivyo kusaidia sheria kutekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote naomba Mheshimiwa Waziri apokee pongezi zangu za dhati kabisa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ustawi wa Jamii Mwenyezi Mungu amjalie kila la kheri katika utendaji wake wa kazi na majukumu mazito ya siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana kwa hotuba yake nzuri yenye mipango mizuri ambayo naamini ukiendeleza juhudi za kuendeleza utekelezaji wake Wizara hii itaendelea kupata heshima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mheshimiwa Waziri nampongeza sana kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake, ameisoma kwa umahiri mkubwa, utulivu wa hali ya juu. Hotuba fupi yenye hoja za Msingi. Hakika umeiva kiuongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri apokee mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Wanawake. Naipongeza kwa kuwa imetekeleza nia ya kutuendeleza wanawake kama ambavyo imekuwa ikituhamasisha wanawake kujikwamua kiuchumi nashukuru sana. Kwa hiyo, ili wanawake wote wanufaike na huduma hii muhimu

jitihada za makusudi zifanyike ili benki hii iwe na matawi nchi nzima na uhamasishaji wa hali na mali ufanyike ili wanawake wengi kwa nchi nzima waweze kuuziwa hisa ili waione benki hii kuwa ni mali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vizuri Wizara iweke utaratibu wa kuelimisha wanawake umuhimu wa kuweka pesa benki na kuchukua mikopo kupitia Benki hii ya Wanawake. Pamoja na yote Mheshimiwa Waziri benki hii imekuwa ikilalamikiwa kwamba ni benki ya wake za wakubwa na wengine wakisema ni Benki ya Wanawake wa CCM jambo ambalo naamini wanasema hayo kwa kutoelewa na kuitambua benki hii ipasavyo. Yakitekelezwa haya niliyoyapendekeza yatafuta na kurekebisha utata huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba asinisahau katika ufalme wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ahsante.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ndio yenye jukumu la kuwezesha jamii kuwapatia watoto haki ya kuishi, kuwaendeleza na kuwalinda. Kwa kuwa ugonjwa wa ulemavu wa ngozi ni wa aina nyingi ukiwemo ulemavu wa ngozi unaoleta albino nyeusi. Aina hii ya Albino huleta magonjwa mengi yaliyo sugu kama ilivyoonekana kumpata mtoto Benedicto H. Charles mwenye umri wa miaka miwili na miezi kumi (2.10) mkazi wa Nyalikungu Maswa, Shinyanga anayekabiliwa na *Photophobin* kwa muda wa mwaka mmoja tangu ulipobainika kwa mtoto huyo. Ugonjwa huu unapompata mtoto ukiwa ugonjwa wa kudumu ambao huusumbua mwili kwa kuupatia mwasho, macho kutoa tongotongo, kutokwa machozi mfululizo. Kwa kuwa ugonjwa huu hudhibitiwa kwa gharama kubwa na kwa kuwa ni ugonjwa unaomwandama mtu kwa maisha yake yote. Je, Wizara ina mpango mkakati upi katika kuwalinda watoto ambao wazazi wao ni maskini ambao watoto wao wanatakiwa kuishi kwa raha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipewe jibu la Serikali.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Jimbo la Igalula wanakuomba Mheshimiwa Waziri kuwaeleza:-

(a) Utaratibu wa kushiriki kwa kuwa wadau wa Benki ya Wanawake Tanzania kwani kipato chao ni duni sana;

(b) Jinsi ya kupata mikopo kutoka Benki ya Wanawake Tanzania;

(c) Wanaomba ukawatembelee tena kwani mwezi Septemba, 2010 ulifika Kata ya Igalula pia wakakukaribisha Kata tisa zilizobaki; na

(d) Jimbo tunaomba Chuo cha Jamii na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Wilaya nzima ya Uyui haina chuo hata kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Iringa nilikuwa mgeni Rasmi 2009 Lungemba Mufindi katika Mahafali, pia Ipogolo Iringa na Ilula *FDC,* maendeleo ni makubwa kutoka vyuo hivi. Tunaomba tusaidiwe.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, kwa rehema na neema zake nyingi sana kwangu ambazo siwezi kuzihesabu, ikiwemo neema ya afya na upeo alionijalia wa kuchangia machache katika bajeti na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kubwa, pana na muhimu sana, kwani maendeleo ya jamii ndio kitu muhimu katika nchi yoyote duniani ikiwemo Tanzania. Mtazamo wa watu wengi ni tofauti na huu wangu, kwani wanaiona Wizara hii kama ni kitu kidogo tu na isiyo na kazi za kufanya. Nasikitika sana Wizara hii kupangiwa siku moja tu ya kujadiliwa bajeti yake. Hii inaonyesha hata Serikali bado haijaona au kutilia maanani ipasavyo umuhimu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuufahamu unyanyasaji wanaofanyiwa wanawake na watoto lakini jukumu la Wizara hii haliishii hapo, ni lazima pia Wizara ipanue macho yake na iwaone pia wanaume wanaonyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia kubaka inaonekana kuwa ni wanawake tu ndio wanaobakwa, lakini wapo wanaume wengi hasa vijana watanashati *(handsome boys)* wanabakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia, mazoea na mazingira ya nchi yetu inaonekana kama ni aibu mwanaume kutangaza hadharani kuwa amenyanyaswa kijinsia na mwanamke. Ni wakati muafaka sasa kwa Wizara hii kulifanyia kazi tatizo hili hasa katika vyuo vya elimu ya juu na zaidi ni katika Wizara na Idara za Serikali. Wanaume vijana hulazimishwa kuingia faragha na wanawake ambao ni wakubwa wao kazini ili aidha, wapatiwe nafasi za masomo au hapo ofisini wafanye kazi kwa utulivu na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wa mitaani ni kubwa, sugu na linaloendelea kukua siku hadi siku! Ipo haja sasa kwa Serikali kujipanga na kulifanyia kazi ipasavyo tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iharakishe kutoa vitambulisho vya Taifa ili mwanamke amjue mwanaume anayezaa nae kwa kuwa na utambulisho halisi na vipimo vya maabara kikiwemo cha *DNA* vitumikie kubaini baba wa kibaiolojia wa mtoto husika, sheria zifanye kazi ipasavyo ili watoto hawa wapewe wazazi wao na walazimishwe kuwalea na kuwatunza kama taratibu za nchi na sheria zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu anaona raha kuzaa na kuzaa si kazi bali kazi ni kulea! Bila Serikali kuwa makini na kutumia ipasavyo sheria zilizopo na kuzirekebisha zilizopitwa na wakati ili kupambana na tatizo la kuongezeka watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila mkakati madhubuti wa kudhibiti watoto wa mitaani kwa kuwabaini wazazi wao na kuwalazimisha kuwatunza watoto wao, tutakuwa na taifa majambazi watoto. Hivi sasa ambapo inakadiriwa kuwa na watoto wa mitaani kiasi laki nane (800,000) na hali imeshaanza kuwa mbaya, je, miaka kumi ijayo hali itakuwaje? Hivi sasa watoto hawa tayari wanaanza *course* za ujambazi huko katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi yamenikuta, wakati nashuka tu kwenye gari yangu kijana wa mtaani ghafla tu na kwa mshangao akakwapua *Side mirror* na kukimbia nayo! Huyo ni kijana asiyezidi miaka 12!! Tatizo hili sasa vijana hawa wanakwapua vifaa vya magari, hata kwenye foleni wakati gari inatembea!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika pabaya na tatizo hili na ni lazima Serikali ilifanyie kazi kwa kushirikisha Wizara hii, Wizara ya Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani na Taasisi nyingine za Kitaifa na hata kuomba msaada Kimataifa ili kutatua janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni janga la Kitaifa sasa na tusipoziba ufa, tutajenga ukuta! Taifa liko katika hali mbaya kwa tatizo la watoto wa mitaani. Tushirikiane kukomesha ili tujenge Taifa lenye maadili kwani inawezekana, timiza wajibu wako.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuongoza Wizara hii na wote wakiwa wanawake. Nadhani Mheshimiwa Rais hakukosea anatambua kuwa akinamama wanaweza. Naamini tunaweza na tunawaombea heri katika kazi zenu za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Wizara kusimamia kwa makusudi suala la uandaaji wa bajeti kwa kuangalia jinsia. Kwa kuwa Sera ya Wanawake ya mwaka 2000 inasema asilimia themanini ya wanawake ndio wafanyakazi zaidi na ndio nguvu kazi vijijini na wanazalisha asilimia sitini ya chakula chote. Hali kadhalika katika masuala ya uzazi. Wanawake hawana maamuzi juu ya idadi ya watoto katika familia ingawa wao ni wazazi na wana jukumu kubwa zaidi la ulezi wa watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sera hiyo hiyo inasisitiza kwamba 90.4% ya wanawake ni wazalishaji mali katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi. Katika kilimo wanawake wanakabiliwa na tatizo la nyenzo duni, ukosefu wa mitaji, ujuzi mdogo na kutokuwa na miliki ya ardhi wakati kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa, ndani ya kilimo kwanza, nani atapuuza ukweli huu? Wanawake wanachangia maendeleo kwa kiwango kikubwa. Tafiti nyingi zimebainisha ukweli huo (Paulina 1963; Uchendu 1965; Ame 1977; Aidoo 1981).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukua kwa miji wanaume wengi toka vijijini wamehamia Mijini na kuwaachia wanawake watoto wanaohitaji kula, kulala, kuvaa, kusoma na hata matibabu. Wanawake ndio wanaoumiza vichwa zaidi kwa matatizo haya. Lakini pamoja na kuwa na Mfuko wa mkopo kwa wanawake, ni wanawake wangapi wanafaidika na Mfuko huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huo mwaka 2010/2011, Jumla ya Sh.128,000,000/= zilitengwa kwa Halmashauri 16. Fedha hizi ni ndogo sana na hazitaweza kuwafikia hasa akinamama waishio vijijini. Hivi Halmashauri ambazo hazijafikiwa na Mfuko huu, akinamama hawa wakafie wapi? Wanawake hawa tumeona ambavyo wanahangaika na ndio wazalishaji wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha Wakurugenzi wa Halmashauri wanaupa Mfuko huu hiyo asilimia tano ili Mfuko huu uweze kutuna na kuwakopesha wanawake walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wa mitaani ni kubwa sana na linasababishwa na matatizo tofauti, lakini kubwa ni lile la utengano katika ndoa, hasa pale akinababa wanapoitenga familia, ama watoto kuachiwa mama peke yake, ni vema pale mama anapokwenda kushtaki Ustawi wa Jamii, Ustawi watilie mkazo kulea watoto wao, ili kupunguza msongamano wa watoto wa mitaani, pale ambapo baba ana uwezo na wakiwa wametengana na mama na hasa uwezo wa mama kama ni mdogo.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe masikitiko yangu ya dhati kabisa. Nailalamikia Serikali kwa kutoipa umuhimu Wizara hii. Kwa mtazamo wangu, Wizara hii ni pana na yenye majukumu makubwa mno. Wizara hii inagusa maendeleo ya jinsia zote wanaume na wanawake na Wizara hii inagusa maendeleo ya watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ingepewa fedha za kutosha na sio bilioni 16 kwani ukiangalia upande wa Maendeleo ya wanawake Wizara hii haisogei na kuwagusa akinamama wa vijijini hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Jimbo la Same Mashariki, nilitegemea wanawake ambao majukumu yao ni mengi mno waguswe na Wizara hii kiuchumi ili waweze kuendeleza jamii wanayoishughulikia mno. Udogo wa bajeti ambayo inatengwa kwa ajili ya Wizara hii, unasababisha Wizara hii ishindwe kuchukua majukumu yake kikamilifu la maendeleo ya watoto wa Tanzania. Watoto wengi ni wale ambao hawana mwenyewe. Watoto wanaozurura mitaani, watoto yatima, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inawafanya Mawaziri washindwe kufanya ubunifu wa kuendeleza jamii kwani bado hawataweza kutekeleza wanayotaka kufanya ili waboreshe jamii yote ikijumlisha wanaume, wanawake na watoto pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni moja, nimsihi Waziri wa fedha pamoja na udogo wa bajeti hii nina hofu anaweza akaipunja Wizara hii pamoja na udogo wa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waziri wa fedha *aji-committ* kwamba hizi bilioni 16 ambazo ni kidogo sana atazitoa zote ili japo zisaidie kuanzisha miradi kwa hatua za mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake. Wizara ihakikishe ufunguaji matawi vijijini ili wanawake wengi zaidi wapate mikopo hadi Jimboni Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na watoto yatima, Serikali ifanye jitihada za kulea au kuchangia vituo vya kulelea watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itengewe fedha za kutosha ili Wizara ipate uwezo wa rasilimali fedha ifanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iandae mafunzo kwa wanawake mpaka vijijini (Jimboni Peramiho) wapate uelewa wa mambo mbalimbali kama ujasiriamali, Sheria za Ndoa, Sheria za Mirathi.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba bajeti yao iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Njombe, Ulembwe kikarabatiwe na kipelekewe bajeti ya kutosha na Chuo cha Rungemba Miundombinu ya Umeme hata wa *Solar* au Maji wawekewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenye ulemavu wa ngozi *Albino* wapewe dawa bure za ngozi kuzuia *Cancer* ya Ngozi kama dawa zingine zinavyotolewa bure nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba za mabenki ni kubwa sana na hadi sasa hakuna tofauti ya kuwakopesha akinamama na wafanyabiashara. Serikali iweke sera ya kuwakopesha akinamama kwa riba nafuu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Wizara hii ina majukumu muhimu kwa jamii. Ina majukumu ya kuangalia ustawi wa jamiii kwa ujumla, na hasa makundi maalum katika jamii kama wazee, yatima na walemavu. Pale Bukoba tuna kambi ya wazee na walemavu, katika Kata ya Nyakato, Tarafa ya Bugabo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara na Serikali kwa kuweka na kuendesha kambi hii. Lakini pale kambini wazee hawa wana maisha magumu sana, kuna wakati wanakaa siku mbili bila chakula. Wanaishi kwa njaa. Pale kambini, yapata miaka miwili iliyopita, nyumba moja ya bweni ilianguka kutokana na mvua na upepo. Kwa sasa lipo bweni moja tu, ambapo wazee wote, wanawake na wanaume wanaishi katika bweni moja, hali ambapo haitakiwi kabisa. Niiombe Wizara ifanye kila linalowezekana mambo haya mawili, chakula na mabweni yafanyiwe marekebisho haraka ili maisha pale kambini yawe ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna watoto wengi yatima, ambao hawana msaada. Niombe Wizara hii ijitahidi kuona namna ya kuwasaidia hawa watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Utumikishwaji wa watoto upo na utaendelea kuwepo, kwani baadhi yao wanafanya hivyo kutokana na kuwalipa ujira mdogo watoto, ambapo kama wangewatuma watu wazima wangetaka ujira zaidi. Je, mbali na kuelimisha jamii juu ya tatizo hili, inachukua hatua gani Wizara kuwasimamia watoto kupata ujira (malipo) yanayostahili pale ambapo imegundulika mtoto amefanyishwa kazi kinyume na sheria. Adhabu gani itatolewa kwa huyo mtu mzima aliyemtuma mtoto na kumnyima haki zake za msingi kama elimu, afya, michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria ya kutotumikishwa watoto ipo, lakini wakati mwingine watoto wenyewe wanalazimika kutumwa au kujituma angalau wapate chakula waweze kuishi. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuwatambua watoto hao, sehemu wanazotumwa, ili waweze kulipwa kwa mujibu wa kazi waliyofanya na haki zao nyingine kama elimu, afya na hifadhi. Aidha, Wizara kuwasimamia watoto wenye mazingira magumu kwa wazazi wao kuwaelimisha na kuwapatia stadi mbalimbali na kuwapatia ruzuku ili wafanye biashara ndogo ndogo waweze kutoa matunzo kwa watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Ukatili huu upo na unaendelea katika nchi yetu kwa visingizio mbalimbali vikiwemo vya mila. Naiomba Wizara iwe na mkakati maalum wa kuelimisha wanawake na wanaume pamoja na makundi tofauti (vijana) ili vita hivi tuweze kushinda. Benki ya wanawake, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki hii, lakini naiomba Wizara, Benki ya Wanawake iwe na mpango mahsusi wa kuwafikishia wanawake huduma za kibenki hasa vijijini kwani ndiko waliko wanawake wengi na ndio wazalishaji wakubwa na huduma hii iko mbali na wao na haina masharti magumu. Ni lini Benki hii itatoa huduma zake kwa upande wa Zanzibar? Au kwa sasa sisi ambao ni wateja wa Benki hii, tukihitaji kupata fedha tutumie Benki gani, tukiwa kule Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. ESTHER NICHOLAS MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika kuwawezesha wanawake kiuchumi. Kama kweli Wizara ina lengo thabiti la kumwezesha mwanamke kiuchumi basi ni fedheha kuona kuwa bila uoga fedha za kumwezesha mwanamke katika ngazi ya Halmashauri inapewa milion nne au nane, tena mara moja tu, toka mwaka 2006 hadi sasa na kuna Halmashauri nyingine bado hazijapata hizi fedha kabisa. Hebu tujiulize hizi milioni nne au nane tunazopeleka katika Halmashauri, tunalenga kweli kumwezesha mwanamke? Ukweli ni kwamba kiasi hiki ni kidogo sana na kwa takwimu zilivyo sasa wanawake ndio idadi kubwa sasa hizi milioni nne mfano, ukiwapa akinamama mia moja ina maana unawapa mtaji wa Sh. 40,000/= tu na kama Halmashauri imepata Sh. 8,000,000/= na mfano kuwapa akinamama 100, ina maana unawapa mtaji wa Sh. 80,000/= tu, hivi tujiulize huyu mama atajikwamua kiuchumi kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ilione hili kwa ukubwa wake na iongeze kiwango cha fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri angalau zitengewe kama milioni 50 au 30 kwa kila Halmashauri na hizi ziweze kutumika kama *revolving funds*. Pia Wizara ihakikishe kwa kila Halmashauri inapata hizi fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) ili kila Mtanzania mwanamke afaidike na Mfuko huu na hasa wale wa kijiji kuliko Mfuko huu kubaki kwa wajanja wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Watoto hawa wanateseka na hawana hatia yoyote. Nashauri Wizara ichukue hatua mbadala ya kuhakikisha watoto hawa wanapata haki zao zote za msingi kama elimu, maisha bora, afya bora ambayo itapelekea kuwa na maisha bora ya baadaye. Tuone ni njia gani mbadala za kufanya mfano, kuongezwa kwa vituo vya kuhifadhi watoto hawa ili kuhakikisha wanapata mahitaji haya muhimu kama nilivyoanisha hapo juu. Pia tuwashirikishe wadau wengi katika ku-*solve* janga hili kwani likiachiwa Wizara tu haitaweza. Pia kuelimisha Umma juu ya athari za kuwa na watoto wengi mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana nzima ya maendeleo ya jamii ni pana sana, hivyo inagusia pia usalama wa raia. Ni dhahiri kuna wanawake wengi wananyanyasika katika ndoa zao na sheria zilizopo zinatoa *loop hole* na wanawake wengi hawajui sheria hizi na haki zao. Juzi tu katika Kijiji cha Nyabironga kuna mwanamke alikatwa mkono wake wa kushoto na miguu yote miwili kwa tuhuma za kuwa na mahusiano na mwanaume mwingine. Katika Wilaya ya Tarime Kata ya Susuni, wasiwasi wangu hapa ni je, Wizara inajua hizi taarifa. Hili limekuwa na janga kubwa na natoa rai kwa Serikali itoe elimu kwa wanawake hasa vijijini ili wajue haki yao na Sheria ya Ndoa.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi. Suala la Benki ya Wanawake Tanzania, imeonekana kwamba tokea kuanzishwa kwa Benki hiyo, imekuwa ikitoa fursa kwa upande mmoja wa Tanzania Bara tu na upande wa Zanzibar bado fursa hiyo haijapatikana. Hivyo, naishauri Wizara kuandaa mpango mkakati wa kutoa mikopo kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto, kadri siku zinavyokwenda mbele kunakuwa na ongezeko la watoto mitaani na ongezeko hilo limekuwa linalitia aibu Taifa, aidha, katika makutano ya njia za Dar es Salaam imekuwa kama *fashion*, kila gari likisimama basi watoto wanalifuata na kuanza kuomba pesa kwa madereva. Hivyo, naishauri Serikali kuandaa mpango maalum wa kuwakamata watoto wote, wanaoranda mitaani na kuwafungulia kambi ya watoto ya Serikali ili kupunguza dosari hizo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kutaka kufahamishwa Kanuni za Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napenda kuchangia kuhusu Serikali kutimiza wajibu wake wa kuandaa mazingira mazuri ya mtoto kama kupata elimu. Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, hivyo Serikali itenge *centers* za watoto yatima na watoto wa mitaani na watoto wote wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusu suala la jinsia na usawa. Napenda kueleza kuwa mchakato wa kuwapata Viti Maalum ubadilishwe, aidha kuwe na utaratibu wa kuongeza Majimbo ambayo watagombea wanawake pekee au kuwe na utaratibu wa wanawake kugombea kwenye kila Wilaya yaani kila Wilaya iwe na Mbunge mwanamke mmoja, kuliko utaratibu huu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchakato wa Katiba mpya, Serikali na wadau wote wa Katiba mpya kuelezea vipengele vya usawa lakini tusisahau vipengele hivyo, lakini visije kutugawa wanawake na wanaume. Watoto wenye ulemavu na *inter-sector programs* yaani Wizara ya Elimu ijue ina watoto wangapi walemavu, TAMISEMI ijue inapojenga madarasa na kadhalika, wakumbuke ujenzi wa vyoo vya walemavu na vifaa vingine na majengo haya ya walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upigaji kura, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inaeleza jinsi gani mtoto ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18, hivyo umri wa kupiga kura upunguzwe hadi miaka 15, kwani vijana hawa wa miaka 15 hadi 18 wengi wako sekondari na wengine wamemaliza hivyo wana elimu ya uraia na wanaweza kutambua kiongozi mzuri ni yupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake walioko vijijini bado wana hali mbaya ya namna ya kupata taarifa za uzazi wa mpango na salama. Hawana *Access* ya kutosha ya kupata mikopo, hawapati mafunzo ya kutosha ya ujasiriamali. Bado wanatembea umbali mkubwa kufuata maji na kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya wanawake kuendelea kupiga wake zao inaendelea. Wanawake bado wanapigwa na waume zao mpaka leo, wananyanyaswa. Ni

lazima tufikirie nje ya *box* ili tuweze kutatua tatizo hili, kumwachia mwanamke eti akipigwa aende kituo cha Polisi, sio njia muafaka kwani wakati mwingine wanawake hawa wanapokwenda Polisi waume zao huwapiga tena. Wizara ijikite kwenye kutekeleza masuala ya wanawake na watoto tu na sio kuendelea na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kutoweka wanawake tupu kwenye Wizara hii. Haiwezekani kuanzia Waziri mpaka Naibu Katibu Mkuu wote wawe wanawake. Tujifunze toka Finland. Wizara ya *Gender* inaongozwa na mwanaume na anafanya vizuri sana. Namshauri Rais atakapofanya *reshuffling* afanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mfumo wa uchaguzi ubadilike ili kuongeza uwakilishi wa wanawake Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wenye ulemavu waangaliwe kwa jicho tofauti. Bado jamii inawanyanyapaa sana.

**MHE. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa Hotuba yao nzuri. Naomba niwapongeze kwa utekelezaji mzuri wa Ilani, kwa kuimarisha *WDF*, Benki ya Wanawake, ukarabati wa vyuo, mafunzo mbalimbali na mambo mengi tu mazuri mliyotekeleza, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ndoa. Mmomonyoko wa mahusiano kati ya wana ndoa umesababisha:-

(i) Watoto wengi wamehamia mitaani kutafuta faraja au maisha.

(ii) Ukimwi pia umefanya mayatima wengi kuhamia mitaani.

(iii) Ndoa nyingi ziko *ICU*.

(iv) Ongezeko la talaka hadi Makanisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote dawa ya ndoa ni nini? Nashauri Wizara iangalie taasisi ya ndoa kwa kutoa semina za kuimarisha ndoa. Washirikishe viongozi wa dini kukemea talaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu ukatili juu ya wanawake. Wanawake wengi wanateseka sana kwa kupigwa, kukosa matumizi, kutelekezwa na manyanyaso mengi. Sheria kali itungwe ili kulinda haki za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ni finyu, bilioni 16 ya mwaka 2011/2012 ni pungufu kwa bilioni tatu. Bajeti hii haitoshi iongezwe. Bajeti ya vyuo 55, milioni 300 haitoshi. Majukumu ya vyuo ni mengi kama vile ukarabati, vitendea kazi na walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napenda kumpongeza kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii muhimu. Inavyoelekea baadhi ya Wabunge hawaelewi maana ya jinsia wala maendeleo ya jamii. Hii ni *cross cutting issue*, kila Wizara, Idara, Mashirika hata Mashirika binafsi wanapaswa kutekeleza suala la jinsia na maendeleo ya jamii na kwamba Wizara hii kazi yake kuu ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Jamii katika kila Wizara, Idara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viti Maalum viti hivi vimewekwa kwa mujibu wa Katiba. Sisi sote tumeapa kuitii, kuitetea na kuitunza Katiba hii. Viti hivi vina lengo maalum. Hata kama hapo baadaye itaamuliwa kufuta jina la Viti Maalum. Viti kwa ajili ya wanawake vitaendelea kuwepo. Kwa hakika, viti hivi ni vya Taifa yaani *National Seats*. Naomba kupendekeza kuwa viti hivi viitwe Viti vya Taifa, sio maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kwa kila hali ili nchi hii iweze kuendelea inahitaji mchango wa wanawake katika jamii yetu. Historia ulimwenguni imeonesha kuwa wanawake wamekuwa wakinyanyasika na kubaguliwa na mfumo dume ambapo mambo mengi yenye kuhusiana na haki za wanawake yamekuwa yakiamuliwa na wanaume. Matatizo mengi yanaambatana na masuala ya imani za dini na madhehebu mbalimbali yakiwa ni mapokeo kuwa Mwenyezi Mungu kuwa aliumba mwanaume na mwanamke akaumbwa kutokana na ubavu uliotolewa kwenye ubavu wa mwanaume, mapokeo haya yamekuwa na madhara makubwa sana katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Ulaya ndizo zilizobaini tatizo la kuwaona wanawake kama viumbe dhaifu na kuchukua hatua. Wakachukua hatua za makusudi za kubadilisha sheria za manyanyaso na kuleta usawa na hatimaye wakaruhusiwa kushiriki katika shughuli za kijamii ikiwemo kuruhusiwa kuajiriwa katika nafasi mbalimbali za viwandani, kwenye vyombo vya dola na kushiriki katika shughuli za kisiasa na maamuzi muhimu kwenye vyombo mbalimbali vya Kiserikali. Matokeo yake nchi za wenzetu ambazo ni za Ulaya na Marekani walipotambua haki za akinamama na watoto wamepiga hatua za maendeleo. Wakushirikishwa katika chaguzi za kidemokrasia kwenye nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko sababu ya msingi ya nchi yetu kuendelea na utaratibu wa kuheshimu haki za wanawake na kuthamini michango yao katika ustawi wa Taifa letu. Naishukuru Serikali kwa hatua yake ya makusudi ya kuwashirikisha wanawake katika Bunge kupitia Viti Maalum na katika nafasi za uongozi ndani ya Serikali na maeneo mengine mengi, kwani kwa hakika wanawake ndiyo walio wengi nchini mwetu na ndiyo wazalishaji mali ndani ya jamii yetu. Kwa ujumla wanawake ni waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu iendelee na utaratibu wa kurekebisha sheria mbalimbali kandamizi ili hatimaye nchi yetu iwe na usawa miongoni mwa wananchi wanaume kwa wanawake. Niombe pia Serikali iendelee kuiongozea fedha Wizara zaidi ili kuongeza ufanisi ili iweze kuboresha pia Vyuo vya Maendeleo nchini.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto kwa huduma nzuri pamoja na Hotuba nzuri. Aidha, nawapongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara kwa Hotuba nzuri. Napenda kuchangia machache kwa nia ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara iharakishe uboreshaji wa sheria zinazowakandamiza wanawake kwa namna moja au nyingine kama Sheria ya Ndoa, Sheria ya Ardhi na Sheria ya Mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iharakishe utengenezaji wa Kanuni za Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009. Sambamba na uandikaji wa kanuni nashauri Wizara iandike *The National Child Protection Policy* ambayo itatoa mwongozo kwa kila mdau anamhudumia mtoto kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, kati ya *NGO's* zote zinazohudumia watoto ni moja tu inayo *Child Protection Policy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iharakishe kukamilisha *Street Children Strategic Plan* pamoja na kutoa ripoti ya *Street Children Survey* iliyofanyika kwa ushirikiano na Shirika la *Railway Children* la Uingereza. Hizi *Documents* mbili ni muhimu sana katika kutengeneza mchakato sahihi wa kushughulikia tatizo la watoto wa mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Benki yetu ya wanawake Tanzania iharakishe mchakato wa kupeleka huduma zao vijijini. Nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya na ninawakaribisha sana Morogoro vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kazi nzuri. Naomba waangalie jinsi watakavyoboresha mitaala yao ili waweze kutoa mafunzo ya uongozi pamoja na namna ya kuboresha hali zao za kiuchumi. Kwa makundi maalum wakiwemo wanawake na vijana. Ningependa pia waangalie namna ya kuendesha mafunzo maalum kwa wastaafu hususan wanaotoka katika Taasisi zetu za ulinzi kwani wengi wao wanastaafu wakiwa na umri mdogo. Hatua hii itasaidia kuwatia moyo pamoja na kuimarisha dhana ya uraia mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa malengo yao ya mwaka 2011/2012.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuanzisha Benki ya wanawake. Benki hii ni mkombozi wa Taifa la Tanzania, kwani ukiwasaidia wanawake basi umesaidia nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha wanawake wote wafaidike na benki hii, lazima benki ifungue matawi yake nchi nzima. Pia benki iendelee kuongezewa mtaji ili wanawake wengi zaidi waweze kukopa. Vile vile Serikali iombe Jumuiya za Kimataifa wachangie mtaji wa Benki ya Wanawake. Tunaiomba Wizara iombe Benki ya Wanawake ifungue Tawi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukeketaji wa watoto na wanawake. Inasikitisha sana hadi leo bado vitendo vya kukeketa wanawake bado vinaendelea. Suala hili lazima lipewe umuhimu wa pekee ili vitendo hivi vikomeshwe. Bado adhabu zinazotolewa kwa wale wanaokamatwa ni ndogo. Hivyo, adhabu iongezwe na wale wanaokamatwa wafungwe maisha. Wakifungwa maisha hawatoweza tena kuendelea kukeketa watu wengine.

**MHE. DKT. AUGUSTINO LYATONGA MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pamoja na pongezi hizo Bajeti ya Wizara hii ya Sh. 16,000,000,000/= ni ndogo, ingefaa fedha hizi ziongezwe kwa lengo la kusukuma maendeleo ya wanawake na makundi yasiyojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatengwe maeneo maalum kwenye Vituo vya Polisi ambapo wanawake wakifanyiwa vitendo vya kikatili wanaweza kujieleza. Katika Jimbo la Vunjo kuna idadi kubwa ya watoto yatima, wanawake wajane, vijana wasio na ajira, hivyo namwomba Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aone jinsi ya kusaidia makundi hayo. Nashauri fedha za kutosha ziwekwe kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Nashauri Vyuo vya Maendeleo ya Jamii viimarishwe, vifanyiwe upanuzi na ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuyachukulia hatua za kisheria Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayojinufaisha kupitia migongo ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Nashauri Halmashauri za Wilaya, majiji na manispaa kutenga asilimia kumi ya mapato yao kusaidia maendeleo ya vikundi vya akina mama na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweke utaratibu wa uimarishaji wa mifumo ya kijamii ya kutunza watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, kwa Bajeti ya bilioni 16.2 tu Wizara hii ni kama Idara. Serikali itoe kauli ama iongeze Bajeti na majukumu ya Wizara ikiwemo kuhamisha majukumu ya ustawi wa jamii toka Wizara ya afya ili kuwa na Wizara yenye tija zaidi. Serikali iongeze fedha kwa kuwa Bajeti ya maendeleo ni chini ya asilimia thelathini na ukiondoa fedha za Benki ya Wanawake fedha za maendeleo ziko chini ya asilimia ishirini, huku Bajeti ya mishahara ikiwa zaidi ya asilimia hamsini ya Bajeti yote ya matumizi ya kawaida. Vol. IV kifungu 3001, kasma 4943, fedha za Benki ya Wanawake (*TWB*) ni vizuri zikatolewa na Wizara ya Fedha moja kwa moja. Fedha za Maendeleo kwa Wizara ziongewe kwenye vifungu 2001, 2002,

2003, 4305 na 5415. Aidha, ikiwa Serikali itaendelea kutumia fedha za maendeleo toka Bajeti husika toka kifungu 3001 basi Serikali irekebishe masharti ya Benki ya Wanawake (*TWB*) ili kuwezesha wanawake wengi zaidi kwa urahisi. Izingatiwe kuwa kwa mwaka wa fedha uliopita, fedha zilizotengwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) ni milioni 128 tu ambacho ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wizara itoe kauli, mwezi Februari na Machi, 2011, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto alitoa kauli yenye kueleza kwamba CHADEMA inafadhiliwa toka nje kwa ajili ya kuandaa maandamano ya kuvunja amani ambayo yatawaathiri wanawake. Nataka kauli iwapo huo ndio msimamo wa Wizara na Serikali na msingi wa msimamo huo potofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara iongeze kasi ya kukamilisha mikakati, kanuni na nyaraka mbalimbali kuhusu maendeleo ya jamii, jinsia na watoto na asasi za kiraia kwa kuwa kwenye Hotuba ya Waziri nyaraka hizo zimeelezwa kuwa ziko katika hatua ya rasimu. Wakati wa Bajeti ya mwaka 2010/2011, Wizara iliahidi kuwa, ingekamilisha rasimu hizo mwaka huu mwezi Machi 2011, Waziri aliahidi mbele ya Rais Kikwete kuwa taratibu za rasimu hizo zingekamilishwa mapema.

**MHE. DAVID ERNEST SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wa mitaani. Wizara inatakiwa itueleze ni namna gani itaweza kukabiliana na watoto wa mitaani hasa wale wanaotoka na kuishi katika mazingira magumu na hatarishi nchini, maana Taifa lenye watoto wengi wa mtaani linaonesha kushindwa kutatua matatizo yake na majukumu ya kuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mirathi kwa wajane. Wizara itueleze ni wanawake wangapi wameweza kutatuliwa matatizo ya mirathi na ni kwa nini kumekuwa na ongezeko na tatizo la mirathi nchini kwa wajane hususan katika maeneo ya vijijini na baadhi ya madhehebu ya dini kuwatenga kama kutowapa kipaumbele wanawake wakati wa ugawaji wa mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mikopo kwa wanawake. Wizara sasa inapaswa kutueleza ni kwa nini imeshindwa kusaidia wanawake hususan maeneo ya vijijini kwani hakuna tofauti kati ya vijijini na mijini kwa wanawake. Binafsi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi tungeomba kuambiwa ni kiasi gani tumepangiwa kwa mwaka huu wa fedha wanawake wa Jimboni kwangu watapata na pia tumepangiwa semina ngapi kwa ajili ya kuwainua wanawake kiujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya wanawake. Tunaomba pia Wizara sasa ielekeze kupanua wigo wa matawi ya Benki ya wanawake hususan katika Jimbo la Mbozi Magharibi ili kuweza kusaidia wanawake wa huku kwani wana shughuli na biashara ndogo ndogo nyingi. Hivyo basi, kufanya hivyo kutawainua wanawake wengi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya wanawake, wanaume na watoto wetu wa ngazi zote. Ni jambo la kusikitisha sana kuona Wizara nyeti kama hii kutengewa fedha bilioni 16,256,000/=. Hizi fedha zitatosha nini kuinua makundi haya yote pamoja na kundi la walemavu. Serikali haioni umuhimu wa Wizara hii ndio maana kila mwaka Bajeti inapunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa mazingira magumu hapa nchini ni tatizo kubwa. Hii ni changamoto kubwa sana kwa Taifa letu na kwa pamoja lazima kuangalia jinsi ya kupambana na tatizo hili. Watoto wa mitaani kila leo wanaongezeka, wamejaa kila kona mijini. Ongezeko la watoto wa mitaani linachangiwa na Serikali kutolishughulikia suala hili kwa uzito unaostahili na pia walezi na wazazi kushindwa kutimiza wajibu wao kikamilifu. Wapo wazazi wanaowatumia watoto kwenda kuomba na kutafuta riziki mitaani. Wapo wazazi wanaofanya vitendo vya ukatili kwa watoto hata kupelekea watoto kukimbia majumbani. Wapo wazazi au walezi ambao hawajishughulishi kuona nini mtoto anafanya, yuko wapi na kwa muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wote ni wa Taifa na mara baada ya kuzaliwa analindwa na sheria na anatakiwa kupatiwa haki zake zote za msingi, ni wajibu wa Serikali na jamii kuhakikisha watoto wote wanaishi vizuri. Watoto wa mitaani wana uwezo mkubwa, wana vipaji mbalimbali, wana ujuzi na wanaweza wakiwezeshwa. Tunaitaka Serikali sasa watueleze hapa Bungeni kwamba ni mipango gani ya uhakika imeandaliwa ya kushughulikia suala la watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu unyanyasaji wa watoto. Vitendo vya unyanyaswaji, uonevu wa watoto na ukatili kwa watoto unaendelea kuongezeka kila leo, watoto wadogo wanabakwa, wanalawitiwa, wanachinjwa katika maeneo mbalimbali. Taarifa hizi za ukatili kwa watoto zinafika kwa vyombo vya dola lakini hazifanyiwi kazi kikamilifu na kwa wakati. Polisi wamekuwa wakichukua rushwa na kuwalinda watuhumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi/walezi wanawadhibu watoto wao adhabu mbaya sana, kubwa za kuwaumiza, za kuwatosa wapate adhabu kubwa ya kuwakomesha kabisa vitendo hivi kwa watoto. Mahakama zinachelewesha sana kesi zinazowahusu watoto miaka inapita kesi hazizungumzwi, vitendo vya uonevu kwa watoto vinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iweke Mahakama maalum kwa ajili ya kushughulikia masuala la watoto kama ilivyofanya kwa kesi za mauaji ya albino na leo hii vitendo vile kwa walemavu wa ngozi vimepotea. Serikali itekeleze ipasavyo masuala yote ya watoto kwani ndio viongozi, walezi, wazazi na nguvu kazi ya Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, suala la walemavu kwa sehemu kubwa limeachwa kwa *NGO's*, Taasisi za Dini na watu binafsi. Hawa walemavu ni sehemu ya Watanzania na wanastahili haki zote kama wananchi wengine. Lazima Serikali iandae utaratibu na mipango madhubuti itakayowezesha walemavu wote kupata huduma zao na kuishi vizuri.

Wapo wenye uwezo mkubwa sana na uelewa wa kubuni miradi ya maendeleo na kuweza kuzalisha. Wanachohitaji ni uwezeshwaji wa mitaji, vitendea kazi na vyombo vya usafiri kwa wale walemavu wa viungo. Wamekuwa wanakaa mitaani kuomba misaada na hivyo kuishi kwa kutegemea hisani na huruma za wapita njia. Serikali ieleze Bungeni, mipango gani imeandaliwa kwa kundi hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilete sheria hapa Bungeni ya kutoa adhabu kali kwa wale wanaume wote watakaowabaka au kulawiti watoto. Sheria hiyo ieleze wazi ni mwanya wa kuwahasi (*castration*) kwa wale wote walishindwa kutumia haki waliyopewa kwa mambo ya manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wafadhili ijenge kambi au chuo kwa watoto wa mitaani. Kwenye kambi hiyo kuwepo viwanda vidogo vidogo na ufundi wa aina mbalimbali. Watoto wote wa mitaani wawekwe pamoja na kuweza kuzalisha kwa kutumia *talents* na maarifa waliyonayo na watakayopewa. Kuwepo vitengo vya kilimo, bustani za mboga, matunda na kadhalika. Kenya wameweza, leo Mombasa hakuna mtoto wa mitaani, Vietnam wameweza hakuna watoto wa mitaani, sisi kwa nini tusiweze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilete sheria ya kumlinda mwanamke katika kurithi mali za mumewe pale mumewe anapofariki. Mila na desturi za makabila mbalimbali zinawanyanyasa wanawake na watoto pale baba anapofariki. Ndugu wanaangalia mali tu hawaangalii haki za watoto wala haki za wanawake wajane.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa miaka mingi sasa haina tija inayotarajiwa kwa kuwa baada ya matatizo ya baadhi ya masuala wanayoyasimamia baada ya kupungua yanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tatizo la watoto wa mitaani linaongezeka badala ya kupungua, lakini hatujaona jithada za Serikali kutatua au kulipunguza kwa kuwa kuendelea kuwaacha watu wazima wenye nguvu za kufanya kazi wakiendelea kuomba mchana pamoja na watoto wao ambao hawasomi na wako katika hatari ya kugongwa na magari na usiku wakilala pembeni mwa barabara na Serikali inaona na inajua na kuliacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuweka mikakati madhubuti ya kupunguza au kuliondoa kabisa tatizo hilo kwa kutunga sheria kali, kuwa na vituo maalum vya kilimo ambapo viboreshwe kwa kuweka miundombinu kama, zana za kisasa za kilimo, makazi, shule za awali, msingi, ufundi kila Mkoa ili kupeleka watoto hao pamoja na yatima ambapo ni tatizo linalozidi kuongezeka siku hata siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maafisa Maendeleo walioko katika Halmashauri nchini wanaonekana kama hawana kazi kutokana na kukosa mafungu, usafiri wa kuweza kuwafikia wananchi, hasa wanawake waishio vijijini ambako hakuna

vyombo vya habari vya kutosha na kupata taarifa mbalimbali za jamii, kiuchumi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Waziri anieleze umuhimu wa siku ya wanawake duniani na kama uko umuhimu ni kwa nini siku hiyo husherehekewa kwa matamko au ujumbe ambao Kitaifa hufanyika katika mikoa kimzunguko, lakini wanawake hawapewi fursa ya kiuchumi hata nauli ili washiriki maadhimisho hayo, lakini kibaya zaidi siku hiyo viongozi wa Kitaifa toka chama tawala hugharamiwa na kuacha makundi mengine yajitegemee na kupelekea ubaguzi na kuzorotesha maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho hayo wakati yanafanyika Kitaifa ndani ya Mkoa mmoja, mikoa mingine na Wilaya huachwa ikihangaika yenyewe kwa kuwa Wizara haitoi chochote, haipeleki fedha za kuwezesha maadhimisho ya siku hiyo muhimu ambapo ni siku pekee kama ingeweza kuadhimishwa vizuri ingetumika kuelimisha wanawake katika masuala mbalimbali bila kujali itikadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa ya uhakika kuwa, Waziri mhusika alipokwenda Mkoani Morogoro hususan Wilaya ya Kilombero, pamoja kuwa alitumia fedha za Serikali ambapo wanawake wengi walijitokeza kumsikiliza yeye alitumia muda huo kukashfu Vyama vya Upinzani badala ya kuunganisha na kuelimisha jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo sio utawala bora na hiyo tabia iachwe kabisa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wanaume ya kutafuta kukorofishana na wake zao ili ama wawafukuze wake zao wakijua kwamba watoto nao watawafuata mama zao. Mbinu hii inatumika ili kukwepa majukumu ya kulea na kusomesha watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili haliwapati wanawake wa vijijini tu, bali ni tatizo linalowapata wanawake wengi wakiwemo wa mijini na hata baadhi ya viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuogopa aibu na kudhalilika, kuna wanawake wengi sana wanashindwa kwenda kupigania haki zao Mahakamani kwa kuogopa aibu. Kutokana na kuishi na machungu, mateso yasiyokuwa na ufumbuzi, hasa inapotokea kuwa mnyanyasaji yuko kwenye mtandao wa kisiasa au kiuchumi, wanawake wanapoteza maisha yao ama kwa ajili ya maradhi kama shinikizo la damu ama kwa kujiua ili wajipumzishe na mateso yao na mateso ya watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi wa wanawake wametoa malalamiko yao Serikalini kwa madhumuni ya kisaidiwa angalu kupata makazi baada ya wanawake hawa na watoto wao kuondolewa kwenye makazi na kuporwa kila kitu zikiwemo mali walizochuma akina mama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtaka Mheshimiwa Waziri husika asipuuze malalamiko yanayoletwa Serikalini na baadhi ya wanawake ambao wamejikuta

wamenaswa kwenye ulimbo wa mateso yasiyo na ufumbuzi kutokana na historia za kisiasa za wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alielewe na kulitilia maanani tatizo hili nami niko tayari kumpatia ushirikiano wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuichangia hoja hii kwa maandishi, nianze na jinsia. Kwanza kabisa niseme Wizara hii inanigusa kwa njia moja au nyingine kwa sababu mimi ni jinsia ya kike. Katika Taifa lolote duniani mwanamke ni muhimili mkubwa wa Taifa lolote lile duniani. Kwa mantiki hiyo basi, ni lazima kuweko na sheria inayomlinda mwanamke ili ajue haki na wajibu wake ili ajione kwamba yeye ni mchango mkubwa ndani ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake ni wanawake. Ni imani yangu kwamba lazima mtapigania haki ya kumkomboa huyu mwanamke mwenzenu hasa wa kule vijijini ambaye hajui kusoma wala kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutegemea kama Wizara hii itapangiwa pesa ndogo kama hii kwa maendeleo. Hivi kweli ndiyo tunataka maendeleo kwa vitendo au ni vya makaratasini tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Wizara iongezewe fungu ambalo litaratibu shughuli za wanawake ambao hawafikiwi. Pia patungwe sheria mahsusi itakayomlinda mwanamke na haki zake pindi tu akiachika. Tuondokane na mila ambazo zinamnyina haki mwanamke ili kuepusha wanawake wasijingize katika wimbi la umalaya/ukahaba, pia kuepusha watoto wa mitaani, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na mayatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa mtoto anayetafutiwa haya maendeleo, kwanza patungwe sheria itakayomlinda mtoto huyu. Pia pawepo na Kamati ambayo itaratibu masuala ya mtoto na haki zake. Mara nyingi ndoa zinapovunjika familia husambaratika hasa baba anapokuwa ni mlevi. Matokeo yake huwafanya watoto wake kuwa ni wake zake.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Zanzibar baba akitembea na mtoto wake huwa tunasema ni mchawi, kwa imani yetu tu. Sasa kama kukiweko na kitengo hicho ambacho kitaratibu shughuli za mtoto na haki zake, na hatua kali zitungwe kwa yeyote anayefanya na atakayefanya kitendo chochote kile kwa njia moja au nyingine, basi hatua kali zana zichukuliwe ili iwe fundisho kwa jamii nzima ya Taifa hili. Zilindwe na zitetewe haki za mtoto ambaye ni Taifa letu la kesho na kesho kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na ukeketaji. Hivi Wizara imetoa elimu kiasi gani kwa hawa watu wenye jamii hii? Kwani kifungo tu bado siyo suluhisho. Ila elimu

ndiyo itakayombadilisha mtu, kwani masuala ya kimila nayo yanataka busara zaidi na siyo kutumia nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Maendeleo ya mtoto ya mwaka 2008, naona Serikali bado haijafanya kazi kwa ufanisi kwa hali ya sasa inavyoonyesha na hata sheria yenyewe haikuwa bayana. Sera ya Maendeleo ya wanawake na jinsia nayo pia bado haijampatia haki ya kujua yeye kama yeye kujielewa kama ni chimbuko la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimehamasika nichangie kwenye hii mikopo ya wanawake. Naomba nifahamu kuhusu hii mikopo ya wanawake. Mikopo hii ni kwa ajili ya wanawake wa Tanzania Bara tu. Hii benki ya wanawake kwanini basi isianzishwe na Zanzibar ambayo nayo ni Tanzania pia? Kwani kuna vikundi vya *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo mchango wangu. Naomba kuwasilisha. Wanawake ni chimbuko la maendeleo.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake na upendo wake mkubwa kuweza kuniwezesha kusimama au kupata fursa hii ya kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba yake nzuri. Pia nawapongeza Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutetea, kulinda haki ya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaelekeza katika nyanja zifuatazo: Watoto wanaoishi katika mazingira magumu, wanawake vikongwe na wanawake wanaoishi na virusi vya ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaoishi katika mazingira magumu au kwa jina lingine ombaomba, kwa kweli ni janga la Taifa. Ni aibu kubwa unapofika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha, unakutana na watoto ambao wamezagaa ovyo, hawajui cha kufanya na wala hawaelewi waende wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ilione hili kama ni suala ambalo linatupunguzia heshima kama Taifa kuwepo na mpango ambao utawezesha hawa watoto waweze kuishi sehemu moja katika Mikoa husika na wapewe huduma muhimu, kuliko kuwaangalia tu kana kwamba tunafurahia maisha hayo wanayoishi watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipochukua hatua za haraka na kuwaacha watoto hawa wazagae hovyo, watajifunza tabia ambazo sidhani kama kuna mtu ambaye ataweza kuwazuia tena. Tutakuwa tumetengeneza majambazi ambao watatuvamia wenyewe. Tutakuwa na vijana ambao hawana maadili, tutakuwa na vijana wavuta bangi na tutakuwa na vijana wanaovuta madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanawake wakongwe, katika sehemu za vijijini, sehemu za Mikoa ya kanda ya ziwa, bado kuna tatizo la akina mama wazee kuuawa kwa imani za kishirikina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi kuwa na sheria kali ambayo itafanya hawa watu wanaowaua akina mama kwa imani za kishirikina waweze kunyongwa hadharani ili tuweze kukomesha kabisa tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu akina mama wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Tunaipongeza sana Wizara ya Afya kwa kazi nzuri inayofanya katika kuhamasisha watu wote kupima afya zao. Lakini katika kupata majibu haya, akina mama wamekuwa wakikimbiwa na wanaume zao baada ya kugundulika wameathrika na ugonjwa huu wa Ukimwi. Wanawake hawa wamekuwa wakiwaachia mzigo mzito wa kulea watoto peke yao na hao wanaume hukimbia na kuhamia sehemu nyingine mbali. Cha kusikitisha zaidi, wanaume hawa huenda kuoa wanawake wengine watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa tuwe na sheria ambayo itawabana akina baba hawa wenye tabia kama hizo ambazo zinatudhalilisha sana sisi akina mama. Pia ni njia ya kueneza zaidi ugonjwa huu wa Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika Wizara hii ambayo ni mtambuka kwa maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa kuhakikisha ndoto ya wanawake wa Tanzania kuwa na Benki inatimia, kwa kuanzisha rasmi Benki ya wanawake wa Tanzania ambayo ni Benki pekee kwa wote. Naiomba Wizara iendelee na kufungua madirisha madogo ya Benki hii katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kuwafikia walengwa wengi. Naishukuru sana Benki hiyo kwa kufungua dirisha dogo Wilayani Kibaha. Hata hivyo, natoa rai kwa Benki hii kufungua madirisha madogo katika Wilaya za Bagamoyo, Rufiji, Mkuranga, Kisarawe na Mafia ili kuwafikia wanawake wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza zaidi kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Wizara hii ni mtambuka inayoshughulikia masuala mbalimbali ya jamii nzima, bado Serikali haijaipa kipaumbele, kwani kwa kiasi kikubwa imepunguza bajeti hasa ya maendeleo kwa mwaka huu wa

fedha 2011/2012. Kwa mwaka huu ni kiasi cha shilingi bilioni 4.853 zimetengwa ukilinganisha na mwaka 2010/2011 ambapo jumla ya shilingi bilioni 8.278 zilitengwa kwa shughuli za maendeleo. Kati ya hizo, mpaka kufikia Aprili 30, 2011 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 3.928. Ni wazi kuwa shughuli nyingi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2010/2011 hazikufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la bajeti ya maendeleo ya mwaka huu 2011/2012, naomba nijieleze kwenye kifungu 6329 - *Rehab of folk development colleges (FDCs)* ni Sh. 393,167,000 tu zilizotengwa wakati hali ya miundombinu katika vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi *(FDCs)* ni mbaya sana. Kiasi hiki kwa kweli hakitoshi kabisa. Mkoa wa Pwani una vyuo vitatu vya maendeleo ya wananchi vilivyopo Kibaha, Ikwiriri na Kisarawe. Hali ya miundombinu kwa vyuo hivi ni mbaya sana. Nina hakika hakuna ukarabati wowote uliofanyika katika miaka ya karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na viwango vya ufaulu kwa wanafunzi wa Mkoa wa Pwani kuwa ndogo, tegemeo letu lilikuwa vyuo hivi vya wananchi. Hata hivyo, uchakavu wa miundombinu, ukosefu wa pesa za kuendeshea na utendaji kazi na walimu umefanya vyuo hivi kudahili wanafunzi wachache na kusababisha idadi kubwa ya vijana kukosa fursa ya kujiendeleza ha hivyo kukosa fursa ya kujiajiri. Hivyo, naishauri Serikali itenge pesa za kutosha kwa ajili ya kukarabati vyuo hivi vya wananchi ili viweze kudahili wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Wizara ya Maendeleo ya Jamii na watoto ikae mezani na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuratibu namna ya kuhuisha vyuo vya wananchi kuwa vyuo vya ufundi – *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Wilaya, majiji na Manispaa, zinatakiwa kuchangia asilimia 10 kwenye mfuko wa maendeleo ya wanawake na vijana. Hata hivyo, Halmashauri nyingi hazitengi hiyo asilimia kama ilivyokusudiwa, badala yake inatenga tu kasi cha pesa kisichozingatia uwiano wa asilimia 10 ya mapato ya ndani. Mfano, Wilaya ya Bagamoyo mwaka 2010/2011 ilitengewa kiasi cha shilingi milioni kumi tu kwa mfuko huo, kati ya maoteo ya mapato ya zaidi ya shilingi milioni 800. Naiomba Wizara, chini ya kitengo cha tathmini na ufuatiliaji, kifanye ukaguzi kwa Halmashauri ambazo hazitimizi masharti haya na kuzichukulia hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuipongeza Wizara kwa kuendesha mafunzo ya kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake, watoto na maalbino. Nimefarijika sana kuona kifungu 6259 kimeongezewa pesa kiasi cha shilingi milioni 935.1 toka shilingi milioni 297.7 za mwaka 2010/2011 kwa ajili ya kuongeza kazi ya mapambano dhidi ya ukatili kwa wanawake, watoto na albino ambao tumeshuhudia matukio hayo yameongezeka sana. Naomba mafunzo haya yafikie ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Waziri kwa kazi yenu

nzuri mnayofanya kwenye Wizara hii muhimu kwa jamii. Napenda kushauri/kupendekeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa uwezeshaji wanawake, nionavyo mimi kuna umuhimu sasa wa kuimarisha maeneo muhimu ambayo yatawajengea akina mama uwezo kamili hatua kwa hatua katika shughuli endelevu za kiuchumi. Mafunzo katika nyanja zifuatazo ni muhimu sana:-

(a) Ujasiriamali;

(b) Uzalishaji wa huduma muhimu kulingana na mahitaji ya soko *(production of special products/services according to market requirements);*

(c) Mafunzo maalum ya ufungashaji huduma *(packaging)*; na

*(d) Export oriented training.* Mafunzo haya yatawawezesha akina mama kufahamu mambo muhimu ya biashara kimataifa ambayo wanatakiwa kuyajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ni jeshi kubwa na lenye uwezo wa kuzalisha lakini halijawezeshwa kiukweli. Mpaka sasa historia inaonyesha kwamba fedha zilizopelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo kila Wilaya haijawahi kuzidi Sh. 8,000,000/=. kiwango hiki ni kidogo mno kuwekeza kwa jambo lolote katika kundi lolote la akina mama linalofanya shughuli yoyote kiuchumi. Fungu hili lazima liongezwe ili uwekezaji ulete tija na ufanisi.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuwasilisha hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia eneo moja tu la matunzo ya watoto katika vituo maalum (*Day Care Centres*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo napenda kuwasilisha maoni ambayo nimetumwa na mke wangu mpendwa, Mrs. Elisafina Chiza kuhusu haja ya kuanzisha vituo vya kulea/kutunza watoto wadogo, wenye umri wa kuanzia miezi mitatu hadi miaka minne. Mke wangu amepata mawazo hayo baada ya kuona jinsi wanawake wengi wenye watoto hususan wafanyakazi katika sekta rasmi na isiyo rasmi wanavyopata taabu na watoto wao. Tatizo kubwa ni pale ambapo watoto wadogo wanaachwa nyumbani chini ya ulinzi na malezi ya wahudumu wa nyumbani (maarufu kawa majina ya *"house girl"* au msichana wa kazi. Uzoefu unaonyesha kwamba watoto wengi wanapata mateso ya kimwili na kiafya kwa sababu nyingi. Kwa mfano, baadhi ya ma-*house girl* wao wenyewe ni watoto, hawana uelewa wala saikolojia ya watoto wadogo, hawana usafi unaokidhi mahitaji ya mtoto na wakati mwingine wanatumia muda mwingi kufanya shughuli zao (kama kuandika meseji kwenye simu) wakiwaacha watoto bila msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa mama Chiza ni kwamba Serikali ihamasishe wanawake kuuanzisha *Day Care Centres* zitakazotoa fursa kwa wanawake (wazazi) kuacha watoto wao katika vituo vyenye usalama zaidi wakati wao wenyewe wakiwa kazini. Pamoja na vituo hivyo kutoa malezi bora kwa watoto, vitatoa ajira kwa wanawake wenye ujuzi wa malezi na makuzi ya watoto wakiwemo walimu na manesi waliostaafu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*declare of interest* ili kuonyesha mfano. Mama Chiza tayari amesajili kituo cha watoto kinachoitwa *Safina Supper Nunny Day Care Centre*, mjini Dar es Salaam na mwitikio wa wazazi ni mkubwa. Mama Chiza anaishauri Serikali kuliwezesha jambo hili kutekelezeka.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukeketani ni aina moja kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji huu huongezeka mwaka hadi mwaka na hii inamnyima sana mtoto wa kike kwa kupunguzwa viungo vyake alivyozaliwa navyo kuondoshwa bila sababu ya msingi wala haina maana yoyote katika maisha yake ila kumehatarishia maisha yake wakati wa uzazi tu. Serikali ina mkakati gani wa kulimaliza tatizo hili ili kuondoa kabisa hizi desturi zilizopitwa na wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iwahimize sana Maofisa wa Maendeleo ya Jamii kufanya kazi zao kwa ufanisi ili hizi mila potofu kandamizi ziondoke kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya *FDC* vimebaki majengo tu na majengo bila vitendea kazi na walimu hicho sio chuo, ni gofu tu. Naiomba Wizara kushughulikia kwa kina vyuo hivi ili vijana wetu wapate ajira kwa kuajiri wenyewe baada ya kumaliza Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya kuhusiana na maendeleo ya jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba Wizara ina changamoto nyingi ikiwemo ukatili wa kijinsia kama vile mauaji, vipigo kwa akina mama na watoto, ukeketaji, mzigo mzito wa kazi kwa akina mama na watoto pamoja na matatizo ya uonevu wakati wa mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizi, ninao ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itilie mkazo elimu kwa jamii kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii juu ya haki na usawa wa kijinsia. Maafisa hawa ndio wahamasishaji wakubwa wa maendeleo kupitia miradi mbalimbali ya Serikali, binafsi, na vikundi.

Serikali iwatumie Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kuwawezesha kufanya kazi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma jinsi akina mama maendeleo walivyokuwa wakizunguka katika maeneo mbalimbali wa kuelimisha jamii kuhusu miradi, mapishi na malezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa zinazotolewa kwa ajili ya mikopo wakati mwingine hawaziwafikii akina mama wengi na badala yake huwafikia akina baba tena wenye uwezo. Naishauri Wizara iweke mikakati itakayowawezesha wanawake kunufaika na fursa hizo kama vile mabilioni ya *JK*, miradi ya *TASAF, MJADU*, Mikopo kutoka Benki ya wanawake, mikopo ya Halmashauri, *SIDO* na kadhalika ili kuwakomboa wanawake kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara mwakani iongezwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema juhudi iendelezwe ya kuainisha shughuli za *VETA* na *FDC* kwa manufaa ya ajira ya vijana wetu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na mwelekeo mzuri wa utendaji kazi kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ushauri na kutoa maombi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Halmashauri chache zimeweza kupata fedha kutoka katika mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, wakati Halmashauri nyingine nyingi ikiwemo Muheza kukosa fedha. Tatizo kubwa ni kuwepo Watendaji wasio waaminifu ambao huingiza vikundi hewa kupewa mikopo na hatimaye kutorejesha. Tunashauri Wizara ifanye ufuatiliaji ndani ya Halmashauri na kuomba ukaguzi ufanyike katika Halmashauri badala ya kuacha fedha za mfuko mikononi mwa Halmashauri bila ukaguzi unaosimamiwa na mfuko wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji wa teknolojia katika vyuo, majedwali Na. 14, na Na. 15 yanaonyesha jinsi teknolojia mbalimbali zilivyotolewa na kutarajiwa kutolewa 2011/2012 katika vyuo mbalimbali. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kipate teknolojia ya mashine za kuhifadhi matunda na mboga za majani hasa ukizingatia kuwa Wilaya ya Muheza inaongoza kwa matunda mengi kama machungwa na maembe. Nimeona itaingizwa katika mwaka 2011/2012, nashauri ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusaidie kutoa teknolojia hiyo ya mashine ya kuhifadhi matunda na mboga za majani kwa kikundi cha wanawake cha *MUWAMU* kinachojihusisha na utengenezaji wa *juice* katika kiwanda chao Muheza mjini. Kikundi kina wanachama 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahisani kutoka Sweeden wametoa mashine ya *Windmil* ili kuwezesha uzalishaji wa umeme kwa ajili ya chuo, kiwanda tangu mwaka 2008/2009. Pamoja na kuandikia Wizara kusaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kugharamia ufungaji wa *Windmil* hiyo hadi leo Julai, 2011 hakuna kilichofanyika. Naomba Wizara kuchukua jukumu hilo ili kusaidia chuo kupata umeme. Pamoja na jitihada zinazoendelea kupata umeme wa *TANESCO* ambapo mwelekeo ni mdogo na dhamira yangu kuongeza umeme wa *Solar* katika mabweni ya wanafunzi 2011, bado *windmil* inahitajika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ni watu muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu. Wanawake huwa mstari wa mbele katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Lakini mara nyingi kwa wale waishio katika maeneo yaliyo pembezoni mwa Wilaya hususan Wilaya yangu ya Masasi, wanawake hawa hawashirikishwi kikamilifu katika mafunzo, mikopo na kadhalika pale zinapotolewa katika maeneo yaliyopo mjini. Kwa mfano, mafunzo ya ujasiriamali na mikopo. Mambo huwafikia pale tu ambapo watendaji wao wa Kata au wa Vijiji ni makini na maeneo yao. Vijiji vingine wanasikia tu ya kuwa kuna mikopo inayotolewa kwa ajili ya ujasiriamali au *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mikopo hiyo iliyo mingi huwa ni migumu kwa walala hoi kwa vile utaratibu wa kutoa pesa ndipo wapate pesa kulingana na ugumu wa maisha, huwafanya wafanyabiasha walio wengi kushindwa kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hali hiyo, ni vyema Serikali ikaangalia upya utaratibu utumikao katika kuhakikisha kuwa wale waishio bila matumaini, watumainishwe, kwani kwa kukosa viongozi wenye uchungu na maendeleo katika maeneo yao, pawe na uwezekano wa kupeleka viongozi wa Wilaya ili waamshe hawa wanawake waliokata tamaa. Wanawake ndio walezi wakubwa wa familia zao na kukosa kwao huduma za kuendeshea familia zao na maisha yao ndiyo umaskini unavyozidi kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu watoto walio katika mazingira magumu na wale wa Mitaani. Natambua uwajibikaji wa Serikali katika kuhakikisha kuwa watoto hawa wanahudumiwa ingawa ni wachache. Ila sehemu nyingi watendaji huwa ni sehemu ya kuonyesha kama Serikali haiwajali watoto hawa. Kwa mfano, kulikuwa na utaratibu uliotolewa na Serikali wa kuwajengea nyumba baadhi ya watoto wenye mazingira magumu. Pamoja na nia njema ya Serikali, watendaji katika baadhi ya vijiji walivuruga mpango huo na kufanya utaratibu huo usikamilike. Mfano mmoja ni pale kijijini kwangu Nanganga – Masasi, vifaa vilitolewa ikiwemo na saruji, bati na vifaa vyote kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya vijana wa Marehemu Azizi. Nilishuhudia saruji ikiibwa na kuuzwa. Matokeo nyumba ile haikufikia lengo lililokusudiwa. Hivyo ni vyema Serikali ihakikishe mambo yanayokusudiwa kwa nia njema kwa walengwa yanafikiwa.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia kwenye hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwepo na Mfuko wa Maendeleo ya wanawake na tumeona kiasi cha fedha kilichokopeshwa toka mwaka 2006 hadi 2010 kwa Halmashauri 128: Je, Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujiji ilipata mgao huu? Ni wanawake wangapi walifaidika na mkopo huu? Kwanini Halmashauri nyingine zimepata takriban miaka yote na nyingine kukosa kabisa na vigezo gani vimetumika kugawa mikopo hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuishauri Serikali kwamba kutokana na kuongezeka kwa wimbi la watoto yatima na hasa wanaozagaa Mitaani kama maeneo ya Morocco Dar es Salaam na hata kwenye majiji makubwa ikiwemo Mwanza na Arusha, Serikali iweze kujenga vituo vingi zaidi vya kulelea watoto yatima na gharama za kuwatunzia ningependekeza kama wafanyakazi wanavyokatwa *income tax,* basi kikatwe kiasi ambacho kitachukua jukumu hili la ulezi wa watoto yatima na wa Mtaani.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi. Nawapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Sophia M. Simba, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto - Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Katibu Mkuu Bibi Kijakazi R. Mtengwa, Naibu Katibu Mkuu Bibi Anna T. Maembe pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mtazamo wa kuleta maendeleo kwa Watanzania hususan wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, jinsia na watoto chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama kwa ushauri wao mzuri katika Wizara hii muhimu ambao umesaidia sana kuboresha utekelezaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara muhimu sana kwa Maendeleo ya Watanzania, hususan wanawake na watoto ingawa daima imekuwa inatengewa fedha ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na umuhimu wa Wizara hii, naomba sana Serikali kutoa kipaumbele kwa Wizara hii kwa kuongeza kiwango cha fedha katika bajeti hii na zijazo ili kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ndani ya Wizara hii. Ninategemea majibu ya Serikali juu ya ombi langu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mama Sarah Mwaga -Mwenyekiti wa Shirika lisilo la kiserikali *(Afnet)* kwa kazi nzuri aliyofanya ya kusaidia kwa kiwango kikubwa kukomesha mila hatarishi ya ukeketaji kwa Wilaya za Manyoni na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shirika hili utendaji wake umesimama kutokana na kukosa fedha, ninaomba Serikali ilisaidie Shirika hili la *Afnet* ili liendelee

kufanya kazi yake nzuri ya kutoa elimu ya kuacha ukeketaji ambao ni mila hatarishi sana pamoja na kuwafichua Mangariba wanaofanya kazi hii ya ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninategemea majibu ya Serikali wakati Waziri na Naibu Waziri wanajibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kuwa Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* Singida - Ndugu Mlade, amefanya kazi kubwa sana akishirikiana na watumishi wote kukiendeleza chuo hiki kwa kuboresha majengo, kuongeza majengo, kuboresha taaluma mbalimbali chuoni hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hadhi ya chuo kilipofika, naiomba Serikali kukipandisha daraja Chuo hiki cha Maendeleo ya Wananchi Singida kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii ili wananchi waweze kunufaika nacho zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasubiri majibu ya Waziri au Naibu Waziri wakijibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa kuanzisha benki ya wanawake Tanzania, inayotoa huduma nzuri sana kwa kuwakopesha wanawake pamoja wajasiriamali. Kwa kuwa Benki hii bado changa, kwa kupanua huduma, yaani kufungua matawi Mikoani, naomba Serikali ifungue matawi hata ya kanda ili wanawake wengi waweze kuwekeza kwenye benki yao na kisha kupata gawio na mikopo kanda ya kati tawi liwe Singida ambako wanawake wengi wananiomba wapatiwe huduma hiyo. Ninasubiri maelezo ya Mheshimiwa Sophia M. Simba, Waziri mwenye dhamana na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania na ama Naibu Waziri, mdogo wangu mpendwa, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali kwamba kati ya Wizara muhimu ni pamoja na hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutokana na majukumu yake kwa jamii. Hivyo basi, naiomba Serikali sasa kuamua rasmi kuajiri Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wa Kata ili kusogeza huduma kwa Watanzania. Nitashukuru endapo Serikali itakuwa imetenga fedha kuajiri kupitia bajeti hii. Nasubiri maelezo kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kumkomboa mwanamke katika nyanja mbalimbali za kijamii ingawa bado yapo maeneo ambayo wanawake na watoto hawajapata kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi anavyojitahidi kuteua wanawake katika nafasi mbalimbali za uwakilishi wakiwemo Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, najua na jitihada zake Rais, Mheshimiwa Anna S. Makinda - Spika wetu, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa sheria zote zinazogandamiza wanawake na watoto zirekebishwe na zianze kufanya kazi mapema ili wanawake waanze kupata haki zao, mfano Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na nyinginezo. Ninaamini Serikali itatoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona watoto wengi wanazagaa Mitaani hadi kufikia hatua ya kuwa vibaka au ombaomba. Kwa kuwa katika Manispaa ya Singida kipo kituo cha watoto wa mazingira hatarishi kiitwacho Kititimo ambacho hakina mfadhili baada ya mfadhili aliyekuwa anakihudumia kurudi Ulaya baada ya muda wake kumalizika, naiomba Serikali kukihudumia kituo hiki kwani sasa hivi kina tatizo kubwa la kifedha na majengo kuchakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hawana usafiri zikiwemo Halmashauri ya Singida, Iramba, Manyoni na Manispaa ya Singida, jambo ambalo linakwamisha majukumu yao. Ninaomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii na nawatakia kheri katika utekelezaji.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiunga mkono hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa asilimia mia moja. Kwanza naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuwatafutia wanawake na watoto haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii yetu ya Tanzania, hata Afrika nzima kwa ujumla, kwa mwanamke kupata ujauzito (mimba) akiwa nje ya ndoa au kabla ya kuolewa ni jambo lisilokubalika. Hata hivyo, Jamii zimekuwa zikijitahidi kuondoa tatizo hili bila mafanikio. Sasa umefika wakati kuweka hatua madhubuti ya kutungwa sheria kali ya kuwalinda wali, pamoja na kutekeleza mikataba ya kimataifa juu ya haki zao.

Pia iko haja ya kupata tafsiri ya Mwali ni nani? Pendekezo langu ni kwamba, Mwali ni mwanamke ambaye hajaolewa na ambaye umri wake ni chini ya miaka 25 au mwenye umri kati ya miaka 18 hadi ishirini 21 na awe hajawahi kuzaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu, msichana aliyepata mimba wakati anasoma, aweze kurejeshwa tena shuleni katika mwaka wa masomo unaofuata, kufuatia kujifungua au wakati mwingine wowote unaoonekana unafaa na Taasisi ya Elimu lakini kwa hali yoyote ile usimamishwaji huo usizidi miaka miwili ya masomo. Mtu yeyote ambaye atahusika na kumpa ujauzito mwali atakuwa ni Mkosa na awajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iongeze hatua za ziada katika kudhibiti watoto wa Mitaani, maana tatizo hili linatia aibu kwa Taifa letu. Ushauri wangu ni kwamba Wizara ikishirikiana na Serikali kuu, kujengwe vituo mbalimbali ili kuwadhibiti watoto hao. Sambamba na hayo, Jamii ielimishwe katika kupinga tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naipongeza sana hotuba ya Wizara hii kwa jinsi ilivyoandaliwa kwa makini na kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa uthubutu wao wa kuanzisha Benki hii. Hii ni ukombozi mkubwa kwa wanawake wa kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Benki hii kuanzishwa Dar es Salaam, naomba Benki iendelee kuanzishwa pia Mwanza. Hili ombi nalileta nikiwa na sababu zifuatazo:-

- Mwanza ni mji wa pili kwa ukubwa baada ya Dar es Salaam;
- Mwanza ni kitovu cha biashara mbalimbali za kitaifa na kimataifa;
- Mwanza ni mji wa watu wengi (idadi ya watu wengi) na hasa hasa wanawake;
- Mwanza ina *SACCOS* nyingi sana za wanawake zilizosajiliwa na zisizosajiliwa;
- Wanawake wa Mkoa wa Mwanza wana mwamko mkubwa wa sekta za kibiashara na hasa wa mjini kati; na
- Mwanza ni ya wakulima, wavuvi na wafanyabiashara. Hivyo Mwanza ina mzunguko wa Fedha mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache na mengine mengi ambayo Watanzania wanayafahamu kuhusu Mkoa huu, ni halali kuwa baada ya kuanzishwa Benki hii Dar es Salaam, basi ombi kwa Wizara hii kufikiria kuanzisha Benki hii Mkoa wa Mwanza karibuni sana na tunatanguliza shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la watoto kuzagaa mitaani katika mazingira hatarishi ni tatizo linalolikumba Taifa zima. Tusipolichukulia kwa umuhimu wake, Taifa litaathirika katika kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iendelee kwa kasi kubwa kutoa elimu kwa jamii ya Watanzania kuhusu athari za tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGOs* zote zinazojihusisha na malezi ya watoto hawa zieleweke nchi nzima, kama kweli sera zao ni sahihi, kwa kulenga malezi ya watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Semina/Elimu itolewe hasa kwa wanawake tu ambao mara nyingi ndiyo chanzo cha malezi mabaya ya watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali ifikirie suala la kujenga *Centres* (vituo maalum) kwa watoto wa mitaani hasa kwa watoto ambao hawana wazazi kabisa na ndiyo maana wakawa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa jitihada zake inazofanya kuwahamasisha wanawake. Wizara imejikita hasa kwa wanawake wajasiriamali, lakini akina mama wa nyumbani bado kuna changamoto nyingi. Hawa ndio wazalishaji wakubwa wa kilimo na hawafaidi matunda ya jasho lao. Matunda hayo hufaidi baba au waume zao. Hawa akina mama wanahitaji nyenzo za kilimo ili waweze kuzalisha ziada itakayowasaidia kupata mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuhusu Benki ya wanawake. Naomba Benki ya Wanawake ipanuliwe mtandao wake. Hii benki ifungue matawi kila Mkoa na Wilaya kwani huko ndiko wako wanawake wengi. Benki isibaki Dar es Salaam tu. Naomba Mheshimiwa Waziri awaeleze wanawake lini huduma hii wataipata? Ikumbukwe vijijini huko ndiko wanawake masikini wako. Hata vifo vya mama na watoto vinachangiwa na umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ijitahidi kutoa machapisho yanayoelezea ukatili wa wanawake na watoto. Bado kuna mila potofu za kumnyanyasa mwanamke. Pia wimbi la watoto yatima na mitaani wanazidi kuongezeka. Naomba Wizara iwajengee uwezo walezi wa watoto hawa hasa upande wa lishe. Wizara ihakikishe inaweka vituo kila Kata ambavyo vitajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Wizara hasa Bibi Maendeleo wapatiwe vitendea kazi, kwani wanatembea kwa miguu. Naomba wapatiwe usafiri. Wizara iangalie uwezekano hata wa kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto – Mheshimiwa Sophia Simba kwa umahiri wa kazi zake pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wao wote kwa kazi nzuri pamoja na hotuba nzuri waliyoiandaa. Naunga mkono hoja mara mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu Benki ya Wanawake. Ukweli ni kwamba Benki hii haifuati maadili ya kibenki na tayari ipo njiani kufilisika. Hata watendaji wake hawafuati sheria za kibenki ambazo zinaelekezwa na Benki Kuu. Je, tunawasaidia nini akina mama wa Tanzania.

Vilevile sina budi kuulizia suala hilo la Benki ya Wanawake kwa Zanzibar, kwamba imefikia hatua gani? Kwani ahadi zimekuwa nyingi, lakini mafanikio

hayaonekani, hata matayarisho madogo madogo ya kuonesha dalili kuwa Benki hiyo ipo katika matayarisho hayaonekani. Je, Benki hiyo italetwa lini Zanzibar ili akina mama wanufaike na Benki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vhuo vya Maendeleo ya Jamii *(FDC)* tayari vipo katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania. Viliwekwa kwa ajili ya kuwanufaisha akina mama kuweza shughuli zao za ujasiriamali. Lakini vyuo hivyo havikidhi haja ya mafunzo hayo. Mafunzo yanayotolewa ni kupika na kushona. Shughuli hizo kimaendeleo siyo ya kumnyanyasa mwanamke, ni madogo, kwani hizo ni kazi zake za kila siku. Kumsaidia mwanamke ni kumfundisha kutengeneza batiki, ufugaji bora, ukulima bora wa mboga mboga, kuchanganya matunda kwa ajili ya *juice* bora, *packages* na kadhalika. Kama Wizara itachukua umuhimu huo kwa akina mama kuwapa elimu bora, basi vyuo hivyo vingeliweza kuendelea vizuri na kujiendesha vyenyewe na kufanikiwa vizuri badala ya leo vyuo hivyo kuonekana vinadororora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Maendeleo ya Jamii Ukurasa wa 21 – 25, kwanza naipongeza Wizara pamoja na Waziri - Mheshimiwa Sophia Simba kusogeza maendeleo kwa jamii bila ya kujali jinsi ya kuwapatia mafunzo wananchi 31,877 yenye ujuzi na stadi mbalimbali wakiwemo wanaume 16,468 na wanawake 15,409. Vile vile na katika mwaka 2011/2012 itaendelea kutoa mafunzo kwa wananchi 34,750 ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Wizara hii ni kumsaidia mwanamke na wakati inatoa mafunzo zaidi kumuangalia mwanamke. Lengo kuu ni kumpunguzia mzigo wa kazi mwanamke, ili kujiongezea tija, ubora wa kazi utakaomletea ufanisi. Ukiangalia vipaumbele vingi vipo mjini, siyo vijijini. Hata hiyo elimu asilimia kubwa wanapata waliopo mjini. Sasa kwa makusudi, Wizara hiyo isaidie Watanzania waishio vijijini ili kumkomboa mama anayeishi kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara ichukue hatua ya kuhamasisha akina mama kujinunulia *HISA* na hilo liwe funzo kuu kwa kumgombea mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Mtoto wa Afrika - Kauli mbiu ilikuwa "Tuungane pamoja kuchukua hatua za haraka kushughulikia tatizo la watoto wanaoishi mitaani." Tatizo hilo ni sugu ingawa mara kwa mara Mheshimiwa Waziri tunamwona katika Luninga akizungumzia suala la watoto wa mitaani, hata hivyo ninampongeza. Lakini bado watoto wa mitaani wamezagaa, ombaomba ya watoto hao nyingi hata kujiingiza katika wizi, na hata wale watoto wa kike kubakwa. Suala hili lipo kidogo tu katika ukurasa wa 30 – 33. Wizara haikueleza kwa kirefu ni vipi angeweza kuwasaidia watoto hao. Je, watoto hao wataendelea mpaka lini kuishi maisha hayo yenye mazingira duni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba yake juu ya masuala ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watoto wa mitaani ni kubwa sana na linaliletea aibu Taifa letu. Hata hivyo jamii hii inakuwa ikikabiliwa na matatizo mbalimbali, ikiwemo kupata elimu, kupata matibabu na vile vile kupata nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuona jamii haipati misaada katika kutoa elimu ili ijikomboe. Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe kipaumbele kulitatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watoto ambao ni yatima, hawana mtu wa kuwashughulikia, na kwa maana hiyo, kuwafanya watoto hawa kukabiliwa na matatizo mengi, ikiwemo ugonjwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri awapangie mazingira mazuri yatima hawa ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Maendeleo izingatie zaidi wale ambao uwezo wao siyo mzuri na wametawaliwa kisheria kwa maana kwamba maendeleo yanapatikana bila tegemezi yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya jinsia yamekuwa kwa kiasi kikubwa sana, hali hii inaleta udhalilishaji. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kuliangalia hili na pale inapobaini, hatua za kisheria zichukuliwe.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Sophia Nyambi Simba - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu - Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara husika kwa umakini wa hali ya juu. Pia pongezi nyingine ziwaendee Watendaji Wakuu wa Wizara kwa kufanya kazi bega kwa bega kwa lengo la kuiletea jamii ya Watanzania maendeleo yenye kujali jinsia bila kuwasahau watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia bajeti ya Wizara hii, mchango wangu utakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali ya CCM kwa kujenga vyuo hivi takribani kwa kila Wilaya hapa nchini kwetu. Vyuo hivi vililenga zaidi kuwasaidia watu wa rika na kada tofauti tofauti ili waweze kupata ujuzi/maarifa yatakayowawezesha kujiajiri au kupata stadi za maisha. Kwa kiasi fulani jambo hili linawezekana kwa kipindi hicho vyuo hivyo vilipojengwa. Vyuo hivi pia vilikusudiwa kuwaandaa vijana wetu kupata maarifa ya awali yatakayowawezesha kufanya mitihani na wakifanikiwa kufaulu ili iwe rahisi kwao kujiunga na chuo/vyuo vya *VETA* hapa nchini. Shabaha hii iliwalenga zaidi vijana ambao hawakubahatika kupata Elimu ya Sekondari au hata ambao hawakupata Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na lengo hilo zuri, lakini vyuo hivi vimeshindwa kukidhi malengo hasa ya msingi ya kuanzishwa kwa vyuo hivyo. Tatizo kubwa linaloonekana linalovikabili vyuo hivi ni kuwa Wizara au Serikali imevitelekeza. Sijui kwanini Serikali imevitelekeza vyuo hivi? Serikali haitoi huduma za msingi katika vyuo hivi. Hakuna watumishi wakufunzi, hakuna wanafunzi, hakuna vifaa vya kufundishia na kujifunzia, hakuna mtaalam maalum wa kufundisha, na mbaya zaidi hata watumishi hawalipwi mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto ndiyo inayomiliki vyuo hivi, binafsi naishauri Wizara hii ishirikishe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili Wizara hizi zote mbili zione ni namna gani zitakavyoweza kuvisaidia vyuo hivi, au ikibidi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ikabidhi vyuo hivi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili viwe vyuo vya *VETA* kwa kila Wilaya. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iviboreshe vyuo hivi kwa kivikarabati, kuvipatia watumishi/wakufunzi, kuvipatia nyumba za watumishi, kuvijengea vyumba vya kujifunzia (karakana) na hata kuvipelekea vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Lengo hili likishatimia, basi vyuo hivi viitwe Vyuo vya *VETA* vya Wilaya. Tufikiri zaidi juu ya dhana hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala la huduma kwa mtoto wa kitanzania katika karne hii ya 21 ya Sayansi na Teknolojia. Huduma kwa watoto wa Tanzania hususan wanaoishi vijijini na wale wanaoishi katika mazingira magumu, bado inasuasua. Binafsi nataka Waziri anisaidie kujibu maswali yafuatayo:-

-  Wizara imefanya tafiti ngapi ili kubaini mazingira wanayoishi watoto wa kitanzania?

-  Wizara inawasaidiaje watoto wa Tanzania wa Vijijini ambao bado hawana mwamko wa elimu?

-  Wizara inawasaidiaje watoto wa Tanzania wanaonyanyaswa na kutumikishwa majumbani kwa kufanya kazi za ndani huku wakilipwa ujira mdogo?

-  Wizara inawatambua watoto mayatima wa Tanzania na maisha wanayoishi?
-  Wizara inakabilianaje na tatizo la ubakaji, ulawiti na vitendo vyote viovu wanavyofanyiwa watoto wa Tanzania?

-  Wizara inahakikishaje kuwa inadhibiti mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojikusanyia fedha nyingi toka kwa wahisani/wafadhili kupitia mwamvuli wa watoto yatima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitakuwa busara kama sitaweza kugusia suala la wanawake katika Maendeleo yetu ya Jamii. Ni ukweli ulio dhahiri na wazi kuwa wanawake wa Tanzania hasa wale wa vijijini wananyanyasika sana. Wanaonewa, Wanapigwa ovyo ovyo, wanabakwa, wanakeketwa, wanafanya kazi ya uzalishaji mali zaidi ukilinganisha na wanaume, wanalima mazao ya chakula cha kulisha familia,

wanapika chakula cha familia, wanaokota kuni, wanachunga ng'ombe, wanakamua maziwa na wanachaguliwa wanaume wa kuwaoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, wanawake wa Tanzania bado wanabaguliwa kijinsia. Bado wanawake wa Tanzania wanadharauliwa. Bado wanawake wa Tanzania wanaonewa sana. Bado wanawake wa Tanzania wananyanyasika sana. Bado wanawake wa Tanzania wananyimwa haki zao za msingi. Namwomba tena Waziri wa Wizara husika anisaidie kujibu maswali yafuatayo:-

- Wizara imefanya tafiti ngapi ili kubaini mila na desturi za jamii zetu zinazoendelea kumdidimiza mwanamke?

- Je, Wizara inasaidiaje wanawake wa Tanzania ili waweze kujua haki na wajibu wao katika jamii?

- Je, Wizara inawasaidiaje wanawake wa Kikurya wanaopigwa na kunyanyaswa na waume zao?

- Je, Wizara inatoa msaada gani wa kisheria kwa wanawake wanaobakwa kila kukicha?

- Je, Wizara inawasaidiaje wanawake wa jamii za wafugaji kama vile Wamasai ili waweze kukabiliana na hali ngumu ya maisha inayowakabili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweka msisitizo kuwa wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Waziri na Naibu Waziri wasikae tu ofisini, watembelee maeneo mbalimbali ya nchi ili kubaini matatizo na changamoto zinazowakabili watoto na wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ndio asilimia kubwa ya nguvu kazi ya Taifa letu. Lakini cha kushangaza wenzetu akina baba hawataki kulifahamu hili na matokeo yake ni kutuona sisi watu dhaifu sana na tusio na uwezo wowote mbele yao. Inasikitisha sana kuwa hata miongoni mwa Wabunge wenzetu wanafikia mahali wanatudharau sisi Wabunge wa Viti Maalum. Iweje Mbunge aseme kuwa Viti Maalum kwa wanawake vifutwe kwa sababu tunatia hasara Taifa, wakati tupo hapa kwenye Bunge, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja, basi akemee sana jambo hili la dharau kwa wanawake wa Viti Maalum na waliotudharau. Tunawajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali Mbunge wa Jimbo la Ziwani alitudharau wanawake wa viti maalum kupitia *TBC*. Alisema kuwa

tunaliongezea Taifa hasara na kazi yetu ni kujipamba na kujitia vidani. Hivi nani asiyejua kama tumeletwa duniani kwa kujipamba na kuwafurahisha waume zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine naomba vipimo vya *DNA* vipunguzwe bei ili iwe rahisi kwa wanawake kuwatambua baba za watoto wao, ili wawabane wahudumie watoto wao na Taifa lipungukiwe na watoto wa Mitaani.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba aliyowasilisha leo hii asubuhi hapa Bungeni.

Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi Wa Rehema kwa kunijalia afya njema. Pili, nitumie nafasi hii kuwashukuru wanawake wa UWT Mkoa wa Tanga, kwa kunichagua na hivyo kuniwezesha kuteuliwa na Chama Changu, Chama cha Mapinduzi, kuwa Mbunge wa Viti Maalum katika Bunge lako hili Tukufu. Ni matumaini yangu kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa ufanisi kulingana na matarajio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, namshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Namuahidi Mheshimiwa Rais kwamba sitamuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia kwa namna ya kipekee, mume wangu mpendwa Paschal; wazazi wangu Mzee Mwalimu na Bi.Mzuri; ndugu, jamaa na marafiki kwa kuniunga mkono toka kipindi cha mchakato wa uchaguzi na hadi sasa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nitambue mchango mkubwa wa dada yangu Mwanaali Makwaya katika malezi ya watoto wangu wadogo – Faith na Ayana Mariedo. Katika kipindi chote ambacho nakuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa, nakuwa na amani kwa kutambua watoto wangu nimewaacha katika mikono salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuniongoza vyema, Katibu Mkuu Kijakazi Mtengwa, Naibu Katibu Mkuu Anna Maembe, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri mnaonipatia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale

ambao walichangia kwa maandishi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, atawatambua wakati akihitimisha hoja yake basi mimi nisifanye hivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wa hoja yetu walikuwa wengi, hivyo naomba nichukue nafasi hii kujibu baadhi ya hoja. Majibu yangu yatalenga hoja zilizoelekezwa katika maeneo mawili. Eneo la Maendeleo ya Jamii na kama muda utatosha nitazungumzia kuhusu masuala ya haki za watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la maendeleo ya jamii hoja mbalimbali zilijitokeza na kubwa Wabunge walitaka kujua ni kiasi gani kilichotengwa kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Hoja hii ilichangiwa na Wabunge wapatao 10 na niseme kwamba katika bajeti yetu ya mwaka huu tumetenga kiasi cha sh. 393,197,000/= kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Sophi kilichopo Wilayani Ulanga, Mkoani Morogoro na tumetumia kigezo gani ni kwa sababu Chuo hiki sasa hivi kiko katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili iliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, Wizara imejipanga vipi katika kukabiliana na changamoto za ajira kutokana na wingi wa vijana wanaohitimu darasa la saba na kidato cha nne ili kuongeza vyuo vingine kwa kila Mkoa wa Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna ongezeko kubwa la wahitimu wa elimu ya msingi na sekondari na hii ni kutokana na kazi nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya ujenzi wa shule za Kata. Wizara imeboresha mitaawala ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa mwaka 2002 ili kuongeza fani zinazokidhi mahitaji ya ajira kwa wakati uliopo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ina mpango wa kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25 ili pamoja na mafunzo yanayoendelea kutolewa pia vitoe mafunzo ya ufundi *study* kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli takwimu ambazo tunazo sasa hivi zinaonesha kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2010, vijana karibu laki tano wamemaliza darasa la saba hawako katika vyuo vya *VETA* na pia hawako katika shule za sekondari. Kwa hiyo, ni kweli tunakubali kwamba kuboresha vyuo hivi ni muhimu katika mpango mzima wa kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeulizwa na Waheshimiwa Wabunge, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi vipewe kipaumbele ili kuharakisha maendeleo vijijini. Wizara inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuwa kama nilivyosema awali vyuo hivi ni muhimu sana katika kuharakisha maendeleo vijijini kwani vinatoa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii na *study* za maisha na maarifa kwa wananchi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2010/2011 imekarabati majengo na miundombinu katika Vyuo 34 vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Aidha, Wizara itaendelea na juhudi za kuongeza bajeti yake ili kukidhi

mahitaji ya wanafunzi na wakufunzi na pia kuhakikisha tunakuwa na vitendea kazi vinavyokidhi mafunzo yanayohitajika na jamii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina dhamira ya dhati na ya kweli ya kuviboresha Vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi na ndiyo maana mkitazama Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, mwezi Juni, 2011 mtaona katika ile *chapter* ambayo inazungumzia masuala ya *Human Capital Development*, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vyote 55 vimeweka, tuviboreshe, tuhakikishe kwamba tunaweka miundombinu na walimu kwamba wanapewa ujuzi wa fani mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Kuhusu suala la mitaala, kuna hoja zimezuka kwamba mitaala inayofundishwa imepitwa na wakati, watu wanafuma, wanasuka ukili, kwa nini kusiwe na mafunzo kama ya ujasiriamali. Mawazo yote ya Waheshimiwa Wabunge ni mazuri na kama nilivyosema tumeboresha mitaala ya Vyuoi, hivi sasa washiriki walioko katika Vyuo hivi pia wanapata mafunzo ya ujasiriamali, hivyo ni imani ya Wizara kuwa washiriki ambao watahitimu mafunzo katika vyuo hivi, watakuwa na elimu na maarifa ya ujasiriamali ambayo vitawezesha kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililoulizwa kwamba matumizi madogo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwamba viko *under utilised* na kama nilivyojibu, sisi kama Wizara tutaendelea kuhimiza wananchi kujiunga na mafunzo yanayotolewa na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kuvitangaza, lakini pia nawaomba Waheshimiwa Wabunge mkajaribu pia, wakati mnapokaa katika vikao vya Halmashauri, kuongea na Halmashauri husika, ni jinsi gani tunaweza tukahakikisha kwamba vyuo hivi vinatumika kwa ajili ya manufaa ya Halmashauri husika kwa ajili ya wanachi husika na kwa ajili ya jumuiya husika zinazozunguka Vyuo hivyo. Kwa mujibu wa taratibu zetu, Mwenyekiti wa Bodi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni *DED*, Mkurugenzi wa Halmashauri husika. Kwa hiyo, kama Halmashauri iko *committed* imeona chuo kimekaa hakitumiki vizuri, wanaweza wakaja na mpango mzuri, wakauliza hapa, vijana wa hapa wanataka *skills* gani ili waweze kuendelea. Kwa hiyo, naomba niwahamasishe Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge mnatakiwa kuingia kwenye Bodi za Uendeshaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeulizwa ni kuhusu kada nzima ya maendeleo ya jamii, imechangiwa na Wabunge mbalimbali kwamba, ni muhimuSerikali kutenga fedha kwa ajili ya kuajiri wataalam wa maendeleo ya jamii katika ngazi za Kata ili kusogeza huduma kwa Watanzania. Nakubali kwamba, hivi sasa tuna upungufu wa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata na Maafisa hawa kwa kweli tuseme ni muhimu sana katika mustakabali mzima wa maendeleo ya jamii kama ilivyoelekezwa katika Sera yetu ya Maendeleo ya Jamii. Hivi sasa ni asilimia 56 tu ya Kata zote ndiyo zina wataalam wa maendeleo ya jamii. Jumla ya Kata 1,213 hazina wataalam wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, Wizara inaomba iendelee kuzihimiza Halmashauri nchini, kupitia TAMISEMI ili zitenge fedha za kutosha ili ziweze kuwaajiri wataalam hao katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, tuna agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, alilolitoa mwaka 2008 kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii waajiriwe katika kila Kata. Agizo la Waziri Mkuu ni agizo halali na linatakiwa kutekelezeka haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo pia limeulizwa kwamba Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri haziko katika hali nzuri, zinahitaji kujitathmini na kujipanga vema katika kutekeleza majukumu yake ya msingi. Huu ni ushauri tunauzingatia, ni kweli kwamba ukienda katika Halmashauri, Idara ya Maendeleo ya Jamii unaikuta ni Idara nyonge, haina bajeti, haina fedha, haina gari, wanakuwa kama vile ni *spare tyre*, kwamba huyu leo ana shughuli ya UKIMWI anakuchukua, kesho huyu ana mambo ya kilimo unachukuliwa. Yaani wanakuwa hawana hata *working plan* ambazo wanaweza wakajiwekea kwamba kwa mwaka huu wa fedha natakiwa kufanya kazi moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize tu kwamba, tutakuwa na miradi mizuri sana ya kilimo, ya afya, ya elimu lakini bila kuzishirikisha Idara za Maendeleo ya Jamii hatutaweza kufika popote, kwa sababu wao ndiyo wenye wananchi, wao ndiyo wanajua jinsi ya kuwafikia wananchi, wao ndiyo wanajua ni jinsi gani ya kuwahamasisha wananchi. Kwa hiyo, nitumie fursa hii tena kuzikumbusha Halmashauri kwamba ni muhimu kuzijengea uwezo Idara za Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri husika na ikiwemo kuwapatia vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri ili waweze kuwafikia wananchi wengi zaidi, hivyo kusimamia na kuhamasisha jamii kuhusu ushiriki wao katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ambayo yameulizwa ya kuhusu *theme* hii ya maendeleo ya jamii ni ya Jimbo moja moja, tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie lile ambalo amelizungumza Mheshimiwa Lema kwamba tumeijenga Tanzania gani, kwamba sasa hivi watu hawataki kufanya kazi, wamekaa tu, wanachangia harusi, wanachangia vipaimara, lakini hawachangii maeneo ambayo ni muhimu kwa maendeleo yao. Kwa ufupi Mheshimiwa Lema nimwambie ndiyo maana tuna Sera ya Maendeleo ya Jamii. Lengo la Sera hii ambayo inasimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ni kujenga ari, mwamko na hamasa kwa jamii ili kuweza kushiriki katika shughuli za maendeleo na kujiletea maendeleo yao ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lema naomba utusaidie pia kama Mbunge wa Jimbo, ukikaa katika vikao na wananchi uendelee kuwahamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa Wizara yetu, kila mtu yuko *involved*, sio kwamba kazi hii inatakiwa kufanywa na Sophia Simba na Naibu Waziri wake, kila mtu ana *role* ya ku-*play*, kuhakikisha kwamba jamii inashiriki vizuri katika mchakato mzima

wa maendeleo ya jamii na ndiyo maana ukitaka ukitazama Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, inazungumzia kwa uwazi kabisa, jamii inatakiwa kuchukua hatua gani ili kuweza kushiriki katika maendeleo ya nchi kwa ujumla na sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto *entry point* yetu ya kuingia katika kuhamasisha jamii ni hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata na wanatakiwa wawepo katika *level* ya Wilaya na katika *level* ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema, hawa tunawatumia kama vile chachu ya mabadiliko, wao ndiyo wanatakiwa waende vijijini, wao ndiyo wanatakiwa wakae na wananchi kuwahamasisha, lakini na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge pia tuendelee kuwahamasisha wananchi wetu. Kwa mfano, wakati nilipokuwa mdogo nikisoma vitabu, wanasema Maafisa Maendeleo ya Jamii wakati wa miaka 1980/1970 walikuwa *very active* na ndiyo waliweza kweli kuhimiza maendeleo ya nchi, siasa ni kilimo, kilimo kwanza, elimu ya kufa na kupona, lakini kwa nini sasa hivi hatuoni jamii ikishiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Halmashauri yake awatumie na apiganie kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii wawezeshwe ili kuweza kuleta mabadiliko ya fikra na mitazamo ndani ya jamii katika Jimbo lake. Hali kadhalika nachukua fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kama nilivyosema ni la moja kwa moja kwa mfano, chuo cha maendeleo ya jamii Rungemba, kwa nini kisibadilishwe kutoka stashahada hadi shahada. Hii ilikuwa ni hoja ya Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa. Nmwambie Mheshimiwa Mgimwa kwamba chuo hiki kilianza kwa kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya cheti na baadaye stashahada kwa wanawake, Wizara itazingatia ushauri wa kuanzisha mafunzo ya taaluma hii katika ngazi ya shahada ya kwanza mara tu utaratibu na wakati utakaporuhusu, kuna masuala ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Muheza, kuna masuala ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Singida. Yote haya nitaomba tuyajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naomba niingie katika eneo la haki za watoto. Kuna hoja mbalimbali zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kwanza ni lini Kanuni za Sheria ya Mtoto zitakamilika, hoja hii imetolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa John Mnyika. Niseme tu, ni kweli Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 20, Novemba, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa tuko katika mchakato wa kukamilisha taratibu za kanuni, awamu ya kwanza ya uandaaji wa kanuni za Sheria ya Mtoto zilizoandaliwa imekamilika, tumeandaa kanuni za kuwasili mtoto (*adoption)*, kanuni za udhibiti wa vituo vya kulelea watoto mchana (*children's home regulations)*, kanuni za vituo vya kulelea watoto, *(day care centres)* na kanuni za utumikishwaji wa watoto (*child labour regulations)*. Katika awamu ya pili pia kanuni ambazo zimeandaliwa ni pamoja na kanuni za ulinzi na haki za mtoto *(child protection and right regulations)*, lakini sasa

hivi pia tuko kwenye mchakato wa kuanzisha kanuni za uanzishaji wa Mahakama za watoto. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaendelea vizuri na muda si mrefu tutakuwa tumekamilisha utengenezaji wa kanuni husika zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ilikuwa ni ukatili dhidi ya watoto kwamba vitendo hivi vya ukatili dhidi ya watoto vimeongezeka tukisikiliza kupitia vyombo vya habari, redio, magazeti na televisheni. Ni kwamba Sheria ya Kumlinda Mtoto dhidi ya ukatili ipo na ni Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009, sisi kama Wizara tutahakikisha tunasimamia utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo lilitolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba iwepo sheria ya kuwabana akinababa wanaotelekeza watoto wao. Niseme pia Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, imebainisha kwamba mzazi ana wajibu wa kumtunza mtoto ikiwemo kutoa chakula, malazi, mavazi, matibabu. Sasa wale akinababa ambao wanakataa kutunza watoto wao ambao wamewazaa wenyewe, kuna utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako Tukufu niwashauri wazazi wanawake waende katika vyombo vya Serikali, kuna jinsi ya ku-*prove* kwamba huyu mtoto ni wa baba fulani au sio wa baba fulani. Kumewekwa njia mbalimbali kwa mfano, kama kuna cheti cha ndoa au kama katika kile cheti cha kuzaliwa mtoto kumeandikwa jina la huyo baba, huyo baba anatambulika kisheria kwamba ana haki ya kumtunza huyo mtoto. Kwa hiyo, akinamama inabidi mwandikishe majina ya wazazi ambao mna uhakika nao kabisa ndiyo akinababa wa watoto wenu. Lakini pia siku hizi kuna suala la *DNA test* kama baba anakataa kutunza mtoto wake, basi tunawashauri wazazi pia wakapime ili wathibitishe ubaba na Mahakama iweze kutoa hukumu ya matunzo kwa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kubwa la watoto wanaoishi mitaani na katika mazingira magumu. Niseme kwamba, ni kweli tatizo hili linaongezeka. Utafiti uliofanywa na Shirika Lisilo la Kiserikali la Uingereza mwaka 2009 chini ya uratibu wa Wizara ya Maendelo ya Jamii, Jinsia na Watoto unaonesha kuongezeka kwa watoto wa mitaani katika Mikoa saba ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya na Arusha. Sababu kubwa kwa nini watoto wetu wanakimbilia mitaani ni ukatili dhidi ya watoto, njaa na umaskini, ukosefu wa upendo na usimamizi madhubuti wa watoto na kuvunjika kwa ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Sheria imeweka wazi mamlaka husika ya kushughulikia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Kifungu cha 94 cha Sheria ya Mtoto ya 2009kinatamka wazi kwamba wajibu wa kulinda na kukuza haki za mtoto aliyepo katika eneo husika ni wa Serikali za Mitaa. Sheria imekwenda mbali zaidi inasema Serikali za Mitaa zina wajibu wa kuwa na orodha ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuwapa msaada, kuishi kwa staha ndani ya jamii na kuwaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitumie Bunge lako Tukufu kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge, wahakikishe kwamba Serikali za Mitaa zinatimiza majukumu

yao ya kuhakikisha kwamba, watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu wanaishi kwa haki na staha kulingana na haki za mtoto. Sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii tutaendelea kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wadau mbalimbali kama nilivyosema Serikali za Mitaa, lakini pia tayari tumeunda kikosi kazi cha Kitaifa cha kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi mitaani, tuangalie ni mifumo gani na mikakati gani madhubuti inaweza kutusaidia kutuepusha na tatizo hilo. Aidha, nitoe rai kwa familia na jamii husika kwamba ni jukumu letu wote kuhakikisha watoto wanaishi kwa staha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wametoa mifano hapa, kwa mfano Zanzibar, wanasema mtoto baba yake amekufa, mama yake amekufa analelewa na shangazi, analelewa na mjomba, ni kwa nini jamii imebadilika sasa hivi, zamani ulikuwa unaweza kuishi tu kwa jirani yako wala msiwe mnahusiana. Kwa hiyo, nasema ni jukumu letu sisi wote jamii ya Kitanzania kuhakikisha kwamba tunalitatua tatizo la watoto wanaoishi mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vituo vya kulelea watoto, ushauri huu ulitolewa na Waheshimiwa Wabunge, tumeupokea na ni kwamba niseme tu Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 imeweka utaratibu wa uanzishwaji wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wenye ulemavu wa ngozi, Wizara itaendelea kuelimisha jamii kuepukana na mila zenye kuleta madhara, pia tutaendelea kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wadau mbalimbali kama *Under the Same Sun* kuhakikisha kuwa watoto hawa wanaendelezwa kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ajira na ukatili dhidi ya watoto. Nitumie Bunge lako Tukufu kujibu hoja za Wabunge kwamba Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 imeweka utaratibu wa kutoa ajira nyepesi kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 14 na inazuia kazi za udhalilishaji kwa watoto chini ya miaka 14 na inazuia kazi za udhalilishaji kwa watoto chini ya mikaa 18. Aidha, ajira ya watoto majumbani ni moja ya kazi zinazodhalilisha watoto kwa kuwapa kazi nyingi na mishahara midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kuja mbele yako kujibu hoja zilizotolewa leo hii. Lakini kabla sijafanya hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote waliojeruhiwa kwenye ajali ya *Bus* la Hood huko Morogoro. Mwenyezi Mungu awape afueni ya haraka majeruhi na kwa wale waliopoteza maisha, Mwenyezi Mungu azipe familia zao mioyo ya subira na roho za marehemu zipumzishwe mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda hapo asubuhi nilishindwa kupeleka salamu zangu kwa wadau wangu wengi, hivyo nachukua nafasi hii kuwapongeza wanachama wa Chama cha Mapinduzi pamoja na wananchi kwa

kukichagua Chama cha Mapinduzi na hivyo kuendelea kuongoza nchi yetu kwa amani na usalama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu nyingi kwa viongozi wa UWT wakiwemo Wenyeviti na Makatibu wote wa Mikoa, Makatibu wa Wilaya, Makatibu Kata na Makatibu wa Matawi. Kwani bila ya wao leo hii nisingesimama hapa mbele yenu. Vile vile salamu hizi za shukurani ziwaendee Wenyeviti wote na wanachama wote wa UWT. Nawahakikishia kwamba Chama na Jumuiya zake zinatambua kazi kubwa inayofanywa nao. Mungu aendelee kuwajaza hekima na afya tele. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kwa namna ya pekee kuwashukuru Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyowasilisha hapa Bungeni leo asubuhi tarehe 21 Julai, 2011. Kwa michango yao mizuri ya kina yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Jumla ya Waheshimiwa 131 walichangia hoja yangu, ambapo Waheshimiwa 13 wamechangia kwa kauli. Waheshimiwa 110 wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa wanane wamechangia kupitia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetiwa moyo sana na pongezi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na jinsi walivyoonesha umuhimu wa kuongeza Bajeti. Tunathamini michango yote iliyotolewa. Si rahisi kuzijibu hoja zote katika kipindi hiki kifupi nilichopewa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itazijibu hoja hizo zote kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwataja waliochangia kwa kauli humu Bungeni na kuwatambua. Wa kwanza Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Mchungaji Dokta Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Meshack Opulukwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia Wizara yangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Mkenge; Mheshimiwa Phillipa Geofrey Mturano, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, Mheshimiwa Naomi Mwakyoma, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti waliochangia kwa maandishi wapo Waheshimiwa Wabunge 101. Nao ni Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Amos Makalla,

Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Waridi Bakari Jabu, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mheshimiwa Esther Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Engineer Gerson Hosea Lwenge, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Shekifu Henry Daffa, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Victor Mwambaswa, Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mheshimiwa Subira Hamisi Mgalu, Mheshimiwa Dokta William Augustino Mgimwa, Mheshimiwa Engineer Christopher Chiza na Mheshimiwa Amina Andrew Clement. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Sabrina Hamza Sungura, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Salome Daud Mwambu, Mheshimiwa Fakharia Khamisi Shomar, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Rukia K. Ahmed, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Geofrey Weston Zambi, Mheshimiwa Mariam A. Mfaki, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Ignas Malocho na Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wapo Mheshimiwa Christowaja Gerison Mtinda, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Omar Ahmed Baduwel, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Profesa Kalikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Susan Aslem Jerome Lyimo, Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Magareth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Athumani Rashidi Mfutakamba, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamisi, Mheshimiwa Mkiwa Abdallah Kimwaga, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Janson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha na Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Dokta Lucy Sewere Nkya, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Beatrice

Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa James Daud Lembeli, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Mahamoud Abuu Jumaa, Mheshimiwa Fenela Mukangala, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Madeye, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Engeneer Stella Manyanya, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Agnes E. Hokororo, Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Naomi Mwakyoma, Mheshimiwa Sarah Msafiri, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi na Mheshimiwa Josephat S. Kadenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wote hawa ambao wamechangia. Niseme tu, michango yao mingi ilikuwa katika kujenga zaidi na kutupa maoni yao jinsi wanavyoona tunaweza tukaendeleza vizuri. Kwa hiyo tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Jamii kama kawaida yake imeendelea kutuelekeza yale ambayo inaona tunahitajika kuyafanya vizuri zaidi. Nasi tunasema tunaenzi maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa manufaa ya Wizara yetu na kwa manufaa yetu na kwa manufaa ya jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amenukuu kwa usahihi dhana ya maendeleo ya jamii kuwa ni hatua ya kuwawezesha watu kutambua uwezo walionao wa kubaini matatizo na uwezo wa kutumia rasilimali zilizopo, kujikita katika kujitafutia kipato na maisha bora. Aidha, maendeleo ya jamii ni sekta mtambuka, ikimaanisha kwamba, inashabihiana na sekta zote zinazohusiana na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kuu la Wizara yangu ni kuhakikisha wananchi wanajengewa uwezo kupitia Wataalam wa Maendeleo ya Jamii walioko kwenye Halmashauri ili waweze kushiriki kikamilifu katika kutekeleza mipango ya sekta mbalimbali. Hivyo, kuziwezesha sekta hizo kukidhi mahitaji na vipaumbele vya jamii. Kwa kuzingatia azma hiyo ya Serikali na Wizara yangu inasimamia na kuendesha mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya stashahada na shahada ili kuwezesha Taifa kupata wataalam wa maendeleo ya jamii na pia mafunzo ya maarifa stadi mbalimbali ambazo huwawezesha wananchi kuzalisha kwa tija zaidi na hivyo kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwarifu tu Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuwa usambazaji wa maji safi na salama, uhamasishaji wa lishe bora na usafi wa mazingira, vyote vinalenga katika kuimarisha masuala mbalimbali yanayolenga kuboresha afya kwa kuwa jukumu hilo linaweza kushughulikiwa na Wizara ya Afya. Ingawa Serikali imefanya mengi katika kuendeleza jamii katika maeneo kama elimu, afya, lishe, huduma za maji safi na salama na kadhalika. Ni kweli kuwa bado zipo changamoto nyingi. Lakini ni vizuri kujivunia mafanikio ambayo nchi yetu imeshayapata, kwa mfano, licha ya matatizo ya kibajeti, Tanzania bado inategemea kufikia malengo ya *millennium* kuhusiana na udahili wa wanafunzi katika elimu ya msingi na sekondari na kupunguza vifo vya watoto wachanga na walio na umri chini ya

miaka mitano. Si vibaya kujilinganisha na Mataifa mengine, lakini si vema kufanya hivyo bila kuzingatia pia uwezo wa kiuchumi wa nchi tunazojilinganisha nazo. Hata hivyo, ningependa kuungana na Waheshimiwa Wabunge ambao walionesha kutofurahishwa sana na kauli ya Mheshimiwa Naomi wakati alipokuwa akizungumza kuhusu kutokuwepo na majukumu ya kutosha kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani pamoja na maoni yake mengine mazuri, katika ukurasa wa tatu *paragraph* ya tatu, amezungumza na namnukuu. "Viashiria hivi vinatoa ushahidi wa wazi kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kiasi kikubwa kabisa Wizara isiyo na majukumu". Aliendelea hivyo katika ukurasa wa nne *paragraph* ya sita kwa kusema, nanukuu. "Kambi ya Upinzani inawataka Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Waziri Mkuu wamshauri Mheshimiwa Waziri kuondoa dosari hii ya kuwa na Baraza kubwa la Mawaziri, huku likiwa na majukumu yanayojirudia na kuingiliana kwa baadhi ya Wizara."

Hapa alikuwa akizungumzia kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii inaingiliana majukumu na Wizara nyingine. Wizara ya Maendeleo ya Jamii inafanya kazi ya kuhamasisha wananchi kuweza kupokea hayo ambayo yanatoka katika Wizara mbalimbali, iwe Afya, iwe Elimu. Maafisa wa Maendeleo ya Jamii ndiyo wenye kazi ya kuhamasisha wananchi wawatoe watoto wao wawapeleke kwenye mashule. Ndiyo wao wenye kazi ya kuhamasisha akinamama waende wakapime *clinic* na kadhalika na kadhalika ikiwemo masuala ya kujitolea kujenga shule, masuala ya miundombinu na mengi mengineyo. Kwa hiyo, ningependa mwenzangu wa Upinzani na wenzangu wa Upinzani wajue kwamba, haya ni masuala mtambuka, Wizara yetu inashughulikia kama *catalyst* wa kusaidia wananchi kuelewa hayo mambo ili waache zile tabia za zamani, wajiletee maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu pia ndiyo wapigaji debe wakubwa ambao wamehakikisha kwamba wanawake tumefika hapa Bungeni kwa wingi pamoja na nia nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini mpiga debe nyuma, Wizara ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazaramo wana msemo wanasema "Asiyejua kumshukuru binadamu mwenzie hata Mungu hatajua kumshukuru." Wizara hii imetoa mchango mkubwa kwetu sisi Wabunge wa Viti Maalum humu humu Bungeni na mpaka idadi yetu imekuwa kubwa kama ilivyokuwa hivi. Kwa hiyo, nahisi Mheshimiwa Mbunge alighafilika kidogo. Yuko hapa kutokana na mwamko mkubwa wa Serikali ambao changamoto zote zinatoka Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Ni vizuri siku zote kukubali ulikotoka na unakokwenda kwamba Wizara hii imetufikisha hapa sisi wanawake kwa kupitia Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa niendelee kujibu hoja za Waheshimiwa mbalimbali. Waheshimiwa wengi wamezungumzia kuhusu fungu dogo lililotengewa Wizara. Nakubaliana nao Waheshimiwa Wabunge kuwa bajeti iliyotengwa

kwa Wizara ni ndogo. Hata hivyo, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wizara ili kutekeleza majukumu yake. Ni matumaini yangu kuwa bajeti ya Wizara itazidi kuongezeka kadri mapato yatakavyoongezeka. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Wizara imeandaa programu ya Maendeleo ya Jamii inayoainisha maeneo ya kipaumbele ili kujenga hoja ya kuhakikisha kuwa bajeti ya Wizara inaongezeka. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua umuhimu wa majukumu makubwa ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Anne Kilango Malecela alizungumzia kuhusu kuhakikisha fedha zilizotengwa katika bajeti zinatolewa. Ni kweli Wizara itawasiliana kwa karibu sana na Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha zote zilizotengwa kwa mwaka 2011/2012 zinatolewa. Hata hivyo, ni lazima tukumbuke kwamba zile fedha zinazotengwa siyo zimewekwa, zinakusanywa. Kwa hiyo, bajeti ni zile zinazopatikana na hizo ndiyo zinapelekwa kwenye Wizara. Kwa hiyo, itategemea sana na makusanyo na ndiyo maana bajeti zetu kwa yale ambayo tulikuwa tumebajetiwa hatukupata pesa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo anasema, Wabunge wahusishwe katika kuweka vipaumbele. Hilo tunalifanya na tunashirikiana na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge katika kupanga vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu mikakati ya kukabiliana na unyanyasaji na ukatili wa wanawake na watoto. Ni wengi sana, nikianza kuwataja nitachukua muda mrefu. Kwa hiyo, napenda niende moja kwa moja katika kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia masuala ya unyanyasaji, ukatili kwa wanawake na watoto ikiwemo vipigo, ubakaji, ukeketaji na manyanyaso mbalimbali, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kuwaelimisha wasimamizi wa Sheria ambao ni Jeshi la Polisi, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Viongozi wa Vijiji na Kimila na Watendaji wa Kata kuhusu kupinga ukatili dhidi ya watoto na wanawake. Wizara pia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi kupitia vyombo vya habari, redio na televisheni, filamu maalum iliyoandaliwa na Wizara yangu na kampeni mbalimbali za Kitaifa na za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeweka mazingira mazuri kwa asasi za kijamii na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto wenye ulemavu wa ngozi. Baadhi ya Wilaya zimeunda Kamati za kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limejitokeza sana ni linalohusu ukeketaji wa watoto wa kike. Waheshimiwa Wabunge, Serikali kwa kushirikiana na

wadau mbalimbali, imeendelea na juhudi za kupambana na tatizo la ukeketaji hapa nchini. Wizara yangu, inaratibu Sekretarieti ya kutokomeza ukeketaji, ambayo inahusisha taasisi za Serikali, asasi za kiraia, mashirika ya kidini na vyombo vya habari. Kupitia Sekretarieti hii, jamii zinazojihusisha na ukeketaji, zimeendelea kuhamasishwa na kuelimishwa kuhusu madhara yake. Vilevile watendaji na wasimamizi wa sheria wamepewa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Adhabu ya 169 (a), inatamka wazi kwamba mtu yeyote ambaye mtoto yuko chini ya usimamizi wa mtu huyo, akamtendea vibaya au kumkeketa au kumuacha au mtu huyo kumsababishia mtoto huyo kukeketwa na yeye mwenyewe kumkeketa, atakuwa ametenda kosa la ukatili. Hivyo, kosa hili halihusu Mangariba peke yao kupewa adhabu, bali linahusu watu wote hata wale ambao wanawapeleka watoto kukeketwa, adhabu hiyo itawakuta. Aidha, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Sehemu ya II, Kifungu cha 13 na 14 kinachohusu ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili, ukiwepo unaosababishwa na mila; inatamka kuwa, *"Mtu yeyote atakayehusika na kosa kama hilo, atapewa adhabu ya kulipa faini isiyozidi 5,000,000/= au kifungo cha muda usiozidi miezi sita au vyote kwa pamoja."* Mapambano ya kutokomeza ukeketaji yanahusu jamii nzima, taasisi mbalimbali, wataalam wa ugani, vyombo vya habari, viongozi mbalimbali ikiwemo pamoja na sisi Wabunge, tunatakiwa tuwe mstari wa mbele kupiga vita masuala ya ukeketaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wabunge wengi wameulizia kwamba Wizara imejipangaje katika kufuatilia suala la marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mirathi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na wadau wengineo, tumeainisha na kutoa mapendekezo ya marekebisho mbalimbali kama vile Sheria ya Mirathi, Sheria ya Urithi ya India ya mwaka 1865 na Sheria za Kimila zinazowakandamiza wanawake, pamoja na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizi yaliwasilishwa kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria, kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa pia walitaka kujua, tangu Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 je, sheria hii imepunguza matatizo ya udhalilishaji na ubakaji kwa kiasi gani? Kulingana na taarifa tulizopata kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, zinaonesha kuwa matatizo ya ubakaji yanapungua. Kwa mfano, kati ya mwaka 2009/2010, matukio ya ubakaji yamepungua kwa matukio 742, sawa na 10.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vinavyotumika kupelekea fedha ya Mfuko wa Wanawake *(WDF)* katika Halmashauri mbalimbali. Ningependa kuwafahamisha kuhusu vigezo vinavyotumika kuzipatia Halmashauri mbalimbali fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ni kwa Halmashauri husika kurejesha fedha za Mfuko baada ya kurejesha hapo awali katika kipindi cha mwaka mmoja kama ilivyoainishwa katika mkataba kati ya Wizara na Halmashauri husika. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mgimwa, ambaye ameuliza swali hili; kwa vile, Wabunge ni Wajumbe wa Kamati ya Mkopo, ngazi ya Halmashauri, ahimize Halmashauri ya Mufindi kurejesha fedha walizopatiwa mwaka 2008/2009, wakirejesha, basi wanapata mkopo mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwambalaswa, anaulizia kuhusu wanawake wa Mbeya, ambao ni wajasiriamali wakubwa, 80% ya wafanyabiashara kwenye masoko wahamasishwe ili waanzishiwe *SACCOS* ambayo itawasaidia. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali imeendelea kuwahamasisha wanawake kujiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)*. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba Mbeya nao wanatakiwa wafanye hivyo, lakini tutalifuatilia kwa karibu zaidi ili kujua wanafanyaje pale katika Halmashauri, kwa sababu, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii waliopo pale ni kazi yao kuwahamasisha wanawake kuanzisha *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mila na desturi zinazowakandamiza wanawake. Waheshimiwa Fatma Mikidadi na Godfrey Zambi na wengineo, walitaka kujua kuna mkakati gani? Mikakati ya kutokomeza mila na desturi za makabila mbalimbali zinazomkandamiza na kumdhalilisha mwanamke na mtoto wa kike, ni pamoja na kurekebisha baadhi ya sheria zinazowakandamiza wanawake au kutunga sheria zinazolinda haki za wanawake. Mkakati mwingine ni kuelimisha na kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari, filamu na kampeni mbalimbali za Kitaifa na Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie riba kwa mikopo inayotolewa. Sera ya Taifa ya Mitaji Midogo midogo, imeelekeza Taasisi za Kifedha kupanga riba za mikopo wanayopatiwa wakopaji na mara nyingi riba zinazopangwa na taasisi hizo zinazingatia gharama za uendeshaji wa taasisi hizo. Hata hivyo, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, umeweka 10% ili kuwawezesha wanawake wengi, hususan wale waliopo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeulizwa swali pia kuhusu Wizara kufuatilia utendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara inafuatilia kwa karibu utendaji wa mfuko huo. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wafuatilie Mfuko huo kwani wao ni Wajumbe katika Kamati ya utoaji mikopo katika Mfuko huo wa Wanawake, *WDF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fedha za Mfuko wa Wanawake, kutolewa Bara peke yake. Hili limeulizwa na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad wa Magogoni. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Hamad kuwa, kwa upande wa Zanzibar nao wanao Mfuko maalum wa kuwakopesha wanawake wa Zanzibar na Pemba, unaosimamiwa na Wizara ya Kazi, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linasema wanawake hawafaidiki na *SACCOS, VICOBA* na *WDF,* kwa vile hawana taarifa na taasisi hizo za *WDF*. Hivyo, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, waajiriwe kila Kata. Nakubaliana naye kwamba tunahitaji kuwa na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata. Lakini kwa sasa, Waheshimiwa Wabunge, Mfuko wa *WDF* ni Mfuko ambao Madiwani wote wanaufahamu na kila pesa inapokuja wakati wa mgawo, Waheshimiwa Wabunge, ni Wajumbe wa Kamati ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limeongelewa sana ni kuhusu Benki ya Wanawake. Kulikuwa na maoni kwamba, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Benki ya Wanawake Tanzania, kwa kuandaa mpango wa biashara na utendaji wa Benki ya Wanawake. Lakini pia kuna maswali kwamba Benki ifungue Matawi mengi zaidi. Hili limesemwa karibu na Wabunge wengi sana ambao nimewataja hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ina mkakati wa muda mrefu na muda mfupi ambao unaonesha jinsi Benki itakavyojipanua. Ieleweke kuwa hii itakwenda sambamba na upatikanaji wa mtaji. Aidha, mipango ya baadaye ya Benki ya Wanawake Tanzania, ni kufungua Matawi mengi mikoani ikiwa ni pamoja na Zanzibar, ambako mawasiliano yameshaanza. Ieleweke kwamba, fedha shilingi bilioni mbili zinazotolewa kila mwaka na Serikali kwa kipindi cha miaka mitano ni kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa benki hii. Hata hivyo, bado fedha hizo ni za Serikali, kwani Benki itakapoimarika na kuanza kuuza hisa zake kwa wananchi, hususan wanawake, Serikali inaweza kuamua kurejesha fedha hizo Serikalini pasipo kuathiri utendaji wa Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Devota Likokola wa Viti Maalum na Mheshimiwa Chiku Abwao, wanasema kufanyike utafiti katika masuala ya jinsia. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali yatolewe kwa Watendaji wa Ugani, ili waelimishe jamii husika. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa, mafunzo ya ujasiriamali yamekuwa yakitolewa na Maafisa Maendeleo ya Jamii na wadau wengine ambao huwa wanatoa mikopo mbalimbali. Pia kuna wakati wa maonesho, kabla ya maonesho kunakuwa na mafunzo ambayo taasisi kama hiyo *TF,* imekuwa ikitoa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali ambayo yamekuja kuhusu Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Waheshimiwa, walitoa ushauri kwamba, Sheria ya *NGOs,* inahimiza *NGOs* kuisadia Serikali, lakini *NGOs* nyingine wanakuwa wapinzani wa Serikali kupitia maandamano, aidha *NGOs* zielekezwe kuendeleza shughuli zao vijijini. Serikali inayatambua Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa ni wabia muhimu katika ujenzi wa maendeleo…

*(Hapa umeme ulikatika ghafla na kumfanya Mtoa Hoja, kushindwa kuendelea kusoma majibu ya hoja)*

**MWENYEKITI:** Tuendelee!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni! Naomba mshumaa! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Pole sana Mheshimiwa Waziri. Sasa, tusubiri kidogo.

*(Hapa umeme ulirudi na Mtoa Hoja akaendelea kusoma majibu ya hoja)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, kuwa ni Wabia muhimu katika ujenzi wa maendeleo ya Taifa. Aidha, *NGOs* zinasajiliwa kwa

lengo la kusaidia juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo ya kijamii na siyo vinginevyo. Aidha, katika kusajili *NGOs,* Wizara yangu imekuwa ikisisitiza umuhimu wa *NGOs* kusambaa vijijini badala ya kujazana mijini tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amos Makalla, alisema *NGOs* zinahangaika kulea watoto wa mitaani na waishio katika mazingira magumu, lakini Serikali haichangii! Serikali inatambua mchango mkubwa wa *NGOs* nchini ikiwa ni pamoja na zile zinazolea watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Ni nia ya Serikali kusaidia mashirika haya kutekeleza majukumu yao kikamilifu pindi hali ya fedha itakapokuwa nzuri. Hata hivyo, mpaka sasa *NGOs* hizi huwa zinapata fedha kutoka katika taasisi mbalimbali ambazo sisi Serikali tunakuwa na makubaliano nazo na zinatoa pesa moja kwa moja kwenye *NGOs* kusaidia shughuli za watoto yatima pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CBOs* zinasaidia sana kuharakisha maendeleo. Hata hivyo, Wizara yangu haijasajili *CBOs,* kwa vile hizi hupata kutambulika tu na Halmashauri, huwa hazisajiliwi popote. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kuhamasisha watu wake kujiunga wenyewe katika *CBOs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, anauliza Wizara kuwa, inahakikishaje kuwa inadhibiti *NGOs* zinazojikusanyia fedha nyingi kutoka kwa Wahisani Wafadhili kupitia mwamvuli wa watoto yatima? Ni kweli zipo tuhuma za wadau wa *NGOs* kujinufaisha kwa fedha za Wafadhili zinazotolewa kuwasaidia watoto yatima. Wizara yangu inafuatilia na kupata kutoka katika *NGOs* taarifa za mwaka za utendaji kazi na taarifa za fedha zinazokaguliwa na mkaguzi anayetambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Ali Khamis Seif anauliza, je, Wizara imejiundia utaratibu gani wa kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa unafanywa kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea? Aidha, mashirika haya yanatumia fedha kutokana na michango ya wahisani mbalimbali. Je, Wizara ina wataalam wa mahesabu ili kukidhi hoja? Kwa mujibu wa Sheria ya *NGO* ya Namba 24 ya mwaka 2002, *NGOs* zote zilizosajiliwa hutakiwa kuleta taarifa za kazi za mwaka na tarifa za fedha zilizokaguliwa. Aidha, katika ngazi ya Mkoa na Wilaya, wapo Wasajili wasaidizi ambao hufuatilia utendaji kazi wa *NGOs* katika maeneo yao. *NGOs* ambazo hazitoi taarifa za fedha kwa mujibu wa Sheria, hufuatiliwa na hata kupewa taarifa ya kusitishwa usajili wao. Aidha, utaratibu unafanyika ili kuwawezesha wahisani wanapotoa fedha kwa *NGOs,* tufahamishwe ili iwe rahisi kufuatilia utekelezaji na matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali ambayo yanahusu masuala ya utawala, Mheshimiwa Henry Shekifu, anasema motisha na upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Mabugai. Upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wa kada mbalimbali hufanyika kulingana na nyaraka za maendeleo ya utumishi wa kada husika. Mtumishi anapokuwa amekidhi sifa au vigezo vinavyomwezesha kupandishwa cheo, hupandishwa; kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kwenye ikama yake, imewaombea watumishi 220 kupandishwa vyeo, wakiwemo watumishi wa Chuo cha

Maendeleo ya Jamii, Mabugai, kwa kutekeleza Waraka wa Maendeleo ya Utumishi, Namba 7, wa mwaka 2002, kuhusu miundo ya utumishi wa kada zilizopo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambao ni Maofisa wa Maendeleo ya Jamii na Wakufunzi wa Vyuo Vya Maendeleo ya Jamii na Wananchi, ambayo inaboresha maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mialiko ya kutembelea Majimbo mbalimbali imepokelewa, mfano kwa Mheshimiwa Injinia Athuman Mfutakamba. Maombi yamepokelewa na ratiba zitapangwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mfutakamba, tutahakikisha kwamba, tunakuja Jimboni kwako Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omar Nundu, anaulizia mirathi ya Mheshimiwa Omar Sambuli wa Chuo Cha Ufundi Arusha, haijalipwa tangu 2003. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, haina Vyuo Vya Ufundi bali ina Vyuo Vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi. Aidha, tumepitia orodha ya watumishi, hatuna jina la marehemu huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**TAARIFA**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Sikutaka ku-*interrupt* maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba asahihishe kwa sababu aliyechangia kwa kuzungumza ni Martha Umbulla na sio Anastazia Wambura.

**MWENYEKITI:** Taarifa ameipata. Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 53 – WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**

Kif. 1001 *Administration and General…*Sh. 2,199,647,000/=

*(Hapa Mwenyekiti alikuwa akiwataja majina Waliosimama)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kupata ufafanuzi wa moja ya maswali ambayo niliandika kwenye mchango wangu wa maandishi. Kwanza niipongeza tu Serikali kupitia Wizara hii kuanzisha Benki ya wanawake, ambayo nina hakika itawasaidia wanawake wengi lakini pia na wanaume.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa pongezi usitoe nenda kwenye *point*.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia dakika zangu tatu, nitatumia dakika zangu tatu vizuri tu, naomba kujua, pamoja na mkakati ambao Wizara unao kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanapata mikopo. Lakini nataka nijue kati ya wale wanawake karibu 800 na kitu, ambao wamepata mikopo ni wanawake kiasi gani ambao wanaotoka mikoa nje ya mikoa ya Dar es Salaam, wakiwepo wanawake wa Mbozi, Mbeya pamoja na wanawake wengine katika nchi hii, wangapi wamefaidika na mikopo hii?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Zambi kama ifutavyo: Hilo ni suala la takwimu ambazo itanibidi nizifanyie kazi zaidi. Lakini niseme tu kwamba hii ni benki mpya imeanzishwa na ina nia za kufika huko kwa siku za baadaye. Kwa hiyo, kwa sasa hatuna takwimu tu ya kujua wanawake na wanaume wangapi, lakini wapo wanawake ambao wanatoka mikoa mingine, ambao wanakuja na kuomba mikopo katika benki hii. Nitashukuru kwamba baada ya hapa nionane na Mheshimiwa Zambi ili niweze kumsaidia kumpa hizo takwimu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nataka kufahamu kumekuwa na malalamiko mengi ya unyanyasaji mkubwa wa kijinsia sehemu za kazi. Hali haiko tofauti katika kazi ya usanii, kwa maana kwa wasanii wa kike ambao wanajihusisha na kazi za sanaa; filamu, muziki, mpaka wafikie hatua ya wewe kumuona kwenye *TV* au kumjua wanakuwa wamepitia hatua na adha ngumu sana kwa maana ya kunyanyaswa kijinsia kama hongo ya kuwasaidia kufika pale wanapofika. Hili lipo hawawezi tu kusema, sasa ninachotaka kufahamu, Serikali ina taarifa kiasi gani na ina mipango gani ya kuwalinda dada wetu hawa ili hata wanapokuja kuwa na mastaa wakubwa, wabaki na hadhi, heshima na utu wao kama walivyokuwa akina Miriam Makeba na wengine? Nashukuru.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimjibu Mheshimiwa Mbilinyi kama ifuatavyo: Taarifa za unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake katika fani ya sanaa ni sawa na unyanyasaji wa sehemu nyingine yoyote. Kwa hiyo, hawa wanastahili na wao pia waende kwenye vyombo vinavyohusika ili wapate haki yao. Ikiwa ni unyanyasaji, uwe majumbani, uwe unyanyasaji kazini, kuna sheria ambao zinaonesha kwamba wanaweza kupata haki yao. Kwa hiyo, namshauri kwamba kama ana ushahidi atusaidie tuweze kuwasaidia hao mabinti zetu wanaonyanyaswa. Haitoshi kusema wapo, wapo tu ni vyema tukawajua na yeye kama Mbunge ambaye anatoka kwenye fani nadhani atawasaidia vizuri zaidi kwa kutumia sheria iliyokuwepo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kutoka kwa Waziri ni kwa sababu gani kwa miaka mitano mfufulizo, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwamba pale Kahama,

ahadi kila siku ni kwamba kitakarabatiwa na vitendea kazi mtapewa, lakini ahadi hizo hazitekelezeki hazitimizwi, nilitaka kujua tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi katika swali la Mheshimiwa Lembeli kwamba ni kweli Wizara ilikuwa na mpango wa kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikiwemo Chuo cha Kahama, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti hatukuweza kukamilisha bajeti hiyo. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeweka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwa hiyo, namwomba atuvumilie avute subira.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala la udhaifu mkubwa katika vyombo vya dola na vya sheria katika kushughulikia suala la watoto wanaonyanyaswa, ikiwepo kubakwa, kulawitiwa na vitendo vingine vya ukatili na niliishauri Serikali kwamba, waje na mpango na utaratibu utakaosababisha zile kesi za namna hiyo kuweza kufanyiwa *fast truck* kama ilivyofanywa kwa mauaji ya maalbino, ili kuondoa tatizo hili. Kwa sababu kesi hizi huwa zinakaa muda mrefu, watuhumiwa wanatamba mitaani, vitendo vinaendelea na wale wanazidi kusononeka, je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala hili?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba, Wizara inaendesha semina na mafunzo kwa Maafisa wa Polisi na wa Mahakama, ili waone umuhimu wa kushughulikia kesi hizo kwa haraka. Kwa hiyo, kwa sababu hii ni kesi ya jinai, inahitaji ushahidi. Pia tunaomba wananchi ambao wanagundua makosa kama hayo, wahakikishe yanapotokea wanapata ushahidi wa kutosha, ili inapokwenda mbele kwenye mkono wa sheria iweze kushughulikiwa kwa haraka zaidi. Panapokuwepo na ushahidi kesi inasikilizwa kwa haraka zaidi kuliko inavyokuwa tu kusema kwamba kumetokea jambo, inabidi lazima lifanyiwe uchunguzi, kwa sababu lazima kuwe na ushahidi.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nataka ufafanuzi mdogo tu kuhusu hii mikopo inayotolewa kupitia Halmashauri kupeleka kwa wanawake, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri alisema kwamba zile Halmashauri ambazo zimeweza kulipa ama kurejesha mikopo yao vizuri ndiyo wanaendelea kupewa mikopo. Sasa nataka kupata maelezo kwamba zile fedha ambazo zimerejeshwa kwa ukamilifu, pamoja na riba, nidhani kwamba zile Wilaya ambazo zimerejesha vizuri zisingepewa tena bajeti kutoka Wizara bali wangeendelea kuzungusha zile fedha ambazo walizirejesha. Naomba kupata ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Martha Umbulla kwamba, fedha hizi ni fedha ambazo ni *revolving*, kwa hiyo, ni lazima zirudi ili waendelee kupata na kila wanapoleta wanaongezewa kiwango kikubwa zaidi, wakirudisha, tunatoa milioni nne, tulianza kwa milioni mbili, walipoendelea wakarudisha wakapewa milioni nne. Kwa

hiyo, hizi ni fedha ambazo ni za Serikali, lazima nazo tuzi-*account fo*r, kwa hiyo, lazima tuendelee na utaratibu huo. Lakini sisi Wizara inatoa mfuko huu lakini na kwenye Halmashauri pia wanalazimika kutoa fedha kama hizi ambazo zimeingia kwenye Mfuko wa vijana na wanawake. Kwa hiyo, zipo pesa ambazo zinaendelea, hii ni kama chachu kutoka katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuonyesha umuhimu wa kuwa na mifuko ya kusaidia wanawake.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika mchango wangu wa maandishi nilizungumza masuala kadhaa kuhusu jinsia, maendeleo ya jamii, watoto na asasi za kiraia. Naamini nitapata majibu ya kimaandishi kwa manufaa ya wananchi wa Jimbo la Ubungo. Lakini niulize tu kuhusu suala moja mahususi la kisera kupitia mshahara wa Waziri. Tarehe 26 Februari, 2011, tarehe 3 Machi, 2011 na tarehe 7 Machi, 2011, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, amenukuliwa na vyombo vya habari, gazeti moja pamoja na kumwona moja kwa moja kupitia luninga *TBC* na *Channel* 10. Akisema kwamba Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimepewa pesa kutoka nje kwa ajili ya kuandaa maandamano, yenye lengo la kuvuruga na amani na alikuwa akiwaeleza wanawake wasijitokeze kwenye maandamano hayo. Sasa ningependa kupata kauli rasmi ya Serikali kupitia Bunge kuhusu suala hili, kwa sababu hii ni ofisi ya umma, nafasi ya Uwaziri ni nafasi ya umma na tuhuma hizi ni nzito, kuhusu msingi wa tuhuma hizi na ukweli wa tuhuma hizi ambazo mimi mwenyewe nimeziona moja kwa moja kupitia vyombo vya habari.

**MWENYEKITI:** Samahani, tunajadili masuala ya bajeti ya wanawake, jinsia na watoto. Suala hili ni nje kabisa ya Kanuni ile ya 64, ni suala ambalo liko nje ya mjadala, naomba nimwite mwingine tuendelee.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 52, inazungumzia kwamba pesa katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwenye Halmashauri imekuwa *allocated* ni bilioni moja. Sasa ningependa kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kazi ya Maofisa wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu kwa sababu unaweza ukakuta kwamba kuna wanawake wa soko kuu kule la Mwanjelwa, wanawake wa Uhindi, wanauza michele hawana uwezo na wala hawajahamasika. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko la kazi hususan za hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa swali lako zuri, Maafisa Maendeleo ya Jamii, ndiyo wanaosimamia Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake ambao unakwenda katika kila Halmashauri ambapo Wabunge wote ni wajumbe katika Mfuko huo. Maafisa Maendeleo ya Jamii wana kazi ya kuhamasisha wanawake katika kuanzisha miradi ya kujiletea maendeleo, miradi midogo midogo ambayo inaweza kuwaletea maendeleo. Maafisa Maendeleo ya Jamii, wanaweza kutusaidia kutengeneza hata andiko la kuweza kupata fedha katika mfuko huu au katika mfuko mwingine. Kwa hiyo otherwise mfuko huu upo *concern*, Afisa wa Maendeleo ya Jamii anahusika kuhamasisha na kuwaelekeza wafanyeje ili waweze kukopa katika Mifuko hiyo. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na Mheshimiwa Waziri amezungumzia teknolojia mpya katika kutafuta uhalali wa mtoto. Lakini teknolojia hii inapatikana mijini tu na ni ghali mno. Je, Serikali itawasaidiaje, Watanzania wengine ambao uwezo wa vipato vyao ni vidogo lakini pia wanahitaji teknolojia hii katika matumizi yao. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni kwamba mojawapo ya njia za kuweza kutambua uzazi wa mtoto ni kutumia *DNA*, ni kweli kwamba gharama kidogo ni kubwa. Lakini nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nimelipokea na tutalifanyia kazi, tuone ni kiasi gani wanawake pia ambao hawako mjini wakaweza kupata huduma za *DNA*.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilijenga hoja na nilikuwa nataka ufafanuzi kutoka kwa Waziri na sasa nimekamata huu mshahara wake kwa kuwa siku ya wanawake duniani inapoadhimishwa Waziri ni mmojawapo anayekwenda katika maeneo mbalimbali kuhamasisha wanawake na kutoa ujumbe kwa wanawake bila kujali Vyama vyao vya Siasa. Lakini siku ya wanawake mwaka huu 2011, Waziri alifika Wilaya ya Kilombero na katika mkutano ule alihamasisha wanawake wakatae kuingia kwenye maandamano ya CHADEMA, badala ya kuhamasisha wanawake washikamane katika kufanya maendeleo yao. Sasa Waziri anaweza akaniambia nini na je, ile ziara ni ya Kichama au Kiserikali?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Susan Kiwanga, kwamba ile ziara ilikuwa ya Kiserikali na niliwahamasisha wanawake waendelee kujiletea maendeleo yao, wafanye kazi zao badala ya kwenda kufanya maandamano. Niliwafahamisha Wanawake kwamba wanapoteza muda mrefu katika kujiunga na maandamano ambayo hayana faida kwao, waende wakalime na kufanya shughuli za kujiletea maendeleo. Hilo ndilo nililowaambia Wanawake na naendelea kuwaambia tena kwamba maandamano hayana tija, akinamama tutafute maendeleo yetu na ya watoto wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya!

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na furaha ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri sasa hivi ninaomba nimuulize pia kuwa hivi karibuni nimejifunza kwamba kuna mikataba ambayo *NGOs* huwa zinaingia na Serikali ili kuweza kujulikana uhalali wake lakini hata pia katika kupata misamaha kwa mfano ya vibali vya kazi.

Lakini baada ya kufuatilia zaidi tukagundua kwamba hayo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanasajiliwa katika Wizara zaidi ya moja ikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri aidha kwa kutumia nafasi ya sasa au wakati mwingine tungepewa ufafanuzi mzuri juu ya mashirika hayo na usajili wake na tofauti zake ili wananchi waweze kufaidika na fursa zinazotolewa kwa ajili ya mashirika kama hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshiwa Waziri unajibu swali moja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, maswali yake kwamba…

**MWENYEKITI:** Unatakiwa kujibu swali moja tu, Kanuni inasema unajibu swali moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa!

Ni kweli kwamba Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanasajiliwa na Wizara yangu lakini ikumbukwe kwamba Sheria hii ya kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ilianzishwa mwaka 2002. Kwa hiyo, huko nyuma Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalikuwa yakisajiliwa na Wizara nyingine kama *Home Affairs* na *BRELA,* pia inasajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kwa hiyo, kuna vyombo vingi ambavyo vinasajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa hiyo, sisi tunawapa wale ambao wamesajiliwa kwingine cheti cha ukadilifu kwamba tunawafahamu na wao wanaingia katika mfumo wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regia!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeelezea *concern* yangu kutokana na Wizara hii kwamba inaongozwa na wanawake watupu yaani Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wote ni wanawake. *(Makofi)*

Natambua ni Wizara ya Wanawake lakini haimaanishi kwamba ni lazima viongozi wakuu wawe wanawake. Hivyo nilitoa pendekezo kwamba ni vema wakamshauri Mheshimiwa Rais atakapofanya *reshuffling* basi achanganye kama ambavyo Finland wanafanya, Wizara ya Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto inaongozwa na mwanaume na anafanya vizuri. Waswahili wanasema mchawi mpe mwana akulele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regia hili ni suala la uteuzi wa Rais kwa *power* alizonazo kwa vile Waziri hawezi kujibu, naomba kumuita Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hujanisikia, nimeomba ushauri…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regia hakuna swali la pili naomba ukae. Mheshimiwa Leticia Nyerere!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba kuna wanawake wananyanyasika hawaendi polisi kwa kuhofia aibu na kudhalilika. Anatambua kabisa

kuna wanawake wananyanyasika hawaendi kuomba haki zao mahakamani kwa kuhofia aibu au kudhalilisha familia.

Mheshimiwa Waziri alipotoa…

**MWENYEKITI:** Tafadhali uliza swali!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namuomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli, analizungumzia vipi hili kwa sababu anatambua kabisa kuna wanawake wanaona aibu kwenda kutoa taarifa za unyanyaswaji?

**MWENYEKITI:** Wapo pia wanaume wanapigwa majumbani. Mheshimiwa Waziri majibu! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba wapo wanawake ambao wanaona aibu lakini pia wapo wanaume wengi zaidi ambao wanaona aibu kwenda kuripoti kuwa wananyanyaswa na wake zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la unyanyasaji ni suala ambalo linaleta maumivu kwa hiyo ni haki ya yule anayenyanyaswa kwenda kutoa taarifa na Wizara yangu katika kuhakikisha huo woga unatoka ndiyo maana tunakuwa tunawahamasisha akinamama wajitokeze na ndiyo maana kumetungwa Sheria mbalimbali ambazo zinamuonyesha mwanamke kwamba ana haki ya kutotendewa unyanyasaji ambao siku zote ulikuwa unaonekana kama ni kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kunyanyaswa ilikuwa ni jambo la kawaida lakini kutokana na sera nzuri za Chama cha Mapinduzi tumetunga Sheria za *SOSPA,* tumetunga Sheria ya Mtoto na Sheria nyingine nyingi ambazo zinawafanya wanawake sasa kutembea kifua mbele na kusema hatutaki kunyanyaswa. Kwa hiyo, vyombo vipo na Maafisa wanaohusika na kupokea kesi hizo wanapata mafunzo, pia kuna madeski ambayo yanashughulikia masuala ya wanawake ambao wanakwenda kutoa hizo *report.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Japokuwa swali langu nilikuwa nataka kuuliza kama Mheshimiwa Leticia Nyerere kuhusu kuweka madawati katika vituo vya polisi kutokana na usiri wa mambo ya kubakwa na unyanyasaji wa wanawake, sasa naona kama Waziri alitaka kuanza kulizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mikoa mingi sana hakuna hili dawati la kuripoti kuhusu unyanyasaji katika vituo vya polisi, kwa hiyo ninaomba…

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Ninaomba kujua kwamba Waziri analisemeaje kuhusu kuweka madawati katika vituo vya polisi ili kusikiliza kesi za unyanyasaji hasa ubakaji kwa wanawake na watoto kwa sababu wanawake wengi na watoto hawaendi kuripoti kwa sababu hakuna dawati ambalo wanaweza wakaelezea usiri wako. Je, Mheshimiwa Waziri analielezea hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba ni kweli kwamba bado hatujaweza kuanzisha madawati ya kijinsia katika vituo vyote vya polisi lakini lengo letu tukishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria chini ya maboresho ya Sheria au *Legal Sector Reform Program* tunategemea kwamba tutaanzisha madawati haya katika vituo vingi kadri inavyowezekana na tunasaidiwa na wenzetu wa *NGO* kwa mfano *WLAC* na *WILDAF* katika kuhakikisha kwamba madawati haya yanakuwepo na ninawashauri na wanaume msiogope kwani linaitwa *gender desk* haliitwi dawati la wanawake, ni madawati ya jinsia katika vituo vya polisi. Kwa hiyo, unakwenda pale unakaa *chamber* kama umepigwa unatoa malalamiko yako, zamani ukienda polisi ulikuwa unaambiwa haya mambo kayamalizeni kifamilia, lakini siku hizi siyo kifamilia ni kosa la kisheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimira Dkt. Mrema!

**MHE. DKT. AGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Serikali imetoa agizo kuhamasisha Halmashauri, Wilaya, Majiji na Manispaa kwamba kila unapokusanya michango, ushuru na kodi 10% ya fedha zile unazokusanya ziende kusaidia makundi ya akinamama pamoja na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Vunjo sioni haya makundi ya akinamama ambao ni wengi na ya watoto yakisaidiwa michango hiyo. Sijui Waziri utanisaidiaje kule Vunjo kuhakikisha kwamba akinamama na vijana waliopo kwenye vikundi wananufaika na hiyo michango inayochangwa au kodi zinazokusanywa. Yangu ni hayo tu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali hili la Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee* kama ifuatavyo:-

Anachosema ni kweli, wakati Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru alipokuwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali ilitoa maelekezo kwamba kila hela zinazokusanywa katika Halmashauri kwa maana ya *own source,* 5% itengwe kwa ajili ya akinamama na 5% kwa ajili ya vijana. Kama anavyosema ni kweli zipo Halmashauri ambazo zimekuwa zinalalamika kwamba kiasi kinachopatikana katika Halmashauri ni kidogo na kwa hiyo hawatengi. Maelekezo ya Serikali kuhusu suala hili

ni 5% ya kiasi chochote kinachopatikana katika Halmashauri, ndiyo maelekezo ya Halmashauri. *(Makofi)*

Pia maelekezo ya Serikali kwa sasa ni kwamba tukienda katika Halmashauri tukakuta kwamba Halmashauri haikufanya hivyo kwa kisingizio kwamba kiasi kilichopatikana ni kidogo tunatoa tozo na ndiyo maana *Local Authorities Accounts Committee* wanamuandikia Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa maana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kupendekeza kwake kwamba tozo hiyo itolewe kwa wale ambao wamehusika yaani ambao hawakutenga kiasi hicho. Kwa hiyo, utaratibu huo upo na tumeendelea kuupigania na kuusimamia ili kuweza kuwasaidia akinamama na vijana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchuchuli!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi pia nipo kwenye mfuko huo wa *WDF*. Tunaona kwamba kwa kiasi kikubwa marejesho ya mfuko huo yamekuwa hafifu, lakini kuna changamoto ambazo zipo wazi kama hii ambayo Maafisa Maendeleo ya Jamii wengi wanaonekana kwamba wanashindwa kufuatilia marejesho kwa sababu hawana pesa kwa ajili ya ufuatiliaji.

Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba je, wanawasaidia vipi Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kuhakikisha kwamba wanafuatilia hizi pesa za marejesho na zinapatikana ili ziweze kuzunguka kama nilivyosema ni *revolving fund* wanawake wengine waweze kupata hizi pesa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Kurthum Mchuchuli swali lake kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwanza kabla hawajatoa fedha hizi wanatoa mafunzo ambayo yanawasaidia kujua jinsi ya kurejesha na kufuatilia marejesho ni jukumu lao Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa vile hawatakiwi wawakopeshe watu ambao baadaye watapotea. Kwa hiyo, mara nyingi tunapendelea wakikopesha kwenye vikundi, kwenye vikundi mmoja anaweza akapotea lakini wengine wakapatikana. *(Makofi)*

Lakini pia hilo la marejesho ndiyo linaziponza Halmashauri nyingine zisipate hizi pesa kwa sababu kama hazikurejeshwa basi hiyo Halmashauri haipati tena. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge ambao ni sehemu ya ile ya Kamati ya kugawa zile pesa tuhakikishe kwamba wanaokopeshwa wana uwezo wa kurudisha. Ikumbukwe tu kwamba pesa hizi siyo nyingi ni kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kama akinamama ntilie, wanaoshona na kadhalika. Ni fedha kidogo sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1); "Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti anaweza

kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila ya kuhoji. Kwa mujibu wa Kanuni hii naongeza dakika zisizozidi 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jasson Rweikiza!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua mipango ambayo Wizara inayo katika kusaidia vijana na watoto yatima ambao wako wengi sana huko vijijini na mitaani ambao hawana msaada, unakuta wako watatu au wanne kwenye familia lakini msaada wao ni mkubwa wao ambaye labda ana miaka kumi au nane, huyo ndiye ni mzazi wao ambaye ni ndugu yao. Sasa Wizara ina mpango gani mahususi wa kusaidia watoto hawa yatima ambao wako wengi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Jasson Rweikiza kuhusu tatizo la watoto yatima linavyoshughulikiwa. Kwa bahati mbaya sikumsikia vizuri sana lakini nadhani aliulizia kuhusu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza naomba urudie swali lako.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba kuna vijana wengi au watoto ambao ni yatima ambao hawana wazazi wote wawili na hawana msaada wa ndugu, jamaa wala msaada wowote ule. Je, Wizara ina mpango gani ambao ni mahususi kusaidia hawa kwa sababu wanazurura na kuomba tu msaada kwa Wabunge, kwa jamii kwa ujumla na ni ombaomba barabarani. Sasa Wizara ina mpango gani mahususi wa kusaidia hawa vijana ambao kwa kweli ni wengi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii!

**NAIBU WAZIRI W AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kushirikiana na *UNICEF* miaka minne iliyopita walitengeneza kitu kinachoitwa *COSTET Plan* kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na ndiyo sababu tukaanza kupata pesa kwa ajili ya miradi mingi ambayo imekuwa ikiendelea nchini kutumia fedha za *Global Fund*, *PEPFA* pamoja na fedha za *Family Health International* na Serikali pia inachangia kidogo kupitia katika Ofisi ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kuna tatizo kwamba fedha za *Global Fund* kupitia *PACTE* haziji lakini naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inalifanyia kazi na *Global Fund* wamekubali kwamba wataendelea kutoa hizo pesa kwa hiyo Serikali itatoa, wafadhili watatoa na naomba Halmashauri zetu pia ziangalie namna ambavyo zitasaidia katika uwasaidie watoto yatima. Lakini ile *COSTET Plan* ipo na imepelekwa kwa wadau wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina!

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu nilisema Serikali za Mitaa zimeshindwa kuwachukulia hatua wazazi wote wanaotelekeza watoto wao na nikaishauri Wizara jukumu hili lipelekewe sehemu nyingine. Mheshimiwa Waziri ushauri wangu umeupokea namna gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mitaa ni Serikali, kwamba Serikali za Mitaa zimeshindwa kuwaangalia watoto, mahali popote unapokuwa na watoto wa mtaani wamepotea, hawana baba wala mama Serikali duniani kote huingilia kati. *(Makofi)*

Kinachofanyika katika Halmashauri na maelekezo ambayo tumeyatoa katika Halmashauri na ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya amelizungumza suala la Halmashauri hapa ni kwamba tunakuwa na *inventory*, wapo watoto ambao wanajulikana lakini umeshindwa kujua baba yake na mama yake ni nani na vijiji vimeelekezwa kwamba hawa wawape nafasi za kwanza kwa wale watoto ambao wanatakiwa kusaidiwa kwa ajili ya suala la shule. Kwa hiyo, Halmashauri tunachokifanya tunapitisha pale na yale majina yanapelekwa katika *Ward Development Committee* ambayo Mwenyekiti wake anakuwa ni Diwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wamekuwa wanapewa kipaumbele, wale watoto ambao wanajulikana kabisa kwamba hawana mtu yeyote wa kuwaangalia pale. *(Makofi)*

La pili, tumeelekeza katika Halmashauri zetu kwamba itakuwa ni kazi ya Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba tunawatafuta wale ndugu wa watoto ambao wanaonekana kwamba hawana baba wala mama. Kazi hii inaendelea kufanyika na tunaendelea kutafuta kwamba ni nani ambao ni ndugu wa karibu kabisa waweze kuwasaidia wale watoto. *(Makofi)*

Kwa hiyo, si kweli kabisa kwamba Halmashauri kwa maana ya Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji zimeshindwa kuwaangalia watoto hawa, tunafanya hivyo pamoja na kwamba tunajua kwamba tatizo hilo ni kubwa kuliko tunavyofikiri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilifu!

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile watoto wa mitaani sasa hivi Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba limekuwa ni tatizo kubwa kuliko tunavyofikiria na wengi wao hawana baba wala mama na taabu yao hawana hata mahali pa kupata chakula. Je, Serikali sasa ipo tayari kuandaa utaratibu au kitengo maalum cha

kuangalia hawa watoto yatima au watoto wa mitaani ambao wanateseka ndani ya nchi yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba watoto wa mitaani limekuwa ni tatizo kubwa kwani wapo wa aina nyingi. Kuna watoto ambao wana wazazi wao ambao hawataki kuwajibika, wanaenda nao mitaani, wengine mzazi anakaa pembeni, mtoto anaomba. Kuna aina mbalimbali za watoto ambao wako pale mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ni kwamba jukumu la kuhakikisha watoto wanaondoka mitaani ni jukumu ambalo limewekwa katika Serikali za Mitaa na kule kuna utaratibu ambao umetolewa chini ya Sheria ya Mtoto ambayo tumeitunga. Tumeweka Kanuni kwamba watoto wote wawe *registered* ili wajulikane katika mtaa fulani ni watoto gani wana wazazi wao, ili tuwe na *inventory* ya kujua watoto wameondoka katika kijiji peke yao bila mzazi wameenda mjini. Kwa hiyo, lile tatizo ambalo linaonekana katika miji mikuu tunaamini kwamba kama miji midogo na vijijini, hili la kuweka *register* ya watoto likitekelezwa ni mojawapo ya kuhakikisha kwamba watoto hawa watapungua mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia turudi kwa jamii ambayo inatakiwa iwajibike. Jamii imepoteza yale maadili ya kuishi na watoto wao na kuona kwamba mtoto anapaswa alelewe na wazazi, lakini sasa imebadilika unakuta mtoto anatafuta, mzazi amekaa pembeni. Hili halikubaliki na kwa sasa Sheria imeiagiza Ustawi wa Jamii iweze kuwakamata hawa watu na kuwarudisha kila inapotokea. Kwa hiyo, polisi na ustawi wa jamii, wanalishughulikia suala hilo kikamilifu ili kuhakikisha wanapungua ingawa wanarudi. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mchango wangu wa maandishi, pamoja na pongezi ambazo nilimpa Mkuu wa Chuo cha Maendeleo Singida, Ndugu Mlade, nilimuomba Mheshimiwa Waziri kwamba chuo hicho Ndugu Mlade amekiboresha sana kwa kukarabati majengo, amejenga majengo mapya, kweli hakina hadhi ya Kisingida tena, kina hadhi ya Kitaifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali? Uliza swali!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nikamuomba Mheshimiwa Waziri kwamba chuo hicho kipandishwe daraja kiwe Chuo cha Maendeleo ya Jamii, nilikuwa naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo; ni kweli kati ya Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi, Chuo cha Singida ni chuo ambacho kwa kweli kinafanya vizuri sana na naomba nilipokee ombi la Mheshimiwa

Mbunge na kuahidi kwamba tutaona labda tukipandishe hadhi sasa hivi ili kiwe Chuo cha Maendeleo ya Jamii badala ya kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba bado kuna lengo la kuwepo kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa hiyo, inabidi tutazame, labda tunaweza tukasema tuwe na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, halafu pia *at the same time* kiwe kinatoa mafunzo kwa ajili ya maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea na tutalifanyia kazi.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua udhibiti wa Serikali kwa mashirika yanayotoa mikopo kwa wanawake hasa wa ngazi ya chini, kwa mfano, *Finca, Pride, Black,* kwa sababu mashirika haya yamejihusisha sana kibiashara kuliko katika mahusiano ya kuwaendeleza wanawake ambao ni wateja wao, kama wanavyojitangaza na hivyo kuwasaidia badala ya sasa kuwatelekeza na hasa wanaposhindwa kurejesha mikopo yao.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hilo. Mimi nitalichukua ili nishirikiane na wenzangu ili tuone tunalishughulikiaje suala hilo ambalo limekuwa tatizo sana kwa akinamama kutokana na taasisi nyingi za namna hiyo ambazo zinakopesha na kuwa *conditions* ngumu ngumu ambazo mara nyingine wanawachukulia vitu vyao. Kwa hiyo, naomba nilichukue. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nilipokuwa nachangia nilikerwa na tabia ya wanaume na wanawake ambao wanafanya vitendo vya jinsia moja kitendo ambacho kinadhalilisha jamii, kinakwenda kinyume na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ambayo inathamini desturi na mila za Mtanzania na vilevile dini pia inakataza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwamba uletwe Muswada hapa tupitishe Sheria dhidi ya matendo yanayofanywa na watu kama hawa, sikujibiwa. Naomba nijibiwe sasa kwamba Serikali inatoa kauli gani dhidi ya watu kama hawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, lakini naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba mtu yeyote ambaye anakwenda kinyume na maumbile yake aliyopewa na Mwenyezi Mungu, ni ugonjwa wa akili. Tunasema kwamba ana tatizo la *sexual orientation and practice* kwa hiyo anahitaji kupewa matibabu ya ugonjwa wa akili na kupelekwa kwa *psychiatrist*. *(Kicheko)*

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wanawake wa Tunduru wameomba nimuombe Waziri atoe kipaumbele kwenye kukamilisha ukarabati na uboreshaji wa Chuo cha Nandembo, ili waweze kupata

mafunzo na maelekezo mbalimbali ambayo yatawasaidia katika kuleta maendeleo kule Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atuthibitishie hilo ndani ya Bunge lako Tukufu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Devotha Likokola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyojibu kwamba lengo letu ni kuviboresha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi, lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti hatutaweza kukarabati vyuo vyote. Hata hivyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba Chuo cha Nandembo nacho kinafanyiwa ukarabati na kipapewa kipaumbele. *(Makofi)*

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nilipochangia nilizungumzia suala la watoto wa mitaani. Nilisema kwamba Serikali ijenge kituo kikubwa cha kuwalea watoto hawa. Tatizo hili ni kubwa sana na linatisha, ni sawasawa na bomu ambalo linaweza kulipuka *time* yoyote. Watoto hawa hawakai vijijini, wanakimbilia mijini wanakusanyika, nguvu kazi ya Taifa inapotea, watoto hawa tukiwaachia watakuja kuwa majambazi, wengine watakuwa vibaka, watoto watazidi kuzaliana humo mitaani na tatizo litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge kituo kikubwa cha kuwalea watoto hawa na pia kiwape mafunzo ya ufundi na mali ili waweze kuja kujitegemea wenyewe baadaye. Je, Serikali inasemaje katika hili?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo kikubwa kwa watoto wa mitaani hauwezi kuwa ndiyo suluhisho kwa sababu hata wale watoto ambao wanawekwa kwenye vituo, wengine wazazi wao wanaenda wanawachukua. Huwezi ukamnyang’anya mtu mtoto wake ukampeleka kwenye kituo kwani ana haki ya kuwa na mtoto wake. Lililopo ni kwamba jamii ihakikishe inakaa na watoto wake. Pia kuwapeleka watoto kituoni siyo suluhisho, inatakiwa ichukuliwe kama *step* ya mwisho kabisa kwa sababu watoto wanatakiwa wakae na familia zao badala ya kukaa kituoni.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilionesha mshangao wa kiwango cha fedha kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kuwa kidogo sana shilingi 4,000,000/= au shilingi 8,000,000/= lakini pia ningependa Waziri anipe ufafanuzi wanatumia kigezo kipi ku-*allocate* hizi *funds* kwenye Halmashauri husika kwani ukipitia jedwali alilotupa kuna baadhi ya Halmashauri kuanzia mwaka 2006 mpaka sasa hivi hazijapata kabisa *fund* yoyote ile. Kwa hiyo, ningependa kujua ni kigezo kipi wanatumia wakati wana-*locate* hizi *funds* na kuna Halmashauri nyingine zimepata zaidi ya mara tatu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tulieleze vizuri. Kwanza kwamba kiasi hiki kimepanda, kiasi kile kilikuwa siyo shilingi 4,000,000/= kama kilivyo sasa hivi. Kiasi ambacho kilikuwa kinatolewa wakati ule kilikuwa ni shilingi 2,000,000/=. Kigezo ambacho kimekuwa kinatumika hapa ni kwamba ile Halmashauri ambayo imeonesha kwamba imerudisha kufuatana na maelekezo haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameyazungumzia hapa, hicho kinakuwa ni kigezo cha kutosha kuonesha kwamba kuna *compliance* kwa hiyo wanaendelea kupewa.

Kwa hiyo, ndiyo maana unaona inaweza ikajitokeza mara moja, mara mbili, kama unavyoona Magu wamepelekewa pale na wakarejesha kama alivyokuwa anaeleza hapa Mheshimiwa Waziri. Hawa watakachofanya *next time* wanapeleka tena pale pale kwa sababu hiyo tabia inajengeka pale. Sasa ni kweli kwamba zipo Halmashauri nyingine ambazo zinaonekana mpaka sasa hivi hazijapata na hili limejibiwa pia hapa kwamba inatokana na ufinyu wa Bajeti yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kusema hapa ni kwamba tabia ambayo imejitokeza ni kwamba zipo Halmashauri nyingi, sisi ni lazima tukiri hiki kinachosemwa na Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba zimepelekewa hizi fedha lakini hawakurudisha na hizi fedha kama zinavyoelezwa hapa ni fedha ambazo zinatakiwa zifanye mzunguko ili watu wengi zaidi waweze kupata hiyo mikopo. *(Makofi)*

**MHE. BEARTRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ningependa ku-*declare interest* kwamba moja ya fani zangu ni maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu kuuliza na katika mchango wangu wa maandishi pia nimeainisha. Baada ya madaraka mikoani kwa kweli kiungo kikubwa ambacho kinaweza kikasaidia kazi zikaenda katika Halmashauri ni Maafisa Maendeleo ya Jamii. Sasa hivi Maafisa Maendeleo ya Jamii, wamekuwa ni ma-*mc* wakati wa sherehe za Mbio za Mwenge, wanakimbizana na mambo ya UKIMWI, wanakimbizana na mambo ambayo hayaendani na fani yao. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ameeleza majukumu ya Maafisa Maendeleo ya Jamii, lakini kwa sisi Maafisa Maendeleo ya Jamii tunaona tumefunikwa ndani ya Wizara ile kwa sababu sasa hivi jinsia ni ajenda ya Kimataifa, watoto ni ajenda ya Kimataifa, kwa hiyo, zinapewa kipaumbele, ndiyo maana kila linalozungumzwa hapa ni wanawake, ni nini, lakini maendeleo ya jamii kama maendeleo ya jamii hai-*feature* hapo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa ni wakati yeye na Wizara yake wakae chini wafikirie wafanyaje, kwa sababu nina hakika kabisa kazi za maendeleo ya jamii zikiainishwa ipasavyo na Bajeti itaongezeka katika Wizara hii kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana aweze kutuletea mapendekezo katika siku za usoni ili atuambie kwamba pengine hata Wizara hii iweze kutenganishwa, Maenedeleo

ya Jamii ikae yenyewe na iwe na majukumu yake ambayo tunayaelewa sisi maafisa maendeleo asilia.

**NAIBU WAZIRI, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge wa Kilindi. Ni kweli tunatambua utaalam wake mkubwa katika fani hii ya maendeleo ya jamii na analolisema ni kweli pale Wizarani, Idara ya Maendeleo au na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri wanaonekana kama wanyonge. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshapitisha mpango wa kuboresha fani hii ya maendeleo ya jamii. Kama nilivyosema wakati nachangia tunataka turudishe ile *role* ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kama ilivyokuwa *immediately* baada ya Uhuru ambapo walikuwa na nguvu kubwa sana katika jamii, ikilinganishwa na ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niseme tu kwamba tutamtafuta Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, katika kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru tunataka kupata hizo na tuta-*acknowledge* kutoka kwenu kwamba tuboreshe vipi suala zima la maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilipokuwa nasoma katika Kitabu cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 44 jedwali namba moja kuna orodha ya Halmashauri ambazo zimekopeshwa fedha kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kuanzia mwaka 2006/2007 mpaka mwaka 2009/2010, miaka mitano mfulilizo. Katika orodha hiyo pamoja na wilaya nyingine, Wilaya ya Ileje haijawahi kupata mkopo kutoka mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, Wilaya ya Ileje pamoja na wilaya nyingine ambazo hazijapata mkopo wa aina hii, zitakuwa za kwanza kupewa kipaumbele iwapo zitatimiza masharti ambayo nategemea kuyasimamia ninapotoka hapa? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge wa Ileje kwamba kumekuwa kuna Halmashauri nyingi sana ambazo zimekuwa zikiomba ziweze kupata huu mkopo ambao unazungumzwa hapa, lakini kikwazo kikubwa ambacho kimekuwa kikijitokeza na ambacho Mheshimiwa Waziri amekiri hapa ni ufinyu wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumaini yangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri atakuwa amechukua pia haya maombi, wale ambao wamejitokeza kwamba hawajapata mikopo mpaka sasa hivi, matumaini yangu ni kwamba huko mbele ya safari Serikali itawakubalia ili walau waweze kupewa kipaumbele ili wapate mikopo kama vile ambavyo wenzao wamekuwa wanapata. *(Makofi)*

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii nilimuuliza Mheshimiwa Waziri nikitaka kujua kuhusu *Tanzania House of Talents (THT),* kwa sababu kimsingi na inavyofahamika na

wadau wengi wa sekta hii au hii *industry*, inaonekana *THT* inafanya kazi kama kampuni. Sasa nikataka kujua wakati wa *initial registration* yake ilisajiliwa kama kampuni au *NGO?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge anipe muda wa kuweza kulijibu suala hili ambalo linahusu Wizara nyingine pia. *(Makofi)*

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kiwango cha shilingi 30,000,000/= kilichotengwa kwa ajili ya masuala ya UKIMWI nina hofu kwamba ni kidogo sana. Ningependa kujua ni kwa ajili ya shughuli zipi, ni posho, makongamano au ni kwa ajili ya nini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zimetengwa kwa ajili watumishi wa Wizara wale ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI, kwa hiyo ndiyo maana zimekuwa ndogo namna hiyo ili waweze kuendelea kufanyakazi vizuri.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi na michango mingine ya Waheshimiwa Wabunge waliongea, nilihoji kuhusu sheria kandamizi ambayo inawabagua wanawake wanapoolewa na raia ambao si Watanzania, wanapokuja na waume zao hapa nchini, waume zao wanatakiwa kuishi kwa *visa*, lakini wanaume wanapooa wanawake ambao si raia wa Tanzania wanaporudi nchini wanawake wao *automatically* wanapewa uraia wa nchi hii. Kwa nini sheria hiyo ni kandamizi na Wizara ina mkakati gani kuweka mambo sawa ili wanawake wapate haki ya kuchagua wanaume wanaowapenda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge ni sheria Na. 6 ya mwaka 1995 na hilo suala tayari tunalo katika Wizara na Idara inayohusika ya Uhamiaji. Kabla hatujaenda katika sheria yenyewe, kwa maagizo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tunatazama suala zima la Sera ya Uhamiaji katika nchi yetu. Miongoni mwa masuala ambayo yanatazamwa limo hilo suala ambalo analizungumzia Mheshimiwa Mbunge. Ahsante. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts………………..*Shs. 506,254,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning............................*Shs. 566,249, 000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*………………………Shs. 160,260,000
Kifungu 1005 - *Info, Education and Comm.*…..............Shs. 157,683,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*…….Shs. 288,775,000

Kifungu 1007 - *Information, Comm. and Tech.*….........Shs. 91,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Training and Folk Dev.*Colleges……..Shs. 3,879,738,000

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2001 *item 221400 Hospitality Supplies and Services* kina shilingi 475,330,000/=. Sijui Waziri anaweza kunipa maelezo kamili ya matumizi ya fedha zote hizi, wakati kuna sehemu ambazo kama za ununuzi wa vifaa vya kufundishia umeviwekea shilingi 54,600,000/=. Lakini viburudishaji umeviweka shilingi 400,000,000/= na zaidi. Sasa naomba maelezo yako.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinahusu masuala ya vyakula kwa wanafunzi wa vyuo vyetu 55, vyakula vyao viko hapa. Hata hivyo tumejibana sana, lakini hizi zinaenda kwa ajili ya vyakula vya vyuo 55 ambavyo viko katika Wilaya mbalimbali hapa nchini.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Community Development.*………………………………………………Shs.1,596,484,000
Kifungu 2003 - *Community Development College–Tengeru*…..........................…Shs. 982,676,000
Kifungu 3001 - *Gender Development*…………………………………………………Shs. 327,439,000
Kifungu 3002 - *Children Development*………………………………………………..Shs. 295,374,000
Kifungu 4001 - *Non-Government Organizations*……………………………………….Shs. 351,117,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 53 –WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**

Kifungu 1001 - *Administration and General.*……………………………………………..Shs. 40,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*…………………………………………………………Shs. 871,688,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Training and Folk Development Colleges…*............................................Shs. 693,167,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri katika kitabu chake na hotuba yake asubuhi alieleza ni namna gani ambavyo vyuo hivyo *FDC's* zimepewa fedha kidogo kwa ajili ya ukarabati. Nazungumzia kifungu 6329.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vyuo hivi karibu 55 kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri. Lakini vyuo hivi vimepewa shilingi 393,167,000/= kwa ajili ya ukarabati wa vyuo ambavyo wote ni mashuhuda kwamba ni vichakavu sana. Najua Bajeti ya Serikali ni kidogo, lakini Waziri anaeleza nini, nini *commitment* ya Serikali katika ukarabati wa vyuo hivi ambavyo tunajua manufaa yake vikiwa katika hali chakavu sana navyo vinatengewa pesa kidogo hivi kwa ajili ya ukarabati?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Zambi kwa *concern* yake kuhusu kuufanyia ukarabati wa vyuo vya *FDC's.* Ni kweli kwa mwaka huu wa fedha tuna shilingi 393,167,000/= ni kwa ajili ya kukarabati Chuo cha Sofi kilichopo Ulanga na *commitment* yetu ni kwamba kama nilivyoeleza Mheshimiwa Mbunge Zambi, mimi nadhani ni mafanikio makubwa kwa vyuo kuingia katika Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Tunaomba mtusaidie kuhakikisha kwamba angalau sasa ule mpango unatekelezeka katika eneo la *FDC.* Lakini hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali kwamba vyuo vimeingia kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ina maana ina dhamira ya dhati ya kuvikarabati vyuo vyote kikiwemo na chuo cha Mheshimiwa Mbunge Zambi anakotoka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Community Development*……………………………………………………Shs. 96,333,000
Kifungu 2003 - *Community Development College – Tengeru*………...............………Shs. 100,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 – *Gender Development*……………………………………………………Shs. 2,935,190,000

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania na hasa wanawake wa jimbo la Peramiho na kwa kuwa Waziri wa Fedha yupo hapa ndani ninaomba atusaidie kutambua kitu kimoja.Ninazungumzia kile kifungu kidogo cha 4943.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho ni cha shilingi 2,935,190,000/= ambazo mwaka huu zimetengwa kwenye *ceiling* ya Wizara ya *Development Budget* badala ya kuchukuliwa shilingi 2,935,190,000/= hizo moja kwa moja kupelekwa kwenye Benki ya Wanawake ili wanawake waweze kufikiwa na Benki hiyo maeneo yote, badala yake *ceiling* ya Wizara imejumlishwa na shilingi 2,935,190,000/= na kusababisha Wizara hii kuwa na fedha kidogo sana za *Development Budget.*

Kwa kuwa Waziri wa Fedha yupo hapa ndani ninaomba kujua ni namna gani Serikali itachukua hiyo *commitment* ya kuchukua shilingi 2,935,190,000/= za ahadi ya Rais kutoka Hazina na kuzipeleka moja kwa moja kwenye Benki ya Wanawake ili kuiacha hii Wizara iendelee kuwa na *ceiling* ya *Development Budget* peke yake na kuweza kutekeleza majukumu ya kiutekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ndani ya Wizara? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama kama ifuatavyo; shilingi zote 3,000,000,000/= zinatoka Hazina, hakuna ambayo inatoka mahali pengine. Kwa hiyo, zote ni fedha za Serikali kutoka Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais aliahidi kutoa shilingi 2,000,000,000/= kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano na huu utakuwa ni mwaka wa tatu. Sasa tumetoa shilingi 2,000,000,000/= kwa ajili ya Benki na shilingi 1,000,000,000/= kwa ajili ya Wizara, hivyo ndivyo ilivyotokea. Sio kwamba tumetoa shilingi 1,000,000,000/= kutoka Hazina na nyingine zimetoka mahali pengine. Ningependa kutumia nafasi hii kuelezea kwamba Benki hii ni ya wanawake. Lakini mpaka sasa hivi wanawake hawajachangia kitu, shilingi 4,800,000,000/= ni za Serikali. Kilichotolewa ni akinamama kama walichangia sasa hivi ni asilimia 97 kabla hatujatoa shilingi 2,000,000,000/= za mwaka huu. Zile shilingi 4,000,000,000.8 ambazo tumetoa asilimia 97 ni pesa za Serikali. Tukitoa tena mwaka huu shilingi 2,000,000,000/= itakuwa imewahi *completely* ile sehemu ndogo ambayo iliyochangiwa na wanawake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu Benki hii ni ya akinamama ningependa kuwaomba akinamama ili Benki hii kweli iwe Benki ya Wanawake tufanye mpango, akinamama wakutane ama kwenye Mkutano Mkuu ama kwenye aina yoyote ya mkutano ili muamue kuchangia Benki ya Akinamama. Vinginevyo inakuwa ni Benki ya Serikali na kwa sababu masharti yake na mengine yote hakuna tofauti na *NBC, Twiga Bancorp* lakini tuamue kwamba Benki ya Serikali lakini wanawake wapewe kipaumbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeeleweka.

**WAZIRI WA FEDHA:** Lakini kama tunaamua kwamba Benki hii ni ya akinamama nashauri kabisa kwamba akinamama mkae chini, mfanye uamuzi, mchangie Benki hii ili angalau kuwe na *share* fulani ya akinamama katika Benki hii. Akinababa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeeleweka, Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa sikubaliani kabisa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha nitauliza suala tofauti ili Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni vizuri ukalifanyie kazi zaidi.

Mimi nitauliza suala mahsusi kuhusiana na kasma hiyo hiyo ya 4943…

**MWENYEKITI:** Naomba uongee kwa ufupi na Mawaziri wajibu kwa ufupi. Dakika tatu tu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka. Nilikuwa nasema kwamba kwa mujibu wa hotuba ya Waziri ukurasa wa sita unaonyesha kwamba Benki hii imetoa mikopo kwa wanawake 893 peke yake. Lakini wanawake waliokwenda kupewa mafunzo ni takriban wanawake 4,000. Sasa nimefanya wastani kama nimetumia shilingi 8,000,000,000.4 kwa idadi hiyo ya waliopewa mikopo ni kama wastani wa kati ya shilingi 3,000,000/= mpaka shilingi 5,000,000/= kwa mkopo mmoja ambao ni pesa nyingi.

Niseme kwamba naunga mkono hii Benki kupatiwa pesa za kutosha. Lakini nilitaka kupata ufafanuzi malengo ya mwaka huu ya benki kwa sababu inaonyesha kwamba wanaokopeshwa ni wanawake wenye uwezo. Mimi binafsi nilikuwa nikihamasisha sana wanawake wa jimbo langu wa maeneo ya Makurumla, Manzese na kadhalika kwenda kupata mikopo. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aseme tu kwa mwaka huu wa fedha kwa hizi shilingi 2,000,000,000/= zinazopelekwa na Serikali wanakusudia kwa maana ya *target* kukopesha wanawake wangapi ili tuwe na hakika wa kuhamasisha wanawake wengi kutoka Makurumla? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika uwe *brief* na Waziri ajibu *brief*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ufupi sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa vigumu kusema tutawakopesha Wanawake wangapi kwa hizo shilingi 2,000,000,000/=. Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanawake wa aina zote wanafika pale, lakini wengi ni Wanawake ambao ni wajasiriamali ambao wanaanza kwa kupewa mafunzo kama alivyoona kuna Wanawake wengi sana wamepewa mafunzo na waliopewa mikopo ni wachache. Kwa hiyo wapo ambao wanaendelea kusubiri wakiweza kufikia yale masharti kwa sababu Benki hii sio *charity* ni Benki kama Benki nyingine. Kwa hiyo lazima kufuata yale masharti ili waweze kupata mikopo ipasavyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 - *Children Development*……………………………………………….Shs. 116,941,500

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii, nitatumia muda mfupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki cha 3002 kuna hivi vifungu vyote vitatu hapa. Hii miradi ya kusaidia maendeleo ya watoto wetu, lakini inashangaza kwamba kwa miaka yote tulikuwa hatutengi fedha tunategemea fedha za nje. Naomba Serikali itueleze ni lini itatenga fedha kwa ajili ya hivi vifungu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba nimjibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba hali ya Bajeti itakapoboreka zaidi basi miradi hii itaendelea kupatiwa pesa kama ilivyokuwa huko nyuma.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umetutupa mkono, naomba tuendelee.

Kwanza kabisa napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa mlioonyesha katika hoja hii. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wa Wizara hii. Bunge hili limetoa baraka kwenu tunawatakia utendaji kazi mzuri kwa ajili ya manufaa ya watu wetu katika Wizara hii. *(Makofi)*

Kabla ya kuahirisha nina matangazo yafuatayo, Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Bunge anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 22 Julai, 2011 kutakuwa na tafrija ya Waheshimiwa Wabunge kwenye viwanja vya Bunge eneo la maegesho ya magari kuanzia saa 2.00 usiku. Tafrija imeandaliwa na Kampuni ya *Vodacom* mnaombwa mshiriki tafrija hii kwa ajili yenu Waheshimiwa Wabunge wote. Nawashukuru sana na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.17 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 22 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*